Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Tano – Tarehe 15 Mei, 2014**

*(Kikao Kilianza Saa tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, leo ni siku ya Alhamisi, kwa hiyo Kiongozi wa Kambi ya Upinzani hayupo hata ukikaa karibu hapo wewe siyo kiongozi. Kwa hiyo, nitaendelea na wengine kadiri walivyoleta, tunaanza na Mheshimiwa Eugen Mwaiposa.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na :-

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:**

Hotuba ya Makadirio ya Matumizi na Mapato ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. NYAMBARI C. NYANGWINE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. CYNTHIA H. NGOYE (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA ULINZI NA USALAMA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumuzi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Katiba na Sheria Kuhusu Makadirio, Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MHE. KHATIB SAID HAJI (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI JUU YA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Kuhusu Makadirio, Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

**MASWALI KWA WAZIRI MKUU**

**SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu kama nilivyoanza kusema, leo hatuna Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ambaye kwa mujibu wa Kanuni anatakiwa kuanza. Kwa hiyo, nitamwita Mheshimiwa Eugen Mwaiposa.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kabisa kupata nafasi hii ya kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Waziri Mkuu, mvua zilizonyesha nchini mwaka huu hasa kuanzia mwezi wa tatu zimeleta madhara makubwa sana katika baadhi ya Mikoa.

Mfano mkoa wa Pwani, Dar es Salaam, Morogoro na kwingineko nchini. Kwanza niipongeze sana Serikali kwa kutumia *TANROADS* kwa jinsi ambavyo suala hili limeshughulikiwa hasa kuhakikisha kwamba wamerudisha mawasiliano kati ya Wilaya na Wilaya na Mikoa na Mikoa.

Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu madhara makubwa mengine yametokea kati ya kata na Kata na vijiji na vijiji ambayo mpaka sasa ninavyoongea kwa baadhi ya kata na Kata hakuna mawasiliano kabisa.

Mfano mdogo tu katika jimbo la Ukonga hakuna mawasiliano kati ya Kata ya Gongo la Mboto na Ulongoni, Kata ya Kivule na Msongola, Kata ya Ukonga na Gongo la Mboto. Lakini hata Kata ya Kitunda na Magole. Swali langu Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inasaidia sasa mawasiliano haya kurudi katika ngazi hizo ili wananchi waweze kuendelea na shughuli zao za maendeleo?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli anavyosema Mheshimiwa Eugen Mwaiposa tulipata madhara sehemu nyingi hapa nchini. Lakini Serikali imejitahidi sana kujaribu kurejesha hali ya kawaida na kuwezesha usafiri kuendelea kama kawaida.

Lakini kwa upande wa Mkoa wa Dar es Salaam, ni kweli kuna baadhi ya Kata ambazo tumepata hilo tatizo, lakini tulipokuwa tumepata nafasi ya kuzungumza na Mkuu wa Mkoa jambo la kwanza nililosisitiza ni kwamba lazima Manispaa zitambue kwamba barabara hizo ziko chini ya himaya zao na ni jukumu lao la kwanza kuhakikisha wanasimamia utengenezaji wa madaraja hayo na za sehemu zile ambazo zimekatika. Nikamwambia vile vile kwamba upande wa Serikali tutakapokuwa tumepata maombi ya ziada kwa maana ya kwamba uwezo wenu umeishia mahali fulani, basi na sisi tutaangalia tuone namna ya kusaidia ili kurejesha hiyo hali ya mawasiliano. *(Makofi)*

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nimwulize swali moja tu la nyongeza. Kwa kuwa Manispaa zetu nchini nyingi ikiwepo Manispaa ya Wilaya ya Ilala uwezo wake wa kifedha ni mdogo na kwa kuanzia tu walikuwa wametenga shilingi bilioni 1.5 ambazo hazikuweza kusaidia. Lakini kwa kuwa Manispaa hiyo hiyo ilileta maombi ya Shilingi bilioni 4.5 ili kuweza kupatiwa fedha kutoka kwenye Mfuko wa maafa. Je, suala hilo sasa limefikia wapi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sina jibu la haraka haraka kwenye hilo eneo labda mpaka ni-*check* na Katibu Mkuu wangu ili tuweze kujua kama walifanikiwa kupata fedha kidogo au kiasi gani kwa ajili ya kurejesha mawasiliano ya barabara katika Jiji letu la Dar es Salaam.

**SPIKA:** Niwaombe tena mnaouliza maswali naomba muwe *very brief* kusudi wote wafikiwe ama sivyo mtu akihutubia tu basi itakuwa muda hautoshi, Mheshimiwa Desderius John Mipata.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2010 Mheshimiwa Rais alitoa ahadi nyingi kwa wananchi na zilichukuliwa kama ni mkataba wa kuchaguliwa kwake ili akishachaguliwa aweze kutekeleza mambo mbalimbali hayo aliyokwishaahidi.

Mfano ninautoa ni katika jimbo langu la Nkasi, Mheshimiwa Rais aliweza kuwaahidi wananchi kutengeneza barabara tatu zinazounganisha kanda mbili tofauti muhimu sana, Ukanda wa Mwambao na ukanda wa Ufipa ya Juu.

Barabara hizi Halmashauri katika kuhakikisha kwamba inatekeleza ahadi ya Rais, chini ya uwezo wake, ilipendekeza barabara hizi ziweze kupandishwa hadhi jambo ambalo halijawezekana.

Lakini pia yalitumwa maombi maalum chini ya mfuko wa dharura yenye thamani ya shilingi bilioni tatu lakini tumepata milioni mia nane tu kwa barabara Kanakala, Kitosi na Wampembe. Barabara ya Minde na Namanyere haijapata kitu chochote na muda uliobaki haunihakikishii kwamba inawezekana ahadi hii ikatekelezwa. *(Makofi)*

Je, Serikali bado inawaaminisha wananchi kwamba ahadi zote za Mheshimiwa Rais zitatekelezwa kabla ya muda wa kipindi chake kwisha?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, nia ni hiyo, dhamira ni hiyo, lakini kwa sehemu kubwa inategemea vilevile fedha ambayo inapatikana. Mliomba bilioni tatu mmepata milioni mia

nane ni kweli haijafikiwa kiwango kinachotakiwa, lakini hiyo haina maana kwamba ahadi hiyo haitatekelezwa. Hata kule kutoa hicho kiasi cha fedha ni kuonyesha dhamira kwamba bado nia iko pale pale. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama tumeshindwa kwenye mwaka wa fedha ambao unaishia Juni mwaka huu, lazima tuangalie uwezekano wa mwaka huu ambao utaishia Juni mwaka kesho, (2015). Kwa hiyo mimi nadhani tuendelee tu kukumbushana na sisi tutajitahidi kujaribu kutoa msukumo zaidi ili barabara hizo ziendelee kuhudumiwa na bahati nzuri ni barabara ambazo nazijua nimetembea kule wakati wa ziara zangu. Kwa hiyo, tukishirikiana naamini tunaweza tukasaidia tukapunguza ile kero.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri, nina swali moja la nyongeza. Pamoja na juhudi na ukweli alioueleza Mheshimiwa Waziri Mkuu juu ya azma ya Serikali kutekeleza ahadu za Mheshimiwa Rais. Lakini wapo watendaji ambao wanabeza juhudi za Waheshimiwa Wabunge, watendaji na viongozi wa Serikali wanaobeza juhudi ya Waheshimiwa Wabunge nikiwemo mimi katika kipindi nilichokaa hapa cha miaka mitatu na nusu. Barabara hizi nimezisemea sana, nimeandika barua Ofisini kwako, nimeweza kwenda Ofisi ya TAMISEMI kumwona Katibu Mkuu. Jitihada zote nilizozifanya ziliwezesha kupata kiasi kidogo tu cha fedha hizo, lakini wako viongozi na watendaji wa Serikali wanaobeza juhudi zangu.

Je, Serikali ina kauli gani juu ya watendaji wanaobeza juhudi za viongozi waliochaguliwa na wananchi kama mimi. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni dhahiri ni vigumu kwangu kulisemea kwa uhakika kwa sababu sina hakika ni viongozi gani wanaobeza au wanaoona kwamba hufanyi kazi yako vizuri.

Lakini mimi nadhani kubwa wewe ni Mbunge, jukumu lako unalifahamu. Hayo mengine yanaweza yakasemwa lakini wewe tekeleza wajibu wako, watu wako wata-*appreciate* hao wengine wanaobeza ukipata nafasi basi ninong'oneze tuone ni akina nani, wanabeza kwa misingi gani, tuweze vile vile kuwashughulikia.

**SPIKA:** Shughuli nzito kabisa, Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami nipate kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Waziri Mkuu katika Mkutano wa kumi na nne mwaka jana nilipata kusimama hapa na kuongea kero ya wananchi wanaoishi katika Kata ya Kaniha, kijiji cha Kaniha na Kijiji cha Mpago ambao walikuwa wanasumbuliwa kwamba wanaishi ndani ya hifadhi. Lakini nashukuru kwa maelekezo yako uliyoyatoa na timu ya wataalam uliyotuma iende kufanya kazi japo haijafika kule lakini walau wanapata unafuu japo leo tena katika vyombo vya habari imejitokeza watu wanabeza sisi tunawatetea wananchi inaonekana hakuna kazi tunayoifanya.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, wananchi hawa pamoja na kilimo wanachoshughulika nacho lakini ni wafugaji wa nyuki. Mwaka jana wamesumbuka sana kupata kibali cha kwenda kurina asali yao. Hata mwaka huu dalili hizo zinajitokeza. Nini kauli yako Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu wananchi hawa kupatiwa vibali vya kwenda kurina asali?

**SPIKA:** Kwa sababu yeye ni mtu wa asali basi ajibu, Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mimi ni mlaji wa asali sana, lakini mpenzi sana wa sekta hiyo. Sehemu nyingi nilishatoa maelekezo kwamba alimradi hawa wananchi ni wale ambao madhumuni yao kwa uelewa wa vyombo vinavyohusika ni hiyo ya kwenda kurina asali hawana madhara kwenye maeneo haya. Ni suala la usimamizi tu kama kuna hofu hii hofu isichanganywe na uhalisia kwamba misitu ile lazima ifanye kazi vile vile ya kusaidia jamii katika kujaribu kupunguza matatizo waliyonayo ya kifedha. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kama liko hilo maalum kwa ajili ya eneo lako mimi nitaongea na Mkurugenzi wako, tutaongea na Waziri wa Maliasili hili si tatizo watendaji wanalikuza bure tu kwa sababu maeneo mengi misitu ile ndiyo vile vile kiini cha wananchi kuweza kufanya hiyo shughuli ambayo unaisema. Kwa hiyo, tutazungumza na Maliasili nadhani ni vizuri wakaelewa hiyo kwamba ni muhimu sana kwa maendeleo ya watu vile vile. *(Makofi)*

**SPIKA:** Siyo lazima uulize swali la pili kama umeridhika, Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru na nimefarijika na majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni wananchi wa Kata ile ya Kaniha pamoja na jirani zangu wa Ushirombo. Lakini Mheshimiwa Waziri Mkuu mpaka sasa wanacho kiasi kikubwa sana sana cha asali ambayo imekosa soko. Unawasaidiaje kupata soko la asali yao? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, labda nimwombe tu rafiki yangu Mheshimiwa Mbassa kwa sababu haya mengine tunaweza tukayatatua vizuri zaidi tukae tu mimi nitakusaidia tutalimaliza hili bila kuchelewa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ndiyo uzuri wa kufanya kazi ana kwa ana inakuwa ni nzuri zaidi, Mheshimiwa Murtazar Ali Mangungu.

**MHE. MURTAZAR A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ningependa kumwuliza Waziri Mkuu kwamba kwa kipindi kirefu hivi sasa Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali katika kuboresha huduma za afya lakini yapo madai ambayo yana ukweli kwamba wananchi wamekuwa wakiuziwa madawa ambayo ni ya bandia na hayakidhi viwango na yanaingizwa kwa kiasi kikubwa kutoka nje. Imefikia hatua mpaka makampuni haya yanatumia vifungashio vya makampuni mengine kiasi cha kusababisha wananchi wanapata hasara ya fedha na wanapoteza maisha. Nini tamko la Serikali kwenye kudhibiti uagizaji huu wa madawa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, analolisema Mheshimiwa Mangungu ni kweli tatizo hilo lipo kama mnavyoliona kwenye bidhaa nyingine vile vile. Lakini ninachoweza kwanza ni kuwasihi sana Watanzania hawa ambao wanafanya biashara ya madawa kuzingatia kanuni stahiki kwa sababu uhai wa binadamu huwezi ukauthaminisha kwa urahisi kiasi hicho.

Ni kweli unataka fedha lakini lazima ujue kwamba unahatarisha vile vile uhai wa wenzako pale unapokuwa unafanya biashara ya dawa ambazo hazina sifa zinazotakiwa. Sasa hili ni jukumu letu sisi wote kama Watanzania, lakini kwa upande wa pili nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mangungu Serikali inajitahidi sana kupitia vyombo vyake na hasa *TFDA,* wakala ambaye ndiye anasimamia masuala ya vyakula na dawa mbalimbali.

Lakini vile vile tumekuwa vile vile na utaratibu wa mara nyingi kupita kwenye *pharmacy* hizi na kufanya ukaguzi wa dharura na kila tulipobaini tatizo hili hatua stahiki zimechukuliwa.

*TBS* nao wamesaidiana sana na vyombo hivi vingine kila ilipobainika kwamba madawa yaliyoingizwa ni feki hatua stahiki zilichukuliwa tukaharibu zile dawa kwa sababu hazikukidhi vigezo vinavyotakiwa.

Kwa hiyo, mimi nadhani tutaendelea na hizo juhudi na mimi niombe vyombo vyetu viongeze tu kasi ya usimamizi ili tuweze kuepusha kuhatarisha maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZAR A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini nilitaka nijue kwamba kwa sasa Serikali iko tayari kuchukua hatua kali dhidi ya maharamia hawa ambao wanasababisha vifo kwa wananchi ikiwa ni pamoja na kufilisiwa na kunyongwa hadharani kwa sababu wao wanasababisha vifo? *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naelewa sana uchungu alionao Mheshimiwa Mangungu kwenye jambo hili. Lakini mimi nadhani kikubwa wale wote ambao wamekuwa wakibainika wengi wao tumewapeleka mahakamani kwa sababu ni lazima utaratibu wa kisheria ufuatwe.

Kwa sheria zilivyo hapa sisi hatuna ule utaratibu wa kunyonga watu hadharani mara nyingi huwa ni jambo linafanyika na ni nadra na hii nilitaka nikwambie ni nadra sana viongozi wetu katika eneo hili wanapata taabu kidogo kwa sababu roho ya mtu kuiondoa nayo ina tatizo lake.

Lakini ninachoweza kukuhakikishia ni kwamba mkondo wa sheria utachukua mkono wake kila itakapoonekana kwamba kuna watu wamevunja sheria hizi za dawa.

**MHE. SUZAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu swali langu lilikuwa linataka kujengeka pale alipoanzia Mama Mwaiposa kwa maafa yaliyotokea ndani ya nchi yetu, kutokana na mabadiliko ya hali ya nchi. Lakini katika mkoa ambao umeathirika sana ni mkoa wa Morogoro. Mpaka hivi sasa hali iko tete sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiwanga, kama liliulizwa na yule tena wewe huwezi kuuliza.

**MHE. SUZAN L. KIWANGA:** Najenga kwenye mazingira mengine.

**SPIKA:** Nenda moja kwa moja kwenye hoja yako tu.

**MHE. SUZAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Hivi sasa ninavyozungumza Wilaya ya Kilombero yenye Kata 23, Kata 14 hazina mawasiliano kabisa. Watu wanakufa, akinamama wajawazito yaani kuanzia Ifaraka mpaka kuelekea Tanganyika Masagati na Uchindile, hakuna mawasiliano.

Lakini usafiri ambao wanautegemea ni wa treni tu, kama unavyosikia kwenye vyombo vya habari juzi na jana wafanyakazi wa *TAZARA* wamegoma kwa kutolipwa mishahara ya miezi mitatu.

Sasa ningeomba kauli ya Serikali ni namna gani mnaokoa wananchi wa wilaya hizo, Kilombero na Ulanga kwa usafiri ambao ni mmoja tu sasa walikuwa wanautegemea usafiri wa *TAZARA* kwa kuwalipa mishahara yao wafanyakazi wa *TAZARA* na kupeleka miundombinu fungu maalum kwa ajili ya kuboresha miundombinu Wilaya ya Kilombero na Ulanga.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, mkoa wa Morogoro kwa upande wa Kilombero, Ifakara kule ni kweli mvua zilikuwa ni nyingi sana kama ilivyokuwa kwenye mikoa mingi.

Kwa hiyo, kivuko cha Kilombero ilikuwa ndiyo adha ya kwanza ambayo mimi niliarifiwa na tukasema tufanye kila litakalowezekana, ikibidi tukaomba na jeshi ili waone kama wanaweza wakatusaidia kuendelea kutoa huduma katika maeneo hayo ili waweze kupata huduma hiyo ya msingi, wakati tunasubiri maji yale yaweze kupungua.

Umeunganisha na suala la *TAZARA*, ni kweli *TAZARA* tatizo lake tunalijua na tunalishughulikia. Imani yangu ni kwamba tutakamilisha hilo zoezi mapema ili usafiri wa *TAZARA* uweze kurejea tena katika hali ya kawaida mapema. Tukifanya hilo nalo litachangia kiasi fulani kwa ajili ya kusafirisha wananchi katika eneo hilo la Morogoro.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Kiwanga tena unatakaje, ndege sasa. *(Makofi)*

**MHE. SUZAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, hilo la *TAZARA* limefanyiwa haraka sana kwa sababu kama nilivyosema hali ni tete watu wanakufa hasa akinamama. Maana hospitali ya rufaa iko Ifakara tu.

Lakini kata 14 hazina hospitali na barabara ni mbovu. Sasa nilikuwa naomba je, kwa fungu la maafa uko tayari sasa kuisaidia Wilaya ya Kilombero kwa haraka zaidi ili irejeshe miundombinu ya barabara katika kata 14 kuanzia Ifakara mpaka Tanganyika Masagati, hadi Uchindile?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, Kata 14 si kwamba zimepangwa mstari mmoja kwenye reli hapana. Kata si kata 14 zimezagaa katika eneo pana zaidi kidogo. Ndiyo maana nimesema tatizo lake ni kubwa kuliko inavyoelezwa, ziko ambazo zinaweza tukazifikia kwa njia fulani, ukiwezesha kuvusha watu kwenye kivuko wengine wanaweza wakafika huko.

*TAZARA* ninayozungumza mimi ni kwa maana ya kuwezesha usafiri kwa ujumla wake uweze kuanza kufanya kazi haraka. Sasa suala lako ni mishahara na mimi nimesema tunalifanyia kazi mapema itakavyowezekana, fedha zipatikane ili usafiri uweze kurejea. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN HILARY NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona, kwanza nikupongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kujibu maswali vizuri. Swali langu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mwaka 2014 ni Mwaka wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Kuna Kata nyingi na baadhi Vijiji vimegawanywa ili kuleta ukaribu wa huduma.

Je, hizi sehemu zimeshagawiwa ni lini Serikali itazitolea maamuzi ili watu wajipange kwa ajili ya Uchaguzi?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, sikuelewa sana swali lake labda alirudie kidogo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, ulirudie.

**MHE. STEPHEN HILARY NGONYANI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, mwaka 2014 ni mwaka wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kuna Kata nyingi na baadhi vijiji vimegawanywa kwa ajili ya ukaribu wa huduma.

Je, Serikali imeweka mikakati gani kwa hizi sehemu ambazo zimeshagaiwa ambazo tayari ziko kwako ili zitolewe maamuzi ili wanachi wajue ni wapi pa kuanzia.

**SPIKA:** Naona sasa umeelewa vizuri Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli huwa tunao utaratibu tuliotangaza kwamba kama tuna maeneo ya namna hiyo vijiji vile vile tuliomba tuzipate mapema, na tumepokea maombi mengi.

Kwa hiyo, kubwa hapa ni uchambuzi kwanza wa kina kuona kama ni Kata zipi, ni vipi vinaweza kukidhi vigezo tukishamaliza lile basi tutatoa taarifa bila kuchelewa. Kwa hiyo, nataka nikuahidi tu kwamba kwa upande wa Kata, kwa upande unaozungumza nadhani zoezi linakwenda vizuri.

Punde tukishamaliza tutalitoa mapema tu kabla wakati haujafika kwa sababu lazima tuhakikishe inaingilia au inaendana pamoja na kazi ya Tume ya Uchaguzi wanapoanza kuweka maeneo yao kwa ajili ya uchaguzi. Lazima na sisi kazi yetu tuwe tumekwisha kuimaliza. Kwa hiyo, tutalifanya mapema sana. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN HILARY NGONYANI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa majibu yako mazuri. Kuna vijiji toka mwaka 2010 mpaka leo hii vimeomba kuwa vijiji kamili na mpaka leo hii havijatolewa maamuzi hasa kwenye kijiji cha Mkameni, Kata ya Mkomazi, na kwenye kijiji cha Lusanga Kata ya Kirenge, Mheshimiwa Waziri Mkuu wananchi hao wamepata usumbufu kwa muda mrefu naomba sasa tamko kwamba vijiji vile ni lini vinakuwa Serikali kamili ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Aah! Siyo kazi yake hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:**Mheshimiwa Spika, kama ni tangu 2010 inawezekana havikuwa na sifa maana vijiji vingi tuliweza kuvipitisha tu wakati ule. Lakini madamu sasa tuko kwenye mchakato huu mwingine hakuna ubaya mkarejesha tena ombi lile ili tuone kama pengine kumekuwa na mabadiliko katika vigezo vya msingi ili tuweze kuona kama uwezekano huo upo.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, Mheshimiwa Waziri Mkuu nchi yetu ya Tanzania ina misitu mingi sana lakini tuna tatizo kubwa sana la madawati hasa kwa shule za misingi za vijijini na shule za Kata za sekondari, na hii inapelekea watoto kutofanya vizuri mitihani yao kufuatana na uhaba wa madawati.

Je, sasa Serikali inaweza ikatamka nini kuweka mikakati kwa ile misitu inayomilikiwa na Serikali kuweza kuchonga madawati kwa kila wilaya nchini?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli lipo hilo tatizo na wakati nilipokuwa kwenye maadhimisho ya wiki ya elimu, nilijaribu kulieleza sana na jana nilipokuwa kwenye Mkutano wa *ALAT* nimetoa maelekezo mahususi. Kwa hiyo, nimetaka kila Halmashauri wahakikishe hili tatizo wanalipangia *program* ndani ya mwaka mmoja kuweza kuondoa tatizo hili kwa kiasi kikubwa, kwa sababu hatuna tatizo la rasilimali ya kuweza kuwezesha kumaliza hilo jambo.

Mheshimiwa Spika, nimewaambia jana kwamba nadhani kwamba dhamira ndiyo inakosekana kwenye maeneo mengi. Kwa hiyo, nataka nihakikishie tu kwamba tutalisukuma sana jambo hili kwa nguvu ili tuweze kumaliza tatizo lake.

**MHE. KHATIB ALI SAID:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Mheshimiwa Waziri Mkuu, zoezi la uandikishaji vitambulisho vya Taifa, limemalizika upande wa Tanzania Zanzibar likiwa limeacha makovu la wananchi kadhaa, kunyimwa kupata haki hiyo ya vitambulisho vya Taifa. Mheshimiwa Waziri Mkuu nikupe mfano katika majimbo machache ya wilaya yangu ya Micheweni, jimbo la Konde, raia 500…

**SPIKA:** Hapana, uliza swali la msingi hiyo vijiji itatupotezea muda.

**MHE. KHATIB ALI SAID:** Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kauli ya Serikali kuhusu hatima ya raia walionyimwa Vitambulisho vya Taifa?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, hata kama angekuwa ni yeye ni Waziri Mkuu akaulizwa swali gumu namna hiyo asingeweza kulijibu. Kwa sababu uandikishaji ule ni uandikishaji unaozingatia sheria, una taratibu zake na kila wanaposema hustahili lazima kuwe na sababu.

Kwa hiyo, mimi nadhani cha msingi hapa kama una maeneo na watu ambao unao kabisa hili halikuzingatia utaratibu wamenyimwa bila sababu za msingi, mimi ningeshukuru tu kwamba hayo utuandikie halafu tujaribu kuzungumza na Tume, tuone watupe maelezo gani kwanini jamii hii imeachwa wakati sifa za msingi za kisheria bado zinawaruhusu. Mimi nadhani nikilipata kwa njia hiyo naweza nikasaidia vizuri zaidi.

**MHE. KHATIB ALI SAID:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu takriban wengi wanaonyimwa vitambulisho hivi ukichukulia hesabu yao inalingana kabisa na walionyimwa vitambulisho vya Uzanzibari. Kwa maana hiyo inaendelea kuwaacha wananchi hawa hawatatambulika kama Wazanzibar, wala Watanzania.

Je, kwa muktadha huu, Serikali yako iko tayari sasa iwapo juhudi zote zitashindakana kuwatambua wananchi hawa na kuwapatia vitambulisho?

Serikali iko tayari kuwatangaza wananchi hawa kama ni raia wasiotakiwa na nchi yao, hivyo mashirika ya kutetea haki za binadamu na yanayopokea wakimbizi wawe tayari kuwapokea Wazanzibari ambao hawatakiwi na Zanzibar wala Tanzania? Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kauli yako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mbona wewe hujajibu kwamba utaandika? Mbona hujajibu kwamba utaandika halafu uendelee na hayo maneno? Utaandika maana yake alikuomba uandike.

**MHE. KHATIB ALI SAID:** Mheshimiwa Waziri Mkuu nitaandika. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema inawezekana una hoja ya msingi kabisa kwa sababu mimi siwezi nikai-*refute* hiyo, lakini maelezo yale ya jumla yanaweza yasinisaidie mimi kusaidia kutoa ufafanuzi mzuri. Inawezekana kabisa idadi hiyo ni kubwa lakini lazima urudi na kusema kwanini wameachwa sheria ndiyo kikwazo au kuna tatizo jingine.

Sasa kama sheria ni kikwazo siwezi nikasema mimi kinyume na hiyo sheria, kwa hiyo lazima turudi kwenye sheria tutatue tatizo la sheria ili tuweze kutoa nafasi kwa hilo jambo jingine. Kwa hiyo, mimi nilikuwa nafikiri hapa labda ni suala tu kukaa tukajaribu kuona tatizo hasa liko wapi halafu tuone kama kuna njia ya kuweza kulimaliza. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:**Mheshimiwa Waziri Mkuu, walimu kwenye nchi hii wana matatizo mengi sana na kero nyingi sana wanazopata. Moja ya kero walimu hawa ulazimishwa kujiunga na vyama vyao bila ridhaa yao wenyewe na katika kulazimishwa kujiunga kwenye vyama hivi inabidi wavilipie ada. Walimu wanalalamika nchini kote kuwa hawapati msaada wowote kutoka vyama hivi kuwasaidia wao wanapokuwa na matatizo.

Je, Serikali inaweza ikatoa mwongozo kwa wale walimu ambao hawana nia ya kujiunga na vyama vyao basi wasiingizwe kwa ulazima?

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, labda nikubaliane tu ni rai yake, lakini itabidi tuifanyie kazi, mimi nadhani ni jambo la msingi lakini lazima tukae chini tuone msingi wake ukoje tukifanya hivyo maana yake nini lakini vinginevyo nadhani mimi sina ugomvi sana na hilo unalopendekeza.

**SPIKA:** Waheshimiwa muda wa maswali umekwisha hamjafanya vibaya sana maana wawili tu ndiyo wamekosa. Kwa hiyo, tunatendelea. Katibu tuendelee. *(Makofi)*

**MASWALI YA KAWAIDA**

**SPIKA:** Wanasema Waziri Mkuu ahsante sana kwa kujibu vizuri maswali yaliyo mengi na nyie waheshimiwa ahsante kwa kuulizwa maswali kwa kifupi ndiyo tumefika hapa, lakini mjifunze kuuliza kwa kifupi zaidi. *(Makofi)*

Maswali ya kawaida tunaenda na ofisi ya Rais, Mahusiano na Uratibu, Mheshimiwa Said Mohamed Mtanda, atauliza swali hilo kwa niaba yake Mheshimiwa Murtaza Mangungu.

Na. 61

**Mkakati wa Kuinua Uchumi wa Mkoa wa Lindi**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. SAID M. MTANDA)** aliuliza:-

Mkoa wa Lindi umewekwa kwenye orodha ya Mikoa iliyo nyuma kimaendeleo katika Taifa:-

(a) Je, Serikali sasa ipo tayari kuja na mpango mkakati wa kuinua Uchumi wa Mkoa huo na hasa katika Sekta ya Kilimo, Elimu, Uvuvi na Uzalishaji Gesi?

(b) Je, ni fedha kiasi gani kitatengwa kwa ajili ya kutekeleza mpango huo maalum wa kuinua uchumi wa mkoa huo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Saidi Mohamed Mtanda, Mbunge wa Mchinga, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali iko tayari na inayo mpango na program mbalimbali za kuinua uchumi wa nchi na kipato cha mwananchi mmojammoja na mkoa wa Lindi ukiwemo. Baadhi ya *program* na mikakati inayotekezwa katika sekta hizo kwa malengo ya kuinua uchumi ni kama ifuatavyo:-

(i) Sekta ya kilimo na Uvuvi, katika mpango wa mwaka 2014/2015 kilimo, ufugaji na uvuvi ni miongoni mwa vipaumbele vilivyoainishwa katika mpango huo. Wananchi wa Lindi na Mtwara iwapo watashiriki kikamlifu katika kuanzisha miradi ya kilimo, uvuvi na mifugo kupitia mipango ya Serikali kama *ASDP* na hatimaye kuuza mazao ya chakula kwa makampuni yanayojihusisha na gesi, kipato cha wananchi wa maeneo hayo kitaongezeka.

(ii) Uzalishaji gesi, Serikali ilipitisha sera ya gesi asilia, ya mwaka 2013 na kupitia Wizara ya Nishati na Madini tumeandaa mpango mkakati wa miaka mitano ya utekelezaji wa sera ya gesi na tayari imeanza kutayarisha rasimu ya sheria ya gesi. Ni matumaini yetu kuwa sera hiyo itakuwa kwa manufaa ya wananchi wote wakiwemo wananchi wa mkoa wa Lindi na Mtwara.

(iii) Elimu, kupitia *program* ya MMEM, MMES Serikali itaendelea na juhudi za kuboresha elimu katika mikoa yote na kwa mkoa wa Mtwara na Lindi ukiwemo.

Aidha, kwa kutilia mkazo elimu chini ya MMES na MMEM, vijana wengi wa Mtwara na Lindi watanufaika na kufaidika katika kupata ajira katika makampuni yanayoshughulikia gesi au viwanda vinavyojengwa Mtwara kama matokeo ya uvumbuzi wa gesi.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa Bunge lako Tukufu liko katika mchakato wa kupitisha Bajeti ya Serikali 2014/2015 kiasi cha fedha kitachotumika katika kutekeleza mipango hiyo kitajulikana mara baada ya Bajeti ya Serikali kupitishwa na Bunge lako Tukufu.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kunipa fursa niulize maswali mengi ya nyongeza kutokana na umuhimu wa suala hili.

La kwanza, katika kuinua uchumi, ni lazima kuboresha miundombinu, ni sababu zipi za msingi ambazo Serikali inaweza ikatueleza wananchi wa mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ambapo wiki iliyopita wamedhalilika na wamepata shida wanashiriki vipi kwenye uchumi wa gesi hawana barabara Serikali haiku tayari kumaliza kipande cha Ndundu Somanga.

Je, ushiriki huu utapatikanaje, kama ikiwa Barabara hii haikamiliki?

Wananchi wa Tandahimba, Masasi na kadhalika, wamekuwa wakililalamikia hili kila siku na Serikali imeamua kutokulijibia nataka majibu ya Serikali katika hilo?

La pili, kwamba kwa kipindi choe tumekuwa tukiweka vigezo vya idadi ya watu kama ni moja kati ya vinavyoangaliwa katika kupeleka maendeleo katika maeneo. Unawezaje kukuza idadi ya watu, ikiwa hatuwezi kuboresha miundombinu na huduma ambazo zinachangia watu kulundikana.

Imefikia wakati Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaam wanawaambia wananchi wetu wasije Dar es Salaam na sisi tusiende Dar es Salaam, na sisi tutawaambia wananchi wetu wasipeleke mazao wanayozalisha wala vyakula ambavyo vinatoka katika maeneo yetu. Sasa hamwoni kwamba hii italeta mpasuko baina ya wananchi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kuhusu miundombinu ni kweli kwamba miundombinu ni muhimu sana katika kuondoa vikwazo vya maendeleo na barabara ya Dar es Salaam kwenda kusini imetengenezwa lakini ni kweli vilevile kwamba kuna sehemu ya Ndundu, Somanga ambayo bado haijakamilika na Serikali imekwishachukua hatua imepeleka fedha kwa ajili ya mkandarasi wa eneo hilo kumaliza.

Matumaini yetu ni kwamba kazi hiyo itafanyika na adha ambayo inatokana na eneo hilo itafika mwisho wake hivi karibuni.

Swali la pili, juu ya Idadi ya watu kuwa kigezo cha Maendeleo ni kweli. Kwamba idadi ya Watu kuwa kigezo cha maendeleo ni kweli kwamba Idadi ya Watu ni mojakati ya vigezo vinavyofuatwa katika kugawa rasilimali za Taifa.

Hata hivyo, hicho siyo kigezo pekee, viko vigezo vya miundombinu, mazingira katika maeneo ambayo watu wanaishi bila kujali idadi yao, hilo ni jambo vilevile ambalo ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba wananchi wanafaidika na maendeleo yao bila kufanya idadi ya watu kuwa kikwazo. Nimekwenda katika sehemu mbalimbali za Mkoa wa Lindi na nilishuhudia kwamba hatua mbalimbali zinachukuliwa katika elimu.

Hatua mbalimbali zinachukuliwa katika utengenezaji barabara zinazounganisha Wilaya na Wilaya. Zote hizo zinaweza zikatumika katika kukuza na kuwasaidia wananchi wa Lindi kupata maendeleo ya haraka. *(Makofi)*

**MHE. SALUM KHALFAN BARWANY:** Mheshimwia Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Mkoa wa Lindi ni miongoni mwa Mikoa mitatu ya Kandaya Kusini ambayo tayari kupitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi walihakikisha kwamba watachukua hatua kwa Mikoa ile ambayo iko nyuma kimaendeleo.

Tulikuwa na mpango wa maendeleo wa *Mtwara Corridor* ambayo ilihusha Mikoa ile lakini takribani sasa zaidi ya miaka mitatu au minne tupo katika Bunge hili bado mpango wa *Mtwara Corridor* haupo. Je, tunataka kauli ya Serikali mpango wa *Mtwara Corridor* ambao tayari ilikuwa ni dila ya maendeleo ya Mikoa ya Kusini umeishia wapi kwa sasa? Ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Mtwara *Corridor* na mpango mzima wa Mtwara *Corridor* unaendelea kutekelezwa na miradi mahususi ambayo iko katika mpango wa kutekeleza *Mtwara Corridor* ni pamoja na utengenezaji wa miundombinu.

Kwa mfano, hivi sasa kunatengenezwa barabara inayotoka Masasi kwenda Mangaka, Tunduru, mpaka *Mbamba Bay* hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa *Mtwara Corridor* kwa ajili ya kufungua eneo hilo.

Vile vile mpango wa *Mtwara Corridor* ni mpana kwa mfano, uchimbaji wa chuma na Makaa ya Mawe katika eneo la Mchuchuma na Linganga na Mpango wa utengenezaji wa Reli kutoka eneo hilo kuunganisha na Bandari ya Mtwara ni sehem ya *Mtwara Corridor*.

Mimi nadhani hakuna kitu peke yake kinaitwa *Mtwara Corridor* lakini vitendo na miradi hiyo ndiyo inayotekeleza kitu kinaitwa *Mtwara Corridor.*

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Fedha, mheshimiwa Halima James Mdee. Mheshimiwa Waziri haya!

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuongezea majibu mazuri ya Mheshimiwa Wasira naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge na ndugu zangu wote wa Lindi na Mtwara kwamba, katika miaka mitano inayokuja, uwekezaji mkubwa katika nchi hii ambao haujawahi kutokea popote utakuwa Lindi na Mtwara. (*Makofi*)

Kwanza Kampuni ya *Symbion* inajenga *mega watts* 600 na za umeme na wanajenga *transmission line* ya kilo vote 400 kutoka Mtwara mpaka Songea. Makusudi hapo ni umeme wa uhakika kuwa Mikoa ya Kusini na Umeme mwingine kuuzwa Msumbiji na Malawi.

Kwa sasa hivi kiwanda kikubwa kabisa cha *cement* katika Kanda ya Afrika Mashariki kinajengwa Dangote watakuwa wanazalisha sementi za kiasi cha tani milioni moja kwa mwaka. Hakuna sehemu nyingine yoyote.

Kingine kikubwa kabisa ambacho kituchukua labda miaka mia moja kabla hatujawekeza ni kwamba, hivi karibuni makampuni ya mafuta na gas yatafanya uamuzi wa kujenga mtambo wa kipekee kabisa wa kusafirisha gas iliyosindikwa ambayo itakuwa kati ya tani milioni tatu na milioni tano na gharama yake ya uwekezaji ni kati ya Dola za Marekani bilioni kumi na tano na bilioni ishirini.

Kwa hiyo, huo ni uwekezaji ambapo haujawahi kutokea popote Afrika Mashariki, ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Naomba tuendelee na Wizara ya Fedha, swali la Mheshimiwa Halima James Mdee. Kwa niaba yake Mheshimiwa John J. Mnyika, atauliza swali hilo.

Na. 62

**Uuzwaji wa Hisa za Uda**

**MHE. JOHN J. MNYIKA (K.n.y MHE. HALIMA J. MDEE)** aliuliza:-

Kumekua na sintofahamu nyingi juu ya taratibu zilizotumika wakati wa uuzwaji wa Hisa za Serikali zilizokuwa katika Shirika la Usafiri Dar es salaam *(UDA)* na uuzwaji wa Hisa zilizokuwa hazijatengwa bado:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya utata huo?

(b) Kwa sasa ni nani mmiliki wa Shirika la Usafiri Dar es Salaam *(UDA)*?

(c) Je, mgawanyo wa Hisa kwa sasa ni upi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM KIGHOMA MALIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Wazuri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, lenye sehemu a, b na c, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Shirika la Usafiri la Dar es Salaam *UDA* lilianzishwa mwezi Mei mwaka 1974, chini ya Sheria ya Makampuni *Companies Ordinance Cap.* 212, kwa mtaji ulioidhinishwa wa shilingi 1,500,000,000/= *Authorized Share Capital* sawa na hisa 15,000,000,000/= kwa bei ya shilingi 100 kwa kila Hisa. Kati ya Hisa hizo, Hisa Milioni 7,119,697/= ziligawiwa na kulipwa, *paid up capital* na hivyo kubaki na Hisa 7,880,303 ambazo hajigawiwa yaani *unalloted shares*.

Terehe 1 Oktoba, 2000, Serikali iliamua kuipa Halmashauri ya Jiji Hisa 3,631,000 kati ya hisa zake hizo 7,119,000 sawa na asilimia 51 na kubakiza Hisa 3,488,000 sawa na asilimia 49 ya hisa zilozogawiwa na kulipiwa.

Kwa hiyo, Umilikiwa wa Shirika la UDA ni asilimia 51 Halmashauri ya Jiji na asilimia 49 Serikali kupitia msagili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2006, Serikali iliamua kuuza hisa zake asilimia 49 ili kupata mwekezaji mahiri na mwenye uwezo wa kuliboresha shirika hilo la *UDA*. *PSRC* iliagizwa kusimamia zoezi hilo, hata hivyo *PSRC* walishindwa kumpata Mwekezaji aliyekidhi vigezo vilivyowekwa.

Mheshimiwa Spika, Januari 2010 Bodi ya *UDA* iliiarifu Serikali kwamba amepatikana mwekezaji Kampuni ya *Simon Group* ambaye angeuziwa Hisa za Serikali pamona na Hisa 7,800,000 ambazo zilikuwa hazijagawiwa mwaka 1971 wakati *UDA* inaanzishwa kwa maana ya *unlloted shares.*

Baada ya kupokea pendekezo hilo, Serikali iliagiza Bodi ya *UDA* kutoendelea na kusitisha mpango huo wa kuiuzia *Simon Group* Hisa zozote kwa kuwa utaratibu wa kumpata Mwekezaji huyo ulikuwa umekiuka taratibu na misingi ya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo basi:-

(a) Hisa za Serikali ndani ya Shirika la *UDA* hazijauzwa;

(b) Mmiliki wa Shirika la *UDA* ni Halmashauri ya Jijiji na Serikali kupitia Msajili wa Hazina; na

(c) Mgawanyo wa Hisa halali ni kama ulivyosajiliwa kwenye usajili wa makampuni kwa maana ya Halmashauri ya Jiji asilimia 51 na Serikali kupitia Msajili wa Hazina asilimia 49. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, majibu ya Mheshimiwa Waziri yanadhihirisha udhaifu mkubwa wa Serikali, Wizara ya Fedha, Wizara ya Katiba na Wizara ya TAMISEMI.

Nasema hivyo na nitauliza maswali mawili kwa sababu hapa ninayo ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo Waziri Mkuu aliahidi Bunge kwamba Ukaguzi utafanyika, ukaguzi ukafanyika na ripoti ikakamilika tarehe 30 Machi, 2011.

Pamoja na kuwa ripoti kwenye ukurasa wa 13 na kurasa nyingine mbalimbali imebaini kwamba kuna ufisadi kwenye mauzo ya Kampuni ya *UDA*. Mpaka sasa hivi tunavyozungumza na Serikali hapa inakiri kwamba, mauzo hayakuwa halali na umiliki ni wa Jiji pamoja na Serikali Kuu kupitia Msajili wa Hazina.

Lakini mpaka tunavyozungumza hivi sasa umiliki wa kampuni uko mikononi mwa kampuni mwa kampuni ya *Simon Group* na ndiyo ambayo inaendesha biashara hii ya *UDA*. Ningependa kupata kauli ya Serikali kutoka kwa kweli kwa Waziri Mkuu ambaye alikabidhiwa hii ripoti siku zote na imefanywa siri. Kauli ya Serikali. (*Makofi*)

Ni kwa nini baada ya kubaini Ufisadi wote huu, bado Kampuni ya *Simon Group* inaendelea kuendesha Shirika la *UDA* mpaka hivi leo? (*Makofi*)

Pili, ni kwa nini baada ya kubaini Ufisadi wote huu, Mwendesha Mashataka wa Serikali baada ya kesi ya awali kufunguliwa alikwenda kuwasilisha Hati Mahakamani ya kwamba wale watuhumiwa wote wa *UDA* waliopelekwa Mahakamani hawana mashtaka wala hawana kesi ya kujibu. Kwa nini Serikali imewachia watuhumiwa?

Mheshimiwa Spika, mambo haya yasipojibiwa tutaamini kwamba jambo hili linahusu vigogo wa CCM na mnalindana katika ufisadi huu. Naomba majibu ya Serikali. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nilifikiri utaondoa shilingi. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM KIGOMA MALIMA)**: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la *UDA* lina mazingira yenye utata mkubwa na kwa bahati nzuri mazingira yenye utata huo yako pande zote mbili za wamiliki. Kwa upande wa Serikali sisi tuna hisa zetu ambazo kimsingi Bodi ya *UDA* ulipo omba kumumilikisha *Simon Group* aliambiwa *categorically* na barua zipo.

Kwa ushauri wa Mwanasheria Mkuu, kwa ushauri wa CHC ambayo ilikuwa, kwa sababu hii ni kampuni ambayo iko kwenye *specification* na kwa ushauri wa *Treasury Registrar* kwamba huna mamlaka ya kuuza Hisa za Serikali. Lakini kuna upande wa pili wa suala la UDA ambaye ni Jiji lenyewe.

Katika Jiji hilo Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mnyika mumo humu ndani. Kwa hiyo, maana yangu ni kwamba, kuna maamuzi yaliyofanyika Jiji ambayo ndiyo… *UDA* ina Bodi ya watu wanne na katika hao wajumbe wa Bodi mmoja ni Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, sasa ninachosema ni hivi, baada ya kubaini mazingira ya utata yaliyokuwemo pale, *DPP* alirudisha ile kesi na Serikali sasa hivi kupitia Takukuru na Vyombo vingine inaendelea. Ile kesi haijamalizika, ile kesi haijamalizika na kwa hiyo kwa hatua tuliyofikia masuala yako Takukuru na kwenye vyombo vingine ili kupata kina na maelezo ya ziada ya suala hilo.

Mheshimiwa Spika, niseme kwamba mwenye Mamlaka ya kuuza hisa za Serikali ndani ya *UDA* ni Serikali yenyewe. Serikali haijauza Hisa za *UDA*. Kwa hiyo, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Mnyika kwamba, katika jambo hili pande mbili husika, zinakazi ya kufanya katika jambo hili, ninyi ndani ya Jiji mna kazi ya kufanya kwa sababu hizi ni mali zenu ambazo zimeuzwa nje ya utaratibu na Serikali imepeleka suala hili Takukuru na Takukuru inafanyia kazi na tunataka kufikia hatua ya kupata maelekezo yaliyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza lazima niseme, hatua ya kwanza ilikuwa taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambayo ni hii hapa na mimi ninayo na humu nadni Mkaguzi wa

Serikali ametoa maelezo kuhusu mambo moja, mbili, tatu ambayo anasema kwamba ukiukwaji wa mauzo ya hisa za *UDA* ni wa wazi kabisa. Kwa hiyo, katika hilo taasisi nyingine ambazo zinafanyia kazi suala hilo zinaendelea kufanyia kazi.

Mheshimwia Spika, kwa hiyo, kusema kwamba viongozi wakuu wa CCM wanahusika katika hilo, si kweli kwani viongozi wakuu wa CCM hawaendeshi shirika la *UDA*. *(Makofi*

**SPIKA:** Tunaendelea muda umekwisha maswali bado mengi, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, anauliza swali linalofuata.

Na. 63

**Watumishi Waliostaafu Miaka ya Nyuma Hadi, 2004**

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA** aliuliza:-

Wafanyakazi wa Serikali waliostaafu miaka ya nyuma hadi kufikia mwaka 2004, pensheni yao inashughulikiwa na Hazina wakati wafanyakazi waliostaafu baada ya 2004 pensheni zao hushughulikiwa na Mfuko wa Pensheni ya Watumishi wa Umma na watumishi hao waliostaafu miaka ya nyuma hadi mwaka 2004 waliopandishiwa pensheni ya mara ya mwisho mwaka 2009.

(a) Je, ni lini Serikali itapandisha kiwango cha pensheni cha sasa cha shilingi elfu hamsini (50,000) ambacho ni kidogo sana kwa hali ya maisha ya wastaafu hao ambao wanazidi kuishiwa nguvu?

(b) Tume ya Ntukamazina ya kuboresha Maslahi ya Watumishi wa Umma ya Mwaka 2006 ilipendekeza Serikali kuongeza pensheni kila inapoona uchumi unaboreka.

Je, ni nini uhuishaji wa pensheni ya wastaafu litakuwa jambo la kawaida?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa naiba ya Waziri wa Fedha, anomba kujibi swali la Mheshimiwa Deogratius Aloys Ntukamazina Mbunge wa Ngara lenye sehemu(a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya vigezo vinavyotumika kuboresha maslahi ya wafanyakazi wa umma na wastaafu ni ongezeko la mapato ya Serikali yanayotokana na kukua kwa uchumi. Katika kipindi cha muongo mmoja sasa uchumi wa Tanzania umekuwa kwa wastani wa asilimia 6.5. Ukuaji huu wa uchumi umeboresha mapato ya Serikali sambamba na ongezeko la mahitaji ya Jamii na maendeleo kutokana na ongezeko la idadi ya watu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, uzoefu unaonyesha kwamba, kasi ya ongezeko la mahitaji ya Jamii na maendeleo ni kubwa kuliko ongezeko la mapato. Kwa mantiki hii Serikali imekuwa na changamoto ya kuongeza…

**SPIKA:** Niwaombe Waheshimiwa utulivu!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA – (MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU):** Sambamba na ukuaji wa uchumi. Hata hivyo, Serikali itaangalia uwezekano wa kuboresha viwango vya pensheni kwa nia huisha ili wastaafu nao waweze kupata unafuu wa maisha.

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa ongezeko la mahitaji ya Jamii na maendeleo ni kubwa kuliko ongezeko la mapato.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha makusanyo ya mapato yanaongezeka na mapato haya yanayo ongezeka yanasimamiwa vizuri zaidi kuliko ilivyo sasa, ili Serikali iwe na uwezo wa kuongeza mishahara pamoja na pensheni kwa wafanyakazi wote?

Swali la pili, kwa kuwa wastaafu ninao wazungumzia walilitumikia Taifa hili kwa uadirifu na uzalendo mkubwa sana na sasa hawana nguvu ya kuwa na vyanzo vingine vya mapato na kwa kuwa uchumi wetu unakuwa kwa asilimia 7 kama tunavyoambiwa.

Je, Serikali haioni ni wakati muafaka wa kufikiria kukifanya kima cha chini cha pensheni ambacho ni 50,000 kwa sasa kuwa nusu ya kima cha chini cha mshahara ambao tumeambiwa ni kama 260,000 na huenda mwezi Julai ikaongeza? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU):** Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Ntukamazina *concern* yake ya dhati kabisa kabisa ya mafao ya wastaafu. Kwa mantiki hiyo, kama Serikali tupokee ushauri wake na tuahidi kwamba tutafanyia kazi kama nilivyotoa kwenye jibu la msingi kwamba hali hiyo itaangaliwa kufuatana na uwezo wa Serikali kutokana na mapato. Hata hivyo, kwenye swali la kwanza alilosema Serikali sasa ina mipango gani?

Mheshimiwa Spika na Wabunge niseme kwamba Serikali imejipanga na moja ya mkakati tulionao kwanza katika Bunge hili hili ambalo tunaendelea tutaleta mapendekezo ya kupunguza kwa kiwango kikubwa sana misamaha ya kodi.

Tutaomba Wabunge watuunge mkono kwenye hilo, tutafuta baadhi ya misamaha ya kodi ambayo kufutwa kwake hakuta athiri shughuli za maendeleo ya taifa.

Pili, tunategemea pia kuleta mapendekezo ya kubadilisha sheria itakayosaidia kuweza kuwa na usimamizi bora wa fedha za umma, pamoja na makusanyo kwa ujumla ili kuwa na njia nzuri ambayo itatuhakikishia kupunguza ama kumaliza kabisa tatizo la ukwepaji wa kodi.

Mheshimiwa Spika, wiki iliyopita niliongea na mawakala wa forodha nikawambia tutasaidia sana wao kutengeneza mazingira ya ukusanyaji lakini nikawaomba tusaidiane kuhakikisha kwamba tunafichua matatizo yanayohusiana na ukwepaji wa kodi. Kwenye kukwepa kodi, kwenye kutumia vibaya kodi na kwenye kuiba hivi vyote viko sambamba.

Mtu anayegusa mali ya umma hakuna atakayekuwa un-*touchable*. Kwa hiyo, tushirikiane Wabunge pamoja na Watanzania kuhakikisha tunamaliza la ukwepaji lakini

tusaidiane Wabunge kupunguza misamaha ya kodi na tutasimamia ili kuweza ku-*boost* mapato na kuweza kuangalia ushauri huo aliotoa.

**SPIKA:** Muda haupo tunaendelea na swali linalofuata Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleoya ya Makazi, swali la Mheshimiwa Abasi Zuberi Mtemvu na kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Ndungulile, anauliza kwa niaba yake. *(Makofi)*

Na. 64

**Wawekezaji wa Ndani Kushirikishwa Ujenzi wa Mji Mpya wa Kigamboni**

**MHE. DKT. FAUSTINE NDUGULILE (K.n.y. MHE. ABASI ZUBERI MTEMVU)** aliuliza:-

Katika Ujenzi na uendelezaji wa Mji Mpya wa Kigamboni:-

Je, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imewashirikishaje wawekezaji wa ndani kama vile *PPF, NSSF, PSPF, GEPF, NHC* na Makampuni mengine ya Kitanzania yanayojihusisha na *Real Estate?*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO NA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo na Makazi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abasi Zuberi Mtemvu Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2007 Serikali iliandaa mipango kabambe wa kuendeleza Mji mpya wa Kigamboni kwa mujibu wa Sheria ya Mpango Miji namba 8 ya mwaka 2007 pamoja na Sheria ya Utwaji Ardhi, namba 47 ya mwaka 1967. Mpango huu umeainisha maeneo ya matumizi makubwa ya ardhi vikiwemo viwanda, makazi, taasisi ya Elimu, biashara utalii na miundombinu.

Katika mwaka 2013/2014 Serikali imeunda wakala wa uendelezaji wa mji mpya wa Kigamboni yaani *Kigamboni Development Agency* kwa lengo la kusimamia na kuratibu uendelezaji wa mji wa Kigamboni.

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba baadhi ya mashirika ya Serikali kama shirika la Nyumba la Taifa yaani *National Housin*g Corporation *(NHC),* Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF)* yameanza utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi wa mji mpya Kigamboni kwa kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa nyumba za makazi na biashara ndani ya eneo la mradi.

Hadi Mei, 2014, Shirika la Nyumba la Taifa limekamilisha ujenzi wa nyumba 209 za gharama nafuu kwa ajili ya kuuza katika eneo la Kibada, vilevile mradi wa ujenzi wa nyumba 216 umeanza eneo la mwongozo. Aidha Shirika la Nyumba la Taifa, linaendelea kutayarisha mpango kabambe kwa ajili ya uendelezaji la eneo la Uvumba lenye ekari 202 ambalo likikamilika zitajengwa nyumba za makazi 7000 za gharama nafuu, gharama ya kati na za biashara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF)*, imekamilisha nyumba 300 za makazi Kibada na kuendelea na ujenzi wa daraja linaloanzia Kurasini hadi vijibweni.Aidha, *NSSF* kwa kushirikiana na kampuni ya kizalendo iitwayo *Azimio Real Estate,* kwa sasa inaendelea na mradi mkubwa wa ujenzi uitwao Dege ECO *Village* wa nyumba za makazi

na biashara 7500 katika eneo la Mwongozo ambapo kwa awamu ya kwanza, inajenga nyumba 2500.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamilia kujenga mji mpya wa Kigamboni ili kuwa mji wa kisasa ambao utakuwa kitovu cha kuchochea maendeelo ya kiuchumi na kijamii katika Jiji litakaloweza kushindana na miji mingine duniani kwa lengo la kuwa kivutio kwa wawekezaji wa ndani na nje.

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, natoa wito kwamakampuni ya Kitanzania kujitokeza na kuwekeza katika ujenzi wa mji mpya wa Kigamboni kwa sababu, mradi huu unatekelezwa kwa ushirikiano wa sekta binafsi, yaani *Public Private Partnership (PPP)*.

**MHE. DKT. FUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyogeza.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Naibu Waziri, kuna taarifa ambayo ametoa siyo sahihi. Miradi ambayo anaiongelea ni miradi ambayo inafanywa na sekta binafsi na wala haiko katika mpango wa mji mpya wa Kigamboni. Nasema hivyo kwa sababu mradi huu unaendeshwa kwa mujibu wa sheria Namba 8 ya Mipango Miji ya Mwaka 2007, mpaka sasa hivi ile *Master Plan* haijakamilika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, utekelezaji wa mji mpya wa kigamboni haujaanza rasmi. Nilitaka nitoe ufafanuzi ili kauli ambayo ameitoa Mheshimiwa Waziri, ilikuwa kidogo siyo sahihi.

Kwa kuwa Serikali sasa hivi inakabiliwa na uhaba mkubwa wa fedha, kwa nini fedha ndogo ambayo iliyokuwepo, isielekezwe katika miundombinu ili basi sekta binafsi ije iweze kuwekeza, badala ya huu mpango wa sasa hivi ambao Serikali inataka kung'ang'ania kulipa fidia na wao kwenda kuuza kwa wawekezaji?

Pili, kwa kuwa Serikali kupitia katika tangazo la gazeti la mwaka jana ilitwaa Kata tatu za Kisarawe Two, Kimbiji na Pemba Mnazi, bila ridhaa ya Manispaa ya Temeke ambayo kisheria ina mamlaka na mipika ya uendelezaji wa eneo lile. Eneo lililotwaliwa ni asilimia 75 ya manispaa nzima ya Temeke, suala hili tulishaliwasilisha sisi kama Wabunge wa mkoa wa Dar es Salaam.

Je, ni lini Kata hizi zitarejeshwa katika Manispaa ya Temeke?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, naomba kujibu maswali matatu…

**SPIKA:** Naomba ujibu mawili tu.

**NAIBU WAZIRI WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mawili tu, maana nimeulizwa matatu ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Ndugulile, kama ifuatavyo:-

Kwamba miradi inayofanywa haipo katika *Master Plan.* Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumtaarifu Mhehsimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba, mradi wa Kigamboni, *Master Plan* yake ipo tayari na ndiyo inayofuatwa na ndiyo maana haya yote yanafanyika.

Ambacho bado tu ni suala ambalo ni *detailed design*, ambayo ina *stages* zake, ambapo *stage* muhimu ni ile ambayo itashirikisha wananchi katika kuhakikisha kwamba wanaelewa kitu gani kitafanyika sehemu gani, lakini *Master Plan* ipo na ndiyo inayo-*accommodate* haya yote yanayofanyika.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, ni uhaba wa fedha na kwamba kwa nini Serikali isiache mpango wake wa kulipa fidia na badala yake wananchi wale washirikishwe na wawekezaji wengine watakaokuja kwenye maeneo yao. Jambo hili bado tunaendea kulizungumza, kwa sababu halikuwepo katika mpango wa awali na Mheshimiwa Mbunge alikuwa akishiriki katika hatua zote.

Tunaendelea kulizungumza na hata kwenye Kamati tumelizungumza, acha tuendelee nalo tuone namna gani tunaweza tukaangalia hiyo *option* nyingine ambayo Mheshimiwa Mbunge anaizungumza.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na muda umeshapita. Mheshimiwa Riziki Omar Juma, atauliza swali.

Na. 65

**Kujenga Mahabusu za Watoto**

**MHE. RIZIKI OMARY JUMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Mahabusu za watoto ili kuwapunguzia udhalilishaji na manyanyaso wanapochanganywa na watu wazima?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria za kitaifa na za kimaitafa zinaelekeza kuwa watoto wenye mgogoro wa sheria wasihifadhiwe kwenye mahabusu na magereza ya watu wazima bali wawe na mfumo wao wenyewe ambao hapa nchini upo chini ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kutokana na upungufu wa mfumo uliopo nchini, Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto Duniani *(UNICEF)*, imeanza mradi maalum wa kulifanyia utafiti tatizo hilo na kutoa mapendekezo ya kiufundi ili hatimaye uandaliwe mpango wa kupata suluhisho la kudumu.

Mheshimiwa Spika, lengo ni Tanzania kuwa na mfumo mahsusi wa kushughulikia watoto wenye mgogoro wa sheria*(Juvenile Justice System)* kwenye mahakama za watoto, mahabusu za watoto na shule za maadilisho ya watoto watukutu. Kwa sasa nchi nzima ina mahabusu sita za watoto, mahakama moja na shule ya maadilisho ni moja tu. *(Makofi)*

Hata hivyo, Serikali ina mpango wa kujenga Mahabusu za Watoto kila mkoa hapa nchini ambapo kwa kuanzia mikoa ya Mwanza, Dodoma, Arusha na Morogoro, inapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ambalo linakwaza kuwa na kasi ya uekelzaji wa jambo hili ni ufinyu wa Bajeti. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI OMARY JUMA:**Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali maiwli ya nyongeza. Kwanza naombanimshukuru Mheshiwa Waziri kwa majibu yake, lakini naomba nimwulize maswal mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali yetu huwa na mipango mizuri na kuanzisha miradi ambayo mingi huwa tuna-*fail* njiani kuitekeleza. Kituo cha mahabusu ya watoto kule mtwara kimeanza kujengwa miaka kadhaa iliyopita, na hadi sasa hakijamalizika kituo kile kwa kukosa uzio, *furnitures*, mpaka kituo hicho kimefikia kuchakaa sasa, jambo ambalo litapelekea kutumia fedha nyingine zaidi ili kukiboresha.

Je, namuomba Mheshimiwa Waziri anihakikishie na alihakikishie Bunge hili na watu wa Mtwara pamoja na watoto wetu watukutuku ambao tunatarajia kuwapeleka pale, ni lini kituo kile kitamaliziwa kwa haraka sana pamoja na ufinyu huo wa Bajeti ambao tunao, kwa sababu kituo hicho ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa ulimwenguni sasa hivi mahabusu nyingi ziko katikakatika hadhi nzuri, au na magereza yetu, ni lini Serikali yetu itaweka magereza yetu katika kiwango cha kimataifa, yaani *standard*, ili na mahabusu zetu za watoto ambazo tunaziandaa ziweze kuwa katika hali hiyo ili watoto hao watukutu waweze kupata mafunzo mazuri yanayoendana na ulimwengu huu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa kwa kuwa na hamasa za kutosha na nzuri katika jambo hili la manufaa ya watoto wetu.

Mheshimiwa Spika, ujenzi ambao unaendelea kule Mtwara na hasa katika maeneo yaliyobakia ni jambo ambalo ni kipaumbele katika Serikali na katika Bajeti ambayo itasomwa, hasa ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, tuangalie kama hilo linaridhisha au tunaweza tukafanya jambo na kuweza kulitimiza hili, kwa haraka kama Mheshimiwa Mbunge anavyotaka.

Kuhusu lini magereza yetu yatafikia *international standards*, kwa kiasi cha kawaida magereza yote ni *international standard,* pamoja na kuwa bado kuna maeneo ambayo tunahitaji tuyarekebishe.

Kuhusu suala hili hasa la watoto, wale ambao wataenda magerezani, hili linafanyiwa kazi na hata kwenye Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ambayo iitasomwa leo, kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya kuangalia waototo tunawafanyaje wale ambao watalazimika kufika magerezani.

Hata hivyo, kama nilivyosema, watoto waliobakia tutawafanyia mfumo ambao wao na wazazi wao wataridhika nao. Ahsante sana.

**MWONGOZO**

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Ah, mimi nina kazi bado, mwongozo wapi. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge napanda niwatambue wageni waliopo hapa hapa, tuna wageni 11 wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambao ni Wakazi wa Dunda B, *Kigogo Fresh* Pugu Dar es Salaam. Naomba wasimame wageni hawa wote walipo, ahsante sana, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Wizara ya Katiba na Sheria, ambao ni kwanza ni Katibu Mkuu wa Wizara, Ndugu Fanuel Mbonde, yuko wapi sijui na yupo Mheshimiwa Jaji Kiongozi Mstaafu, Amir Manento, ambaye ni Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Mheshimiwa Jaji uko wapi! Nadhani wapo. *(Makofi)*

Yupo Mheshimiwa Jaji Aloyce Mjuruzi, yeye ni Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria. Ahsante sana Mheshimiwa Jaji, karibu.*(Makofi)*

Yuko Mtendaji Mkuu wa Mahakama Ndugu Hussein Katanga, ahsante sana. *(Makofi)*

Yuko Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa George Masaju, ahsante sana.*(Makofi)*

Yuko Mkurugenzi wa Mashitaka, Dkt. Elieza Fereshi, naomba asimame alipo. Ahsante sana na karibu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Majaji wote wapo, Makamishina wa Tume zilizo chini ya Wizara, Msajili Mkuu wa Mahakama na Msajili wa Mahakama ya Rufaa, Makatibu Watendaji wote wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara, kwa sababu leo ni Wizara yao.

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Mahamoud Mgimwa, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kutoka jimboni kwake, Mufindi Kaskazini ambao ni wachimbaji wadogo wadogo wa madini ya dhahabu na wenyewe hawa wasimame sijui mnachimba huko Mufindi, ahsanteni, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 15 wa Mheshimiwa Michael Laizer, ambao ni Kikundi cha Boresha Mifugo kutoka Longido. Hawa nao wako wapi, Boresha Mifugo, ahaa! Ahsanteni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watatu wa Mheshimiwa Martha Mlata ambao ni madiwani wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Singida Wilaya ya Mkalama. Waheshimiwa Madiwani hawa wako wapi! Ahsanteni sana, karibuni. *(Makofi)*

Tunao wageni ambao wamefika kwa ajili ya mafunzo, ambao ni wanafunzi 56 na walimu sita kutoka shule ya msingi ya Montsory Iloleni Ilemela Mwanza. Naomba wasimame wanafunzi hawa, ahsanteni sana, kumbe mmependeza sana, karibuni sana na msome vizuri.*(Makofi)*

Tuna Ndugu Ramadhan Litika na Cleophace Maregesi, kutoka Sengerema. Naomba wasimame, na wageni wengine wote ambao hatukuwataja hapa tunawakaribisha, kuangalia Bunge ni haki yenu pale inapopatikana nafasi.

Matangazo ya kazi, Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Peter Serukamba anaomba niwatangazie wajumbe wa kamati yake kwamba leo saa 7.30 kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Namba 219.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Mheshimiwa Mussa Azan Zungu, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba, kutakuwa na kikao katika ukumbi Namba 227.

Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto, Mheshimiwa *Capt*. John Komba, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba, kutakuwa na kikao katika ukumbi wa Msekwa C.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Luhaga Mpina, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati yake leo saa saba, watakuwa na kikao chao pamoja na Wizara ya Fedha na Uchumi, kikao hicho kitafanyika katika ukumbi mdogo, nafikiri wa Hazina, Namba 125. *(Makofi)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi, naomba Mwongozo wako, kwa mujibu wa Kanuni ya 46(3), nitaisoma. Waziri Mkuu au Waziri mwingine yeyote au Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaweza kutoa majibu ya nyongeza kwa majibu yaliyotolewa na Waziri.

Mheshimiwa Spika, ningeomba mwongozo wako, ili uruhusu Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika jambo hili la *UDA*, kwa sababu maswali ya nyongeza, yote mawili hayajajibiwa kwa ukamilifu. Niliuliza, ni kwa nini *Simon Group,* bado anaendelea kumiliki Shirika la *UDA*, wakati Serikali imejibu kwamba wamiliki ni Jiji na Serikali Kuu. Lakini ni kwa nini *Simon Group* mpaka sasa hivi ninavyozungumza, anaendelea kumiliki na kuendesha Shirika la *UDA*. Hili swali halijajibiwa.

Nikauliza vilevile, ni kwa nini pamoja na makosa kubainika bayana ya rushwa, yameelezwa humu, kigogo mmoja wa CCM anayetajwa humu ni Mheshimiwa Idd Simba, wakati huo wakati anafanya ufisadi unaotajwa kwenye hii ripoti, akiwa Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi wa CCM, sasa…

**SPIKA:** Mheshimiwa hukutakiwa uanze tena kujadili, si ndivyo. Kwanza kipindi cha maswali kimeisha. Kwa hiyo, hiyo hoja yako haifiti hapa. Siyo kipindi cha Maswali, tafuta utaratibu mwingine wa kupata majibu. *(Makofi)*

Katibu tuendelee!

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Matumizi ya Mwaka 2014/2015 Wizara ya Katiba na Sheria**

**SPIKA:** Mheshimiwa mtoa hoja!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria, kwa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, hotuba nitakayoisoma sasa ni muhitasari tu wa hotuba kamili ambayo Waheshimiwa Wabunge wamegawiwa. Ninaomba hotuba yote kama ilivyogawiwa iingie kwenye kumbukumbu za Bunge, yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Spika, ninasimama mbele ya Bunge lako Tukufu kwa mara ya kwanza toka niteuliwe na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kuwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Kwa hiyo, kabla ya kuwasilisha mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Katiba na Sheria, kwa Mwaka 2014/2015. Naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kunipa heshima hii kubwa. *(Makofi)*

Ninapenda kumhakikishie Mheshimiwa Rais na Watanzania wenzangu wote, kwamba nitafanya kazi kwa bidii, uadilifu na kujituma kwa uwezo wangu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sasa uniruhusu nitoe pole zangu za dhati kwako, kufuatia vifo vya Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Dkt. William Augustao Mgimwa, aliyekuwa Mbunge wa Kalenga na Waziri wa Fedha. Mheshimiwa Said Ramadhan Bwanamdogo, aliyekuwa Mbunge wa Chalinze, Mungu awalaze mahali pema peponi. Amin.

Mheshimiwa Spika, ninayo furaha kuwapongeza Wabunge wapya, Mheshimiwa Yusuph Salim Hussen, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Chambani, Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Kalenga na Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Chalinze. Ninawatakia heri na mafanikio katika majukumu yao mapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, natoa pongezi na shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Katavi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake ambayo imetoa mwelekeo wa shughuli za Serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nikupengeze wewe binafsi kwa kuliongoza vyema Bunge hili tukufu na kuweka mazingira yaliyoziwezesha Kamati kutimiza majukumu yake kikamilifu na kutusimamia vizuri.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Katiba Sheria na Utawala, chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mbunge wa Sengerema.

Maoni, ushauri na maelekezo yao yameiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa mafanikio. Tutaendelea kuzingatia ushauri wa Kamati hii wakati tukitekeleza malengo yetu kwa mwaka huu wa fedha na katika siku zijazo kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba na Makamu wake Mheshimiwa Jaji Augustino Ramadhani kwa kuiongoza vyema Tume hiyo. Ninawapongeza pia wajumbe wote kwa kazi kubwa waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, Rasimu ya Katiba waliyoiwasilisha imetuwekea msingi mzuri wa kujadili uandishi wa Katiba mpya, jambo ambalo lina mchango wa pekee katika kujenga mustakabali wa taifa letu. Ni matumaini yangu kwamba tutapata Katiba bora itakayotuongoza kwa miaka mingi ijayo, itakayoimarisha umoja wetu na itakayoleta utangamano wa kitaifa na ustawi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha taasisi zote tunazozitaja kwa urefu katika aya ya nane ya hotuba hii, ambazo kwa pamoja zinatekeleza majukumu ya Wizara kama yalivyoainishwa kwenye tangazo la Serikali nambari 20 la mwaka 2010.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria, kwa kuzingatia dira yake ya upatikanaji haki kwa watu wote na kwa wakati inasimamia na kutekeleza majukumu yafuatayo:- Masuala ya kikatiba na kisheria, shughuli za uendeshaji wa mashauri na utoaji haki, utekelezaji wa haki za binaadamu na utawala bora, shughuli za utafiti, urekebu na uandishi wa sheria, kuishauri na kuiwakilisha Serikali katika masuala ya kisheria ndani na nje ya nchi. Wizara yangu inatekeleza

pia shughuli za usajiri, ufilisi na udhamini; inaratibu taasisi za mafunzo zilizo chini yake na kusimamia maslahi na maendeleo ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nifanye mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2013/14. Katika mwaka huu wa fedha Wizara yangu ilitekeleza malengo mbalimbali iliyojiwekea kwa kuzingatia majukumu ambayo tumeyataja kwa urefu katika aya ya tisa ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nifanye mapitio ya baadhi ya kazi hizo kama ifuatavyo:- kwanza, kuratibu mchakato wa mabadiliko ya Katiba. Katika kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na mfumo imara wa sheria unaozingatia mahitaji ya wakati tulionao, Wizara ya Katiba na Sheria ilisimamia na kuratibu mchakato wa kihistoria wa kuandika Katiba. Tofauti na michakato miwili iliyopita ya mwaka 1965 na 1977, safari hii mchakato wa kuandika Katiba ulihusisha…

**SPIKA:** Waheshimiwa naomba utulivu, wanaotoka waondoke kimya kimya. Na wengine wananendelea huku tunasema hawasikii.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Wananchi wameshiriki moja kwa moja kwa kutoa maoni yao mbele ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba au kwa maandishi. Halikadhalika watashiriki kufanya uamuzi wa mwisho kuhusu Katiba inayopendekezwa kupitia kura ya maoni. Hii ni historia.

Mheshimiwa Spika, Tume hii ilifanya kazi ya kukusanya maoni kutoka kwa mwananchi mmoja mmoja na kupitia Mabaraza ya Katiba ya Wilaya na kitaasisi. Baada ya zoezi hili Tume iliandaa ripoti iliyojumuisha Rasimu ya Katiba. Ripoti hiyo iliwasilishwa kwa Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mnamo tarehe 30 Desemba 2013.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea ripoti ya Tume, Mheshimiwa Rais aliitisha Bunge Maalum ambalo lilianza kazi rasmi kwa kupokea Rasimu ya Katiba iliyowasilishwa tarehe 18 Machi 2014. Hadi sasa Bunge Maalum limejadili sura ya kwanza na sura ya sita kama hatua za awali za uchambuzi wa rasimu hiyo.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine tuliyotekeleza ni kuimasha Haki za Binaadamu na Utawala Bora. Katika kipindi cha mwaka 2013/14 Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora imetoa elimu kwa umma katika masuala ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora. Elimu iliyotolewa ilihusu sheria za ardhi na umiliki wa mali pamoja na aina nyingine za elimu ambapo wananchi 8,529 kutoka katika Kata 69 na Shehia saba walifikiwa. Pamoja na kutoa elimu Tume ilipokea malalamiko 923 ya aina mbalimbali katika kipindi hicho, yakiwemo yale yanayohusu migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, Tume iliandaa Mwongozo wa Utawala Bora wenye lengo la kukuza uelewa katika eneo hili. Jumla ya nakala 25,000 za mwongozo huo zilisambazwa kwa watendaji wa ngazi za Vijiji na Kata ili waweze kuzingatia misingi ya utawala bora na haki za binaadamu wanapotekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, hadhi ya Tanzania kuhusu haki za binaadamu imeendelea kuwa nzuri ndani na nje ya nchi yetu. Ni wajibu wa Wizara yangu kukuza na kuendeleza mafanikio yaliyokwishapatikana. Katika muktadha huo, kipindi cha 2013/14 Wizara iliandaa mpango kazi

wa kitaifa wa Haki za Binaadamu utakaodumu toka 2013/17, uliozinduliwa na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Mohamed Gharib Bilal tarehe 10 Desemba, 2013. Kupitia mpango huu wadau mbalimbali watapata fursa ya kujadili na kutekeleza masuala ya haki za binaadam.

Mheshimiwa Spika, uzinduzi huu ulikwenda sambamba na uzinduzi mwingine wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Haki za Mtoto 2013 – 2017. Mpango huu unabainisha majukumu ya wadau mbalimbali katika kutekeleza haki za mtoto kama zilivyoainishwa katika sheria ya mtoto ya mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaratibu shughuli za Kamati ya Kitaifa ya kuzuia mauaji ya kimbari ambayo imeundwa chini ya itifaki ya Nchi za Maziwa Makuu ya kuzuia mauaji ya kimbari. Kamati hii ina jukumu la kujenga uelewa na kuishauri Serikali juu ya viashiria vinavyoweza kuathiri amani na kusababisha vitendo vya ukatili kwa binaadamu.

Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, pamoja na kutoa elimu kwa umma juu ya masuala ya amani Wizara imewajengea uwezo viongozi wa dini na madhehebu mbalimbali katika mikoa ya Arusha, Mbeya, Mwanza, Mjini Magharibi, Morogoro na Tanga. Katika mikoa hii viongozi wa dini waliunda Kamati za amani zitakazokuwa na jukumu la kuhakikisha amani inadumishwa katika mikoa hiyo na hivyo kuchangia amani ya nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika uendeshaji wa shughuli zake, azma ya Serikali ni kuongeza uwazi katika ngazi zote za utendaji. Kama sehemu ya kufikia lengo hili, Serikali ilijiunga na Mpango wa Kimataifa wa Uendeshaji wa Serikali kwa uwazi, yaani *Open Government Partnership* mwaka 2011. Tamko la Tanzania katika kutekeleza matakwa ya ubia huu ni kuweka mazingira ya upatikanaji wa taarifa kwa lengo la kuongeza uwazi na uwajibikaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali nzuri ya utawala bora na kuzingatiwa kwa haki za binaadamu kwa nchi yetu hivi karibuni kumekuwa na tuhuma nzito kuhusu ukiukwaji wa haki za binaadamu. Tuhuma hizo zilitokana na utekelezaji wa *Operation* Tokomeza ambayo ililenga kuwasaka na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria watu wote waliokuwa wanajihusisha na vitendo vya ujangili katika hifadhi za taifa na mapori tengefu. Kwa kuzingatia uzito wa tuhuma hizi Mheshimiwa Rais ameunda Tume ya Uchunguzi yenye hadidu za rejea zifuatazo:-

Kuchunguza namna *Operation* Tokomeza ilivyofanyika, kuchunguza kama maofisa walioendesha *operation* hiyo walifuata sheria, taratibu na hadidu za rejea walizopewa, kuchunguza endapo maofisa walioendesha *operation* hiyo walivunja sheria, taratibu, na hadidu za rejea zilizotolewa, kuchunguza kama kuna watu waliovunja sheria wakati wa *operation* hiyo na kuona kama hatua walizochukuliwa watu hao au mali zao zilikuwa sahihi. Kushauri hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa mtu yeyote aliyevunja sheria, taratibu na kwenda kinyume na hadidu za rejea zilizokuwapo katika kutekeleza *operation* hiyo. Mwisho kushauri mambo yanayopaswa kuzingatiwa wakati wa kuandaa *operation* nyingine kama hiyo ili mambo yaliyojitokeza katika *operation* hii yasijirudie.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine Wizara yetu imetekeleza ni kusikiliza na kuendeleza mashauri nchini. Kwa kuzingatia dira ya upatikanaji haki kwa watu wote na kwa wakati, Wizara yangu imeongeza kasi ya kuendesha na kusikiliza mashauri yaliyosajiriwa mahakamani. Kasi hiyo imetokana na mikakati mbalimbali na malengo mahususi ambayo Mahakama ya Tanzania imejiwekea, ya kusikiliza mashauri kwa ngazi zote za Mahakama. Utaratibu huu unaweka wastani wa idadi ya mashauri yatakayosikilizwa na kila ngazi ya Mahakama kwa kila mwaka. Katika Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu lengo ni kumaliza mashauri mapya ndani ya

miezi 24, Mahakama ya Hakimu Mkazi katika muda usiozidi miezi 18 na Mahakama ya Mwanzo kumaliza mashauri mapya ndani ya miezi 12.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu umesaidia kupunguza mrundikano wa mashauri kwa kiasi kikubwa ambapo hadi kufikia Desemba 2012 Mahakama ya Tanzania ilikuwa na jumla ya mashauri 114,278 yaliyohusu masuala ya madai, jinai na ardhi.

Katika mwaka 2013 Mahakama ilisajiri mashauri mapya ya aina hiyo 168,068 na kufanya idadi ya mashauri yaliyokuwepo kufikia 282,346. Hadi mwezi Desemba 2013 jumla ya mashauri 182,237 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi, sawa na asilimia 65 ya mashauri yote yaliyosajiriwa mahakamani. Mashauri yaliyobaki mahakamani ni 100,190 na tunaonesha katika kiambatisho 'A' ambacho ni sehemu ya hotuba yangu.

Mheshimiwa Spika, mkakati huu umeanza kwa mafanikio ambapo hivi sasa mashauri mengi yanayosajiriwa mahakamani yamekuwa yakimalizika katika kipindi kisichozidi miaka miwili. Wizara yangu itaendelea kubuni njia mbalimbali zitakazosaidia kuondokana na tatizo la mrundikano wa mashauri na ambalo linaathiri utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaratibu na kusimamia utekelezaji wa mpango wa kutenganisha kazi ya upelelezi wa jinai na uendeshaji wa mashitaka. Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana hadi sasa ni pamoja na kupungua kwa tuhuma za wananchi kubambikiziwa kesi na kupungua kwa idadi ya wafungwa na mahabusu magerezani. Kabla ya kuanza kwa mpango huu mwaka 2007 kulikuwa na wafungwa 22,626 na mahabusu 20,210. Tangu wakati huo idadai ya wafungwa na mahabusi imekuwa ikipungua kadiri Wizara inavyoendelea kueneza utekelezaji wa mpango huu katika Mikoa na Wilaya mbalimbali. Katika mwaka wa fedha 2013/14 Idadi ya Wafungwa ilipungua kutoka 16,869 mwezi Juni 2013 hadi wafungwa 15,659 mwezi Machi 2014; na idadi ya mahabusu ilipungua kutoka 17,046 mwezi Juni 2013 na kufikia mahabusu 16,647 mwezi Machi 2014. Kwa ujumla idadi ya mahabusu na wafungwa wote imepungua kutoka 42,832 kwa mwaka 2007 hadi 32,328.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa dawa za kulevya Kurugenzi ya Mashitaka pamoja na Mahakama ya Tanzania zimeanza kutekeleza utaratibu maalum wa kukamilisha usikilizaji wa mashauri 28 ya dawa za kulevya yaliyosajiriwa Mahakama Kuu. Mashauri haya yamepangwa kusikilizwa katika kikao maalum cha Mahakama Kuu kitakachofanyika kuanzia mwezi Juni 2014 ili kuongeza kasi ya usilikilizaji wa mashauri hayo.

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na utekelezaji wa mikakati maalum ya kusikiliza mashauri tisa ya jinai ya wizi wa shilingi 29,800,000,000 zilizokuwa katika Akaunti ya Madeni ya Nje *(External Payments Areas Account – EPA)* iliyokuwa Benki Kuu. Pamoja na mashauri haya hivi sasa Kurugenzi ya mashitaka inaendesha jumla ya mashauri 14 yanayotokana na makosa ya utakatishaji wa fedha kiasi cha Shilingi 56,000,000,000 zilizopatikana kwa njia ya uhalifu; na mashauri mengine 70 ya kukutwa na nyara za Serikali zenye thamani ya Shilingi 45,000,000,000 kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa mashauri yanayohusu rushwa, hadi mwezi Aprili 2014 kulikuwa na jumla ya majalada 404 ya uchunguzi wa makosa mbalimbali ya rushwa yaliyowasilishwa katika Kurugenzi ya Mashitaka kutoka TAKUKURU. Kati ya hayo majalada 202 yaliandaliwa hati za mashitaka, 103 yalirudishwa TAKUKURU kwa ajili ya uchunguzi zaidi na majalada 98 yanaendelea kufanyiwa uchambuzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/14, Wizara ikishirikiana na taasisi mbalimbali iliongeza jitihada zake za kukabiliana na vitendo viovu wanavyofanyiwa watu

wenye ulemavu wa ngozi. Jitihada hizi zimechangia kiasi kikubwa kupungua kwa idadi ya matukio ya aina hii. Hata hivyo, ni masikitiko yetu kwamba juzi tu tarehe 12 Mei mwanamke mmoja mwenye ulemavu wa ngozi aliuawa kikatili na kukatwakatwa viungo vyake. Wizara inatoa pole, lakini tunaahidi kushirikiana na taasisi nyingine kwamba tutaongeza juhudi za kukabiliana na matukio haya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mashauri ya ukiukwaji wa haki za binaadamu, Wizara yangu iliendesha mashauri sita kwenye Mahakama ya Afrika ya Haki za Binaadamu na Haki za watu iliyopo Arusha. Mashauri haya yanajumuisha mashauri manne mapya ambayo bado yanaendelea, na mashauri mawili ambayo yametupiliwa mbali kutokana na waombaji kutotimiza matakwa ya sheria.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha jumla ya mashauri 750 yalisajiriwa mahakamani ambapo Serikali ilishitaki au kushitakiwa au kufunguliwa mashauri ya Katiba. Kati ya hayo mashauri yaliyosikilizwa na kutolewa uamuzi ni 89. Serikali ilishinda mashauri 77 yenye thamani ya shilingi trilioni 2.2 na kuokoa kiasi hicho cha fedha. Serikali ilishindwa mashauri 12 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 25.9.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali za kupambana na vitendo vya uhalifu bado kumekuwepo na matukio ambayo baadhi ya watu wamejipatia mali kinyume cha Sheria. Kwa kutambua hilo, Wizara yangu imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya kukiimarisha kitengo cha utaifishaji na urejeshaji wa mali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu kinachojulikana kama *Assets Recovery and Forfeiture Section.*

Kati ya Julai 2013 na Machi 2014, Mahakama iliamuru kurejeshwa serikalini jumla ya mali na fedha zinazofikia thamani ya zaidi ya shilingi milioni 233 baada ya watuhumiwa kutiwa hatiani.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha utoaji wa huduma za kisheria ni kazi nyingine ambayo Wizara yangu imetekeleza. Wizara imeboresha mazingira ya upatikanaji haki kwa wananchi, ikitambua kwamba uwakilishi mbele ya vyombo vya sheria ni haki ya msingi. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014 Wizara iliandaa Rasimu ya Waraka wa kutunga Sheria ya huduma ya Msaada wa Kisheria ili kuwapa wananchi fursa ya kupata msaada wa kisheria.

Mheshimiwa Spika, wakati utaratibu wa kutunga sheria hii ukiwa unaendelea Wizara imeanzishwa Sekretarieti ya Msaada wa Kisheria ili kuratibu utoaji wa msaada huo kwa wananchi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/2014 jumla ya wananchi 12,809 walipata huduma ya msaada wa kisheria kupitia Sekretarieti hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine tuliyoifanya ni kuhakiki na kushiriki majadiliano ya mikataba mbalimbali. Wizara yangu imetoa ushauri wa kisheria kwa Serikali unaozingatia ubora na weledi na pia imeendelea kushiriki katika majadilano mbalimbali ya mikataba ya kibiashara, mikutano ya kitaifa, kikanda na kimataifa kwa manufaa ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ili kulinda maslahi ya nchi katika mikataba Serikali imefanya mabadiliko ya sheria ya ununuzi yaani *Public Procurement Act* ya 2011. Pamoja na mambo mengine sheria hii inazitaka Wizara, tasisi na idara za Serikali kupata ushauri wa kisheria kutoka Ofisi ya Mwanashieria Mkuu wa Serikali, kabla ya kufunga Mkataba wowote wenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 50. Mabadiliko haya yamechangia kuongezeka kwa Mikataba inayowasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kuhakikiwa, kutoka Mikataba 120 mwaka 2013 hadi 375 kufikia Machi, 2014. Hali hii imeepusha Serikali na Mikataba isiyo na Maslahi kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Uandishi wa Sheria na Hati za Serikali. Katika mwaka 2013/2014 Wizara yangu iliandaa jumla ya Miswada 11 iliyojadiliwa na kupitishwa na Bunge lako Tukufu kuwa Sheria. Miswada hiyo tunaitaja katika aya ya 38 kwa urefu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine tulilolifanyia kazi ni kufanya utafiti na tafsiri ya Sheria. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2013/204, Tume ya Kurekebisha ilifanya mapitio na utafiti wa mifumo ya sheria mbalimbali. Utafiti wa kwanza ulihusu mfumo wa sheria wa utatuzi wa migogoro ya ardhi. Utafiti wa pili ulihusu mfumo wa sheria unaosimamia huduma ya hifadhi ya jamii kwa Wazee. Mwisho Tume ilifanya utafiti kuhusu sheria zinazolinda watumiaji wa bidhaa. Tafiti hizi zimelenga kubaini upunguru uliopo ili hatua muafaka ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, ufanisi katika utekelezaji wa sheria unategemea sana uelewa wa wananchi kuhusu Sheria hizo. Kwa kutambua hilo, Wizara imetafsiri sheria saba kutoka Kiingereza kwenda lugha ya Kiswhaili. Wizara itaendelea kutafsiri sheria nyingi zaidi kwa kuzingatia mahitaji ya jamii na uwezo uliopo. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge wafanye rejea kwa kiambatisho "B" ambacho ni sehemu ya hotuba ya Wizara yangu.

Mheshimwia Spika, katika kuimarisha Ustawi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashairki, Wizara yangu kwa kushirikiana na nchi wanachama, imeeendelea kufanya mapitio ya sheria zinazosimamamia haki za ubunifu na hakimiliki. Lengo ni kuhakikisha kuwa sheria za nchi wanachama zinauwiana na sheria za Jumuiya hiyo kama ambavyo nchi hizi zimekubaliana katika kutekeleza itifaki ya soko la pamoja. Kazi nyingine tuliyoifaya ni kuimarisha shughuli za usaliji, ufilisi na udhamini.

Mheshimwia Spika, usajili wa matukio muhimu ya binadamu yaani vizazi, vifo, ndoa, talaka na watoto wa kuasili una lenga kulinda na kuhifadhi haki za binadamu na haki za uraia. Aidha usajili huu unaiwezesha Serikali kupata takwimu sahihi kwa ajili ya Mipango mbalimbali.

Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014 Wizara imeboresha mfumo wa usajili wa vizazi kwa kusogeza huduma hii hadi ngazi za chini kama vile Kata na Vituo vya Tiba. Maboresho haya yamefanyika kupitia Mpango wa Usajili wa Vizazi kwa Watoto Wenye Umri wa Chini ya Miaka Mitano, mpango uliozinduliwa rasmi mkoani Mbeya mwezi Julai, 2013.

Mheshimwia Spika, utekelezaji wa mpango huu, umeongeza idadi ya watoto wa umri chini ya miaka mitano waliopatiwa vyeti vya kuzaliwa kutoka watoto 37,090 kabla ya mpango huu kuanza, hadi 169,477 Machi, 2014. Hii ni sawa na ongezeko la asimilia 31.4 la watoto wote wa umri wa chini ya miaka mitano katika Mkoa huo wa Mbeya.

Mheshimiwa Spika, mbali na usajili huo mkoani Mbeya, Wizara imefanya usajili wa kawaida katika sehemu nyingine za Tanzania Bara kwa jumla ya vizazi 493,817, ndoa 14,031, talaka 53, vifo 34,460 na watoto wa kuasili 30. Halikadhalika jumla ya hati 182 za wadhamini wa vyama vya siasa, makanisa, misikiti na mali za vikundi vya kijamii vilisajiliwa. Tunaomba muangalie kiambatisho "C" cha hotuba yangu.

Mheshimwia Spika, katika kuimarisha taasisi za mafunzo ya sheria, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara imeiimarisha, Taasisi ya Mafunzo ya Wanasheria kwa Mafunzo ya Wanasheria kwa Vitendo na Chuo cha Uongozi wa Mahakama. Hadi kufikia Machi, 2014, jumla ya wanafunzi, 293, walihitimu mafunzo ya uanasheria kwa vitendo na kustahili kusajiliwa kuwa Mawakili, ikliinganishwa na mwaka 2012/2013 ambapo wahitimu walikuwa 272. Kwa upande wa Chuo cha Uongozi wa Mahakama jumla ya wanafunzi 896 walihitimu katika ngazi ya cheti na stashahda. Vile vile Wizara imeanzisha Tawi la Chuo cha Uongozi wa Mahakama katika Jiji la

Mwanza na kudahili wanafunzi 95 kwa mara ya kwanza mwaka 2013/2014. Jitihada hizi zitaongeza Idadi ya wataalam wenye sifa za kuajiriwa katika fani mbalimbali za sheria.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine tuliyoifanya ni kuboresha miundombinu ya utoaji haki. Ubora wa huduma unaotolewa na taasisi za sheria unategemea ubora wa mazingira na miundombinu ya utoaji haki. Kwa kuzingatia umuhimu huo, katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi 2014 Wizara yangu imefanya mambo yafuatayo:- Imekarabati Masjala kwenye Mahakama ya Rufani, Mahakama Kuu Kanda za Dar es Salaam na Mtwara, imepata washauri elekezi kwa ajili ya kukarabati Mahakama za Mwanzo 10 na kujenga Mahakama za Mwanzo mpya 25. Utaatibu wa kupata Wakandarasi umetengazwa kwenye Magazeti ya tarehe 11 na 12 Mei, 2014.

Mheshimiwa Spika, kazi nyingine iliyofanyika ni kujenga uzio wa Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba, kutenga vyumba vya ofisi za Majaji na Makatibu Muhtasi na kuziba sehemu ya wazi ya paa. Wizara yangu imeboresha Masjala 71 za Mahakama mbalimbali kwa kuzikarabati na kuziwekea mfumo wa kielektroniki wa kutunza kumbukumbu za majalada. Halikadhalika imekamilisha ukarabati wa Mahakama za Mwanzo za Mgandu, na Mwamagembe katika Mkoa wa Singida. Hivi sasa Wizara yangu inakamilisha ujenzi wa bweni la wanafunzi katika Chuo cha Uongozi wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Wizara vile vile imefungua Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mkoa wa Geita na inakamilsha taratibu za kuanza ukarabati wa ofisi katika Mikoa ya Simiyu na Katavi. Wizara yangu vilevile imekamilisha ujenzi wa jingo la Wakala wa Usajii, Ufilisi na Udhamini, imekamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa mfumo mpana wa mawasiliano *(wide area network)* utakaounganisha Makao Makuu ya Ofisi ya Mwanasheiria Mkuu wa Serikali, Kurugenzi ya Mashtaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mkoa wa Dar es Salaam, ili kuboresha huduma zetu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu kuhusu mradi wa *E-Justice* utakaorahisisha uendeshaji wa mashauri ya jinai umekamilika. Mradi huu utaunganisha Mahakama, Magereza na Ofisi za Mikoa za Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa njia ya mtandao ili kuleta tija na ufanisi katika kazi zetu.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania, imejiimarisha, katika matumizi ya TEHAMA kwa kuanzisha mfumo endelevu wa upatikanaji wa takwimu mbalimbali. Mfumo huo umeanza kufanya kazi, katika Mahakjama ya Rufani, Mahakama Kuu katika Divisheni za Biashara, Kazi na Ardhi na Mahakama Kuu Kanda ya Dar es salaam. Itakapofika Desemba 2014, Mahakama nyingi nchini zitakuwa zinatumia TEHAMA katika ukusanyaji na utunzaji wa Takwimu.

Mheshimwia Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini umeanzisha Utaratibu wa kupokea taarifa za usajili wa vizazi kupitia simu za mkononi, mara tu mototo anaposajiliwa kwenye Kata au Kituo cha Tiba. Hivi sasa utaratibu huu, unafanyika Mkoani Mbeya kwa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano. Sambamba na hilo mwananchi yeyote nchini anaweza akapata taarifa za huduma za huduma za RITA kupitia simu za mkoani kwa kutuma neno RITA. Kwenda Nambari 15584 na Tovuti ya Wakala www.rita.go.tz.

Mheshimiwa Spika, vilevile Wizara yetu inatambua umuhimu wa elimu kwa umma. Wizara inatambua kuwa wananchi wana nafasi muhimu katika kuimarisha utawala wa sharia, misingi ya haki za binadamu na utawala bora. Kwa kuzingatia hilo Wizara imetoa elimu kwa umma kwa njia mbalimbali, zikiwemo redio na runinga. Pia Wizara ilishiriki maonesho ambapo

jumla ya vitabu 25,000 na vipeperushi 2,800 kuhusu haki za binadamu na misingi ya utawala bora vilisambazwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatekeleza *program* na miradi mbali mbali ya kuboresha sekta ya Sheria. Utekelezaji huu unalenga kuimarisha mifumo ya utoaji haki na kukuza uwezo wa taasisi za sheria katika kutoa huduma bora. Hadi sasa *program* hii imewezesha kutengenanishwa kwa shughuli za upelezi na mashtaka. Kufanya mapitio ya sheria mbalimbali na kuanzishwa kwa taasisi ya mafunzo ya uanasheria kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Mchi, 2014, shughuli nyingine muhimu zilizotekelezwa ni pamoja na kufanya tathmini ya hali ilivyo hivi sasa na kuishauri Serikali, kuimarisha utendaji wa Sekretarieti ya Huduma ya Msaada wa Kisheria, kuratibu wa uanzishwaji wa maeneo ya kuhifadhi watoto waliokinzana na sheria na kuimarisha madawati ya jinsia na watoto katika vituo vya Polisi na Magereza.

Mheshimiwa Spika, maboresho ya sekta ya sheria ni pamoja na mapambano na rushwa. Wizara yangu ni moja ya taasisi zinazotekeleza Mradi wa Kuimarisha Mapambano na Rushwa Tanzania unaojulikana kwa kifupi kama **STAKA**. Chini ya Mradi huu, jumla ya masjala 68 za Mahakama za Mwanzo ziliboreshwa kuwekewa mfumo wa kielektroniki wa kutunza kumbukumbu za majalada. Mfumo huu umerahihisisha upatikanaji wa taarifa za kimahakama na hivyo kuondoa usumbufu na mianya ya rushwa kwa wale wanaotaka kufuatilia taarifa zao.

Mheshimiwa Spika, vile vile kupitia mradi huu, kitengo cha utaifishaji na urejeshaji wa mali zilizopatikana kwa njia ya uhalifu kimeimarishwa kupatiwa vitendea kazi ambavyo vimesamabazwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ofisi ambazo zipo katika Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara yangu ilichukua hatua za kuziimarisha Kamati za Maadili za Mahakama za Mikoa na Wilaya. Tume ya Utumishi wa Mahakama ilifanya ukaguzi wa kamati hizo kwenye ngazi ya Mkoa na Wilaya katika Mikoa ya Iringa, Njombe, na Ruvuma. Katika ukaguzi huo, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilibaini changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa fedha. Wizara imeanza kukabiliana na changamoto hiyo kwa kuzipatia fedha Kamati za Maadili za Mahakama ngazi ya Mikoa na Wilaya, na katika mwaka 2013/2014 jumla ya shilingi 36,000,000/= zilitolewa kwa Wilaya 18 na shilingi 136,500,000/= kwa Wilaya 91.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imewajengea uwezo watumishi waliopo na kuajiri watumishi wapya ili kuleta tija na ufanisi. Katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Machi 2014, Wizara iliajiri Watumishi wapya 541, ilipandisha vyeo watumishi 487 na kuwezesha watumishi 1,081 wa kada mbalimbali kupata mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inazingatia masuala mtambuka katika utekelezaji wa majukumu yake, haya ni kama vile kuingiza masuala ya jinsia katika sera, mipango na uendeshaji, kuzingatia mahitaji ya watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI na masuala yanayohusu maadili. Na katika kuajiri, kupandisha vyeo na kufanya mafunzo, tumezingatia kwa kikamilifu uwiano wa jinsia na tunayataja haya katika hotuba yetu na tunaomba Waheshimiwa Wabunge waangalie kiambtisho "G" cha hotuba yangu.

Mheshimwia Spika, kuhusu masuala ya UKIMWI, watumishi wa Wizara walipata mafunzo ya jinsi ya kujikinga na maambukizi ya Virusi vya UKIMWI, kupitia kamati za UKIMWI zilizopo katika Wizara na Taasisi. Wizara inawahudumia watumishi wanaoishi na Virusi vya UKIMWI kwa Matibabu na lishe.

Mheshimiwa Spika, mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2013/2014: Katika mwaka huu Wizara yangu ilipanga kukusanya jumla ya shilingi 5,250,454,700/= kama maduhuli ya Serikali kutoka katika vyanzo mbalimbali vya mapato. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014, Wizara ilikusanya 6,007,714,285/= sawa na asilimia 114 ya lengo. Tofauti hii inatoka na ongezeko la makusanyo ya ada za wanafunzi wa Tasisi ya Mafunzo ya Uanasheria kwa Vitendo na maduhuli ya Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 260,656,733,000,/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 205,397,547,000/= ni matumizi ya kawaida, na shilingi 55,259,186,000/= ni fedha za miradi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida shilingi 42,537,999,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 162,860,448,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kati ya fedha za matumizi ya maendeleo, shlingi 44,000,000,000/= ni fedha za ndani na shilingi 11,259,186,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kufikia Machi, 2014 Wizara imepokea kiasi cha shilingi 120,363,406,912/= sawa na asilimia 46 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi 110,763,667,097/= ni fedha za Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 54. Kati ya fedha hizi za matumizi ya kawaida, shilingi 36,312,510,030/= ni mishahara ya watumishi na shilingi 74,451,157,067/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo zilizopokelewa ni shilingi 9,599,379,815/= sawa na asilimia 17 ya fedha zote za maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 5,107,500,000/= ni fedha za ndani na shilingi 4,441,879,817/= ni fedha za nje. Ufafanuzi wa taarifa hizi unapatikana katika kiambatisho "D".

Mheshimiiwa Spika, changamoto zilizopo zinatokana pia na baadhi ya mafanikio tuliyoyaprta. Zipo changamoto mbalimbali, zililizojitokeza wakati wa kutekeleza majukumu yake, changamoto hizo ni pamoja na kuwepo kwa bajeti ndogo ikilinganishwa na mahitaji, mapokezi ya fedha zilizoidhinishwa hayatabiriki na hivyo kuifanya Wizara na taasisi zake kushindwa kutekeleza mipango kazi yao kwa namna endelevu, Wizara kutotengewa fedha za maendeleo za ndani hali ambayo inazilazimu baadhi ya taasisi za Wizara kutumia pesa nyingi kwa ajili ya kulipia kodi ya pango na hivyo kuathiri utekelezaji wa majukumu ya utoaji haki na mazingira ya kazi, wanafunzi wa taasisi za Uanasheria kwa Vitendo kutopatiwa kutoka Bodi ya Mikopo na hivyo kuathiri hali ya utulivu masomoni, uhaba wa vitendea kazi na rasilimali watu, ongezeko la matukio ya makosa ya jinai pamoja na mbinu mpya za kutenda uhalifu na kuwepo kwa mazingira yanayoweza kuhatariha usalama wa Majaji, Mahakimu, Mawakili na watendaji wengine wa Serikali na hivyo kuathiri utendaji wao wa kazi na kuongezeka kwa ujumla kwa mmomonyoko wa maadili miongoni mwa baadhi ya watendaji wanaoshughulika na utoaji haki katika sekta ya sheria.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2014/2015: Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara yangu imepanga kuimarisha utekelezaji wa malengo mkakati iliojiwekea ili kutoa haki kwa watu wote na kwa wakati. Ili kufikia azma hiyo, Wizara itasimamia na kufuatilia utekelezaji wa majukumu yake katika maeneo ya kipaumbele yafuatayo: -

Ufuatiliaji wa Katiba ya nchi na sheria, kufuatilia mchakato wa kutunga Katiba, kufanya maandalizi ya mapitio na marekebisho ya sheria zitakazoguswa na mabadiliko ya katiba, kutoa elimu ya Katiba kwa wananchi kuhusu taratibu za kimahakama zinazopaswa kuzingatiwa katika kudai haki, kushughulikia masuala ya urekebu wa sheria, kushughulikia uandishi wa miswada ya sheria, sera na hati za Serikali, kuhakiki rasimu za mikataba ya Serikali na kushiriki katika majadiliano yanayohusu mikataba.

Mheshimiwa Spika, halikadhilika tutasimamia na kufuatilia utoaji haki kwa kuendelea kusimamia shughuli za uendeshaji na usikilizaji wa mashauri, kuziimarisha Kamati za Maadili za

Mahakama katika ngazi za Mikoa na Wilaya kwa kuzipa mafunzo na kuzifanyia ukaguzi. Kazi hii itaanzia katika Mikoa ya Dodoma, Katavi, Mara, Mwanza, Rukwa, Shinyanga, Singida na Tabora. Kuimarisha utekelezaji wa mpango wa kutenganisha shughuli za upelelezi na mashitaka.

Mheshimiwa Spika, katika kulinda na kuhifadhi hazi za binadamu na utawala wa sheria, kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa na kuendelezwa, kuwasilisha Bungeni miswada mbalimbali inayohusu upatikanaji wa msaada wa kisheria, kulinda mashahidi na waathirika wa vitendo vya jinai, kulinda watu wanaotoa taarifa kwa siri kuhusu vitendo vya uhalifu au ukiukwaji wa maadili.

Mheshimiwa Spika, tutafanya pia marekebisho ya Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, Sheria ya Ufilisi halikadhalika, kueneza mfumo wa usajili wa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano katika Mikoa ya Simiyu na Shinyanga, kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa taasisi za mafunzo za Wizara. Tutaendelea kuimarisha miundombinu ya utoaji haki kwa kujenga nyumba za Majaji, majengo ya Mahakama na majengo ya ofisi, kuimarisha huduma za masijala, kufunga mfumo wa kielektroniki wa *e-justice* kwa ajili ya usikilizaji wa mashauri, kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa taasisi za mafunzo za Wizara.

Mheshimiwa Spika, tutaboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini kupitia Mpango wa Matokeo Makubwa Sasa. Katika kazi hizi tutapunguza mrundikano wa mashauri katika Mahakama zote, kuharakisha ufunguaji na uendeshaji wa mashauri, kufanya mapitio na utafiti wa sheria zinazohusu uwekezaji na biashara na kuhakiki mikataba mapema na kwa weledi.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa masuala mtambuka tutaimarisha kamati za amani za Mikoa kupitia kamati ya kitaifa ya kuzuia mauaji ya kimbari katika Mikoa na Wilaya. Vilevile tutatoa elimu na hamasa kwa wananchi, Waheshimiwa Wabunge, wanahabari na wanafunzi wa vyuo vikuu ili kujenga utamaduni wa amani na utangamano kwa kila Mtanzania. Kuanda na kuratibu awamu ya pili ya shughuli za maboresho ya sekta ya sheria, kuimarisha usimamizi wa maadili na uwajibikaji wa watumishi kazini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zilizopo, Wizara yangu imejizatiti kufanikisha malengo iliyojiwekea katika kutekeleza mpango na bajeti kwa kipindi cha 2014/15.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru wadau wetu wa maendeleo kwa ushirikiano wao na tunawataja kikamilifu katika aya ya 65. Napenda kutoa shukrani za pekee kwa wadau mbalimbali wa sekta ya sheria kwa ushirikiano na ushauri wao uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara yetu kwa mwaka 2013/14 kama yalivyobainishwa katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Mohamed Chande Othman, Jaji Mkuu, Mheshimiwa Jaji Fredrick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mheshimiwa Faki Jundu, Jaji Kiongozi, Ndg. Fanueli Mbonde, Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Ndg. Hussein Katanga, Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania na Ndg. George Masaju, Naibu Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wakuu wote wa taasisi zilizopo chini ya Wizara yangu kama tunavyowataja katika aya ya 67 ya hotuba hii. Napenda vilevile kuwashukuru wafanyakazi wote na wa ngazi zote kwa ushirikiano na kwa kujituma katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, sekta ya sheria ina umuhimu wa pekee katika kuchangia maendeleo ya nchi kiuchumi, kisiasa na kijamii. Wizara yangu ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa inakuza na kuimarisha amani, utawala wa sheria na haki za raia. Kwa kuzingatia dhana hii napenda kutoa wito kwa wananchi wote pamoja na Waheshimiwa Wabunge kuhakikisha kuwa dhamira ya Serikali ya kulinda amani, utulivu na haki za binadamu inazingatiwa na kupewa kipaumbele kwa manufaa ya kizazi kijacho na cha sasa.

Mheshimiwa Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa katika mwaka wa fedha 2014/2015 Wizara yangu inaomba kuidhinishiwa kiasi cha Tsh.231,372,948,000/= kwa ajili ya taasisi, idara na vitengo vyake. Kati ya fedha hizo Tsh.1,346,144,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na Tsh. 48,804,234,000/= ni mishahara. Fedha za maendeleo ni Tsh.48,562,570,000/= kati ya hizo shilingi bilioni 44 ni fedha za ndani na Tsh. 4, 562,570,000/= ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa matumizi ya bajeti kwa Mafungu Saba ya Wizara ni kama ifuatavyo:- Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama, matumizi ya mishahara ni Tsh. 208,764,000/=

Mheshimiwa Spika, tumesambaza karatasi ya marekebisho na ninaomba kwa matumizi mengineyo maombi yetu yasomeke Tsh. 400,271,716,000/=, matumizi ya maendeleo ni Tsh. 00/= Jumla kwa kuzingatia mabadiliko haya ni Tsh. 4, 080,480,000/=

Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, matumizi ya mishahara ni Tsh. 2,426,998,000/=. Matumizi mengineyo Tsh. 8,332,865,000/=, matumizi ya maendeleo kwa ndani ni Tsh. 00/=, matumizi ya maendeleo kwa fedha za nje ni Tsh. 457,149,000/= jumla ni Tsh. 11, 216,912,000/=

Fungu 35 – Kurugenzi ya Mashitaka, matumizi ya mishahara ni Tsh. 5,215,201,000/=. Matumizi mengineyo Tsh. 16,460,826,000/=, matumizi ya maendeleo kwa ndani ni Tsh. 00/=, matumizi ya maendeleo kwa fedha za nje ni Tsh. 468,299,000/= jumla ni Tsh. 22, 144,326,000/=

Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama, matumizi ya mishahara ni Tsh. 35,004,061,000/=. Matumizi mengineyo na hapa kuna mabadiliko kutokana na marekebisho yaliyofanywa, Tsh. 88,260,284,000/=.

Mheshimiwa Spika, matumizi ya maendeleo kwa ndani ni Tsh. 40,000,000,000/=, matumizi ya maendeleo kwa fedha za nje ni Tsh. 1,687,748,000/=. Mheshimiwa Spika, jumla sasa itakuwa ni Tsh. 164, 948,090,000/=

Mheshimiwa Spika, Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria, matumizi ya mishahara ni Tsh. 3,154,642,000/=. Matumizi mengineyo Tsh. 8,028,651,000/=, matumizi ya maendeleo kwa fedha za ndani ni Tsh. 4,000,000,000/=, matumizi ya maendeleo kwa fedha za nje ni Tsh.1,048,621,000/=. Jumla ni Tsh. 16, 231,914,000/=.

Mheshimiwa Spika, Fungu 55 – Tume ya Haki za BInadamu na Utawala Bora, matumizi ya mishahara ni Tsh. 2,041,593,000/=. Matumizi mengineyo Tsh. 4,795,802,000/=, matumizi ya maendeleo kwa ndani ni Tsh. 00/=, matumizi ya maendeleo kwa fedha za nje ni Tsh. 900,753,000/=. Jumla ni Tsh. 7, 738,148,000/=

Fungu 49 – Tume ya Kurekebisha Sheria, matumizi ya mishahara ni Tsh. 717,075,000/=

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ni Fungu 59 na siyo 49.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ni Fungu 59. Asante.

Mheshimiwa Spika, matumizi mengineyo Tsh. 3,856,000,000/=, matumizi ya maendeleo kwa ndani ni Tsh. 00/=, matumizi ya maendeleo kwa fedha za nje ni Tsh. 00/=. Jumla ni Tsh. 4, 573,075,000/=.

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya maduhuli kwa mwaka 2014/15 Wizara yangu inatarajia kukusanya kiasi cha Tsh. 8,577,362,121 kama maduhuli ya Serikali kama ifuatavyo:- Fungu 12 – Tume ya Utumishi wa Mahakama, Tsh. 0/=, Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Tsh. 4,502,000/=, Fungu 35 – Kurugenzi ya Mashitaka, Tsh. 17,103,000/=, Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama, Tsh. 4,115,843,000/=, Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria, Tsh. 4,434,270,121,000/=, Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tsh. 5,644,000/=, Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria, Tsh. 00/=. Jumla ni Tsh. 8,557,362,121/=

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati iliyoshughulikia Wizara hii au Makamu wake, Mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Ngeleja. *(Makofi)*

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 99 (5),(9) na 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, taarifa yangu hii ni muhtasari wa taarifa kamili ya Kamati ambayo naomba *Hansard* irekodi kwa ukamilifu wake kama ilivyo.Wizara ya Katiba na Sheria inahusisha mafungu saba kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameyaainisha.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 3 Mei, 2014 Kamati yangu ilichambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria akishirikiana na Naibu Waziri Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki (Mb), pamoja na Watendaji wa Wizara. Katika maelezo yake Waziri aliieleza Kamati kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2013/14. Itakumbukwa kwamba wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamati yangu ilitoa maoni na ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa kiasi kikubwa ushauri huo umezingatiwa na ushauri mwingine upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali kufuatilia kwa makini utendaji kazi wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba bila kuathiri uhuru wa Tume na kuiwezesha nchi kufikia lengo la kupata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara ilikuwa karibu na Tume katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji bila kuingilia uhuru wake. Kutokana na jitihada hizo Tume ilikamilisha maandalizi ya Rasimu ya Katiba pamoja na taarifa nyinginezo muhimu, na kuikabidhi Rasimu hiyo Serikalini. Aidha, kama sote tunavyojua, Rasimu ya Katiba imeishawasilishwa katika Bunge Maalum la Kutunga Katiba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bajeti ya Bunge la Katiba kufahamika na kuletwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa: Kamati ilielezwa kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83, masuala yote ya Bunge la Katiba yapo chini ya Bunge Maalum la Katiba ambapo fedha kwa ajili ya Bunge hili zinatolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iimarishe Kitengo cha Mikataba kwa kuwajengea uwezo wa kuwapatia rasilimali watu na fedha: Kamati yangu ilielezwa kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inao mpango wa kuwasomesha Mawakili waliopo na watakaoajiriwa ili kuwajengea uwezo kitaaluma katika kushughulikia masuala ya mikataba na masuala mengine ya kisheria. Kwa sasa eneo hili la mikataba kwa muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikal limepewa hadhi ya kuwa divisheni na kuongozwa na afisa mwenye cheo cha Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa *(UNDP)* chini ya Mradi wa *UNDP Support Programme* wamekuwa wakifadhili programu ya mafunzo ya muda mfupi ili kuwawezesha Mawakili wa Serikali na wadau wengine wa Sekta nyingine kuwajengea uwezo wa kuchambua, kujadili, kuandika, kuhakikisha na kusimamia mikataba.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha Uandishi wa Miswada kiweke utaratibu wa kundaa Miswada kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili ili hatimaye inapokuwa imepitishwa na Bunge, kuwepo na sheria moja yenye lugha ya Kiingereza na Kiswahili na hii itawasaida wananchi wengi kunufaika na sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba Serikali imeendelea kuzingatia maelekezo ya Kamati na kuyafanyia kazi kila mara. Kwa hivi sasa Miswada ya Sheria inayowasilishwa Bungeni imekuwa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Kwa mfano, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na Sheria ya Vyama vya Ushirikia.

Mheshimiwa Spika, Serikali iiwezeshe kibajeti Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuajiri watumishi wa kutosha. Kamati ilielezwa kuwa Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitengewa bajeti ya Shilingi bilioni 1.86 kwa lengo la kuajiri watumishi wapya 489. Hata hivyo, kibali cha kuajiri watumishi hao wapya hakikutolewa kutokana na sababu za kibajeti zilizojitokeza. Hivyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imewasilisha tena maombi ya ajira mpya kwa watumishi 489 kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2013/2014 ni kidogo. Hivyo Serikali inashauriwa kuitengea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali fedha nyingi za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mfano, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeomba jumla ya Shilingi bilioni 50 ambazo ni fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ofisi za makao makuu na ofisi mpya za mikoani ili kuondokana na tatizo la

kupanga katika majengo wasiyoyamiliki na wakati mwingine kwa gharama kubwa. Hata hivyo fedha zilizotengwa kwa taarifa zilizopo siyo zaidi ya shillingi 457,149,000/= ambazo ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, Kurugenzi ya Mashtaka iongezewe uwezo kifedha ili iweze kutekeleza vyema mpango wake wa kutenganisha suala la upelelezi na uendeshaji wa mashtaka. Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa Fedha 2013/2014 Serikali iliongeza bajeti ya Divisheni ya Mashtaka kutoka shilingi 10.8 hadi shilingi 20.8 kwa ajili ya kutekeleza malengo yaliyopangwa. Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 divisheni ya mashitaka imetengewa jumla ya shilingi bilioni 22.1

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wizara kununua vifaa vya kisasa kama kompyuta na samani za ndani kwa Mahakama zote nchini. Kamati yangu ilielezwa kuwa Wizara kupitia Mahakama ya Tanzania itahakikisha kuwa Mahakama zake zinapata vitendea kazi muhimu ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kulingana na uwezo wa Serikali kifedha uliopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itoe fedha za maendeleo zilizotengwa kwa Mahakama ili kuwezesha miradi ya ujenzi wa Mahakama kuendelea kama ilivyopangwa: Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi Machi, 2014 Mahakama ilikuwa imepokea fedha kiasi cha shilingi bilioni 5.5 kati shilingi bilioni 42.7 ikiwa ni bajeti iliyoidhinishwa na Bunge lako tukufu.

Mahakama ibuni njia bora zaidi za upimaji wa utendaji kazi wa Mahakimu na Majaji ili kuongeza ufanisi na utendaji wa Mahakama kwenye kazi zake. Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Mahakama imeshaweka utaratibu bora, shirikishi na wa uwazi katika upimaji wa utendaji kazi wa Mahakimu na Majaji kwa kuwa na viwango na idadi maalum vya uondoshaji wa mashauri kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Serikali iimarishe Mfuko wa Mahakama kibajeti ili mfuko huo uweze kukidhi mahitaji ya Mahakama. Kamati ilielezwa kuwa Mfuko wa Mahakama umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Mahakama Sura ya 237. Kwa mwaka 2013/2014 mfuko huu umetengewa Shilingi bilioni 129.69. Hata hivyo, mfuko huu umekuwa ukiidhinishiwa fedha kidogo na pia kutolewa kwa kuchelewa na hivyo kutokidhi mahitaji yake ya msingi. Hali hii inaufanya mfuko huu kutokutekeleza kazi zake kulingana na malengo ya kuanzishwa kwake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Sera ya Mabaraza ya Ardhi ya vijijini kuwa chini ya Wizara ya Ardhi iangaliwe upya na ikiwezekana Mabaraza hayo yawe chini ya Mahakama. Kamati ilielezwa kuwa hili ni suala la kisera ambalo linahitaji muda wa kutosha kulishughulikia kwa kushirikisha vyombo mbalimbali vya maamuzi. Hata hivyo, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria ilifanya utafiti wa Mabaraza hayo na taarifa yake ipo tayari na ilishawasilishwa kwa Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali iipatie Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini kiasi cha Shilingi Bilioni 17 ambacho kilitakiwa kutolewa na Serikali kama ubia katika ujenzi wa Jengo la Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA TOWER)*. Kamati ilielezwa kuwa Wizara iliwasilisha maombi yake Hazina ya kupatiwa kiasi hicho cha fedha katika mwaka wa fedha 2013/14 ambacho ni sehemu ya malipo ya ada ya usimamizi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuahidiwa kiasi cha shilingi bilioni 2 katika bajeti ya mwaka 2014/2015. Kiasi hiki cha fedha kingechangia katika ujenzi wa jengo la Wakala. Hata hivyo, kiasi hicho cha fedha hakikutengwa katika makadirio ya bajeti ya mwaka husika. Jengo la *RITA Tower* linajengwa kwa ubia kati ya RITA na Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Mheshimiwa Spika, mpango wa kusajili watoto wa chini ya umri wa miaka mitano usambazwe katika Wilaya zote nchini ili kuhakikisha watoto wote wanasajiliwa. Kamati ilielezwa kuwa mpango wa usajili wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano ulizinduliwa rasmi tarehe 23 Julai, 2013 katika Halmashauri 10 za Mkoa wa Mbeya na kusajili zaidi ya watoto 132,387. Mpango huu unatarajiwa kuenezwa katika mkoa wa Mwanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 na baadaye kuenezwa katika Mikoa ya Shinyanga, Geita na Simiyu na hatimaye nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, changamoto zinazoikabili Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zilizo chini yake: Katika utekelezaji wa majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara ya Katiba na Sheria ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

Ukomo wa bajeti kwani kiasi cha fedha kinachotengwa kwa Wizara kimekuwa hakikidhi mahitaji halisi ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake na hakizingatii mpango kazi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kukosekana kwa fursa ya kupatiwa mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi ya mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo (*Law School of Tanzania)*. Hali hii inapunguza uwezo wa Taasisi hiyo wa kudahili idadi kubwa ya wanafunzi pamoja na kusababisha migogoro na migomo ya mara kwa mara kwa wanafunzi waliodahiliwa.

Changamoto nyingine ni vitendo vya rushwa kuendelea kujitokeza miongoni mwa watumishi na kusababisha Wizara ya Katiba na Sheria kuwekwa katika nafasi ya pili katika Taasisi ambazo watumishi wake wanahusishwa na rushwa hapa nchini.

Kutotolewa kwa wakati na kwa ukamilifu fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake. Mfano kwa mwaka wa fedha 2013/214 Mahakama ya Tanzania ilitengewa kiasi cha Shilingi bilioni 42.8 kwa ajili ya miradi ya maendeleo hadi kufikia Machi 31, 2014 Mahakama ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi bilioni 5.5 tu.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi wa Serikali kuhusu hoja mbalimbali za Kamati: Wakati wa kupitia taarifa ya utekelejaji wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2013/2014 na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamati yangu iliomba ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo yalionekana yanahitaji ufafanuzi wa ziada.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeyatolea ufafanuzi mambo hayo kama ifuatavyo:- Ufafanuzi kuhusu kufahamika kwa bajeti ya Bunge Maalumu la Katiba kwa Mwaka wa fedha 2013/2014 na kama ilipelekwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilielezwa kwamba bajeti ya Bunge Maalum ya Jumla ya shilingi bilioni 24.4 ilipitishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka huo wa fedha kupitia Fungu 21 - Hazina kwenye kifungu cha *Special Expenditure*. Serikali ilitenga fedha hizo kwa kutambua kwamba Bunge Maalum lingeanza kazi kwa mwaka huo wa fedha na kwa wakati huo mahitaji halisi ya Bunge Maalum yalikuwa hayafahamiki. Aidha, kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika uendeshaji wa Bunge hilo, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 20 katika Fungu 21 – Hazina kwenye kifungu cha *Special expenditure* katika mwaka wa fedha 2014/2015 ili kukamilisha kazi hiyo.

Mheshimikwa Spika, Wizara kutoa maelezo kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali kutokana na athari za *Operation* Tokomeza: Kamati ilielezwa kuwa kufuatia Azimio la Bunge lililoitaka Serikali kuunda Tume ya Uchunguzi ili kuchunguza athari na hatua za kuchukua kwa wale waliohusika na usababishaji wa madhara yaliyojitokeza katika zoezi la *Operation*

Tokomeza, Serikali imeunda Tume ya Uchunguzi chini ya Sheria ya *Commision of Inquiry Act*, Sura ya 32 na kuitangaza kupitia Gazeti la Serikali Namba 131 la tarehe 2 Mei, 2014. Kupitia Tume hiyo, Makamishna watatu wameteuliwa kufanya kazi hiyo kwa mujibu wa hadidu za rejea walizopewa.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa katika kupunguza mashauri mahakamani na msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani. Kamati ilielezwa kuwa Wizara na Taasisi zake wamechukua hatua mbalimbali za kupunguza mashauri mahakamani na idadi ya mahabusu na wafungwa magerezani. Hatua hizo ni pamoja na kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashitaka na kudhibiti kesi zinazopelekwa mahakamani, kutembelea magereza na maeneo ya vizuizi, kuanzisha mifumo ya kielektroniki ya utunzaji wa kumbukumbu za mashauri, kuweka mipango ya kuajiri idadi kubwa zaidi ya mawakili wa Serikali, mahakimu na watumishi wa kada nyingine, kuwa na muda maalum wa kumaliza mashauri mapya kwa kila ngazi ya mahakama kwa mwaka, kuhakikisha kwamba mashauri yote yaliyosajiliwa yanamalizika katika kipindi kisichozidi miaka miwili, kutekeleza mkakati wa kujipima kwa wastani wa idadi ya mashauri yanayotolewa uamuzi kwa kila Jaji na Hakimu,

Mheshimiwa Spika, kuhusu iwapo nakala ya Hati ya Muungano kuthibitishwa na Msajili wa Mahakama badala ya Katibu Mkuu Kiongozi ni ukiukwaji wa Sheria na hasa vifungu vya 83 na 85 vya Sheria ya Ushahidi Sura ya 6: Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu suala hili kwamba vifungu vya 83 na 85 vya Sheria ya Ushahidi Sura ya 6 vinahusiana na nyaraka zinazowasilishwa Mahakamani kama Sehemu ya ushahidi. Kulingana na matakwa ya vifungu hivyo, nyaraka hizo zinazowasilishwa mahakamani ndizo zinazopaswa kuthibitishwa na Mhifadhi *(Custodian)* wa nyaraka husika. Kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Viapo Sura ya 12, Msajili wa Mahakama ni mmoja kati ya watu wenye mamlaka ya kuthibitisha nakala ya hati ama nyaraka. Hivyo, Msajili wa Mahakama kuthibitisha Hati ya Muungano haikuwa ukiukwaji wa Sheria yoyote.

Mheshimikwa Spika, maelezo kuhusu sababu za kupungua kwa bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2014/2015 kutoka bilioni 260 kwa mwaka 2013/2014 hadi kufikia bilioni 230.9 kwa mwaka 2014/2015: Kamati ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa shilingi bilioni 260. Fedha hizo zilijumuisha shilingi bilioni 33.9 za Iliyokuwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Fungu 8, ambapo kwa mwaka huu wa Fedha Tume ya Mabadiliko ya Katiba imemaliza shughuli zake hivyo haikutengewa Fedha. Aidha, program ya Maboresho ya Sekta ya Sheria imemalizika hivyo kufanya fedha za nje kwa mwaka huu kupungua sana.

Mheshimiwa Spika, ufafanuzi juu ya maelekezo ya Mahakama kuhusu kifungu cha 148 cha sheria ya mwenendo wa Makosa ya Jinai na Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye kesi ya Balozi Prof. Costa Mahalu: Kamati ilifafanuliwa kuwa katika kesi ya Prof. Mahalu Mahakama ilikitamka kifungu cha 36(4)(e)cha Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 kuwa ni cha kibaguzi kwa kuwa kinatoa unafuu kwa watu wenye fedha kupata dhamana na kuwanyima haki hiyo wale wasio na fedha. Mahakama haikukitolea maelezo kifungu cha 148 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20. Katika kesi hiyo, Mahakama ilielekeza kifungu cha 36(4)(e) kifanyiwe marekebisho ili kiendane na matakwa ya Katiba.

Serikali haikuridhika na uamuzi huo na hivyo iliamua kukata rufaa katika Mahakama ya Rufani kwa kutoa *notice* ili kupinga uamuzi huo kwa misingi kwamba kifungu cha 36(4)(e) hakikinzani na Katiba. Marekebisho ya kifungu hicho hayajafanywa kwa kuwa rufaa dhidi ya uamuzi huo haijasikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliendelea kuelezwa kuwa chanzo cha kesi hii ni kwamba Prof. Mahalu na mwenzake walishitakiwa kwa kosa la jinai Na.1/2007 katika Mahakama ya Hakimu

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Mkazi Kisutu ambapo dhamana ilizuiliwa kwa mujibu wa kifungu cha 36(4)(e) kinachoweka sharti la kuweka nusu ya kiasi cha fedha kinachohusika katika kesi kwa ajili ya dhamana. Hatua hii ilipelekea Prof. Mahalu kufungua shauri la Kikatiba na kuomba Mahakama kutamka kuwa kifungu hicho ni cha kibaguzi. Wakati Serikali ikiendelea na mchakato wa rufaa kuhusu shauri la kikatiba, shauri la jinai lililokuwa Kisutu lilitolewa uamuzi ambapo Prof. Mahalu aliachiwa huru. Serikali ilikata rufaa dhidi ya uamuzi wa kuachiwa Prof. Mahalu kupitia rufaa Na.135/2012 ambapo baadaye rufaa hii iliondolewa na Mkurugenzi wa Mashitaka nchini *(DPP)*.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kamati yangu iliridhika na ufafanuzi huu uliotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati: Kwa kuzingatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake ili kuboresha utendaji kazi kwa lengo la kuleta ufanisi kwa manufaa ya Taifa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama: Tume ya Utumishi wa Mahakama ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 113 ya Katiba ya Jamhuri Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake, ikisomwa pamoja na Sheria ya Utumishi wa Mahakama, Sura 237, ikiwa na majukumu ya kusimamia maadili na nidhamu kwa watumishi wa Tume/Mahakama pamoja na kuboresha menejimenti ya watu ndani ya Tume na Utumishi wa mahakama. Kutokana na umuhimu wa Taasisi hii, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 Tume haikutengewa fedha za maendeleo, Kamati inaendelea kushauri Serikali kwamba Tume hii itengewe fedha za kutosha na fedha zilizoidhinishwa zitolewe kwa wakati.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara, baadhi ya watumishi wa Wizara wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya rushwa hivyo kusababisha Wizara kuwa katika nafasi ya pili kwa kujihusisha na rushwa, Kamati ina shauri Tume ya Utumishi wa Mahakama ijengewe uwezo ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuthibiti hali hii ya hatari.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali: Wakati wa kupitia utekelezaji wa majukumu na makisio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria Kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazokabili ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, hivyo pamoja na mambo mengine inashauri ifuatavyo ili kuboresha utendaji kazi huo, kwamba:- Kwa kuwa Serikali imeendelea kuijengea uwezo Mahakama ya Tanzania kupitia Mfuko wa Mahakama na kwa kuzingatia kuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni mdau mkubwa katika utekelezaji wa shughuli za Mahakama, Kamati inashauri kwamba maboresho ya Mahakama yaende sambamba na maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kuwa vyombo hivi vinafanya kazi kwa ufanisi katika kuhakikisha kwamba azma ya utoaji haki sawa na kwa wakati inafikiwa.

Mheshimiwa Spika, Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP): Kamati inashauri pamoja na mambo mengine kwamba:- Divisheni ya Mashtaka ijengewe uwezo kwa kupewa kibali cha kuajiri watumishi 489 na kuwapatia mafunzo ili waweze kutekeleza majukumu yao kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mahakama: Kamati iliitembelea Mahakama ya Tanzania mnamo mwezi Februari, 2014 ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi hii katika

Mwaka wa Fedha 2013/2014. Katika ziara hiyo Kamati ilielezwa kuhusu mikakati iliyopangwa na inayotekelezwa juu ya namna ya kupunguza mlundikano wa mashauri Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, moja ya Mikakati ya Mahakama ya kupunguza mlundikano wa mashauri ni kuwa na takwimu sahihi na zinazoaminika za mashauri nchini kote. Mahakama imeainisha mashauri yote kwa miaka yake ya kusajiliwa na kuanza kuyashughulikia kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ni kuanzishwa kwa mpango wa ufanyaji kazi kwa kujipima utendaji kazi *(performance based)*. Katika mpango huo kila ngazi ya Mahakama imejiwekea wastani wa idadi ya mashauri itakayomaliza kwa mwaka. Mfano, Mahakama ya Rufani imeweka lengo la kumaliza mashauri 1200 hadi 1400 kwa mwaka, Mahakama Kuu kesi 220 hadi kesi 250 kwa kila Jaji kwa mwaka na Mahakama za Hakimu Mkazi na Wilaya kesi 250 hadi kesi 300 kwa kila Hakimu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kuwa Mahakama siyo miongoni mwa maeneo sita ya vipaumbele vya Taifa yaliyomo katika Mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa *(Big Results Now - BRN)*.

Hata hivyo, Mahakama katika mpango wake wa ndani imeweza kuandaa na kutekeleza mpango unaofanana na mpango wa BRN na kupata mafaniko makubwa kwa muda mfupi ikiwemo kupunguza mashauri mahakamani.

Kamati inapongeza juhudi hizo zinazofanywa na uongozi wa Mahakama katika kukabiliana na changamoto ya mlundikano wa mashauri Mahakamani na nyingine ili kufikia azma ya kutoa haki kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na kasi hii na tunaamini kwamba kama kasi hii itaendelea, Mahakama inaweza kumaliza kabisa tatizo la mlundikano wa mashauri mahakamani. Pamoja na jitihada hizi Kamati inashauri kama ifuatavyo:- Fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama ziwekewe wigo *(ring fenced)* ili kuhakikisha kuwa zinatumika kwa malengo yanayokusudiwa. Aidha, Fedha za Mfuko wa Mahakama zisifananishwe na fedha za matumizi ya kawaida (OC) bali zipewe uzito stahiki na kutolewa kwa wakati.

Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la ufinyu wa bajeti na kuchelewa kutolewa au kutototolewa kabisa kwa Fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Mahakama, Kamati inashauri kuwa bajeti ya Mahakama iongezwe na fedha zinazoidhinishwa zitolewe kwa wakati ili kuiwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria: Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo mhimili mkuu wa Serikali katika masuala yote ya kisheria katika nchi ikiwa na jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa kunakuwa na utawala wa sheria unaozingatia Katiba na kuwepo kwa mfumo wa sheria unaotoa fursa sawa kwa watu wote katika jamii ili kuweza kuendesha shughuli zao kwa ufanisi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu uliopo nchini ni matunda ya usimamizi makini wa mfumo wa utawala wa sheria, hivyo, ni dhahiri kuwa Wizara hii ni muhimu kwa mustakabali wa Taifa letu.

Kwa kuzingatia unyeti wa Wizara hii na ili iendelee kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati inashauri ifuatavyo:- Kasi ya utoaji wa fedha zinazotengwa na Wizara na kupitishwa na Bunge lako tukufu iongezwe na zitolewe kwa wakati ili kuwezesha ufanikishaji wa utekelezaji wa shughuli hizo.

Kwa kuwa Wizara imekwishapelekewa na Tume ya Marekebisho ya Sheria, Taarifa ya Mapendekezo ya mfumo bora wa utatuzi wa migogoro ya ardhi, Kamati inashauri taarifa hiyo ifanyiwe kazi mapema ili mfumo bora wa utatuzi wa migogoro uanze kutumika kwa lengo la kumaliza migogoro ya ardhi inayoendelea hapa nchini. Pia tunapendekeza kwamba Wizara ipewe kibali cha kuajiri watumishi 22 kama ilivyoomba.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria: Ili kuboresha utendaji kazi wa Tume, Kamati inashauri kama ifuatavyo:- Tume ijengewe uwezo kwa kupewa kibali cha kuajiri Watumishi wa kutosha wenye ujuzi katika masuala stahiki ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, watumishi waliopo wajengewe uwezo kwa kupewa mafunzo katika fani zao.

Pia tunapendekeza Serikali ihakikishe inatoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Tume ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora: Kamati yangu inatoa ushauri ufuatao:- Serikali iimarishe Tume hii kwa kuitengea bajeti ya kutosha na kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa na kuidhinishwa na Bunge zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake na kufikia lengo la Taifa lililokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA): Kamati inashauri kuwa Serikali itoe kiasi cha fedha kinachodaiwa ili kuepuka riba kubwa itakayotokea endapo fedha zitachelewa kulipwa. Kwa upande mwingine, Kamati inaipongeza RITA kwa kazi nzuri wanayoifanya na mafanikio makubwa waliyoyapata katika kutekeleza mpango wa kusajili watoto chini ya umri wa miaka mitano unaojulikana kama *Under Five Birth Registration Initiative* katika Mkoa wa Mbeya na maeneo mengine nchini.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha na malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na bajeti kwa mwaka wa fedha 2014/2015: Ili kutekeleza majukumu ipasavyo, Wizara ya Katiba na Sheria inaomba fedha kwa mwaka 2014/2015 kwa muhtasari kwa mafungu kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria alipokuwa anawasilisha hoja yake mbele ya Bunge lako tukufu.

Kamati yangu inakubaliana na maombi hayo na itawasilisha maombi ya nyongeza ya fedha kwenye Kamati ya Bajeti kwa ajili ya kufikiriwa kama ambavyo Mheshimiwa Spika ulitoa mwongozo wakati tunaendelea na mjadala wa bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, hitimisho: Napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu. Aidha, tunatoa shukrani na kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge lako tukufu kwa jinsi mnavyoendesha Bunge hili.

Pia, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro, Naibu Waziri Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki, Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Jaji Frederick Werema na Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa George Masaju kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hii.

Vile vile nawashukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria na Wakuu wa Taasisi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Spika, kipekee, mimi na Makamu wangu, Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes, Mbunge wa Karagwe, tunawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Kwa heshima kubwa, ninaomba *Hansard* irekodi majina yao kama yanavyoonekana kwenye taarifa yetu kikamilifu. Aidha, ninapenda kuwashukuru kwa dhati Watumishi wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kulisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Pia ninawashukuru Ndugu Matamusi Fungo na Ndugu Maria Mdulugu, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Katiba na Sheria Kama Ilivyowasilishwa Mezani**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014, PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2014/2015**

**1.0 UTANGULIZI**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 99 (5),(9) na 117(11) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili, 2013, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inahusisha mafungu saba ambayo ni: Fungu 12-Tume ya Utumishi wa Mahakama, Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Fungu 35 - Mkurugenzi wa Mashtaka, Fungu 40- Mahakama, Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria, Fungu 55- Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Fungu 59- Tume ya Kurekebisha Sheria.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 3 Mei, 2014 Kamati yangu ilichambua taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro (Mb), Waziri wa Katiba na Sheria akishirikiana na Naibu Waziri Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki (Mb), pamoja na Watendaji wa Wizara. Katika maelezo yake Waziri aliieleza Kamati kuhusu utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati kwa kipindi cha Mwaka 2013/2014.

**UTEKELEZAJI WA MAONI NA USHAURI WA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014**

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati yangu ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi wa Wizara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa kiasi kikubwa ushauri huo umezingatiwa na ushauri mwingine upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ifuatilie kwa makini utendaji kazi wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba bila kuathiri uhuru wa Tume na kuiwezesha nchi kufikia lengo la kupata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara ilikuwa karibu na Tume katika utekelezaji wa majukumu yake ikiwa ni pamoja na kufuatilia utekelezaji bila kuingilia uhuru wake. Kutokana na jitihada hizo Tume ilikamilisha maandalizi ya Rasimu ya Katiba pamoja na taarifa nyinginezo muhimu, na kuikabidhi rasimu hiyo Serikalini. Aidha, Rasimu ya katiba imeishawasilishwa katika Bunge Maalum la Kutunga Katiba.

(ii) Bajeti ya Bunge la Katiba ifahamike na iletwe Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba Sura ya 83, masuala yote ya Bunge la Katiba yapo chini ya Bunge Maalum la Katiba ambapo fedha kwa ajili ya Bunge hili zinatolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.

(iii) Tume ya Utumishi wa Mahakama iongezewe Bajeti yake kwa kutengewa fedha za Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Tume ya Utumishi wa Mahakama haikutengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Bajeti iliyopewa Tume ya Utumishi wa Mahakama kwa mwaka 2014/2015 imefuata ukomo wa Bajeti ya Tume ya Shilingi 2,871,716,000.

(iv) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iimarishe Kitengo cha Mikataba kwa kuwajengea uwezo wa kuwapatia Rasilimali Watu na fedha.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilielezwa kuwa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inao mpango wa kuwasomesha Mawakili waliopo na watakaoajiriwa ili kuwajengea uwezo kitaaluma katika kushughulikia masuala ya mikataba na masuala mengine ya kisheria. Kutokana na uwezo wa Serikali kifedha uliopo katika mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imepanga kumsomesha Wakili mmoja katika ngazi ya Shahada ya Uzamili katika nyanja za mikataba inayohusu mafuta na masuala ya shughuli za ujenzi. Kwa sasa eneo hili la mikataba kwa Muundo wa ofisi ya Mwansheria Mkuu wa Serikal limepewa hadhi ya kuwa Divisheni na kuongozwa na Afisa mwenye cheo cha Mkurugenzi.

Mheshimiwa Spika, Divisheni hii kwa sasa inao Mawakili wa Serikali kumi na nane (18) na inatarajia kuajiri wengine wawili katika mwaka wa fedha 2014/2015. Sambamba na jitihada hizi, eneo la mikataba limetengewa kasma yake ya Bajeti ya kiasi cha Shilingi bilioni 1.34 katika mwaka wa fedha 2013/2014 kwa ajili ya shughuli mbalimbali. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa (UNDP) chini ya Mradi wa UNDP Support Programme wamekuwa wakifadhili Programu ya Mafunzo ya muda mfupi ili kuwawezesha mawakili wa Serikali na wadau wengine wa Sekta nyingine kuwajengea uwezo wa kuchambua, kujadili, kuandika, kuhakikisha na kusimamia mikataba.

(v) Kitengo cha Uandishi wa Miswada kiweke utaratibu wa kundaa Miswada kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili ili hatimaye inapokuwa imepitishwa na Bunge, kuwepo na sheria moja yenye Lugha ya Kiingereza na Kiswahili na hii itawasaida wananchi wengi kunufaika na sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba Serikali imeendelea kuzingatia maelekezo ya Kamati na kuyafanyia kazi kila mara. Kwa hivi sasa Miswada ya Sheria inayowasilishwa Bungeni imekuwa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Mfano, Sheria ya Marekebisho ya Katiba na Sheria ya Vyama vya Ushirikia.

(vi) Serikali iiwezeshe kibajeti Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuajiri watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilitengewa bajeti ya Shilingi bilioni 1.86 kwa lengo la kuajiri watumishi wapya 489. Hata hivyo, kibali cha kuajiri watumishi hao wapya hakikutolewa kutokana na sababu za kibajeti zilizojitokeza. Hivyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imewasilisha tena maombi ya ajira mpya kwa watumishi 489 kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

(vii) Bajeti iliyotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2013/2014 ni kidogo. Hivyo Serikali inashauriwa kuitengea ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali fedha nyingi za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inakubaliana na maoni ya Kamati kuwa bajeti ya miradi ya maendeleo inayotengwa ni kidogo. Hata hivyo, kumekuwepo na jitihada za kuwasilisha maombi Wizara ya Fedha ya kutengewa fedha za maendeleo za ndani lakini jitihada hizi bado hazijafanikiwa kutokana na uwezo wa Serikali kuwa mdogo. Mfano, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeomba jumla ya Shilingi bilioni 50.0 fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Ofisi za Makao Makuu na Ofisi mpya za Mikoani ili kuondokana na tatizo la kupanga katika majengo binafsi kwa gharama kubwa. Hata hivyo fedha zilizotengwa ni shilling 457,149,000 ambazo ni fedha za nje.

(viii) Serikali iboreshe maslahi ya watumishi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuwapa motisha ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha maslahi ya watumishi wake kwa kutoa motisha mbalimbali ili kuongeza tija na ari ya utendaji kazi. Kwa upande wa Mawakili wa Serikali, mishahara imeboreshwa, Mawakili wanalipwa posho kwa ajili ya kodi ya pango la nyumba, na posho ya mavazi. Aidha, watumishi wote wanalipwa posho ya muda wa ziada baada ya saa za kazi na siku za mapumziko.

(ix) Kurugenzi ya Mashtaka iongezewe uwezo kifedha ili iweze kutekeleza vyema Mpango wake wa kutenganisha suala la Upelelezi na uendeshaji wa Mashtaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa katika mwaka wa Fedha 2013/2014 Serikali iliongeza bajeti ya Divisheni ya Mashtaka kutoka Shilingi 10,844,037,000 hadi Shilingi 20,844,037,000 kwa ajili ya kutekeleza malengo yaliyopangwa. Kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015 Divisheni ya Mashtaka imetengewa jumla ya shilingi bilioni 22,144,326,000/=.

(x) Wizara inunue vifaa vya kisasa kama kompyuta na Samani za ndani kwa Mahakama zote nchini.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilielezwa kuwa Wizara kupitia Mahakama ya Tanzania itahakikisha kuwa Mahakama zake zinapata vitendea kazi muhimu ili kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kulingana na uwezo wa Serikali kifedha uliopo.

(xi) Serikali itoe fedha za maendeleo zilizotengwa kwa mahakama ili kuwezesha miradi ya ujenzi wa mahakama kuendelea kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa hadi kufikia mwezi wa Machi, 31, 2014 Mahakama ilikuwa imepokea fedha kiasi cha shilingi 5,508,842,840 kati Tshs. 42, 716, 668, 000/= ikiwa ni bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kutekeleza bajeti, ambazo zimetumika katika kufanya kazi zifuatazo:-

- Kufanya uchambuzi wa kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Mahakama Tanzania.

- Kufanya ukaguzi wa ukarabati wa mahakama nchi nzima kwa kutumia mshauri elekezi (TBA).

- Kuendelea kufanya ukarabati wa Mahakama Kuu, Dar es Salaam na Mtwara ambao unategemea kumalizika ifikapo mwei Juni, 2014.

- Ujenzi wa Mahakama Kuu Bukoba awamu ya Tatu unaendelea na unategemea kumalizika ifikapo Juni, 2014.

(xii) Mahakama ipewe fedha za kujengea majengo ya Mahakama Kuu kwenye Mikoa ya Kigoma, Mara, Lindi, Morogoro, Singida, Manyara, Katavi, Njombe, Simiyu na Pwani ili kupunguza kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa ni azma ya Serikali kuhakikisha kuwa kila mkoa unakuwa na Mahakama Kuu katika kipindi kifupi iwezekanavyo. Hivyo, Mahakama imejizatiti kuhakikisha kwamba dhamira hiyo ya Serikali inatimizwa kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

(xiii)) Mahakama ibuni njia bora zaidi za upimaji wa utendaji kazi wa Mahakimu na Majaji ili kuongeza ufanisi na utendaji wa Mahakama kwenye kazi zake.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Mahakama imeshaweka utaratibu bora, shirikishi na wa uwazi katika upimaji wa utendaji kazi wa Mahakimu na Majaji kwa kuwa na viwango na idadi maalum vya uondoshaji wa mashauri kwa mwaka.

(xiv) Serikali iharakishe kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa Mradi wa tele justice ili Mahakama iweze kuondokana na mfumo wa zamani wa kerekodi mienendo ya kesi kwa njia ya mkono.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Taarifa ya upembuzi yakinifu wa Mradi huu imekamilishwa na kuwasilishwa Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango kwa hatua za kupata fedha na hatua nyingine za utekelezaji.

(xv) Serikali iimarishe Mfuko wa Mahakama kibajeti ili mfuko huo uweze kukidhi mahitaji ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Mfuko wa Mahakama umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Mahakama Sura ya 237. Kwa mwaka 2013/2014 Mfuko huu umetengewa Shilingi Bilioni 129.69. Hata hivyo, Mfuko huu umekuwa ukiidhinishiwa fedha kidogo na pia kutolewa kwa kuchelewa na hivyo kutokidhi mahitaji yake ya msingi. Hali hii inaufanya mfuko huu kutokutekeleza kazi zake kulingana na malengo ya kuanzishwa kwake.

(xvi) Serikali iweke utaratibu wa kutoa motisha kwa Mahakimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilielezwa kwamba Mahakama inajitahidi kutoa motisha kwa watumishi wake wa ngazi mbalimbali kwa kadri bajeti inavyoruhusu. Watumishi wamekuwa wanapatiwa motisha ya aina mbalimbali kama vile kulipa kodi ya pango, kutoa vyombo vya usafiri, kulipa stahili kwa wakati kama fedha za likizo, posho za ziada, matibabu, mazishi; kutoa fursa za mafunzo na kubadilishana uzoefu kwa kuhamia katika vituo vingine kwa muda.

(xvii) Sera ya Mabaraza ya Ardhi ya vijijini kuwa chini ya Wizara ya Ardhi iangaliwe upya na ikiwezekana Mabaraza hayo yawe chini ya Mahakama.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa hili ni suala la kisera ambalo linahitaji muda wa kutosha kulishughulikia kwa kushirikisha vyombo mbalimbali vya maamuzi. Hata hivyo, Wizara kupitia Tume ya Kurekebisha Sheria ilifanya utafiti wa Mabaraza hayo na taarifa yake ipo tayari.

(xviii) Serikali iipatie Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini kiasi cha Shilingi Bilioni 17 ambacho kilitakiwa kutolewa na Serikali kama ubia katika ujenzi wa Jengo la Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini (RITA TOWER).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara iliwasilisha maombi yake Hazina ya kupatiwa kiasi hicho cha fedha katika mwaka wa fedha 2013/14 ambacho ni sehemu ya malipo ya ada ya usimamizi wa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuahidiwa kiasi cha shilingi bilioni 2 katika bajeti ya mwaka 2014/2015. Kiasi hiki cha fedha kingechangia katika ujenzi wa jengo la Wakala. Hata hivyo, kiasi hicho cha fedha hakikutengwa katika makadirio ya bajeti ya mwaka husika. Jengo la RITA Tower linajengwa kwa ubia kati ya RITA na Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF).

(xix) Mpango wa kusajili watoto wa chini ya umri wa miaka mitano (U5BRI) usambazwe katika Wilaya zote nchini ili kuhakikisha watoto wote wanasajiliwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Mpango wa usajili wa watoto walio chini ya umri wa miaka mitano (U5BR) ulizinduliwa rasmi tarehe 23 Julai, 2013 katika Halmashauri 10 za Mkoa wa Mbeya na kusajili zaidi ya watoto 132,387. Mpango huu unatarajiwa kuenezwa katika mkoa wa Mwanza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2014/2015 na baadae kuenezwa katika

mikoa ya Shinyanga, Geita na Simiyu. Hadi sasa Wakala umetambulisha Mpango katika ngazi ya Sekretarieti ya Mkoa na kufanya vikao vya hamasa na Makatibu Tawala wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Waganga Wakuu wa Wilaya na wa Mkoa, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya awali. Kazi hii imefanyika sanjari na kufanya utafiti wa awali (baseline) kama hatua za awali za kuusambaza mfumo huo katika Mkoa husika.

(xx) Matukio ya uvunjwaji wa haki na kutoa ripoti zake mapema ili kuwawezesha Wananchi kujua hali ya Haki za Binadamu.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kwamba utaratibu wa usuluhishi na upatanishi kama mbinu mbadala za kuharakisha utatuzi wa baadhi ya migogoro umeanzishwa.

Kwa kutumia njia hii, Tume imeweza kufanya usuluhishi na upatanishi katika mashauri 25 kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ambapo ufumbuzi wa haraka wa mashauri hayo ulipatikana. Aidha:-

(i) Tume imeendelea kutoa elimu katika maeneo mbalimbali kwa lengo la kuiwezesha jamii kujua misingi ya haki za binadamu na utawala bora;

(ii) Kuendelea kuboresha mfumo wa kompyuta katika kushughulikia malalamiko (Case Management System) pamoja na maboresho katika mfumo wa kompyuta unaopokea malalamiko kwa njia ya ujumbe wa simu (SMS for Human Rights);

(iii) Tume imezindua Mpango kazi wa kitaifa wa Haki za Binadamu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali. Mpango kazi huu utasaidia jamii kutambua na kuzingatia misingi ya haki za binadamu katika kutekeleza majukumu yao; na

(iv) Tume imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake hasa katika fani mbalimbali hasa za uchunguzi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

(xxi) Serikali iipatie Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora fedha za kutosha ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ikiwa ni pamoja na kuchapa Ripoti za Haki za Binadamu za kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2014/15, Serikali imeongeza Bajeti ya Tume kutoka Shillingi 3,795,802,000 hadi Shilingi 4,795,802,000 fedha za matumizi mengineyo ambapo Tume imepanga kutumia ongezeko hili katika kuboresha utekelezaji wa majukumu yake.

(xxii) Serikali iangalie uwezekano wa kurekebisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi kutokana na mifumo iliyopo kutokidhi mahitaji na hali halisi ya sasa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Tume imekamilisha Taarifa ya Mapitio ya Sheria zinazohusiana na Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi. Taarifa hiyo imekwisha wasilishwa kwa Waziri wa katiba na sheria kwa hatua za maamuzi.

**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI WIZARA YA KATIBA NA SHERIA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE**

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Wizara ya Katiba na Sheria ilikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

(i) Ukomo wa bajeti kwani kiasi cha fedha kinachotengwa kwa Wizara kimekuwa hakikidhi mahitaji halisi ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake hakizingatii mpango kazi wa wizara. Kwa mfano kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 Tume ya Utumishi wa Mahakama imetengewa Tsh 2,871,738,000 wakati mahitaji halisi ni Tsh 4,341,738,000. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imetengewa Tsh 8,332,865,000 wakati mahitaji halisi ni Tsh 13,400,000,000.

(ii) Baadhi ya Taasisi kutegemea majengo ya Ofisi za kupanga kwa gharama kubwa hivyo kupunguza uwezo wa kuboresha huduma zake hali hii inayopunguza ari ya kufanya kazi miongoni mwa watumishi wa wizara . Mfano wa Ofisi zilizo katika majengo ya kupanga ni Ofisi karibu zote zilizoko Mikoani zinazotumiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliyopo Jengo la Sukari House, jijini Dar es Salaam.

(iii) Kukosekana kwa fursa ya kupatiwa mikopo kwa wanafunzi wa Taasisi ya mafunzo ya Uanasheria kwa vitendo(The Law School of Tanzania). Hali hii inapunguza uwezo wa Taasisi hiyo wa kudahili idadi kubwa ya wanafunzi pamoja na kusababisha migogoro na migomo ya mara kwa mara kwa wanafunzi waliodahiliwa.

(iv) Watumishi wa Wizara kuacha kazi na kujiunga na Taasisi nyingine kwa lengo la kutafuta maslahi bora na kusababisha kuongezeka kwa tatizo la uhaba wa watumishi.

(v) Uhaba wa rasilimali watu umeendelea kuwa tatizo katika Taasisi, Idara na Vitengo mbalimbali hivyo kuathiri kiwango cha ufanisi katika utoaji huduma kwa wananchi. Mfano, mahitaji halisi ya Watumishi katika Wizara na Taasisi zake ni 9,351 wakati Watumishi waliopo sasa ni 6,913.

(vi) Vitendo vya rushwa kuendelea kujitokeza miongoni mwa watumishi na kusababisha Wizara ya Katiba na Sheria kuwekwa katika nafasi ya pili katika Taasisi ambazo watumishi wake wanahusishwa na rushwa hapa nchini.

(vii) Mazingira duni ya kufanyia kazi kwa Watumishi wa Wizara pamoja na Taasisi zake hususan ukosefu wa majengo ya Mahakama za Mwanzo, Ofisi za Mawakili wa Serikali pamoja na taasisi nyingine. Hali hiyo inapunguza ari ya kufanya kazi miongozi mwa watumishi wa Wizara na Taasisi zilizo chini yake.

(viii) Uwezo mdogo wa wananchi walio wengi kutumia vyombo vya kutoa haki na huduma za kisheria pamoja na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu mfumo uliopo wa Sheria na Mahakama nchini. Jambo hilo linasababisha baadhi ya Wananchi kujichukulia sheria mkononi kisha kupelekea kuongezeka kwa vitendo vya uvunjifu wa amani na ukiukwaji wa haki za Binadamu.

(ix) Kutotolewa kwa wakati na kwa ukamilifu fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zilizo chini yake. Wizara na Taasisi zilizo chini yake zimekuwa zikichelewa kupata fedha zinazoidhinishwa na serikali au zimekuwa zikipata pungufu au kutopata kabisa. Mfano kwa Mwaka wa Fedha 2013/214 Mahakama ya Tanzania ilitengewa kiasi cha Shilingi 42.8 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo hadi kufikia Machi 31, Mahakama ilikuwa imepokea kiasi cha Tsh Bilioni 5.5 tu.

**UFAFANUZI WA SERIKALI KUHUSU HOJA MBALIMBALI ZA KAMATI**

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia taarifa ya utekelejaji wa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2013/2014 na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa

Mwaka wa Fedha 2014/2015, Kamati yangu iliomba ufafanuzi kwa baadhi ya mambo ambayo yalionekana yanahitaji ufafanuzi wa ziada.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeyatolea ufafanuzi mambo hayo kama ifuatavyo:-

(a) Ufafanuzi kuhusu kufahamika kwa bajeti ya Bunge Maalumu la Katiba kwa Mwaka wa fedha 2013/2014 na kama ilipelekwa Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu ilielezwa kwamba bajeti ya Bunge Maalum ya Jumla ya Sh.Bilioni 24.4 ilipitishwa na Bunge lako Tukufu kwa Mwaka huo wa fedha kupitia Fungu-21 Hazina kwenye kifungu cha" Special Expenditure". Serikali ilitenga fedha hizo kwa kutambua kwamba Bunge Maalum lingeanza kazi kwa mwaka huo wa fedha na kwa wakati huo mahitaji halisi ya Bunge Maalum yalikuwa hayafahamiki. Aidha, kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika uendeshaji wa Bunge hilo, Serikali imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 20.0 katika Fungu 21 – Hazina kwenye kifungu cha "Special expenditure" katika mwaka wa fedha 2014/2015 ili kukamilisha kazi hiyo.

(b) Wizara kutoa maelezo kuhusu hatua zilizochukuliwa na Serikali kutokana na athari za operation Tokomeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kufuatia Azimio la Bunge lililoitaka Serikali kuunda Tume ya Uchunguzi ili kuchunguza athari na hatua za kuchukua kwa wale waliohusika na usababishaji wa madhara yaliyojitokeza katika zoezi la Operation Tokomeza, Serikali imeunda Tume ya Uchunguzi Chini ya Sheria ya Commision of Inquiry Act, Sura ya 32 na kuitangaza kupitia Gazeti la Serikali Namba 131 la tarehe 2 Mei, 2014. Kupitia Tume hiyo, Makamishna watatu wameteuliwa kufanya kazi hiyo kwa mujibu wa hadidu za rejea walizopewa.

(c) Hatua zilizochukuliwa katika kupunguza mashauri mahakamani na msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa Wizara na Taasisi zake wamechukua hatua mbalimbali za kupunguza mashauri mahakamani na idadi ya mahabusu na wafungwa magerezani. Hatua hizo ni pamoja na:-

(i) Kutenganisha shughuli za upelelezi na uendeshaji mashtaka na kudhibiti kesi zinazopelekwa Mahakamani,

(ii) Kutembelea magereza na maeneo ya vizuizi,

(iii) Kuanzisha mifumo ya kielektroniki ya utunzaji wa kumbukumbu za mashauri,

(iv) Kuweka mipango ya kuajiri idadi kubwa zaidi ya mawakili wa Serikali, mahakimu na watumishi wa kada nyingine,

(v) Kuwa na muda maalum wa kumaliza mashauri mapya kwa kila ngazi ya mahakama kwa mwaka,

(vi) Kuhakikisha kwamba mashauri yote yaliyosajiliwa yanamalizika katika kipindi kisichozidi miaka miwili,

(vii) Kutekeleza mkakati wa kujipima kwa wastani wa idadi ya mashauri yanayotolewa uamuzi kwa kila jaji na hakimu,

(viii) Msukumo unaofanyika kupitia Kamati za Kusukuma Kesi, na

(ix) Jukwaa la Haki Jinai la Taifa - Kuchukua hatua madhubuti kuondoa msongamano wa wafungwa na mahabusu.

(d) Kuhusu iwapo nakala ya Hati ya Muungano kuthibitishwa na Msajili wa Mahakama badala ya Katibu Mkuu Kiongozi ni ukiukwaji wa Sheria (vifungu vya 83 na 85 vya Sheria ya Ushahidi ) Sura ya 6.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu suala hili kwamba vifungu vya 83 na 85 vya Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 vinahusiana na nyaraka zinazowasilishwa Mahakamani kama Sehemu ya ushahidi. Kulingana na matakwa ya vifungu hivyo, nyaraka hizo zinazowasilishwa mahakamani ndizo zinazopaswa kuthibitishwa na Mhifadhi (Custodian) wa nyaraka husika. Kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Viapo, Sura ya 12, Msajili wa Mahakama ni mmoja kati ya watu wenye mamlaka ya kuthibitisha nakala ya Hati/Nyaraka. Hivyo, Msajili wa Mahakama kuthibitisha Hati ya Muungano haikuwa ukiukwaji wa Sheria yoyote.

(e) Maelezo kuhusu sababu za kupungua kwa bajeti ya Wizara kwa Mwaka 2014/2015 kutoka Bilioni 260 kwa mwaka 2013/2014 hadi kufikia Bilioni 230.9 kwa Mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilielezwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Wizara iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 260. Fedha hizo zilijumuisha Sh. Bilioni 33,994,588,000 za Iliyokuwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, Fungu-8, ambapo kwa mwaka huu wa Fedha Tume ya Mabadiliko ya Katiba imemaliza shughuli zake hivyo haikutengewa Fedha. Aidha, program ya Maboresho ya Sekta ya Sheria imemalizika hivyo kufanya fedha za nje kwa mwaka huu kupungua sana.

(f) Ufafanuzi juu ya maelekezo ya Mahakama kuhusu kifungu cha 148 cha sheria ya mwenendo wa Makosa ya Jinai na Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwenye kesi ya Balozi Prof. Costa Mahalu

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifafanuliwa kuwa katika kesi ya Prof. Mahalu Mahakama ilikitamka kifungu cha 36(4)(e)cha Sheria ya Uhujumu Uchumi Sura ya 200 kuwa ni cha kibaguzi kwa kuwa kinatoa unafuu kwa watu wenye fedha kupata dhamana na kuwanyima haki hiyo wale wasio na fedha. Mahakama haikukitolea maelezo kifungu cha 148 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Sura ya 20. Katika kesi hiyo, Mahakama ilielekeza kifungu cha 36(4)(e) kifanyiwe marekebisho ili kiendane na matakwa ya Katiba. Serikali haikuridhika na uamuzi huo na hivyo iliamua kukata rufaa katika Mahakama ya Rufani kwa kutoa notisi ili kupinga uamuzi huo kwa misingi kwamba kifungu cha 36(4)(e) hakikinzani na Katiba. Marekebisho ya kifungu hicho hayajafanywa kwa kuwa rufaa dhidi ya uamuzi huo haijasikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliendelea kuelezwa kuwa chanzo cha kesi hii ni kwamba Prof. Mahalu na mwenzake walishtakiwa kwa kosa la jinai Na.1/2007 katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ambapo dhamana ilizuiliwa kwa mujibu wa kifungu cha 36(4)(e) kinachoweka sharti la kuweka nusu ya kiasi cha fedha kinachohusika katika kesi kwa ajili ya dhamana. Hatua hii ilipelekea Prof. Mahalu kufungua shauri la Kikatiba na kuomba mahakama kutamka kuwa kifungu hicho ni cha kibaguzi. Wakati Serikali ikiendelea na mchakato wa rufaa kuhusu shauri la kikatiba, shauri la jinai lililokuwa Kisutu lilitolewa uamuzi ambapo Prof. Mahalu aliachiwa huru.

Serikali ilikata Rufaa dhidi ya uamuzi wa kuachiwa Prof. Mahalu kupitia rufaa Na.135/2012 ambapo baadaye rufaa hii iliondolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP).

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Kamati yangu iliridhika na ufafanuzi huu wa Serikali.

**MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati pamoja na majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria na taasisi zilizo chini yake, Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Wizara na Taasisi zilizo chini yake ili kuboresha utendaji kazi kwa lengo la kuleta ufanisi kwa manufaa ya Taifa kama ifuatavyo:-

**TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA - FUNGU 12**

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Mahakama ilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 113 ya Katiba ya Jamhuri Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake, ikisomwa pampja na Sheria ya Utumishi wa Mahakama, Sura ,237, ikiwa na majukumu ya kusimamia maadili na nidhamu kwa watumishi wa Tume/Mahakama pamoja na kuboresha menejimenti ya watu ndani ya Tume na Utumishi wa mahakama. Kutokana na umuhimu wa Taasisi hii, Kamati inashauri kama ifuatavyo :-

Kwa kuwa katika mwaka wa fedha 2013/2014 Tume haikutengewa fedha za maendeleo, Kamati inaendelea kushauri Tume itengewe fedha za kutosha na fedha zilizoidhinishwa zitolewe kwa wakati.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara, baadhi ya watumishi wa Wizara wamekuwa wakijihusisha na vitendo vya rushwa hivyo kusababisha Wizara kuwa katika nafasi ya pili kwa kujihusisha na rushwa,kamati ina shauri Tume ya Utumshi wa mahakama kujengewa uwezo ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuthibiti hali hii hatari'

Kutokana na uhaba wa fedha Serikalini na ukomo wa bajeti iliyopewa Tume ya Utumishi wa Mahakama, Kamati inashauri Wizara kufanya utaratibu wa kuhamishia kiasi cha Shilingi Bilioni moja na Millioni mia nne(1,400,000,000/=)kutoka mfuko wa Mahakama mapema kwenda Tume ya Utumishi wa Mahakama ili kuiwezesha Tume hiyo kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Kwa kuwa bado hakuna uelewa wa kutosha kwa wananchi kuhusu uwepo wa Tume na Kamati za Maadili za Mahakama pamoja na Majukumu ya yake, Kamati inashauri kuwa Elimu kuhusu uwepo wa Tume pamoja na majukumu yake iendelee kutolewa hasa vijijni ili kuwawezesha wananchi kuitumia kwa kupeleka malalamiko wakiona kuna ukiukwaji wa maadili.

**OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**
**Fungu 16**

Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia utekelezaji wa majukumu na makisio ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria kamati ilibaini changamoto mbalimbali zinazokabili ofisi ya mwanasheria mkuu wa Serikali, hivyo inashauri ifuatavyo ili kuboresha utendaji wake:-

(i) Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ijengewe uwezo katika kitengo cha mikataba kwa kuwapatia mafunzo Mawakili wa Serikali katika masuala ya mikataba ya mafuta na gesi ili kuhakikisha kuwa watendaji hao wanatumika ipasavyo kuishauri Serikali kuingia mikataba yenye tija kwa taifa kuhusu sekta hizo na nyingine.

(ii) Kwa kuwa kumekuwa na kuongezeka kwa matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaosababisha uvunjifu wa amani, Kamati inashauri Serikali iimarishe mfumo wa utoaji haki ili kuhakikisha kwamba amani na utulivu vinaendelea kuwepo na kuimarika kwa wananchi kupata haki sawa na kwa wakati.

(iii) Kwa kuwa Serikali imeendelea kuijengea uwezo Mahakama ya Tanzania kupitia Mfuko wa Mahakama na kwa kuzingatia kuwa Mwasheria Mkuu wa Serikali ni mdau mkubwa katika utekelezaji wa shughuli za Mahakama, Kamati inashauri kwamba maboresho ya Mahakama yaende sambamba na maboresho ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuhakikisha kuwa vyombo hivi vinafanya kazi kwa ufanisi katika kuhakikisha kuwa azma ya utoaji haki sawa na kwa wakati inafikiwa.

(iv) Serikali iendelee kuboresha maslahi ya watumishi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hususan Mawakili wa Serikali ili kuwapa motisha watumishi hao kufanya kazi kwa bidii na kwa uadilifu mkubwa.

(v) Kamati inashauri Serikali itenge fedha za ndani za kutosha na kutoa fedha zinazoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ili iweze kujenga ofisi na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Taasisi hii.

**MKURUGENZI WA MASHITAKA (DPP) - Fungu 35**

Mheshimiwa Spika, Divisheni ya Mashtaka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeanzishwa kupitia Ibara ya 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake kwa ajili ya kutekeleza jukumu muhimu katika Taifa la kuendesha Mashtaka na kuratibu kazi zinazofanywa na vyombo vya uchunguzi kama yalivyoainishwa na Katiba na sheria zingine. Kutokana na umuhimu huo, ili kuimarisha na kuboresha Divisheni hii, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Divisheni ya Mashtaka ijengewe uwezo kwa kupewa kibali cha kuajiri watumishi 489 na kuwapatia mafunzo ili waweze kutekeleza majukumu yao kama ilivyokusudiwa.

(ii) Serikali itoe fedha za matumizi ya kawaida ili Ofisi hii iweze kutekeleza majukumu yake ikiwemo kutembelea magereza, kuendesha mashtaka na kuratibu shughuli zinazofanywa na vyombo vya upelelezi Nchini.

**MAHAKAMA - Fungu 40**

Mheshimiwa Spika, Kamati iliitembelea Mahakama ya Tanzania mnamo Mwezi Februari, 2014 ili kupokea taarifa ya utekelezaji wa Majukumu ya taasisi hii katika Mwaka wa Fedha 2013/2014. Katika ziara hiyo Kamati ilielezwa kuhusu mikakati iliyopangwa na inayotekelezwa juu ya namna ya kupunguza mlundikano wa mashauri Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, moja ya Mikakati ya Mahakama ya kupunguza mlundikano wa mashauri ni kuwa na takwimu sahihi na zinazoaminika za mashauri nchini kote. Mahakama imeainisha mashauri yote kwa miaka yake ya kusajiliwa na kuanza kuyashughulikia kwa kasi kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ni kuanzishwa kwa mpango wa ufanyaji kazi kwa kujipima utendaji kazi (performance based).Katika mpango huo kila ngazi ya mahakama imejiwekea wastani wa idadi ya mashauri itakayo yamaliza kwa mwaka. Mfano, mahakama ya

rufani imeweka lengo la kumalliza mashauri 1200 hadi 1400 kwa mwaka,mahakama kuu 220 hadi 250 kwa kila Jaji kwa mwaka na mahakama za hakimu mkazi na Wilaya kesi 250 hadi 300 kwa kila hakimu kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa kazi za mahakama kwa kuongeza vitendea kazi na rasilimali watu ni mkakati mwingine uliochukuliwa na Taasisi hii ili kupunguza mlundikano wa mashauri

Mheshimiwa Spika, sote tunatambua kuwa Mahakama sio miongoni mwa maeneo sita ya vipaumbele vya Taifa yaliyomo katika mpango wa Tekeleza kwa Matokeo Makubwa Sasa (BRN). Hata hivyo, mahakama katika mpango wake wa ndani imeweza kuandaa na kutekeleza mpango unaofanana na mpango wa BRN na kupata mafaniko makubwa kwa muda mfupi ikiwemo kupunguza mashauri mahakamani. Kamati inapongeza juhudi hizo zinazofanywa na uongozi wa mahakama katika kukabiliana na changamoto ya mlundikano wa mashauri Mahakamani (back logs) na nyingine ili kufikia azma ya kutoa haki kwa wote na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na kasi hii na tunaamini kwamba kama kasi hii itaendelea Mahakama inaweza kumaliza kabisa tatizo la mlundikano wa mashauri mahakamani. Pamoja na jitihada hizi Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Fedha zinazotengwa kwa ajili ya Mfuko wa Mahakama ziwekewe wigo (ring fenced) ili kuhakikisha kuwa zinatumika kwa malengo yanayokusudiwa. Aidha, Fedha za Mfuko wa Mahakama zisifananishwe na fedha za matumizi ya kawaida (OC) bali zipewe uzito stahiki na kutolewa kwa wakati.

(ii) Kwa kuwa kumekuwa na tatizo la ufinyu wa bajeti na kuchelewa kutolewa au kutototolewa kabisa kwa Fedha zinazotengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya mahakama. Mfano katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 Mahakama iliidhinishiwa Sh. Bilioni 42. Hadi kufikia Machi 31, 2014, ni kiasi cha shilingi bilioni 5.5 tu ndizo zilikuwa zimetolewa, Kamati inashauri kuwa bajeti ya Mahakama iongezwe na fedha zinazoidhinishwa zitolewe kwa wakati ili kuiwezesha Mahakama kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

(iii) Mahakama ipewe kibali cha kuajiri watumishi wengine wakiwemo mahakimu wa Mahakama za Mwanzo ili kupunguza tatizo la upungufu wa watumishi sambamba na kuboresha maslahi ya Watumishi hao.

(iv) Kutokana na upungufu na uduni wa Ofisi pamoja na vitendea kazi, Kamati inashauri hatua za makusudi na za haraka zichukuliwe ili kujenga majengo ya Mahakama na kuweka vitendea kazi bora na vya kisasa ili kuamsha ari ya utendaji kazi miongoni mwa watumishi wa Mahakama.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA – Fungu 41**

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo mhimili mkuu wa Serikali katika masuala yote ya kisheria katika nchi ikiwa na jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa kunakuwa na utawala wa sheria unaozingatia Katiba na kuwepo kwa mfumo wa sheria unaotoa fursa sawa kwa watu wote katika jamii ili kuweza kuendesha shughuli zao kwa ufanisi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, amani na utulivu uliopo nchini ni matunda ya usimamizi makini wa mfumo wa utawala wa Sheria, hivyo, ni dhahiri kuwa Wizara hii ni muhimu kwa mustakabali wa

Taifa letu. Kwa kuzingatia unyeti wa Wizara hii na ili iendelee kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Kamati imebaini kwamba utoaji wa fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Wizara hii hauridhishi. Kwa Mfano kwa mwaka wa Fedha 2013/2014 Wizara ilitengewa Sh. 7,069, 331,500. Hadi kufikia Machi, 2014, ni kiasi cha sh 2,355,175,821 tu sawa na asilimia 29 tu ndizo zilizokuwa zimetolewa. Kamati inashauri kuwa kasi ya utoaji wa fedha zinazotengwa na Wizara na kupitishwa na Bunge iongezwe na zitolewe kwa wakati ili kuwezesha ufanikishaji wa utekelezaji wa shughuli hizo.

(ii) Serikali kuweka kipaumbele miradi ya maendeleo na kutenga fedha za ndani kwa ajili hiyo kuliko kutegemea fedha za nje.

(iii) Kwa kuwa Wizara imekwishapelekewa na Tume ya Marekebisho ya Sheria, Taarifa ya Mapendekezo ya mfumo bora wa utatuzi wa migogoro ya ardhi ,Kamati inashauri taarifa hiyo ifanyiwe kazi mapema ili mfumo bora wa utatuzi wa migogoro uanze kutumika kwa lengo la kumaliza migogoro ya ardhi inayoendelea hapa nchini.

(iv) Kamati ilielezwa kwamba Wizara ina upungufu wa watumishi wa kada mbalimbali. Katika kukabiliana na changamoto hiyo Wizara iliomba kibali cha kuajiri watumishi 22 kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 lakini hakikutolewa. Hivyo Kamati inashauri kwamba vibali hivyo vitolewe ili kuijengea uwezo Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA - Fungu 59**

Mheshimiwa Spika, Tume ya Kurekebisha Sheria ni Taasisi ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria iliyoanzishwa kwa mujibu Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria, Sura 171. Majukumu ya Tume ni kufanya mapitio ya Sheria Mbalimbali na kufanya utafiti kisha kuandaa mapendekezo na kuyawasilisha kwa Waziri wa Katiba na Sheria ambaye huyawasilisha Bungeni kwa ajili ya utunzi wa Sheria au kuzifanyia mabadiliko Sheria zinazokuwa zina mapungufu katika kuhakikisha kuwa Sheria za nchi zinaenda sanjari na mazingira ya sasa katika kudumisha utawala wa Sheria na usimamizi wa Haki nchini.

Ili kuboresha utendaji kazi wa Tume, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Tume ijengewe uwezo kwa kupewa kibali cha kuajiri Watumishi wa kutosha wenye ujuzi katika masuala stahiki ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, watumishi waliopo wajengewe uwezo kwa kupewa mafunzo katika fani zao.

(ii) Serikali ihakikishe inatoa fedha zinazotengwa kwa ajili ya Tume ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

(iii) Kwa kuwa Utafiti ni moja ya majukumu ya Tume, Kamati inashauri kwamba Tume ipewe vitendea kazi vya kutosha ikiwemo magari ili kurahisisha usafiri kwenda kufanya utafiti maeneo mbalimbali.

**TUME YA HAKI ZA BINADAMU NA UTAWALA BORA - Fungu 55**

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni idara huru ya Serikali ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria iliyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 129 ya katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Mwaka 1977 pamoja na marekebisho yake ikisomwa pamoja na Sheria ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Sura 391. Majukumu ya Tume

yameainishwa katika Ibara ya 130 (1) ya Katiba. Jukumu kubwa la Tume hii ni kulinda, kutetea na kuhifadhi haki za binadamu nchini. Ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati yangu inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iimarishe idara hii kwa kuitengea bajeti ya kutosha na kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa na kuidhinishwa na Bunge zinatolewa kwa wakati ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake na kufikia lengo na Taifa lililokusudiwa; na

(ii) Kwa kuwa rasilimali watu ni nyenzo muhimu katika ufanisi wowote wa maendeleo,Kamati inashauri Tume ijengewe uwezo kwa kuongeza watumishi wenye ujuzi katika masuala mbalimbali na kupewa vitendea kazi stahiki ili kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**WAKALA WA USAJILI, UFILISI NA UDHAMINI**
**(Registration, Insolvency and Trusteeship Agency-RITA)**

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Usajili ,Ufilisi na Udhamini (RITA) ni idara ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria yenye jukumu la kusajili na kuweka kumbukumbuku muhimu za maisha ya binadamu nchini kwa maendeleo ya Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu wa idara hii kamati inatoa ushauri ufuatao ili kuimarisha na kuboresha idara hii:-

(i) Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) iliingia ubia wa kujenga jengo lake katika mtaa wa Makunganya jijini Dar es salaam. Gharama za ujenzi ilikuwa shilingi bilioni 35 ambapo kati ya fedha hizo, RITA walipaswa kutoa shilingi bilioni 17, lakini hadi sasa wametoa bilioni 1 tu. Kamati inashauri kuwa Serikali itoe kiasi cha Fedha kinachodaiwa ili kuepuka riba kubwa itakayotokea endapo fedha zitachelewa kulipwa.

(ii) Kwa upande mwingine, Kamati inaipongeza RITA kwa kazi nzuri wanayoifanya na mafanikio makubwa waliyoyapata katika kutekeleza mpango wa kusajili watoto chini ya umri wa miaka mitano unaojulikana kama U5BRI-Under five Birth Registration Initiative katika Mkoa wa Mbeya na maeneo mengine nchini. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuuwezesha kibajeti Wakala ili uweze kutekeleza mpango wake ilioubuni wa U5BRI (Underfive Birth Registration Initiatives) na kuusambaza katika mikoa mingine nchini.

**MAOMBI YA FEDHA NA MALENGO YA BAJETI KWA**
**MWAKA WA FEDHA 2013/2014**

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu ipasavyo,Wizara ya Katiba na Sheria inaomba fedha kwa mwaka 2014/2015 kwa muhtasari kwa mafungu kama ifuatavyo:- Fungu 12 –Tume ya Utumishi ya Mahakama (Tsh 3.080.480.000); Fungu 16 –Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Tsh,11.216.912.000); Fungu 35-Kurugenzi ya Mashtaka (Tsh. 22.144.326.000); Fungu 40 – Mahakama (Tsh.166.388.093.000); Fungu 41-Wizara ya Katiba na Sheria (Tsh.16.231.914.000); Fungu 55 –Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Tsh. 7.339.564.000); na Fungu 59-Tume ya kurekebisha Sheria (Tsh.8.577.362.121) kama alivyoeleza Mheshimiwa waziri wa Katiba na Sheria alipokuwa anawasilisha hoja yake mbele ya Bunge lako Tukufu.

**HITIMISHO**

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa fursa hii muhimu ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu. Pia, namshukuru Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Dkt Asha- Rose Migiro, (Mb), Naibu Waziri Mheshimiwa Angela Jasmine Kairuki (Mb), Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Jaji Frederick Werema, (Mb), na Naibu Mwansheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa George M. Masaju kwa ushirikiano wao mkubwa walioutoa wakati Kamati ilipojadili Makadirio na Mapato na Matumizi ya Wizara hii. Vile vile

nawashukuru Katibu Mkuu, Wizara ya Katiba na Sheria na Wakuu wa Taasisi pamoja na Maafisa Waandamizi wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano waliotupatia.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015. Uzoefu wao wa muda mrefu katika masuala mbalimbali kuhusu sekta ya sheria, Haki za Binadamu na Utawala Bora umesaidia kufanikisha kazi hii kwa ufanisi. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. William Mganga Ngeleja, (Mb) - Mwenyekiti
2. Mhe. Gosbert Begumisa Blandes, (Mb)- M/Mwenyekiti
3. Mhe. Abbas Zuberi Mtemvu,(Mb)- Mjumbe
4. Mhe. Nimrod Elirehema Mkono,(Mb) - Mjumbe
5. Mhe. Halima James Mdee, (Mb) - Mjumbe
6. Mhe. Fakharia Khamis Shomar,(Mb) - Mjumbe
7. Mhe. Nyambari C.M Nyangwine, (Mb) - Mjumbe
8. Mhe. Jaku Hashim Ayoub, (Mb ) - Mjumbe
9. Mhe. Felix Francis Mkosamali, (Mb) - Mjumbe
10. Mhe. Rukia Khasim Ahmed, (Mb) - Mjumbe
11. Mhe. Mustapha Boay Akunaay,(Mb) - Mjumbe
12. Mhe. Ramadhan Haji Saleh, (Mb) - Mjumbe
13. Mhe. Tundu Antipas Mughwai Lissu,(Mb) - Mjumbe
14. Mhe. Deogratias Aloys Ntukamazina,(Mb)- Mjumbe
15. Mhe. Jason Samson Rweikiza, (Mb) - Mjumbe
16. Mhe. Ali Khamis Seif,(Mb) - Mjumbe
17. Mhe. Abdallah Sharia Ameir,(Mb) - Mjumbe
18. Mhe. Mariam R. Kasembe,(Mb) - Mjumbe
19. Mhe. Zahra Ali Hamad, (Mb) - Mjumbe
20. Mhe,Shamsi Vuai Nahodha, (Mb) - Mjumbe

Aidha, napenda kuwashukuru kwa dhati watumishi wa Ofisi ya Bunge, chini ya Uongozi wa Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Bunge, kwa kuisaidia na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Kipekee, nawashukuru ndugu Matamus Fungo na ndugu Maria Mdulugu, kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kiidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria na Taasisi zake, kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

William Mganga Ngeleja (Mb)
MWENYEKITI
KAMATI YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA
Mei, 2014

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa ninamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara hii, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Mheshimiwa Spika, yafuatayo ni Maoni ya Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Mpango, Makadirio na Mapitio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2014/2015:-

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ninaomba irekodiwe katika *Hansard* kama ilivyo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria imeanzishwa kwa mujibu wa kipengele cha 12 cha Nyongeza ya Waraka wa Rais uliochapishwa kama Tangazo la Serikali Na. 494 la tarehe 17 Desemba 2010. Majukumu ya Ofisi hii yameainishwa katika Tangazo la Ukasimishaji wa Majukumu ya Kiuwaziri la Mwaka 2010 *(The Ministers (Assignment of Ministerial Functions) Notice, 2010)*, lililochapishwa katika Gazeti la Serikali kama Tangazo la Serikali Na. 494A la tarehe 17 Desemba, 2010. Kwa mujibu wa Nyongeza ya Pili ya Tangazo hilo, pamoja na mengine, Ofisi ya Waziri wa Katiba na Sheria imekasimiwa majukumu ya masuala ya kikatiba, uendeshaji, utoaji wa haki, uendeshaji mashtaka na haki za binadamu.

Mheshimiwa Spika, majukumu haya ni mazito katika hali ya kawaida, kwani mfumo wa kikatiba, haki za binadamu na utoaji haki katika nchi yenye kufuata mfumo wa kidemokrasia ndiyo roho ya mfumo mzima wa utawala. Mfumo wa kikatiba na wa utoaji haki ndiyo unaotofautisha dola iliyoparaganyika (*a failed state*) na dola inayoongozwa kikatiba (*a constitutional state*) na utawala wa sheria (*rule of law*). Majukumu haya ni mazito zaidi katika nchi ambayo, kama ilivyo nchi yetu, inatengeneza Katiba Mpya. Hapa, vilevile, mfumo unaotumika kutengeneza Katiba Mpya ndiyo utakaotofautisha nchi hiyo kuwa *a failed state* au kuwa nchi yenye mfumo imara wa kikatiba na wa kisiasa. Kwa sababu hiyo, kwa vyovyote vile, majukumu ya Wizara ya Katiba na Sheria ni mazito na yenye umuhimu mkubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Bunge Maalum na Harufu ya Ufisadi: Vyombo vya habari mbalimbali hapa nchini vimemnukuu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, akisema kwamba, hadi kuahirishwa kwake, Bunge Maalum limetumia zaidi ya Shilingi bilioni 27. Kama kauli ya Waziri wa Fedha ni sahihi, kiasi hiki cha fedha kitakuwa kikubwa kuliko fedha za Matumizi ya Kawaida ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Divisheni ya Uendeshaji Mashtaka na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, kwa ujumla wao kwa mwaka unaoisha wa fedha. Hiki siyo kiasi kidogo cha fedha katika nchi kama yetu ambayo shughuli mbalimbali za huduma za jamii zimekwama kwa ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati Bunge lako Tukufu linajadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala iliagiza bajeti ya Bunge Maalum iletwe Bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na kupitishwa. Kamati ilitoa agizo hilo kwa sababu wakati Wizara ilikuwa imewasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba, yaani Fungu 08, hakukuwa na Fungu lolote linalohusu Bunge Maalum. Hii ni licha ya ukweli kwamba, hadi kufikia mwaka jana, tayari ilikuwa inajulikana kwamba kutakuwa na Bunge Maalum, kwa sababu vifungu husika vya Sheria ya Mabadiliko ya Katiba vilikwishapitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, Agizo la Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala lilipuuzwa mwaka jana kwani Serikali hii sikivu ya CCM, haikuleta makadirio ya mapato na matumizi ya Bunge Maalum kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Mwaka huu pia agizo hilo limepuuzwa kwani hakuna Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bunge Maalum ambayo yameletwa kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Ili kuhalalisha vitendo vyake vya kupuuza agizo la Bunge lako Tukufu, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Mtengeti Migiro, alidai mbele ya Kamati kwamba, masuala yote ya Bunge la Katiba yapo chini ya Bunge Maalum la Katiba, ambapo fedha kwa ajili ya Bunge hili zinatolewa na

Mfuko Mkuu wa Hazina. Kwa jibu hili, Waziri alitaka kuiaminisha Kamati kwamba, hakukuwa na haja ya fedha za Bunge Maalum kujadiliwa na kuidhinishwa na Bunge lako Tukufu, kwa sababu tu fedha hizo zilikuwa zinatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuoneshwa kwamba, fedha zinazolipwa kutoka kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina hazina budi kuidhinishwa na sheria iliyotungwa na Bunge na matumizi yake kuidhinishwa na Sheria ya Matumizi ya Serikali, sasa Waziri amebadili kauli na kudai kwamba, fedha za matumizi ya Bunge Maalum ziliidhinishwa na Bunge lako Tukufu! Katika Majibu yake ya Hoja za Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala wakati wa kupitia Makadirio ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015, Mheshimiwa Waziri amesema yafuatayo: "Bajeti ya Bunge Maalum ya shilingi bilioni 24.4 ilipitishwa na Bunge katika Mwaka wa Fedha 2013/2014 kupitia Fungu 21 – Hazina kwenye kifungu cha *Special Expenditure*. Serikali ilifanya hivyo kwa kutambua kwamba, Bunge Maalum lingeanza kazi zake katika mwaka huo wa fedha. Wakati huo mahitaji halisi ya uendeshaji wa Bunge hilo yalikuwa hayafahamiki." Waziri ameongeza kusema kwamba, kwa kutumia uzoefu uliopatikana katika uendeshaji wa Bunge hilo, Serikali imetenga kiasi cha shilingi bilioni 20 kwenye Fungu 21 –Hazina kwenye kifungu cha *Special Expenditure* katika Mwaka wa Fedha 2014/2015 ili kukamilisha kazi zilizosalia.

Mheshimiwa Spika, kauli za Waziri wa Katiba na Sheria juu ya masuala yote yanayohusu Bajeti ya Bunge Maalum, hazina ukweli wowote. Kwanza, kuhusu kiasi cha fedha kilichokwishatumika kwa ajili ya Bunge Maalum. Kauli ya Waziri kwamba, kiasi hicho ni shilingi bilioni 24.4, inapingana moja kwa moja na kauli iliyotolewa na Waziri wa Fedha ndani ya Bunge Maalum. Kwa mujibu wa Taarifa Rasmi *(Hansard)* ya Majadiliano ya Bunge Maalum ya Kikao cha Ishirini na Tisa cha tarehe 24 Aprili, 2014, Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, alisema yafuatayo kuhusu matumizi ya Bunge Maalum: "Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha kwamba, hatutumii fursa hii, nasikitika tumechukua fedha, yaani kodi ya Wananchi ambao kila siku wanalia na wameweza ku-*sacrifice* tunakwenda kwenye *twenty seven billions* kwa ajili ya *session* hii, tumeweza ku-*sacrifice* kupeleka umeme kwa Wananchi, hususan vijijini." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiasi kilichotajwa na Waziri wa Fedha kinalingana na kiasi kilichotajwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Utaribu na Bunge), Mheshimiwa William Lukuvi, aliyeiambia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba, hadi linaahirishwa tarehe 25 Aprili mwaka huu, Bunge Maalum lilikwishatumia takribani shilingi bilioni 27.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu linahitaji majibu ya kuridhisha kuhusu mkanganyiko huu katika kauli za Waziri wa Katiba na Sheria na Mawaziri wenzake wa Fedha na Sera, Uratibu na Bunge. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM ilieleze Bunge lako Tukufu ni kauli ya Waziri yupi kati ya hawa watatu ndiyo iaminiwe na kuchukuliwa kuwa ndiyo kauli sahihi na Bunge lako Tukufu? Aidha, kama itajulikana kwamba mmojawapo kati ya Mawaziri hawa watatu ametoa taarifa za uongo kwa Kamati ya Bunge lako Tukufu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka mamlaka ya uteuzi, yaani Rais wa Jamhuri ya Muungano, awawajibishe kwa kuwafukuza kazi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, Waziri anayedanganya Bunge lako Tukufu au Kamati zake siyo tu analidharau Bunge, bali pia anaidharau mamlaka ya uteuzi wake, yaani Rais. Vinginevyo, Bunge lako Tukufu liambiwe kwamba Waziri huyo ametumwa na Rais kuja kudanganya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uongo wa pili wa kauli ya Waziri wa Katiba na Sheria unahusu madai yake kwamba, Bajeti ya Bunge Maalum iko kwenye Fungu 21 – Hazina. Uthibitisho wa uongo huu uko kwenye Kitabu cha II cha Makadirio ya Matumizi ya Umma ya Huduma za Mfuko Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014, kilichowasilishwa Bungeni mwaka jana; na Kitabu hicho hicho kilichowasilishwa Bungeni mwezi huu kwa ajili ya Mwaka wa Fedha 2014/2015. Katika Vitabu

vyote viwili, hakuna kifungu chochote kinachoitwa *Special Expenditure* au kasma yoyote inayohusu Bunge Maalum. Aidha, hakuna kifungu chochote chenye makadirio ya matumizi ya shilingi bilioni 24.4 kwa ajili ya Bunge Maalum au kwa ajili nyingine yoyote katika Kitabu cha mwaka 2013/2014; na wala hakuna makadirio ya matumizi ya shilingi bilioni 20 kwa ajili ya matumizi ya Bunge Maalum katika Kitabu cha mwaka 2014/2015. Vilevile kwenye Vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 na Mwaka wa Fedha 2014/2015, hakuna kifungu chochote kinachoitwa *Special Expenditure* au chenye kiasi cha fedha kilichotajwa na Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, kama hakuna vifungu vyovyote vya *Special Expenditure* kwa ajili ya Bunge Maalum na kama hakuna kiasi chochote kilichooneshwa kwenye Vitabu vya Bajeti, maana yake ni kwamba, Bunge lako Tukufu halijaidhinisha bajeti yoyote kwa ajili ya Bunge Maalum. Kwa kifupi, Waziri wa Katiba na Sheria amelidanganya Bunge lako Tukufu na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni itaona ajabu sana endapo Bunge lako Tukufu litaamua, licha ya ushahidi wote huu, kufunika kombe ili mwanaharamu apite! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maoni yake juu ya Hotuba ya Waziri Mkuu kuhusu Mapitio na Mwelekeo wa Kazi za Serikali na Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Bunge kwa Mwaka 2014/2015, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman A. Mbowe, aliliambia Bunge lako Tukufu kwamba, fedha zote zilizotumika kwa ajili ya gharama mbalimbali za Bunge Maalum hazikuidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Ukweli ni kwamba, hadi sasa Bunge lako Tukufu halijui bajeti yote ya Bunge Maalum, halijui fedha kiasi gani zimetumika kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya miundombinu ya Bunge hili, kwa ajili ya posho, mishahara na stahili mbalimbali za Wajumbe na Watumishi wa Bunge Maalum hadi lilipoahirishwa tarehe 25 Aprili, 2014. Aidha, Bunge lako Tukufu halina ufahamu wowote juu ya gharama za Bunge Maalum pale litakaporudi tarehe 5 Agosti, 2014, kuendelea kujadili Rasimu ya Katiba Mpya.

Katika hali hiyo, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni alitaka maswali yafuatayo yapatiwe majibu:-

(i) Je, bajeti ya matumizi ya Bunge Maalum ni kiasi gani na kwa ajili ya matumizi gani?

(ii) Je, ni kiasi gani cha fedha hizo kimeshatumika hadi sasa na kwa ajili ya matumizi gani?

(iii) Je, ni nani aliyejadili na kupitisha bajeti hiyo?

(iv) Je, ni Sheria gani iliyotungwa na Bunge lipi iliyoidhinisha matumizi haya ya fedha za umma?

(v) Je, ni lini na kwa Waraka gani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliidhinisha matumizi haya?

Mheshimiwa Spika, maswali haya hayajapatiwa majibu yoyote. Badala yake, Waziri wa Katiba na Sheria amelipa Bunge lako Tukufu sababu za kuuliza maswali mengine yafuatayo:-

(a) Je, ni ukurasa upi kati ya kurasa za 55 - 60 zenye makadirio ya Fungu 21 – Hazina kwenye Kitabu cha II ambapo kuna kifungu cha *Special Expenditure* chenye makadirio ya matumizi ya shilingi bilioni 24.4 kwa ajili ya Bunge Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014?

(b) Je, ni ukurasa upi kati ya kurasa za 68 - 73 zenye makadirio ya Fungu 21 – Hazina kwenye Kitabu cha II ambapo kuna kifungu cha *Special Expenditure* chenye makadirio ya matumizi ya shilingi bilioni 20.0 kwa ajili ya Bunge Maalum kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015?

(c) Je, kati ya kauli yake kwamba hadi linaahirishwa Bunge Maalum limekwishatumia shilingi bilioni 24.4 na kauli ya Waziri wa Fedha kwamba Bunge hilo limekwishatumia shilingi bilioni 27, ipi ndiyo kauli ya kweli?

(d) Mwisho, kama itajulikana kwamba kauli yake kuhusu masuala yanayohusu Bajeti ya Bunge Maalum ni ya uongo; yuko tayari kulinda heshima yake iliyobaki kwa kujiuzulu au atasubiri mamlaka yake ya uteuzi imwajibishe kwa kumfukuza kazi kwa kulidanganya Bunge?

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania: Ibara ya 4(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977, inaelekeza kwamba, Vyombo vyenye Mamlaka ya kutekeleza utoaji haki ni Mahakama ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Ibara ya 107A(1) inaweka wazi kwamba, mamlaka ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano itakuwa ni Mahakama. Maoni haya yanahusu Mahakama ya Tanganyika kwa sababu mbali na Mahakama ya Rufani ya Tanzania, masuala ya mahakama siyo mambo ya Muungano.

Katika Mwaka wa Fedha 2013/2014, Mahakama iliidhinishiwa shilingi bilioni 117.580 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 86.600 zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 30.980 kwa ajili ya mishahara. Aidha, Mahakama iliidhinishiwa shilingi bilioni 42.716 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa mujibu wa maelezo ya Makadirio ya Mapato, Matumizi ya Kawaida na Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2014/2015, hadi Machi 2014, Mahakama ilikuwa imepokea shilingi bilioni 72.106, sawa na asilimia 61 (siyo 56 zilizotajwa katika maelezo ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kati ya hizo, shilingi bilioni 36.253 au asilimia 42 zilikuwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 26.652 au asilimia 86 zilikuwa kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za maendeleo, hadi kufikia Machi, 2014, Mahakama ilikuwa imepokea shilingi bilioni 5.508 au asilimia 13 ya fedha zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Mahakama imeeleza katika Maelezo yaliyoletwa mbele ya Kamati kwamba, kutopelekewa fedha zilizoidhinishwa kumeisababishia Mahakama kuendesha shughuli zake kwa ugumu mkubwa. Aidha, mwenendo wa upatikanaji wa fedha za maendeleo umekuwa si wa kuridhisha na hivyo kuashiria kukwama kwa utekelezaji wa Miradi ya Mahakama ambayo mchakato wake umefikia ukingoni.

Mheshimiwa Spika, Ndimi Mbili za Mahakama: Lugha iliyotumika katika maelezo ya Mahakama kuelezea matatizo ya kutopatiwa fedha zinazoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ni ya kidiplomasia, ambayo pengine ndiyo lugha sahihi kwa mamlaka ya utoaji haki katika nchi. Hata hivyo, lugha hiyo haitoi picha kamili na halisi ya ukubwa wa matatizo hayo na inaweza kuwa inapotosha ukweli wa hali halisi. Kwa mfano, Maelezo ya Mahakama yanadai kwamba, Mahakama ya Tanzania imepiga hatua kubwa katika kuondoa mlundikano wa mashauri *(backlog clearance)* na kuonesha ongezeko kubwa la wastani wa uondoaji wa mashauri katika ngazi zote za Mahakama. Hata hivyo, Taarifa ya Waziri inatoa picha kinyume kabisa. Hivyo basi, kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri, upungufu huu wa bajeti umesababisha kukwama kwa shughuli za uendeshaji na usikilizaji wa mashauri na kusababisha kuongezeka kwa msongamano wa mahabusu na wafungwa magerezani. Vivyo hivyo tunaambiwa kama tulivyoambiwa miaka miwili iliyopita kwamba, suala la usafiri kwa ajili ya shughuli za Mahakama limepewa uzito unaostahili. Ili kuthibitisha uzito huo unaostahili, Mahakama inatuambia kwamba, mwaka

2013/2014 Mahakama ilipanga kununua magari 218 na pikipiki 200 kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi na usimamizi wa shughuli za Mahakama.

Hata hivyo, kwa mujibu wa maelezo hayo hayo ya Mahakama, hadi sasa tayari Mahakama imenunua magari saba na imeingia mkataba wa ununuzi wa magari mengine 211 na pikipiki 200 ambayo yanatarajiwa kupatikana mwishoni mwa mwezi Juni, 2014. Kwa maneno mengine, magari saba au asilimia tatu ya matarajio ndiyo yaliyokwishanunuliwa na bado Mahakama inaona huu ni uzito unaostahili! Kwa upande mmoja, Mahakama inatuambia kwamba, umalizaji wa mashauri katika Mahakama ya Ardhi ulikuwa asilimia 99, lakini kwa upande mwingine Wizara inatuambia imeshindwa kufuatilia migogoro ya ardhi. Ulimi mmoja wa Wizara unaliambia Bunge lako Tukufu juu ya kuimarika kwa usimamizi na ukaguzi wa kazi za Mahakama kwa kuongeza vitendea kazi na rasilimali watu. Ulimi mwingine wa Wizara hiyo hiyo, unakiri mbele ya Bunge lako Tukufu juu ya kupungua kwa imani ya Wananchi kwa Serikali kutokana na kukosekana kwa huduma au huduma hafifu!

Mdomo mmoja wa Wizara unasema kwamba, ukaguzi wa Mahakama uliofanywa na Viongozi wa Mahakama ya Tanzania, umesaidia kusikiliza maoni na malalamiko mbalimbali ambayo yamesaidia kuboresha utendaji kazi katika Mahakama husika. Mdomo mwingine wa Wizara hiyo hiyo unakanusha kwa kusema kwamba, Vikao vya Kamati za Maadili vimekwama hivyo kupelekea kuongezeka kwa malalamiko dhidi ya vyombo vya kutoa haki. Aidha, wakati Mahakama inadai, imeendelea kuwapatia motisha na kuboresha masilahi ya wafanyakazi kwa kuwapatia posho za saa za ziada, mikopo, zawadi wakati wa sikukuu za kitaifa na za kidini, mafunzo na usafiri kazini. Wizara inakanusha mambo hayo mazuri kwa kudai kuna kupungua kwa ari ya watumishi kufanya kazi! *Contradictions* hizi kati ya kauli za Wizara na Taasisi yake Kuu zinahitaji maelezo ya kuridhisha kwa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, takwimu zilizorembeshwa: Mahakama ya Tanzania imekuwa na matatizo mengi na sugu yanayotokana na ukosefu wa mgawo wa kibajeti. Matatizo haya yanafahamika na tumeyazungumza sana katika Bunge hili Tukufu. Hata hivyo, takwimu zinazotolewa na Wizara na hasa Mahakama yenyewe zinaleta tatizo lingine ambalo halihitajiki katika mazingira tuliyonayo. Hili ni tatizo la *sexed up statistics,* yaani takwimu zilizorembeshwa. Kuna msemo wa Kiingereza kuhusu takwimu unaosema *statistics are like a woman's bikini. What they reveal is interesting, but what they conceal is vital*! Yaani, takwimu zinafanana na vazi la kuogelea la mwanamke. Zinachokionesha kinapendeza, lakini zinachokificha ndiyo muhimu zaidi! *(KIcheko)*

**SPIKA:** Kwa nini mwanamke siyo mwanaume; si kuogelea tu?

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA:** Msemo huu unajidhihirisha katika takwimu zilizoletwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mahakama ya Tanzania juu ya utendaji kazi wake. Tunaambiwa, kwa mfano kwamba, mwaka 2013 mashauri 168,068 ya aina zote yalisajiliwa. Hata hivyo, kwa mujibu wa takwimu hizo, mashauri 182,237 ya aina zote yalisikilizwa na kutolewa hukumu kwa kipindi hicho na kubaki na mashauri 100,109 ya aina zote hadi ilipofika Disemba, 2013.

Hata kwa mtu asiyekuwa na shahada ya uzamivu ya takwimu, kama ilivyo kwa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni anayewasilisha Maoni haya, hesabu hizi za Mahakama ya Tanzania zina walakini mkubwa. Haiwezekani kwa mashauri 168,000 kufunguliwa katika mwaka mmoja, halafu mashauri 182,000 yasikilizwe na kutolewa maamuzi na bado yabaki mashauri 100,000 katika mwaka huo huo!

Mheshimiwa Spika, tatizo la *sexed up statistics* linaelekea kuwa sugu katika Mahakama ya Tanzania. Miaka miwili iliyopita, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ililalamika kwamba, takwimu za mafanikio ya Mahakama ya Tanzania katika kusikiliza na kutoa maamuzi ya mashauri zinapotosha ukweli.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilisema wakati ule kwamba, kama hali halisi ingekuwa ndiyo hii inayoelezewa na Wizara, basi ni wazi kwamba, nchi yetu ya Tanzania isingekuwa na tatizo la mlundikano wa kesi katika Mahakama zetu zote. Kwa hiyo, Wizara isingekuwa na changamoto za bajeti finyu isiyokidhi majukumu ya Mahakama au ya fedha kutokutolewa kadiri ya mpango wa kazi wa mwaka na kwa wakati kama inavyodaiwa katika Maelezo ya Wizara hayo hayo yanayotangaza mafanikio makubwa katika usikilizaji wa mashauri na utoaji wa maamuzi ya mashauri hayo.

Tofauti na Taarifa ya Waziri ya sasa, Maelezo ya Wizara ya mwaka 2012/2013, yalitoa takwimu zilizoonesha mlundikano wa mashauri ya aina zote katika ngazi mbalimbali za Mahakama. Hivyo, ilikuwa siyo vigumu kugundua kwamba, takwimu za mafanikio makubwa zilikuwa hazilingani na takwimu za mlundikano wa mashauri.

Ndiyo maana tuliweza kusema kwamba, kwa sababu ya kutopatiwa fedha za kukidhi mahitaji yake halisi, Mahakama ya Tanzania imeshindwa kabisa kutatua tatizo la mlundikano mkubwa wa kesi katika ngazi zote. Kwa sababu ambazo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kuzijua, mwaka huu Maelezo ya Mahakama hayana takwimu zozote za mlundikano wa mashauri katika ngazi zote za Mahakama ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutokuwa na taarifa za mlundikano mashauri katika Taarifa ya Waziri na Maelezo ya Mahakama, bado zipo ishara kwamba, hali siyo nzuri. Hivyo, kwa mfano, Taarifa ya Waziri inaonesha kwamba, idadi ya mahabusu magerezani imepungua kutoka 18,203 mwezi Juni, 2012 na kufikia mahabusu 17,284 mwezi Machi, 2014. Hili ni punguzo la mahabusu 919 au asilimia tano tu katika kipindi cha karibu miaka miwili!

Takwimu hizi zinaonesha kwamba, badala ya kupungua, tatizo la mlundikano wa mahabusu linaweza kuwa limeongezeka kwa kiasi kikubwa. Katika hali hii, hitimisho letu kuhusu masuala haya katika bajeti ya mwaka 2012/2013 bado ni sahihi. Kwa ushahidi huu ni wazi kwamba, Mahakama ya Tanzania imeshindwa kutekeleza wajibu wake huu wa Kikatiba kwa sababu ya kunyimwa fedha na vitendea kazi vingine na Serikali hii hii inayodai kwamba dira yake ni haki kwa wote na kwa wakati!

Mheshimiwa Spika, miaka miwili iliyopita Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Mohamed Chande Othman, aliiambia semina juu ya Kudhibiti Ucheleweshaji wa Utatuzi wa Migogoro ya Kibiashara: Usuluhishi Kama Njia ya Kuharakisha Utoaji Haki, iliyofanyika Dar es Salaam tarehe 20 Julai, 2012, kwamba, *case delay is a sign of an inefficient judicial system. Excessive case delays may amount to a denial of justice*. Yaani, ucheleweshaji wa kesi ni ishara ya mfumo wa kimahakama usiokuwa na ufanisi. Ucheleweshaji mkubwa wa kesi unaweza kuwa udhulumaji wa haki. Kauli hiyo ya Jaji Mkuu imerudiwa na Waziri ambaye amesema katika Taarifa yake kwamba, msingi wa dhima ya Wizara yake ni kuwa haki iliyocheleweshwa ni sawa na haki iliyodhulumiwa.

Kama kauli hizi ni za kweli na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini ni za kweli, basi ni kweli vilevile kwamba, maelfu ya mahabusu na wafungwa ambao wamejaa katika magereza yetu wakisubiri maamuzi ya kesi zao na maelfu ya wadaawa ambao kesi zao zimelundikana katika mahakama zetu zote, watakuwa wamedhulumiwa haki zao na Serikali hii ya CCM ambayo sera za utoaji haki za hazitekelezeki.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake ya mwaka 2011/2012, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ilielezea upungufu mkubwa wa watumishi wa ngazi mbalimbali wa Mahakama ya Tanzania ambao ni matokeo ya moja kwa moja ya kunyimwa fedha na Serikali. Tulirudia maelezo yetu katika maoni yetu ya mwaka 2012/2013. Miaka mitatu baadaye, tatizo hili halijapatiwa ufumbuzi wowote na kuna uwezekano linazidi kuwa kubwa zaidi.

Kwa mujibu wa takwimu za Wizara, kwa ujumla wake Wizara ina upungufu wa watumishi 2,521 au asilimia 27 ya mahitaji yake, ambayo ni watumishi 9,351. Kwa upande wa Mahakama, upungufu huo ni asilimia 25 au watumishi 1,891 kati ya 9,627 wanaohitajika. Ili kushughulikia tatizo hilo la uhaba wa watumishi, Serikali hii ya CCM imetoa kwa Mahakama kibali cha ajira mpya kwa ajili ya watumishi 148, ambayo ni sawa na asilimia nane tu ya wanaohitajika ili kuondoa upungufu huo!

Mheshimiwa Spika, katika Maoni yetu ya miaka miwili iliyopita tulieleza jinsi ambavyo Mahakama ya Tanzania imeendelea kufedheheka kwa kuwa mdeni mkubwa na sugu. Wakati tunaandika Maoni hayo, Mahakama ya Tanzania inadaiwa na Majaji na Watumishi wengine wa Mahakama, watoa huduma, wenye nyumba za kupangisha Majaji, Wajenzi na Wazabuni mbalimbali jumla ya shilingi bilioni 5.2. Fedha zote hizo zilikuwa ni madeni ya miaka ya nyuma hadi kufikia Mwaka wa Fedha 2010/2011. Hadi Machi, 2014, kwa mujibu wa Taarifa ya Waziri, madeni ya Wizara kwa watoa huduma na wakandarasi yamefikia zaidi ya shilingi bilioni tano. Kwa maana nyingine, madeni ya Wizara hayajapungua kwa kiasi chochote cha maana tangu Mwaka wa Fedha 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, tulipendekeza, wakati wa mjadala wa Sheria ya Uendeshaji Mahakama, miaka mitatu iliyopita kwamba, badala ya Mahakama kutegemea ukomo wa bajeti unaowekwa na Hazina, sheria ielekeze kama ilivyo kwa Bunge na Vyama vya Siasa vyenye uwakilishi Bungeni na nchi jirani ya Kenya kwamba, bajeti ya Mahakama ya kila mwaka isiwe pungufu ya asilimia tatu ya bajeti ya kila mwaka ya Serikali ili kuiwezesha Mahakama kuwa na uhakika wa fedha zake na kuiwezesha kupanga mipango yake kwa uhakika zaidi.

Pendekezo letu lilikataliwa na limeendelea kukataliwa na Serikali hii sikivu ya CCM. Matatizo ya bajeti ya Mahakama ambayo tumeyaeleza hapa na ambayo tumeyaeleza kwenye Maoni yetu ya kila mwaka, yanathibitisha wazi kwamba, utaratibu wa sasa wa kutegemea mgawo wa Hazina hauwezi kutatua matatizo ya fedha ya Mahakama ya Tanzania.

Kwa mara nyingine tena, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli Bungeni ni kwa nini inakataa kuihakikishia Mahakama fedha zake kwa kurekebisha Sheria ya Uendeshaji Mahakama ili kuweka *a minimum percentage* ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya Mahakama kama ilivyofanya kwa Bunge na kwa Vyama vya Siasa.

Mheshimiwa Spika, hali ya haki za binadamu katika nchi yetu inatisha. Mauaji na mashambulio dhidi ya Viongozi wa Kidini na Waumini wao na sehemu zao za ibada yaliyotokea kati ya mwaka 2012 na 2013 hayajatatuliwa hadi leo. Hakuna mtu yeyote ambaye ameadhibiwa kwa mauaji ya padri mmoja wa Kanisa Katoliki Zanzibar. Hakuna aliyeadhibiwa kwa shambulio la risasi na la tindikali dhidi ya Mapadri wengine wawili wa Kanisa hilo huko huko Zanzibar, wala kwa shambulio la tindikali dhidi ya Msaidizi wa Mufti wa Zanzibar.

Hakuna aliyetiwa hatiani wala kuadhibiwa kwa kuhusika na shambulio la bomu katika Kanisa Katoliki Olasiti Arusha lililoua watu watatu na kujeruhi wengine wengi. Serikali ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni juu ya wahusika wa mauaji na

mashambulio hayo na sababu zake. Hakuna mtu aliyepatikana na hatia ama kuadhibiwa kwa kuhusika na mauaji na mashambulio hayo hadi sasa.

Mauaji na mashambulio ya waandishi wa habari na wanaharakati wengine kama madaktari yaliyotokea kati ya 2012 na 2013 hayajatatuliwa. Pia Maafisa wa Jeshi la Polisi walioamuru mauaji ya mwandishi wa habari Daudi Mwangosi, hawajachukuliwa hatua yoyote. Badala yake, aliyekuwa Kamanda wa Polisi amepandishwa cheo na kuhamishiwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi. Huu ni ushahidi wa wazi kabisa kwamba, mauaji hayo yalipangwa na/au yalifanywa kwa maelekezo ya Serikali ya CCM.

Maafisa wa Idara ya Usalama wa Taifa na wa Jeshi la Polisi waliohusika kumteka nyara na kumtesa Mwenyekiti wa Chama cha Madaktari Tanzania, Dkt. Steven Ulimboka hawajakamatwa hadi leo licha ya majina yao kujulikana. Raia wa Kenya aliyebambikiziwa kesi ya kumteka Dkt. Ulimboka amekwishaachiliwa huru na mahakama. Serikali ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni kuhusu jambo hili. Huu ni ushahidi wa kuhusika kwa Serikali ya CCM katika shambulio hilo. Hakuna aliyekamatwa wala kuadhibiwa kwa kumteka nyara na kumtesa aliyekuwa Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri, Absalom Kibanda. Serikali ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi hadharani au Bungeni kuhusu shambulio hilo linalofanana na shambulio dhidi ya Dkt. Ulimboka. Serikali hii ya CCM ina wajibu kisheria na kisiasa wa kulinda maisha ya Watanzania na mali zao. Imeshindwa kutekeleza wajibu huo kwa Watanzania.

Serikali ya CCM imeitia demokrasia kitanzini na inatishia kuinyonga na kuiua. Mikutano halali ya Vyama vya Siasa vya Upinzani imeshambuliwa kwa mabomu na risasi za moto na Jeshi la Polisi. Watu wengi wameuawa katika mashambulizi hayo na wengine wengi wamejeruhiwa. Viongozi, Wanachama na hata wapita njia tu wamepigwa, kukamatwa na kufunguliwa mashtaka ya jinai kwa kushiriki mikutano halali ya Vyama vya Siasa vya Upinzani.

Jeshi la Polisi likishirikiana na Watumishi wa Idara ya Usalama wa Taifa na Viongozi na Makada wa CCM, wameshirikiana kuwabambikizia Viongozi na Wanachama wa CHADEMA kesi za uongo za ugaidi. Wengi wameteswa kwa ukatili mkubwa baada ya kukamatwa na kuhojiwa katika Vituo vya Polisi katika kesi hizi. Hadi sasa Serikali hii ya CCM haijasema chochote juu ya kufutwa kwa kesi za uongo za ugaidi walizofunguliwa Viongozi na Wanachama wa CHADEMA kama vile Wilfred Lwakatare na Henry Kilewo. Walioshiriki kutunga mashtaka hayo ya kidhalimu hawajachukuliwa hatua yoyote.

Serikali ya CCM imewageuka Watanzania walioipigia kura na kuwaua, kuwatesa na kuwatia vilema vya maisha, kuwabaka, kuwafukuza kwenye maeneo yao na kuwafanya wakimbizi wa ndani au *internally displaced persons (IDPs)*. Badala ya kulinda mali zao, Serikali ya CCM imekuwa mwizi wa mali za Wananchi. Serikali ya CCM imeendesha Operesheni Kimbunga kwa kisingizio cha kuondoa wahamiaji haramu nchini. Matokeo ya Operesheni hiyo ni kwamba, maelfu ya watu wasiokuwa na hatia wa Mikoa ya Kagera na Kigoma, inayopakana na Burundi na Rwanda, walikamatwa, kuteswa na kuporwa mifugo, fedha na mali zao nyingine na makazi yao kuharibiwa.

Utaratibu wa kisheria wa kuwakamata watuhumiwa, kuwapeleka mahakamani, kuwapata na hatia na kuwaadhibu kwa mujibu wa sheria umepuuzwa. Cha kushangaza, Operesheni Kimbunga haikuihusu Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Mara, Mbeya, Mtwara, Rukwa na Ruvuma ambayo inapakana na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Kenya, Malawi, Msumbiji na Zambia ambayo nayo pengine ina wahamiaji haramu. Katika mazingira haya, ni sahihi kuamini kwamba, Operesheni Kimbunga ilikuwa ni lengo la kuwaadhibu watu wenye asili ya Rwanda kwa sababu ya mgogoro wa kidiplomasia kati ya Rais Jakaya Kikwete na Rais Paul Kagame wa Rwanda.

Hata kabla vumbi lililotimuliwa na Operesheni Kimbunga halijatulia, Serikali ya CCM ilianzisha vita nyingine kubwa dhidi ya Watanzania; hii ni Operesheni Tokomeza Ujangili. Licha ya jina lake, Operesheni hiyo imetokomeza maisha ya Watanzania wasiokuwa na hatia yoyote. Makumi ya watu wameuawa, mamia wamejeruhiwa, maelfu wamekamatwa na kuteswa, vijiji vizima vimechomwa moto na makazi ya Wananchi kuharibiwa, mifugo imeuawa ama kuporwa kwa mtutu wa bunduki, mashamba na mazao yameharibiwa na maelfu ya Wananchi wametiwa umaskini mkubwa na Serikali hii ya CCM.

Hatimaye, baada ya kelele kubwa ndani na nje ya Bunge, Operesheni Tokomeza ilisitishwa na Mawaziri wa Ulinzi, Mambo ya Ndani, Maliasili na Utalii na Mifugo wakaondoshwa madarakani kwa sababu ya Operesheni hiyo. Walioua, kutesa na kulemaza Watanzania na kuwaibia au kuharibu mali zao hawajakamatwa wala kuchukuliwa hatua zozote za kisheria.

Operesheni Kimbunga na Tokomeza zilikuwa Operesheni za Kijeshi. Zilianzishwa, kuongozwa na kutekelezwa na Maafisa na Askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na vikosi vingine vya ulinzi na usalama. Operesheni hizi za kijeshi zimefanyika wakati Tanzania haiko vitani na wala haiko katika hali ya vita. Rais Kikwete hakutangaza vita wala kuwepo kwa hali ya vita kwa mujibu wa Katiba ili kuweza kuamuru kutekelezwa kwa Operesheni hizi za kijeshi.
Hakukuwa na maasi au vurugu zozote zozote za kijamii. Kwa sababu hiyo, hakuna Mkuu wa Mkoa yeyote aliyeomba msaada wa kijeshi ili kuwezesha matumizi ya Majeshi ya Ulinzi katika kusaidia mamlaka za kiraia kama inavyotakiwa na Sheria ya Ulinzi wa Taifa, 1970 na Kanuni zake. Kwa kila namna inavyoonekana, Operesheni Kimbunga na Operesheni Tokomeza zilikuwa ni matumizi haramu ya nguvu za kijeshi dhidi ya raia. Kama hii haitoshi, sasa Serikali hii ya CCM inazungumza kuianzisha tena Operesheni hii dhidi ya Wananchi wa Tanzania!

Mheshimiwa Spika, Tume ya Uchunguzi iliyoahidiwa Bungeni na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuchunguza masuala yanayohusu ukiukwaji huu wa haki za binadamu, imeundwa na Rais kupitia Tangazo la Serikali Na. 131 la tarehe 2 Mei, 2014. Tume hiyo inaongozwa na Jaji Kiongozi Mstaafu Hamisi Amir Msumi na Makamishna wenzake, Majaji wastaafu Stephen Ihema na Vincent Kitubio Damian Lyimo.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu na kutambua utumishi uliotukuka wa Jaji Kiongozi Msumi. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina imani kabisa na uteuzi wa Makamishna Ihema na Lyimo. Itakumbukwa kwamba, tarehe 13 Julai, 2012, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ililalamikia uteuzi wa Majaji wa Mahakama Kuu wakiwa wamekaribia muda wao wa kustaafu kwingineko katika utumishi wa umma (na) wanapewa zawadi ya Ujaji kuwawezesha kupata mafao ya Majaji wastaafu ambayo yameboreshwa sana katika miaka ya karibuni.

Ushahidi tuliouwasilisha mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge baada ya Msemaji wa Kambi kushtakiwa kwenye Kamati hiyo kwa kile kilichoitwa kuwadhalilisha Majaji, uliwahusisha Majaji Wastaafu Ihema na Lyimo katika kundi la Majaji ambao uteuzi wao tuliupigia kelele. Sehemu ya ushahidi huo inaonesha kwamba, tarehe 16 Juni, 2003, aliyekuwa Mwenyekiti CCM wa Mkoa wa Singida, Mzee Joram Allute, alimwandikia Rais Benjamin Mkapa, maombi ya kumwondoa Jaji Ihema kama Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania kwa uzembe na kukosa maadili. Mzee Allute alikuwa na kesi kwa Jaji Ihema ambapo Jaji huyo alikalia uamuzi kwa zaidi ya miaka minne hadi aliponyang'anywa faili la kesi hiyo na kukabidhiwa Jaji mwingine aliyeandika uamuzi huo ndani ya wiki tatu!

Mwezi mmoja kabla ya barua ya Mzee Allute kwa Rais Mkapa, Mawakili wake walikuwa wamemwandikia Jaji Mkuu Barnabas Samatta kulalamikia ucheleweshaji wa uamuzi wa kesi

hiyo. Mawakili hao walidai hadhi na heshima ya Mahakama inaporomoka vibaya kama inachukua zaidi ya miaka mitatu kwa Jaji kutafakari na kutoa uamuzi kwa jambo jepesi kama maombi ya pingamizi.

Mheshimiwa Spika, siyo tu kwamba, Jaji Mstaafu Ihema ana rekodi mbaya ya kijaji, bali pia ana rekodi ya kutumiwa na Serikali hii ya CCM kuisafisha Serikali kwa matukio ya ukiukwaji wa haki za binadamu unaofanywa na Watendaji wa Serikali. Mwaka 2012, mara baada ya Jeshi la Polisi Mkoani Iringa kumuua Daudi Mwangosi, aliyekuwa Mwandishi wa Habari wa Kituo cha Televisheni cha Channel Ten, aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, alimteua Jaji Ihema kuongoza Kamati iliyoundwa na Waziri Nchimbi kuchunguza mauaji ya Marehemu Mwangosi. Taarifa ya Uchunguzi wa Kifo cha Mwandishi wa Habari wa Channel Ten Bw. Daudi Mwangosi, iliyoandaliwa na Kamati ya Jaji Ihema ni mfano wa namna ya kuisafisha Serikali kutoka kwenye lawama ya mauaji ya raia wake.

Taarifa hiyo ilitofautiana kimsingi na Taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya Uchunguzi wa Tukio Lililopelekea Kifo cha Daudi Mwangosi Kilichotokea Septemba 2, 2012 Kijijini Nyololo, iliyoandaliwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora; na *Ripoti ya* Timu Maalum ya Uchunguzi Iliyoteuliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) Kuchunguza Mazingira Yaliyopelekea Kuuawa kwa Mwandishi wa Habari Daudi Mwangosi Septemba 2, 2012 Katika Kijiji cha Nyololo, Wilaya ya Mufindi, Mkoani Iringa, iliyotolewa na Baraza la Habari Tanzania *(MCT)* na Jukwaa la Wahariri Tanzania *(TEF)*.

Kwa upande wake, Jaji Lyimo aliteuliwa tarehe 28 Machi, 2007, mwaka mmoja kabla ya muda wake wa kustaafu kwa mujibu wa sheria. Hata hivyo, ilipofika tarehe 26 Oktoba, 2007, Katibu Mkuu Kiongozi wa wakati huo Phillemon Luhanjo, alimtaarifu Jaji Mkuu kwamba, Rais Kikwete ameamua kusogeza mbele muda wa kustaafu wa Mheshimiwa Jaji Vincent Kitubio Damian Lyimo kwa miaka mitatu kuanzia tarehe 28 Machi, 2008, siku ambayo angestaafu kwa lazima.

Uteuzi wa Majaji hawa na wengineo wenye sifa kama hizo, ulilalamikiwa mno na Majaji wengine kiasi kwamba, Kikundi Kazi kwa Ajili ya Kuchambua na Kushauri Kuhusu Ajira ya Majaji Baada ya Kustaafu chini ya Ofisi ya Rais, kilihitimisha katika Taarifa yake tarehe 7 Machi, 2008, inaonekana wazi kuwa suala la ajira za mikataba kwa Majaji ambao wamekuwa wakifanya kazi za Jaji baada ya kufikia umri wa kustaafu ni kinyume cha Katiba.

Sasa Majaji hawa ndiyo wamepewa jukumu la kuchunguza matukio ya ukiukwaji haki za binadamu ambayo hayana mfano katika historia ya Tanzania tangu Uhuru. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni haina imani yoyote na uteuzi wa Majaji Ihema na Lyimo na inapendekeza uteuzi wao ufutwe na Majaji wenye sifa bora zaidi wateuliwe kwa ajili ya kazi hii muhimu. Vinginevyo, matokeo ya Tume ya Msumi hayatakubaliwa na Umma wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mamlaka ya uendeshaji wa mashtaka ya jinai yamekasimiwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa mujibu wa Ibara ya 59B(2) ya Katiba. Mamlaka haya yamefafanuliwa na kutiliwa nguvu na kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa, Na. 27 ya 2008 (*National Prosecutions Service Act, 2008*). Kwa mujibu wa kifungu hicho, Mkurugenzi wa Mashtaka ana mamlaka siyo tu ya kudhibiti mashtaka yote ya jinai, bali pia kuratibu shughuli za upelelezi wa makosa ya jinai. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 17(1) na (3), Mkurugenzi ana uwezo wa kutoa maelekezo ya maandishi kwa Ofisa yeyote wa Umma ili apatiwe taarifa yoyote inayohusu upelelezi au uendeshaji wa mashtaka ya jinai na Ofisa huyo anatakiwa kutii maelekezo hayo.

Ili kumwezesha Mkurugenzi wa Mashtaka kutekeleza wajibu wake wa kikatiba kwa uhuru kamili na bila woga au upendeleo, Mkurugenzi wa Mashtaka amewekewa kinga ya ajira yake. Hivyo, kwa mfano, Ibara ya 59B(4) ya Katiba inaelekeza kwamba, katika kutekeleza mamlaka yake, "Mkurugenzi wa Mashtaka atakuwa huru, hataingiliwa na mtu yeyote au mamlaka yoyote na atazingatia nia ya kutenda haki, kuzuia matumizi mabaya ya taratibu za utoaji haki na masilahi ya umma. Aidha, kwa mujibu wa kifungu cha 19(1) na (2) cha Sheria ya Utumishi wa Mashtaka ya Taifa, sifa, masharti na mafao ya ajira ya Mkurugenzi wa Mashtaka yatakuwa sawa na yale ya ajira ya Jaji wa Mahakama Kuu. Vilevile, kufuatana na kifungu cha 19(3), Mkurugenzi wa Mashtaka hawezi kuondolewa kwenye madaraka yake isipokuwa kwa kushindwa kutimiza wajibu wake kwa sababu ya ugonjwa au kwa kukiuka Kanuni za Maadili ya Kitaaluma chini ya Sheria ya Utekelezaji wa Mamlaka ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 ya Sheria za Tanzania. Hii ndiyo kusema kwamba, kwa mujibu wa Sheria Na. 27 ya 2008, utaratibu wa kumwondoa Mkurugenzi wa Mashtaka kwenye ajira yake hauna tofauti na utaratibu wa kumwondoa Jaji wa Mahakama Kuu kwenye ajira yake.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, utaratibu huu wa kikatiba na kisheria umempa Mkurugenzi wa Mashtaka nyenzo za kutosha kisheria za kupambana na uhalifu mkubwa hapa nchini na vilevile kuzuia matumizi mabaya ya mfumo wa uendeshaji na utoaji haki na hasa hasa ya mfumo wa mashtaka ya jinai. Hata hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashangazwa na kusikitishwa na kushindwa kwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kufungua na/au kuendesha mashtaka yanayohusu matukio makubwa ya uhalifu ambayo yametikisa Taifa letu katika mwaka huu wa fedha na kabla ya hapo.

Tarehe 16 Juni, 2013, mkutano wa hadhara wa kampeni za uchaguzi wa madiwani uliokuwa unafanywa na Viongozi Wakuu wa CHADEMA katika eneo la Soweto Mjini Arusha, ulishambuliwa kwa mabomu na risasi za moto. Watu watatu waliuawa pale pale na mwingine alifia hospitalini baadaye. Wengine wengi walijeruhiwa vibaya. Hadi sasa Serikali hii ya CCM haijatoa taarifa yoyote rasmi, ndani ya Bunge hili au nje, juu ya waliohusika na mashambulizi haya ya kigaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kufahamu hatua zozote, kama zipo, zilizochukuliwa na Mkurugenzi wa Mashtaka kuchunguza tukio hilo la kigaidi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua matokeo yoyote, kama yapo, ya uchunguzi wa tukio hilo.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo linahitaji majibu linahusu utekelezaji wa maelekezo ya Mahakama Kuu ya Tanzania juu ya marekebisho ya sheria ambazo Mahakama Kuu imetamka kwamba zinakiuka Katiba. Kama tulivyosema katika Maoni yetu miaka miwili iliyopita, mfumo wa dhamana chini ya kifungu cha 148(5)(a) cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai ambao unakataza dhamana kwa idadi kubwa ya watuhumiwa wa makosa yaliyotajwa katika aya (e) ndiyo sababu kubwa ya magereza kufurika mahabusu na mlundikano wa kesi za jinai kwa ujumla. Kwa sababu hiyo, Mahakama Kuu ilitamka, katika kesi ya *Jackson s/o ole Nemeteni @ ole Saibul @ Mdosi @ Mjomba na wenzake 19 dhidi ya Mwanasheria Mkuu, Shauri la Madai Na. 117 la 2004*, kwamba bila kuwepo utaratibu uliowekwa na sheria kama inavyoelekezwa na Ibara ya 15(2)(a) ya Katiba, utekelezaji wa masharti ya kifungu cha 148(5)(a) umetumiwa vibaya. Kwa sababu hiyo, Mahakama Kuu ilitamka kwamba, kifungu hicho kinachokataza dhamana kwa watuhumiwa wa makosa ya wizi wa kutumia silaha ni kinyume cha Ibara ya 15(2)(a) ya Katiba.

Kuhusiana na kifungu cha 148(5)(e) cha Sheria ya Mwenendo wa Jinai kinachoweka masharti ya dhamana yasiyotekelezeka kwa watuhumiwa wa makosa ya uhujumu uchumi, Mahakama Kuu katika kesi ya Prof. Dkt. Costa Ricky Mahalu & Mwenzake dhidi ya Mwanasheria Mkuu, Shauri la Maombi Na. 35 la 2007, ilitamka kwamba, kifungu hicho ni cha kibaguzi kwa

watuhumiwa maskini na kinakiuka matakwa ya Ibara ya 13(2) ya Katiba inayokataza ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira.

Kwa kutumia mamlaka yake chini ya ibara ya 30(5) ya Katiba, badala ya kukifuta kifungu hicho, Mahakama Kuu katika kesi zote mbili iliielekeza Serikali ifanye marekebisho katika kifungu cha 148(5)(a) na (e) vya Sheria ya Mwenendo wa Jinai ili kuweka utaratibu bora zaidi wa kushughulikia dhamana za watuhumiwa wa makosa ya wizi wa kutumia silaha na wa uhujumu uchumi. Katika Kesi ya Jackson s/o ole Nemeteni, Mahakama Kuu ilitoa muda wa miezi kumi na nane kuanzia tarehe 13 Julai, 2007. Katika Kesi ya Prof. Dkt. Costa Ricky Mahalu, Mahakama Kuu ilitoa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe 4 Oktoba, 2010. Hii ina maana kwamba, Serikali ilitakiwa iwe imetekeleza maelekezo ya Mahakama Kuu juu ya kifungu cha 148(5)(a) kufikia tarehe 12 Desemba, 2008. Aidha, Serikali ilitakiwa kutekeleza maelekezo ya Mahakama Kuu kuhusu kifungu cha 148(5)(e) kufikia tarehe 3 Oktoba, 2011.

Huu ni mwaka wa tano na nusu tangu kwisha kwa muda uliowekwa katika Kesi ya Jackson s/o ole Nemeteni lakini Serikali haijafanya marekebisho tajwa ya Sheria ya Mwenendo wa Jinai. Aidha, huu ni karibu mwaka wa tatu tangu muda uliowekwa katika Kesi ya Prof. Dkt. Costa Ricky Mahalu lakini Serikali haijatekeleza maelekezo hayo.

Kuhusiana na utekelezaji wa maelekezo ya Mahakama Kuu katika Kesi ya Prof. Dkt. Costa Ricky Mahalu, Mwanasheria Mkuu ametoa maelezo kwamba, Serikali haikuridhika na uamuzi huo na hivyo iliamua kukata rufaa katika Mahakama ya Rufani kwa kutoa notisi ili kupinga uamuzi huo. Mwanasheria Mkuu ameeleza kwamba, marekebisho ya kifungu hicho hayajafanywa kwa kuwa rufaa dhidi ya uamuzi huo haijasikilizwa.

Mheshimiwa Spika, Mwanasheria Mkuu hajasema ni lini Serikali ilitoa notisi ya rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu. Aidha, Mwanasheria Mkuu hajasema kama tayari Serikali imeshakata rufaa hiyo, ijapokuwa maelezo yake yanaashiria kwamba, rufaa hiyo bado haijawasilishwa kwenye Mahakama ya Rufani. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba, Serikali hii ya CCM inaweza kuwa inatumia vibaya masharti ya kifungu cha 14(3) cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki za Binadamu, Sura ya 3 ya Sheria za Tanzania, yaani The Basic Rights and Duties Enforcement Act, Chapter 3 of the Laws of Tanzania. Kifungu hicho kinazuia utekelezaji wa uamuzi wowote wa Mahakama Kuu pale ambapo Serikali imewasilisha notisi ya rufaa yenye kuonesha nia ya kupinga uamuzi husika.

Kwa kutumia kifungu hicho, Serikali inaweza kuzuia uamuzi huo kwa kutoa notisi ya rufaa tu bila kulazimika kukata rufaa yenyewe na utaratibu mzima wa kurekebisha sheria mbovu na za kikandamizaji kwa kutumia Mahakama ukasitishwa. Kwa sababu hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM itoe nakala ya notisi ya rufaa iliyoiwasilisha katika Mahakama ya Rufani katika Kesi ya Prof. Dkt. Costa Ricky Mahalu. Hii ni muhimu ili kuhakikisha kwamba, taarifa ya Mwanasheria Mkuu ni ya kweli. Aidha, kama itathibitika kuwapo kwa notisi hiyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali hii ya CCM kutoa kauli rasmi mbele ya Bunge hili Tukufu ni lini inatazamia kuwasilisha rufaa ambayo tayari imekwishaitolea notisi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na Kesi ya Jackson s/o ole Nemeteni, Serikali haijatoa maelezo yoyote kwa nini haijatekeleza maelekezo ya kikatiba ya Mahakama Kuu kwa karibu miaka sita. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali itoe kauli rasmi kama na lini, inatarajia kutekeleza maelekezo hayo ya Mahakama Kuu. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji kama hii siyo dharau ya Serikali hii ya CCM kwa Mahakama ya Tanzania ni kitu gani?

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha maoni haya, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Viongozi Wakuu wa Vyama vyetu vitatu vinavyounda Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa kufanya maamuzi ya kuendeleza ushirikiano ulioanzia ndani ya

Bunge Maalum, kwenye Bunge lako Tukufu. Kwa sababu ya maamuzi hayo, imewezekana kwa Naibu Waziri Kivuli wa Sheria na Katiba, Mheshimiwa Rashid Ali Abdallah, kushirikiana nami katika kuandaa na kuwasilisha Maoni haya. Naomba nitumie fursa hii, kumpongeza Mheshimiwa Rashid Abdallah, kwa kuteuliwa kwenye nafasi hiyo na kumshukuru kwa ushirikiano wake katika kuandaa Maoni haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya marefu, naomba kukushukuru na wewe binafsi na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitawaita wachangiaji wafuatao; yupo Mheshimiwa William Ngeleja, halafu Fakharia Shomar na Mheshimiwa Raya, tufike hapa kwanza.

Mheshimiwa Ngeleja!

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia fursa hii na kwa heshima hii, ninaomba kusema yafuatayo kuhusu bajeti iliyoko mbele yetu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, kama ambavyo imejitokeza kwenye taarifa na ni taarifa za pande zote mbili, upande wa Serikali lakini pia kwa TAARIFA za Kamati; wote tunakubaliana kwamba, Wizara hii ya Katiba na Sheria ni mhimili muhimu sana katika uendeshaji wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa katika taarifa zetu na uzoefu unaonesha kwamba, bila kuwepo kwa utawala bora ambapo utawala wa Sheria ni sehemu ya utawala bora, nchi haiwezi kutulia na haiwezi kuwa na amani. Sasa tunachokisema hapa ni kusisitiza tu kuhusu ugawaji wa rasilimali fedha, kuwezesha Wizara hii ya Katiba na Sheria pamoja na Taasisi zake ziweze kupata mafungu yanayowezesha kutekeleza wajibu wake; kwa sababu kinyume chake itakuwa ni tatizo kwa Taifa letu.

Sasa tunaona kuna mambo makubwa yanayoendelea ikiwemo hii migogoro ya ardhi ambayo inaendelea katika maeneo mbalimbali. Kwa kiasi kikubwa, wasimamizi wa shughuli hizi ni Wizara ya Katiba na Sheria. Sasa ombi langu, tunatambua ufinyu bajeti, *ceiling* tunazo, lakini ni muhimu sana kuzingatia utoaji rasilimali fedha kwa Wizara hii. Tunafahamu kwamba Wizara hii haimo katika ule Mpango wa *BRN,* lakini bajeti yao siyo kubwa kihivyo na mtu angesema unadhani fedha zingetoka wapi? Kamati ya Bajeti itusaidie sana kutoa mafungu yanayohitajika kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

La pili, ninalotaka kulisema sasa kwa sababu lilikuwa la jumla ni kuhusu Taasisi zilizokuwa chini ya Wizara hii. Moja ni ile Kurugenzi ya Mashitaka. Tatizo ni kubwa, mwaka jana tumejadili, tumekubaliana Taasisi hii iwezeshwe ipate watumishi wengine zaidi ya 489. Ninafahamu kwamba, kuna changamoto mbalimbali katika upande wa Serikali; lakini kama tunavyosema, tusipowawezesha hawa haki za watu hazitopatikana na matokeo yake nchi hii haitatawalika. Kwa hiyo, ninachosisitiza tuangalie sana vibali tutoe lakini pia uimarishaji wa bajeti. Katika taarifa yetu tumesema na mimi kwa sababu naunga mkono hoja hii iliyokuwa mbele yetu, tumesikia habari nzuri ambazo zimesemwa kuhusu utendaji wa baadhi ya Taasisi zilizoko chini ya Wizara hii. *(Makofi)*

Nataka nisemee moja kwa sababu ya ufinyu wa muda, Taarifa yetu imejieleza kwa mambo mengi mazuri na sisi ambao tumebahatika kukaa na hizi Taasisi na Wizara kwa ujumla, tunafahamu kazi kubwa wanayofanya, lakini siyo rahisi kwa dakika saba kusema yote.

Nataka kuzungumzia habari ya Mahakama. Mahakama wanafanya kazi kubwa sana na tunampongeza kwa nafasi hii Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania pamoja na Taasisi yake na Mtendaji Mkuu, Bwana Katanga. Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana kwa usimamizi wa Taasisi zako wewe na Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu inafanya kazi kubwa, lakini wakati mwingine katika mazingira magumu. Sasa nataka kusemea uwezeshaji wa Mhimili huu wa Mahakama. Inaonesha Mhimili huu pamoja na kwamba, tunatambua Mahakama ni Mhimili unaojitegemea na unahitaji kutendewa kama inavyotendewa Mihimili mingine, lakini bado kuna changamoto katika rasilimali fedha.

Nilichokuwa naomba, ombi letu ambalo tumeweka kwenye Kamati yetu, kwa rasilimali zinazotolewa hasa rasilimali fedha, Mhimili huu uwezeshwe. Fedha zake kwa vyovyote itakayotengwa, isiguswe na isitendewe kama ambavyo imejitokeza wakati mwingine, fedha inayotengwa upande wa Mahakama inatumika kama *OC*. Sasa hii si haki, wengine wanaweza wakadhani kwa sababu sasa tuna mchakato wa Katiba pengine haya mambo tutayaweka sawa wakati wa mjadala wa Katiba mpya, lakini tunasema, kwa sababu maisha hayasubiri ukamilishwaji wa Katiba mpya, sisi kwa bajeti hii tuanze kuhakikisha kwamba fedha tunazozitenga tunaziwekea wigo kama tulivyopendekeza kwenye Kamati zisiguswe.

Katika mtiririko wa *allocation,* fedha ziwafikie hawa walengwa na ziwafikie kwa wakati unaohitajika. Tuna tatizo kubwa, kwa sababu ya kutokuwa na utaratibu mzuri, mwaka jana tumepitisha makadirio kwa mpango wa maendeleo, kwa huu Mhimili wa Mahakama shilingi bilioni 42, lakini zilizowafikia mpaka sasa hivi ni bilioni tano tu.

Sasa migogoro yote hii hawa ndiyo wasimamizi; tunafanyaje katika mazingira haya? Naomba sana huu ushauri wa kuwatengea fedha na kuziwekea wigo zisiguswe, tuutekeleze kuanzia sasa ili waendelee kutekeleza majukumu yao.

Lingine ambalo nataka kulisema, kwenye utaratibu wao waliojiwekea wa *BRN,* ku-*fast track* kesi, mashauri mbalimbali yaliyoko Mahakamani. Kwa kweli Mahakama wanahitaji kuungwa mkono kwa kila namna kwa sababu wamefanya kazi kubwa na wakati mwingine katika mazingira magumu kama nilivyosema.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwa sababu nimesikia kengele ya kwanza inatuarifu; nilikuwa napitia hapa na kwa sababu wenzetu wametumia, siwezi kusema ujanja kwa sababu neno hili linaudhi; Taarifa hii imetufikia wakati mjadala unaanza. Taarifa hii ya wenzetu wa Kambi ya Upinzani ina kurasa 24, lakini ukiziangalia zaidi ya asilimia 70 ya hii Taarifa ni malalamiko.

Sasa wote tunafahamu kwamba, jambo hili, kuwepo kwa taarifa hizo za upande wa pili maana yake ni kwamba, ni kuwa na mawazo mbadala. Watanzania wanasikia wataendelea kuyachambua, tunafahamu kwamba Serikali haiwezi kuyafanya yote kwa pamoja na tunafahamu upungufu uliopo. Sisi kwa pamoja tunaendelea kuishauri Serikali itemize wajibu wake, lakini itimize kwa kadiri ambavyo mambo yanawezekana.

Taarifa hii imejaa malalamiko, haitoi mawazo mbadala nini tufanye sasa, zaidi ya yale ambayo wanalalamikia. Ninaomba niseme kwamba, katika siasa ni kama vita na kwa sababu ni kama vita, wakati wote wanapopata nafasi wapiganaji wataitumia. Sisi tunafahamu dunia nzima, upande wowote ambao haupo Serikalini ni rahisi sana kui- *challenge* Serikali.

Leo ukienda Marekani pamoja na kwamba, tunaambiwa uchumi umeanza kukua na taarifa zipo hivyo, lakini ambao hawapo Serikalini, *Republicans* sasa hivi wanapiga kelele.

Hawakubali pamoja na kwamba Wananchi wanaelewa, lakini wakipata fursa kwa kutumia majukwaa kama haya wanalalamika.

Naomba wenzetu muendelee kutafakari, tunafahamu Baraza la Mawaziri la Upinzani hivi karibuni limefanyiwa marekebisho, endeleeni kujipanga vizuri, muisaidie Serikali nini kifanyike badala ya kulalamika tu hapa bila kutoa mawazo mbadala kama ambavyo inakusudiwa kutoka kwenye kanuni zetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba wenzangu pia tuendelee kuiunga mkono hoja ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Halima Mdee!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Kwanza, Mheshimiwa Ngeleja ukisaidiwa fikra asilimia 30 inabidi ushukuru na hizo 70 lazima tuziseme kwa sababu nchi inaelekea kuwashinda, matatizo yamekuwa ni mengi kuliko faraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, nataka Waziri wa Sheria anijibu na ninashukuru Naibu wake alikuwepo kipindi kirefu, ni muda mrefu sana Wizara hii imekuwa ikilidanganya hili Bunge kuhusiana na ujenzi wa Mahakama, hususan Mahakama ya Jimbo la Kawe. Ninaomba nipate majibu kuhusiana na hiyo Mahakama. Pili, hii Wizara ndiyo inasimamia mchakato wa Katiba kuanzia hatua za awali. Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ya Mwaka 2011 ililetwa na Wizara hii kupitia Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Inasikitisha kwamba ni Wizara hii hii ambayo imekuwa inaongoza katika kusigina utekelezaji wa Sheria mabadiliko hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge Maalum la Katiba tumeshuhudia ni kwa namna gani Wizara hii kupitia Mawaziri wake, wamekuwa makuwadi wa kuivunja ile Sheria. Sheria iko wazi, inaeleza michakato mine; inaeleza mchakato wa kwanza wa maoni, inaeleza mchakato wa pili wa Mabaraza, inaeleza mchakato wa tatu wa Bunge Maalum la Katiba na inaeleza mchakato wa nne wa Kura ya Maoni.

Mheshimiwa Spika, masikitiko yangu, chini ya Uongozi wa Viongozi hawa wawili hapa mbele, Bunge Maalum la Katiba likajigeuza sehemu ya kutoa maoni upya. Spika, ulikuwepo, Sheria hii inavunjwa, badala ya Bunge litekeleze wajibu wake wa kujadili na kuboresha na kupitisha, likaanza kufanya utaratibu mpya wa maoni, kinyume na hii sheria. Bunge akiwepo Waziri Mkuu, akiwepo Mwanasheria Mkuu, wanazungumzia Mabaraza kwamba, Sheria hii imeipa mamlaka Mabaraza kubadilisha kabisa maoni ambayo yametolewa na Wananchi; kitu ambacho ni kinyume na sheria hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume imetumia zaidi ya shilingi bilioni 70 …

**SPIKA:** Mimi siyo Mwenyekiti ni Spika.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, napata mzuka.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu sisi inaisimamia Tume ya Warioba. Tume ya Warioba imetumia zaidi ya shilingi bilioni 70. Bunge Maalum la Katiba tunaambiwa limetumia shilingi bilioni 24 na huku kuna shilingi bilioni 27. Hapa kuna utata ambao tunataka mtujibu! Fedha

nyingi zinatumika, tunaenda kufanya kazi ya kisanii kwenye Bunge Maalum la Katiba wakati Sheria imeeleza wazi.

Mheshimiwa Spika, nataka leo Mwanasheria Mkuu wa Serikali atueleze hii Sheria, nafasi ya kifungu cha tisa ilikuwa ni nini? Nafasi ya kifungu cha 18 ilikuwa ni nini? Nafasi ya kifungu cha 25 ilikuwa ni nini? Na nafasi ya kifungu cha 28(b) ni nini? Ninasema hivyo kwa nini?

Mheshimiwa Spika, haiwezekani mfanye usanii wa kuturudisha kwenye Katiba iliyopo sasa, wakati Katiba ya mwaka 1977 inaturuhusu kama tunataka kufanya mabadiliko, tufanye chini ya kifungu cha 98 cha Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasikia Mheshimiwa Rais ameongeza siku 60. Hizi siku 60 kama watu wanaenda kuvunjavunja misingi ya Rasimu ya Pili ya Katiba, misingi ambayo ni chimbuko la maoni ya Wananchi, huo ni usanii na uharibifu wa hela. Mimi sitarajii kabisa kwamba, kuna watu na akili zao timamu, wataenda kwenye lile Bunge wakati Sheria hii imevunjwa, wakati wanajua wanaenda kuvunja ile misingi. Kama dhamira ingekuwa Bunge Maalum ndiyo tutunge, tungeweza tusianzishe mchakato wa Wananchi, tusianzishe mchakato wa Mabaraza, tukaamua sisi wenyewe ndiyo tufanye kila kitu kwa kadiri ambavyo tungetaka. *As long as* kuna hatua nne zilizotambuliwa kisheria, hatua zote nne ni lazima ziheshimiwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi kuhoji uhalali wa hatua ya kwanza, ukahoji uhalali wa hatua ya pili, halafu eti ninyi Makada wa CCM asilimia 95 mmejikusanya huku, mjione ndiyo mna mamlaka ya kubadilisha yale yote yaliyomo kwenye hatua mbili. Hili halikubaliki na tutapambana nje na ndani mpaka kieleweke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la *DPP; DPP* amekuwa akilalamikiwa sana; mbaya zaidi analalamikiwa pia na Afisa Mwandamizi wa Serikali, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, anasema linapokuja suala la kushughulikia rushwa kubwa kubwa, *DPP* amekuwa ni kikwazo. Juzi tuliambiwa hapa suala la *Escrow Account* milioni 200 mnapeleka TAKUKURU, mnapeleka CAG. TAKUKURU wamenukuliwa na Sheria ya 2007 iko wazi, inatamka bayana kwamba, hawezi kutaja wala rushwa wakubwa, mafisadi, haruhusiwi kuwataja kwa majina. Pili, akitaka kufungua shauri la rushwa kubwa kubwa mpaka akaombe kibali kwa *DPP.* Analalamika kwamba, *DPP* amekuwa akibania vibali kwa masilahi yake binafsi. Zaidi wanasema siku sitini zikipita ndiyo imetoka hiyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninatarajia kwamba, Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Waziri wakiwa wanatujibu, watuambie ni kwa kiwango gani Sheria ya TAKUKURU mwaka 2007, italetwa kwa ajili ya kuifanyia mabadiliko. Vilevile ni kwa kiwango gani hizi rushwa kubwa ambazo majalada yamekuwa yanapelekwa kule, *DPP* kwa masilahi yake anayaficha zitapelekwa mahakamani?

Tatu, limeulizwa suala la UDA leo, aliyekuwa mshtakiwa mkuu, aliyeisababishia UDA hasara kubwa …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Tumemaliza tayari, sasa ninamwita Mheshimiwa Ali Khamis Seif

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kunijalia kuwa hai na uzima huu kusimama katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, pili, nina ushauri kuhusiana na suala zima la upatikanaji wa Katiba Mpya. Ninavyoona mimi ni kuwa, utakapoondoka na Rasimu ambayo imeletwa na Tume ya Jaji Warioba, kwa maana ya kuwa tuwe na Muungano wa Serikali mbili, Bunge la Katiba litakuwa halina maana, hili ambalo tunaliita Bunge Maalum. Kwa sababu gani? Bunge lile lipo kwa sababu ya mambo ya Mungano na unapokuwa na Serikali mbili ina maana mambo ya Tanzania Bara, kwa lugha nyingine Tanganyika, yatakuwemo katika Katiba ile. Kwa hiyo, Bunge halali la kubadilisha mambo yale ni Bunge hili. Bunge Maalum la Katiba litakuwa halistahili. Huo ni ushauri.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara ambayo inategemewa kuwapatia Wananchi haki sawa tena kwa wakati. Taasisi ambazo zinahusika zaidi ni Mahakama, *Division* ya Mashtaka na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Dola ina Mihimili mitatu; kuna Serikali ambayo ndiyo Mtendaji, kuna Mahakama na kuna Bunge. Inavyoonekana, Mhimili wa Mahakama unapuuzwa. Inachukuliwa kama ni Wizara au kama ni Idara wakati ule ni Mhimili muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, ushahidi wa kwanza, tuangalie majengo ya Mihimili mitatu. Bunge tumo humu na majengo mengine yako nje ya Ukumbi huu. Utajua kuwa hapa pana hadhi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na inawakilisha miaka hamsini ya Muungano. Ukienda Ikulu hali kadhalika, lakini nenda alipo Mheshimiwa Jaji Mkuu wa Tanzania, jengo alilopo, Ofisi aliyonayo, inasikitisha kweli kweli. Kwa hiyo, hii inaonesha kuwa Mahakama bado haijapewa nafasi inayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo suala la majengo tu, hata uwasilishaji wa fedha za kibajeti baina ya Mihimili hii mitatu, ukiangalia katika suala zima la fedha za maendeleo, Ofisi ya Rais, Ikulu, ambayo tunategemea ndiyo Makao Makuu ya Serikali hapa, katika bajeti ya mwaka 2013/2014, fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya maendeleo ni shilingi bilioni 59.58, zilizopokelewa na Ofisi ya Rais, Ikulu, ni shilingi bilioni 40.90, hii ni sawa na asilimia 69. Bunge, fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge ni shilingi bilioni 8.88, iliyopokelewa ni bilioni 2.95, hii ni sawa sawa na asilimia 36. Mahakama fedha iliyoidhinishwa na Bunge ni shilingi bilioni 42.71, fedha iliyopokelewa mpaka mwezi Machi, 2014 ni shilingi bilioni 5.50, ni asilimia 13 tu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la msingi kwenye Mhimili huu na Serikali ilione hili. Katika hali hiyo itakuwa hakuna majengo, hakuna Mahakama za Mwanzo zinazostahiki, hakuna Mahakama za Wilaya, hakuna Mahakama Kuu. Ikulu 69, Bunge 36, Mahakama 13.

Mheshimiwa Spika, fedha za uendeshaji au fedha za matumizi mengine; Ofisi ya Rais Ikulu asilimia 74 wakati haupo na fedha zipo hapa, Bunge ambalo na mimi nimo ni asilimia 76.1, Mahakama asilimia 56. Hivyo, ni ushahidi mwingine kuonesha kuwa, Mahakama bado hatujaipa nafasi inayostahiki. Inawezekana Mahakama tunaihitaji tukiwa na matatizo yetu lakini hali halisi haishughulikiwi kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, leo Mhimili unaomba wafanyakazi 1,264 kwa bajeti ya mwaka 2013/2014 Mhimili huo unapewa kibali cha watu 148, maana kama Wizara au kama Idara.

Mheshimiwa Waziri anasema kuwa, ili kesi zipungue na mahabusu wapungue, ni lazima Mahakama pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu pamoja na *Division* ya Mahakama …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*

*kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Tunashukuru. Mheshimiwa Raya Khamis, nilimtaja kwanza.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, ningependa kuchangia Hotuba hii ya Katiba na Sheria kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ningependa kuendeleza ambapo Mheshimiwa Mdee ameishia, kuhusiana na suala zima lililopo katika UDA na kesi yake katika Mahakama. Tunaona kwamba, Mahakamani tayari kesi ya UDA ilikuwepo na kiutaratibu kesi lazima iwe imefanyiwa uchunguzi, tayari kuna kila kitu, ndiyo kesi inafunguliwa. Jambo la kushangaza ni kwamba, katika suala hili, hii kesi imefunguliwa *then DPP* akaifuta! Tunataka kujua ni sababu zipi zilizopelekea kesi hii kufutwa na ni lini inatarajiwa kuendelezwa ama kufunguliwa ili tujue ni nini kinaendelea na kitu gani kipo hapo katikati ambacho tunafikiri labda kinataka kufichwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, katika suala ambalo amelizungumzia Halima Mdee na suala ambalo ninaunga mkono Hotuba ya Kambi ya Upinzani ni *issue* nzima ya Bunge Maalum la Katiba. Cha kusikitisha, katika Bunge la Katiba changamoto zake ukurasa wa 33 na 34; nilifikiri kwamba, miongoni mwa changamoto ni jinsi ambavyo tunaliendeleza, Muundo wake haujaridhisha baadhi ya Wabunge ambao ni Wajumbe. Vilevile tunaona kwamba, Bunge hili bado lina mzozo, Muundo wake kwa ujumla bado inakuwa ni utata na haueleweki katika jamii ni kitu gani. Wananchi wengi wanahitaji kujua kuna nini na ni kitu gani na Muundo mzima wa hili Bunge unakwendaje na unakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo yangu na maoni yangu, naomba myachukue na myazingatie. Kwa kuwa Bunge hili bado lina utata, napendekeza Waziri pamoja na kuishauri Serikali, hatuoni umuhimu wa kuleta Muswada katika Bunge hili wa kuamua kulisimamisha Bunge hili la Katiba mpaka pale ambapo Muundo wa Bunge utakapokuwa unaeleweka na kuridhisha. Katika Bunge tuwe tuna mjadala ambao unajadili mawazo ya Wananchi na tuwe na mjadala ambao unaleta masilahi ya Wananchi katika Taifa hili na siyo kujadili itikadi ya watu fulani, ama vyovyote ambavyo ilivyo, kujadili mawazo ya kikundi cha watu wachache badala ya mawazo ya Wananchi kama ambavyo inatarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuelezea *delay* za kesi Mahakamani. Katika Hotuba ya Waziri, ukurasa wa 13, ameelezea vizuri kwamba, wanajitahidi kufanya taratibu mbalimbali kuondokana na mrundikano wa kesi ama *delaying* za kesi katika Mahakama zetu. Ningependa nijue ni kesi ngapi katika kesi ngapi ambazo tayari zimesikilizwa ndani ya muda ambao Waziri ameueleza hapa ndani ya miaka miwili?

Ningependa kujua ni kesi ngapi katika kesi ama watuhumiwa ambao wako ndani si chini ya miaka mitano mpaka sasa zilizosikilizwa katika hizo kesi ambazo anasema zimesikilizwa ndani ya miaka miwili; ama tunakuwa tunasikiliza kesi ambazo tunaangalia huyu ambaye amekuja na hii kesi yupo katika *position* gani ya maisha, tunampa *priority* katika kusikiliza kesi zake. Ningependa kujua, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha atuambie ni kesi ngapi ka ya hizi ambazo mmesema mnajitahidi kuondoa mlundikano wa kesi mahakamani zimesikilizwa ambazo zipo ndani ya miaka mitano bado zilikuwa hazijafunguliwa?

Mheshimiwa Spika, vilevile tunaona kwamba, tuna Tume ya Haki za Binadamu na kuna watu ambao wanashughulika na hiki Kitengo. Bado kuna Watanzania ambao wapo Mahakamani si chini ya miaka tisa mpaka kumi kesi zao hazijasikilizwa. Hakuna utaratibu wowote na hatujui ni lini kesi zao zitafunguliwa kusikilizwa mahakamani. Ningependa kusisitiza

kuundwe *Special Unit* ambayo itakwenda kwenye mahabusu kuwahoji wale wafungwa wana muda gani na kesi zao zitaisha lini? Kwa sababu kuna baadhi ya mahabusu mpaka leo hawajui wana makosa gani na hawajui kesi zao zitaanza lini kusikilizwa na bado mafaili ya kesi zao hayajafunguliwa. Hatuoni kwamba tunawanyanyasa hawa watu kwa kuwaweka ndani kwa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ningependa nitoe ushauri na ningependa kujua suala zima la hao mahabusu ambao wanachukua muda mrefu kukaa ndani. Tume ya haki za binadamu inaliona vipi hili suala na inasema nini kuhusiana na watu kukaa ndani muda mrefu na muda wa unapofika wa kesi zao kufunguliwa na kuanza kusikilizwa watu wale wanaonekana hawana makosa na kuambiwa hawana mashtaka ya kujibu na kuachiwa warudi nje, wakati wameshapoteza muda mrefu wakiwa ndani; ni kitu gani ambacho wenzetu hawa wanalipwa kutokana na kupotezewa muda wao mrefu wakiwa ndani?

Mheshimiwa Spika, ningependa nizungumzie suala zima la rushwa katika Mahakama zetu. Katika *system* nzima na mfumo mzima wa Mahakama zetu, tunaona hizi *delaying* zipo. Unakwenda Mahakamani, Jaji anajua *hearing* leo inatakiwa ama leo kuna *ruling* ya kesi fulani na yeye ndiye ambaye anakupa tarehe, unafika Mahakamani unaambiwa Jaji hayupo. Mbaya zaidi na cha kusikitisha, hakuna taarifa zozote za upande ambao unakwenda kusikiliza *ruling* ama *judgment* inayosimamiwa na yule Jaji, hakuna taarifa zozote zilizopo upande wa pili kwamba Jaji huyu hatakuwepo ana dharura ama ana kitu fulani.

Kwa kweli tunasikitishwa na hili, unakuta kesi tayari imeshafikia *ruling,* inachukua labda miezi sita, saba, mpaka Jaji aje apatikane. Inapelekwa kwa mwingine inapewa tarehe, tarehe ambayo inapewa akirudi anaambiwa tena hayupo ama kama ni *hearing* tayari mashahidi wamepatikana na ni vigumu na inachukua g harama nyingi. Kwa hiyo, tunazidi kuwashushia mzigo watu ambao ilibidi kesi zao ziwe ndani ya muda fulani na tunaona kwamba, zinazidi kuchelewa zinaendelea kuchukua muda zaidi kwa sababu ya Jaji kutokuwepo na kutokutoa taarifa yoyote kwa upande wa pili. Muda mwingine mashahidi wanatoka mikoa mbalimbali ama wengine wako nchi nyingine wanakuja kutoa ushahidi, wakifika wanakuta Jaji hayupo na taarifa hakuna kujua nini ambacho kimetokea, haileti picha nzuri.

Mheshimiwa Spika, bado tunarudi tena katika *system* nzima ya mtindo wa rushwa Mahakamani, *anyway* au vyovyote ambavyo tunaweza kuita kwamba tuna …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** *Time!* Mheshimiwa Fakharia nilimtaja kabla ya hapo.

**MHE. FAKHARIA KHAMIS SHOMAR:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza, naunga mkono hoja ya Wizara. Pili, nataka kuuliza hivi hapa tunazungumzia Bunge la Katiba au tunazungumzia Bajeti? *(Makofi)*

Kwa sababu ninashangaa wanapozungumza watu wakati tulikuwa nao kwenye Bunge la Katiba, wakachukua mpira wakaweka kwapani wakatoka, leo kwenye kipindi cha Bunge la Bajeti wameanza kufufua yale yaliyokuwa yamejificha! Wameondoka hawakuaga na kurudi wanaweza wakarudi sisi hatuna matatizo. Bunge la Katiba litakuwepo mwezi wa nane, rudini tuje tutangaze hoja humu ndani, tujue nini kinachoendelea. Siyo iwe kuchupia chupia katika masuala mengine kuzungumzia mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa nataka kuzungumzia Wizara ya Katiba yenyewe, Wizara Mama. Wizara ya Katiba ndiyo Wizara Mama iliyobeba Taasisi kadhaa. Wizara ya Katiba katika bajeti yake ya mwaka 2013/2014, ilipangiwa shilingi 7,066,331,500. Cha kushangaza, hii fedha huwa hawaipati yote na kama mtu hupati kitu cha kutosha hata kufanya kazi yako kwa ukamilifu haiwezekani. Wamepewa shilingi 2,355,175,821. Utaona hapa kama pana mchezo, hatuitaki Wizara ifanye kazi. Eti Wizara hiyo ina Mahakama, Wizara hiyo ina Afisa Mwanasheria, Wizara hiyo ina Tume ya Haki za Binadamu. Wizara hiyo ina Ofisi nyeti nyeti tunazozitaka ziweze kuweka utawala bora katika nchi yetu na ndiyo hizo Mafungu yake hayapati fedha. Tunategemea wafanye kazi au bado tuwe tunasuasua na kucheza wakati wenzetu watakuwa wanasonga mbele sisi bado tunarudi nyuma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukija mazingira duni ya kufanyia kazi; Wizara pamoja na Taasisi zake, sehemu za kufanyia kazi ziko duni. Imezungumzwa hapa, Ofisi ya Jaji Mkuu ukienda usiombe kuzimwe umeme, maana hata ukifungua madirisha ndani hamwonani. Sasa utakuta vituko vinavyokuweko; sijui tunaangalia Mhimili au tunaangalia kwamba hii ni Mahakama kwa sababu Mahakama ni sehemu inayokwenda kutia watu adabu. Sijui tuzungumze kitu gani! Mahakama haimtii mtu adabu. Kwa sababu sisi tuko nje huku, kama hujatenda maovu huwezi kufika na kila aliyefika kule huwa kama anakwenda kupata elimu ya kuondosha lile alilolitenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utakuta sasa hivi elimu tunayoipata ni duni. Unajua sasa hivi mitaani mtu akiiba kuku au kibaka kafanya jambo kaiba simu, mtu huyu akipatikana atakamatwa achomwe moto, badala ya kupelekwa kwenye Vyombo vya Sheria. Sasa mimi naomba elimu itolewe na watoaji elimu ni hii sehemu ya Sheria na hawa kutoa elimu ni fedha hawapewi, tutegemee maadili yetu yatakuwaje? *(Makofi)*

Itakuwa tukikamatana badala ya kupelekana kwenye Vyombo vya Sheria tunatiana moto. Ina maana baada ya kuweka amani na utulivu, tutaanza kuwa na mazingira ambayo siyo bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho ninataka kukizungumzia ni kuhusu rushwa. Unajua hii ni Taasisi nyeti au Wizara nyeti. Kwa hali halisi ilivyo ni sehemu ya pili katika Taasisi zenye watumishi ambao wanaongoza kwa rushwa. Naiomba Wizara pamoja na Taasisi zake, kwa sababu sisi tunakutegemeeni ninyi, sisi tunakuangalieni ninyi, ikiwa mtaongoza kwa rushwa sasa wanaokuangalieni huku nyuma watafanya nini?

Hali halisi tukiangalia wakati mwingine tunakuoneni ninyi ndiyo mnaotaka rushwa; kumbe na sisi wenyewe huku Wananchi tunaongoza kuwafanya wao wapende rushwa. Sasa bado naendelea kusema, elimu itolewe ili kwa mpokeaji na mtoaji kitu hiki kiwe kimoja hakiwezekani na Tanzania bila ya rushwa inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nitazungumzia kuhusu mahabusu wetu. Mahabusu ni sehemu mbaya na si nzuri kupelekwa kiongozi, raia au kupelekwa watoto. Hivi sasa mahabusu wamejaa katika magereza yetu, kesi haziendi kwa utaratibu uliopangwa. Mwaka jana nilizungumza nikaambiwa imepangwa ratiba ambapo kila mmoja anatakiwa kiasi fulani cha kesi azitekeleze, lakini wanashindwa kutekeleza; sehemu ya kufanyia kazi hawana na fedha za kufanyia kazi hakuna. Sasa naomba atakapokuja Mheshimiwa Waziri atuambie mbinu gani watakazotumia ili hii Wizara iweze kufanya kazi zake kwa uhakika na Watendaji waweze kupata mafao yao kwa uhakika na fedha za maendeleo zipatikane kwa uhakika ili waweze kutekeleza majukumu yao na kujenga maofisi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Elizabeth Batenga; nafikiri yupo?

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii ili na mimi nichangie machache katika Hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo ningependa kuliungumzia ni kasi ya kurekebisha Sheria mbalimbali ambazo zinaonekana zina upungufu. Kwa muda mrefu tumedai Sheria mbalimbali zirekebishwe hasa zile ambazo zinaonesha zinakandamiza wanawake na watoto. Sheria ya Mirathi, Sheria ya Ndoa na nyinginezo ambazo zinakandamiza wanawake na watoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazidi kusisitiza na kuomba kwamba, kasi ya kurekebisha Sheria hizi iongezwe. *(Makofi)*

La pili, elimu kuhusu Sheria. Bunge hili kazi yake kubwa ni kutunga Sheria. Zinapotungwa Sheria, zinawahusu Wananchi wote kwa namna moja au nyingine. Sasa kama Wananchi hawaelimishwi kuhusu hizi Sheria, utekelezaji wake unakuwa ni mgumu. *(Makofi)*

Tunajua kwamba, kutokujua Sheria hakukupi wewe unafuu au haki ya kusema kwamba, hukujua ndiyo maana umekosea. Kwa hiyo, mtu unaweza kutenda kosa bila kutambua unaadhibiwa, lakini kumbe Wizara hii ndiyo inapaswa kutoa elimu kuhusu Sheria zote zinazotungwa na hasa ndugu zetu wa huko vijijini mambo mengine hawayajui. Mheshimiwa Waziri, ameeleza katika Hotuba yake kwamba, wanatoa elimu ya Sheria, lakini niseme tu kwamba haitoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mahakama ndiyo inayotafsiri Sheria na kutoa haki, lakini haki haipatikani mpaka uidai, mpaka uitafute. Katika kutafuta na kudai ni lazima uwe na uelewa. Katika Mahakama inategemea ni jinsi gani utakavyojitetea au utakavyojieleza ndipo utaweza kupata ile haki. Kwa hiyo, mtu wa kawaida kwenda kusimama Mahakamani na kutetea haki yake wakati mwingine inakuwa ni vigumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iendeleze mpango huu ambao imeuanzisha wa kuwapa watu msaada wa kisheria ili watu wasipoteze haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nivipongeze Vyama Visivyo vya Kiserekali, katika shughuli hii ya kusaidia watu ambao wanahitaji msaada wa kisheria. Nitambue Chama cha Wanasheria Wanawake *(TAWLA),* kwa namna wanavyojitahidi kuwasaidia Wananchi na hasa Wanawake katika kudai haki zao. Wameanzisha Mradi wa *Paralegals.* Sasa naomba Wizara iisaidie *TAWLA* katika kuendeleza huu Mpango wa *Paralegals* ili uweze kuenea katika maeneo mbalimbali hasa vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba, Operesheni Kimbunga haikulenga watu wenye asili ya Kinyarwanda. Operesheni Kimbunga ililenga watu wote ambao wako nchini kinyume cha Sheria. Sasa kama mtu yuko Tanzania anakaa isivyo halali kurudishwa kwenu inakuwa nongwa kwa sababu gani? *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba watu wasizidi kupotosha kwamba, Operesheni Kimbunga ilianzishwa kwa sababu ya kuwaadhibu Wanyarwanda baada ya kinachoitwa mgogoro kati ya Rais wa Tanzania na Rais wa Rwanda. Operesheni hii ililenga watu wote ambao walikuwa Tanzania kinyume cha utaratibu. Tanzania inawakaribisha watu wote wanaopenda kuishi kwa amani na kwa kufuata Sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri ili …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante.
**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Amesikia. Waheshimiwa Wabunge, naomba niwakumbushe jambo moja; utaratibu wetu wa kuchangia ni wa kujaza fomu siyo kuleta hapa. Kama jina lako halipo katika fomu zile hupati nafasi hapa. Hata ukisema unampa nafasi yangu mwingine, huyo mwingine lazima awe humu kwenye fomu zangu. Akiwa kwenye fomu zangu hiari yenu kama mnataka azungumze atazungumza, isipokuwa pia nitaangalia aliyechangia mara nyingi kwa mujibu wa Kanuni hawezi kupewa nafasi kama wengine wapo katika orodha ile ile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nakuombeni sana msiniletee vibarua mimi sasa sichangii atachangia mwingine badala yangu aah, tafadhali mkajaze fomu vizuri. Tumesema mtu unaweza ukajaza mpaka Wizara sita unazofikiria unazipenda kwa kulingana na ya kwanza, ya pili ya tatu, vile unavyotaka. Kwa hiyo, hii inakuwa vizuri kwa sababu hata kama anachangia mwingine, lakini si aliomba na yeye. Alistahili kupata lakini labda nafasi haikutosha na wewe ukasema naomba achangie mwingine lakini yumo katika maombi ya siku ya Wizara ile na katika kundi.

Nawaombeni hili mlizingatie kwa sababu niliona vinoti vingi vinasema basi wachangie, hapana. Ambao wanaweza kuchangia bila kuwa wamejaza fomu ni Mawaziri, nao pia watachangia eneo linalohusiana na Wizara zao siyo popote pale na ataondoka mwingine kati yao, atasema ataondoka fulani kwa ajili ya huyu mpaka idadi ile itimie.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba nisitishe shughuli za Bunge mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Mwandosya?

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, ili niweze kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii muhimu. Kwanza naanza kwa kuunga mkono hoja hii na kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Watendaji wote na Wakuu wa Tume zote zilizoko chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo napenda kusema kwamba, Wizara hii ni Wizara muhimu sana, lakini inapata bajeti ndogo sana ambayo inaifanya isiweze kufikia malengo yale yanayohitajika. Kila mwaka ikija hapa tunalalamika kwamba, bajeti ni ndogo. Udogo wa bajeti hii umesababisha hata Mahakama za Mwanzo zisiweze kuhudumiwa vizuri na tukijua kwamba, kule kwenye Mahakama za Mwanzo ndiko waliko wananchi wa kawaida ambao wanahitaji kupata haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna Mahakama nyingi zilizoko Mkoa wa Iringa, Mahakama za Mwanzo, ambazo hazijakarabatiwa ikiwemo Mahakama ya Ruaha Mbuyuni, Kilolo, Mahakama ya Igowole, Mahakama ya Mlolo, Kibaoni, Idodi, Malangali, pamoja na nyumba za watumishi. Kwa hiyo, hili limekuwa ni kero kubwa sana. Majengo yenyewe hayalingani na haki ile inayotolewa kwenye Mahakama. Naomba Wizara iongezewe bajeti ili iweze kufikia maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la kuwafundisha Watoa Huduma au *Paralegals,* Watoa Sheria za Msingi Vijijini. Ningependa kufahamu Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, inatambua Kada hii na inawapa mafunzo, ili waweze kuwa jirani na wananchi. Kwa sababu, wakifundishwa hawa watakuwa vijijini na wananchi pia wataweza kufikiwa kwa kupata elimu, lakini pia kwa kujua haki zao.

Mheshimiwa Spika, hii inaendana na maelezo ambayo Mheshimiwa Waziri ameeleza kwamba, wako kwenye mchakato wa kutunga Sheria ya kuwawezesha wananchi kupata ushauri wa kisheria na hata kama hawana fedha, lakini waweze kupewa ushauri. Napenda kujua; huo Muswada utaletwa lini Bungeni, ili tuweze kupitisha, ili iwe Sheria, wananchi wetu waweze kupata haki zao?

Mheshimiwa Spika, lingine ninalopenda kulizungumzia ni ukatili wa kijinsia, tatizo hili limekuwa sugu. Kwa utafiti uliofanywa na Demografia na Afya nchini ya mwaka 2010 imeonesha kwamba, 45% ya wanawake wenye umri wa kati ya miaka 15 mpaka 49 waliripotiwa kufanyiwa ukatili wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, hili ni tatizo kubwa. Kila siku kuna kesi za ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto. Tunajua kwamba, hata kwa wavulana ipo, lakini tatizo ni kubwa sana kwa wanawake na watoto. Tatizo hili napenda nilipongeze Jeshi la Polisi na Umoja wa Mapolisi Wanawake kwa kuweza kuamua kupambana na ukatili wa kijinsia na napongeza taasisi zote ambazo zimeshiriki. Nataka kujua, ni lini Serikali itaweka Sheria ya Kuanzisha Vituo kila sehemu vya kuhifadhi wahanga wa ukatili wa kijinsia?

Mheshimiwa Spika, nchi nyingine wanavyo hivi vituo na wanashirikiana na taasisi zisizokuwa za Kiserikali. Tumeona kabisa wale wahanga wa ukatili wanahifadhiwa kwa Makatibu Kata. Anapokwenda pale hana mahali pa kwenda au Wenyeviti wa Mitaa. Tunapongea tumesema Jeshi la Polisi kwa sababu, kutumia Polisi Jamii pamoja na *Desk* la Jinsia tumeona kabisa kesi nyingi zinashughulikiwa, lakini tunapenda kujua watahifadhiwa wapi hawa? Napenda kusema kama Sheria haipo, basi turekebishe Sheria, ili kiweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, lingine, naungana na Wabunge waliosema kwamba, kuna Sheria nyingi zilizopitwa na wakati na tunaomba Sheria hizi zirekebishwe. Sina haja ya kuzirudia kwa sababu ni nyingi na zimekuwa kandamizi. Kila mwaka tunaambiwa zinafanyiwa marekebisho, mchakato, lakini hatuoni zikiletwa hapa kuja kubadilishwa na Sheria hizi zimeendelea kuwa kandamizi na nyingi zao zimepitwa na wakati. Sasa napenda kujua ni lini Sheria hizi ambazo tumekuwa tunazipigia kelele zitaletwa hapa, ili tuzirekebishe?

Mheshimiwa Spika, na mojawapo ikiwa ni Sheria ya Mirathi, ambayo inawakandamiza wanawake, wakiwemo wanawake wajane kukosa mirathi. Ikiwemo pia ya kumiliki ardhi, pamoja na kwamba, kuna Sheria ambayo inaruhusu wanawake kumiliki ardhi, lakini kuna Sheria nyingine za kimila ambazo zinakinzana na hii Sheria na kufanya wanawake kukosa haki zao. Sasa ni lini hizo Sheria zitaletwa zibadilishwe?

Mheshimiwa Spika, lingine nimezungumzia uchakavu wa majengo, ni pamoja na Jengo la Wizara. Jengo la Wizara limechakaa, nilikuwa nauliza; hivi jengo hili na lenyewe litafanyiwa marekebisho lini kwa sababu, hata saa nyingine unakwama ndani ya lifti. Kwa hiyo, nafikiri kwamba, kuna haja, kazi nzuri inayofanywa na Wizara hii na Wizara nyeti namna hii inahitaji kuongezewa rasilimali.

Mheshimiwa Spika, nashangaa wale wote wanaolaumu kwamba, hakuna kitu kilichofanyika kwenye Wizara hii, tunaona mabadiliko makubwa. Kuna kazi nyingi ambazo zimefanyika, isipokuwa tunaloona ni tatizo la ufinyu wa bajeti ambalo tunafikiri kwamba, kama wakiongezewa wanaweza wakafanya makubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni ucheleweshaji wa kesi. Kumekuwa kuna malalamiko kwa wananchi, kesi zinachelewa. Sasa tunaelewa yawezekana zinachelewa kwa sababu watumishi wa Mahakama, Mahakimu ni wachache; ni lini Mahakimu wataajiriwa ambao watatosha kwenda vijijini kusikiliza kesi? Maana kwingine unakuta hata Mahakama ya Wilaya haipo; hivi hapa lingine ninalopenda kujua ni lini Mahakama ya Mkoa wa Njombe itajengwa? Maana huu ni Mkoa na tunategemea kwamba, kuwe na Mahakama ya Mkoa ambayo itasaidia kutatua kesi nyingi, maana tunajua kuna maeneo mengi sana hayana Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nishukuru na niipongeze tena Wizara kwa kazi nzuri inayofanya na naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja. Waziri wa Katiba na Sheria amewasilisha hoja yake kwa umakini sana na ilikuwa inapendeza kumsikia, lakini hatukutegemea vinginevyo kutoka kwake.

Mheshimiwa Spika, niseme kuhusu Mahakama na heshima ambayo Mahakama ya Tanzania imeiletea Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba, Kimataifa Mahakama yetu inatambuliwa kutokana na kwamba, Majaji wetu wengi wanachukuliwa kwenda kufanya kazi Kimataifa, pamoja na mchuano mkali sana katika ngazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Jaji wetu Mkuu amekuwa Mwanasheria wa Kimataifa miaka mingi. Kama mtakumbuka Jaji William Sekule ni Jaji sasa katika Mahakama ya Kimataifa ya Jinsia huko *The Hague*. Huko Seychelles kuna Majaji, Jaji Dkt. Bwana, Jaji Msofe, wote hawa wanaitumikia Seychelles katika Mahakama Kuu ya kule; mtakumbuka vile vile kwamba, Jaji Nsekela amekuwa Rais wa Mahakama ya Afrika Mashariki. Sasa hii ni mfano tu wa jinsi ambavyo Mahakama yetu imetuletea heshima Tanzania, lazima tuipongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, si hapo tu, Mahakama ya Tanzania imekwenda mbali sana. Wale ambao mmetembelea Botswana, Swaziland, Lesotho, Afrika ya Kusini na nchi nyingine za Kusini mwa Afrika lazima mmekutana na Mahakimu kutoka Tanzania. Yote hiyo ni heshima kubwa kwa Tanzania kwa hiyo, tunawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, mtakumbuka kwamba, hata Jaji wa Mahakama Kuu ya Kenya amesoma Tanzania. Majaji wengi wa Kenya wamesoma Tanzania. Majaji wengi wa Mahakama Kuu Uganda wamesoma Tanzania kwa kweli, tunajivunia Mahakama zetu.

Mheshimiwa Spika, amani, usalama na utulivu hushamiri palipo na haki na hasa ndio huu umuhimu wa hii Wizara ya Katiba na Sheria, lakini niseme tu kwamba, hapawezi kuwa na haki, hapawezi kuwa amani na usalama na utulivu kama hamna uzalendo.

Mheshimiwa Spika, mimi kama Mbunge Mwandamizi, maana yake nimekaa miaka mingi Bungeni, ningekuwa Marekani wangesema ni *Ranking Member of the House,* nimebaini kwa kweli kushuka kwa uzalendo na upendo kwa nchi yetu ya Tanzania. Uzalendo unashuka na upendo baina ya Watanzania unashuka, hivyo basi, hatutegemei maajabu katika amani, usalama na utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nitoe changamoto kuhusu uzalendo; sijui, labda tungeanzisha mdahalo kuhusu Wimbo wa Taifa hasa baada ya miaka 50 kwa sababu, wimbo wetu wa sasa ni ule wimbo *Kwemboz* ambao asili yake ni Afrika ya Kusini, *Nkosi Sikeleli* Afrika. Sasa baada ya ukombozi, labda wakati huo umefika tunapojadili hata Katiba Mpya, kufikiria Wimbo wa Kizalendo wa Kitanzania.

Mheshimiwa Spika, nafikiri, "Tanzania Tanzania nakupenda kwa moyo wote," ni wimbo wa kizalendo sana sana. Tuanze kufikiria labda sasa huu ndio Wimbo wa Taifa, ili uweze sasa ukarudisha uzalendo wa Watanzania, lakini hili naliweka ili tuweze kulijadili labda sio hapa. Kwa hiyo, mimi naomba uzalendo kwa kweli, utawale Majadiliano ya Bunge Maalum la Katiba; uzalendo na upendo kwa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiongea mtu na mtu na Mheshimiwa Lipumba, Mheshimiwa Mbowe, Mheshimiwa Mbatia, mambo mengi tunaelewana, sijui kwa nini, yanayotutenganisha ni machache. Nasema nikiongea moja kwa moja, mtu na mtu, lakini sasa wakienda wakikusanyika pamoja kinakuja kitu kingine kabisa, kabisa kabisa. Kwa hiyo, nadhani bado kuna uwezekano wa sisi wote kuja na Katiba Mpya, isipokuwa nasema uzalendo na upendo kwa nchi uwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimetoa mapendekezo kwao. Kila nikitoa mapendekezo wanasema haya mazuri, haya ya kufikiriwa, lakini wakienda huko wakirudi katika UKAWA, looh, kinakuja kitu cha ajabu sana. Sasa sijui sababu kubwa ni Mheshimiwa Tundu Lissu, sina uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina uhakika, lakini mimi amenifurahisha sana jana aliposema kwamba, yeye ni Mtanzania. Amezaliwa Tanzania kwa hiyo, huu wimbo wa Tanganyika yeye haujui, yeye ni mtoto wa Tanzania. Sasa Mheshimiwa, kuna mambo ambayo kwa kweli, katika huu mfumo tutumie hiki kipindi kati ya sasa na mwezi wa Nane kwa kweli, kurekebisha mambo mengi tunaweza kuelewana. Kwa sababu, tukienda kwenye mambo ya msingi, mambo kwamba, Muungano ni lazima uimarishwe, tutaelewana. Zanzibar mamlaka yake itambulike na kero zote za Muungano ziweze kurekebishwa, tutaelewana. Mfumo utenganishe gharama za kuendesha Tanzania Bara na Muungano, hilo sio jambo kubwa, tunaweza tukakubaliana. Gharama za mfumo wowote ziwe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha*
*kwa muda wa mzungumzaji)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, ASIYE NA WIZARA MAALUM:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MAHUSIANO NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwanza naanza kwa kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa uamuzi wake wa kuunda ile Tume ya Mahakama kwa sababu, baada ya *Operation* Tokomeza kulikuwa na maneno mengi sana yamesemwa. Bado kuna manung'uniko mengi yanatoka katika maeneo ambako *operation* ilifanyika ambayo yanafika kwetu, yanayoonesha kana kwamba, kulikuwepo na uonevu wa raia. Kwa hiyo, kuundwa kwa Tume

hii, nafikiri kutatusaidia kutupa ukweli juu ya nini hasa kilitendeka, nani alitendewa nini, kwa sababu, Serikali yoyote ya kidemokrasia lazima ijali haki za raia wake.

Mheshimiwa Spika, nataka kuanza na hilo na nampongeza Waziri vile vile kwa hotuba yake nzuri na kwa ushauri aliompa mpaka wakaunda Tume hii; hilo jambo la kwanza kabisa ambalo ningependa kulisema.

Jambo la pili ambalo limefanya nimeomba, ni kwamba, nadhani tusigeuze Bunge hili kuwa Bunge la Katiba. Bunge la Katiba lipo, tena lipo kwa Sheria na Sheria tulitunga wote; sasa kuna watu wanageukageuka, wanasema ooh, Sheria imevunjwa, lakini hawatwambii ilivunjwa kifungu kipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulitunga Kanuni za hilo Bunge tukiwa wote, tena humuhumu. Tukatunga tukakubaliana na Walimu wetu wa Kanuni hizi walikuwa ni Mheshimiwa Jussa pamoja na Mheshimiwa Tundu Lissu, ndio walitupa Semina. Walikuwa wamekaa hapo wanatueleza hii itakuwa hivi, hii itakuwa hivi, hii itakuwa hivi na Kanuni tuliyotunga ambayo haipingani na Sheria, Sura ya 83. Ilikuwa inasema Bunge hilo lilikuwa na Mamlaka ya kubadili, ya kurekebisha, na kadhalika. Sasa leo, wenzetu tena baada ya kuamua kutoka, sasa wanasema tunavunja Sheria. Tunavunja Sheria eti kwa sababu, tunapingana na mawazo ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hapa sio sawa. Leo nimekutana na rafiki yangu Mnyaa nikamwambia mbona siku hizi umenuna sana? Angalau u-*smile* basi, maana unaweza ukapata *blood pressure* bure kwa mambo ambayo hayakuhusu peke yako, lakini hata hakusema; ukweli jamani, tuuzingatie. Kwa sababu, wanasema tunapingana na maoni ya wananchi na mimi nauliza yapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana kule Zanzibar 60% walitaka Mkataba, Tume haikupendekeza Mkataba. 34% walitaka Serikali Mbili, Tume haikupendekeza Serikali mbili, asilimia zimekwisha, hao ni Wazanzibari. Sehemu kubwa ya asilimia ya watu waliotoa maoni walitoka Pemba Kaskazini ukilinganisha na sehemu nyingine yoyote ya Zanzibar. Sasa mnaposema tunapinga maoni ya wananchi, nawauliza mtusaidie yapi? Ya Mkataba? Ya Serikali Tatu? Ya Mbili? Yapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huku Tanzania Bara watu waliosema wanataka Serikali Tatu walikuwa 16,000. Kati ya hao 8,000 walitoka Kigoma peke yake na 7,000 waliobakia wanatoka sehemu nyingine yote ya Tanzania; sasa mnasema tunapingana na maoni ya Kigoma au ya Tanzania? Twambieni basi mtusaidie, maana kwa kweli, unajua watu wazima hivi lazima tuwe tunasema kweli, eeh? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tundu Lissu, alipokuwa anaongea hapa juzi akatwambia unaweza ukadanganya watu wachache kwa muda, lakini huwezi kudanganya watu wote wakati wote. Sasa ninyi mnataka kutudanganya sisi wote wakati wote, hapo kwa kweli, msiwadanganye Watanzania, hapa hakuna hoja. Kama mna hoja iliyowatoa isemeni tu, sisi tunataka mrudi, tena mrudi salama tu. Mheshimiwa Mnyaa, rudi tuongee, kama hamrudi tutatumia Kanuni zile kutafuta akidi na Bunge litaendelea, eeh, lakini msitubabaishe. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, sasa kengele moja imelia, kengele hii inalia upesi kweli, kwa hiyo, nataka kuwaambia, kati ya maoni 37,000 yaliyotolewa Zanzibar, maoni 16,290 yanatoka Kaskazini Pemba au 43%. Sasa hapa kweli, mnaweza mkasemaje kwamba, Wazanzibari au watu wa Tanzania Bara wote wanataka?

Mheshimiwa Spika, hata Mwenyekiti wa Tume alipokuwa anazungumza kwenye Kipindi cha Dakika 45, alifika mahali akakiri kwamba, hawakutumia takwimu kama msingi wa kufikia uamuzi. Sasa kama hivyo ndivyo na sisi sio lazima tutumie takwimu hizi, twende na *logic*. Ni kitu gani ambacho ni *sustainable* kwa maendeleo ya Tanzania? Hatuwezi tu kwenda na takwimu, takwimu na hata Mwenyekiti mwenyewe naye amekiri hazifai kumbe zina matatizo; sasa watu wote wanaotaka Serikali tatu, mlionana nao wapi? Hakuna hoja hapa, hapa hakuna hoja. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya masahihisho na ya kuwasaidia *UKAWA* kujua hawana hoja, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, kupitia maandishi naomba nichangie hotuba ya Wizara hii muhimu kwa ustawi na amani katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara hii iongeze nguvu na mbinu katika utendaji ili kubaini upungufu unaoweza kupelekea baadhi ya wananchi kupoteza haki zao lakini kuteseka na hata kufa. Maeneo ya kutilia maanani ni Mikoa ya pembezoni hasa Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Spika, inasikitisha pale mwananchi anapopokonywa haki yake kwa ushahidi au hali iliyowazi hata kwa mtu ambaye ana elimu ya kawaida. Hali kama hiyo ndiyo baadhi ya watu huchukulia kwa ujumla kuwa Taasisi hii inaendeshwa kwa uonevu na rushwa.

Mheshimiwa Spika, nichukulie mifano mitatu ya wazi ambayo watu wananyimwa haki zao, moja, Mtendaji wa Kata Mushabang'o Wilaya ya Muleba Bwana Charles Rwanshoni ana shauri PT 26/2013 na sasa yupo rumande katika Gereza la Bukoba. Bwana Charles Rwanshoni aliwatuma mgambo kukusanya michango ya kujenga Sekondari ya Nyakatanga. Katika shughuli hiyo mgambo wakatumia nguvu kujilinda dhidi ya mwananchi mmoja aliyewazuia kutenda kazi.

Katika purukushani hizo mke wa huyo mwananchi mkaidi mimba ikatoka wakati anakimbia kumgombelezea mume wake. Alipofika Hospitali ya Rubya baada ya muda mama huyo alifariki. Taarifa ya Daktari ikaeleza kuwa chanzo cha kifo ni:-

(i) Kupata mimba katika umri wa hatari *(old age);* na

(ii) Kuchelewa kufikishwa hospitali.

Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya tambo katika jamii Mtendaji Charles Rwanshoni akafunguliwa mashtaka ya mauaji. Uchunguzi na upelelezi katika ngazi ya Wilaya Muleba ulieleza kuwa suala hili halimhusu Charles Rwanshoni kwa kuwa kwanza hakuwepo kwenye tukio, pili amri ya kutuma mgambo alikuwa anafuata maelekezo ya ngazi ya juu ambayo ni ya Wilaya na tatu taarifa ya Daktari inaonyesha chanzo.

Ofisi ya Mkoa kwa sababu wanazoelewa wao na ambazo ndizo zinatia mashaka wakaamuru Bwana Charles Rwanshoni akamatwe mwaka jana na afunguliwe mashtaka na yupo rumande pasipo kusikilizwa.

Mheshimiwa Spika, mfano wa pili ni shauri la Mheshimiwa Abubakari Said na wenzake watatu – *case 19/2013.* Nyuma ya uonevu huu ni mgogoro wa ardhi katika Kata ya Rutoro. Bwana Abubakari, Diwani Mtendaji wa Kijiji na Mwenyekiti wa Kitongoji walionekana ni watetezi wa wananchi dhidi ya unyanyasaji unaofanywa na wachungaji toka nchi jirani ya Rwanda. Kukamatwa kwao ilikuwa amri ya *RCO* wa Kagera na kubambikiziwa shauri la mauaji. Kama ilivyo kwa shauri la Charles Rwanshoni, mamlaka ya Wilaya *(OCD* na *OCD-CID)* watu hawa hawakuonekana kuhusika na mauaji ya Mnyarwanda aliyelisha mifugo kwenye shamba la mwananchi kwa makusudi.

Mheshimiwa Spika, utetezi ambao upo dhahiri umetupwa na kutozingatiwa na wapo rumande Bukoba. Yamekuwepo maeneo katika jamii na hata sasa yapo kuwa liliwekwa fungu kubwa la fedha ili watu hao wafungwe.

Mheshimiwa Spika, kwa sisi ambao hatukusoma sheria utetezi wa watu hawa upo dhahiri:-

(a) *OCD* na timu ya Muleba iliwajua wauaji ambao baada ya tukio walikimbilia Uganda. *RCO* alielezwa haya na akashikilia msimamo wake.

(b) Mtendaji wa Kijiji ambaye naye aliunganishwa siku ya tukio alikuwa na Mtendaji Kata akisuluhisha shauri, huyo Joseph Kweyamba akiwa Katibu utetezi wa bosi wake *WEO* ulitupwa.

(c) Mheshimiwa Abubakari siku ya tukio alikuwa kwenye Kamati ya Madiwani Muleba umbali wa kilometa 50 na alilala huko, utetezi wa Mkurugenzi na mahali alipolala haukusikilizwa.

(d) Mtendaji wa Kijiji ambaye siku hiyo alikuwa anakarabati/kujenga Kanisa ameunganishwa kwenye shauri.

(e) Eneo hili lipo mbali na vituo vya polisi hakuna miundombinu ya barabara, Diwani, Mtendaji na Wenyeviti wa Vitongoji na Vijiji ndiyo watawala. Iweje wawajibishwe kwa shauri lisilowahusu? Utawala bora unahitajika.

Mheshimiwa Spika, eneo au mfano mwingine ni dhuluma na maamuzi ya uonevu yanayoendeshwa na Mahakimu. Hakimu Bwana Nganyani wa Mahakama ya Mwanzo Rushwa (jina la eneo) amekuwa akipokea rushwa kwa kudai kiwango maalum cha shilingi 50,000/=. Suala hili linajulikana wazi na wananchi wamekuwa wakilalamika kila wapatapo fursa ya kukutana na kiongozi yeyote. Utaratibu wa kawaida wa kimaadili unashindikana kwani Wilaya haina fungu la kuitisha vikao husika. Pamoja na hali hiyo viongozi wote wanakiri kuwa utendaji wa Hakimu huyu unadhalilisha taasisi na mhimili kupita kiasi.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti hii naomba kwa taratibu na sheria zake Wizara na Mahakama ifanyie kazi mifano hii niliyoitoa. Ahsante.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa ukarabati wa Mahakama za Mwanzo za Mwamagembe na Ukimbu (Kayui). Aidha naiomba Serikali ione umuhimu wa kujenga Mahakama mpya katika Kata za:-

(1) Idodyandole;
(2) Rungwa;
(3) Aghodi; na

(4) Ipande.

Mheshimiwa Spika, Kata hizi ni kubwa sana na zipo mbali na Mahakama za Mwanzo za Itigi, Ukimbu na Mwamagembe na hutumia gharama kubwa za kwenda kutafuta haki.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itenge fedha za kukarabati Mahakama ya Mjini Itigi ili iwe na hadhi inayostahili.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kila la kheri na kazi njema kwa mwaka 2014/2015. Nawasilisha.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mchango wangu kwa Wizara tajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya kupitisha Wizara hii kwa masharti ya kuzingatia na kutolea maelezo naomba yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya Nkasi, katika bajeti iliyopita ya Wizara hii tulielezwa juu ya Serikali kutenga fedha kwa ajili ya kujenga jengo la Mahakama ya Wilaya mpaka sasa Hakimu wa Wilaya anaendeshea shughuli za Mahakama ya Wilaya kwenye majengo yaliyotolewa na Mkurugenzi kwa muda. Na katika maelezo ya hotuba ya Mheshimiwa Waziri sijapata kusikia mipango yoyote iliyofikiwa katika azma hiyo kwa utekelezaji wa mipango ya mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa Mahakama za Mwanzo, kiasi kilichotajwa kujenga Mahakama za Mwanzo 25 nchini ni kiasi kidogo sana, kuna kila sababu kuongeza kiasi hiki ili kuona kuwa tunatendea haki vyombo vya utoaji haki kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu rushwa katika Mahakama zetu, hali ya utoaji haki kwa sasa katika Mahakama zetu hasa Mahakama za Mwanzo huzingatia kutoa chochote (rushwa) hata zile haki za dhamana tu watu hulazimika kutoa fedha tena kwa masharti kuwa wasitoe habari kwa mtu yeyote.

Mheshimiwa Spika, ili kukomesha shida hii kwa wananchi labda tuboreshe maslahi ya Mahakimu wetu na kutafuta namna ya kupata ushahidi na kulikabili kwa adhabu kubwa kwa wale wanaoharibu wachukuliwe hatua. Vyombo vya utoaji haki hivi vipatiwe semina na mafunzo ya rejea ili vibaki kwenye maadili yake ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa fedha za kibajeti, Serikali iache kuchelewesha mafungu yaliyoelekezwa kwa Mahakama kama mhimili ili waweze kupanga majukumu yake na kutekeleza hali hii inaweza kushawishi rushwa katika mfumo wake wote.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, naanza na pongezi kwa Mawaziri wa Wizara na Watendaji wa Wizara hii kuleta bajeti yao katika Bunge hili ili tuijadili na kutoa ushauri wetu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ufinyu wa bajeti nianze na kuiomba Serikali iongeze bajeti katika Wizara hii, Wizara hii ina changamoto nyingi sana ambazo bila kuwa na bajeti ya kutosha hatutakuwa tumeitendea haki. Pia tunaiomba Serikali tunapopitisha fedha za bajeti ipeleke kwa wakati ili Wizara iweze kushughulikia miradi ya maendeleo kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ucheleweshaji wa hukumu, inasikitisha sana kesi nyingi ambazo tayari zina vielelezo zinapompa Hakimu kizungumkuti cha kutoa hukumu. Kwa mfano

Mkoa wetu wa Iringa zipo kesi nyingi za ubakaji wa watoto ambazo tayari zina vielelezo lakini hukumu zinachukua muda mrefu sana.

Naomba Mheshimiwa Waziri atolee maelezo pia hata kesi za mauaji ya albino hata wauaji wakikamatwa bado hukumu zinachelewa sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msongamano wa mahabusu Mahakamani, nilitembelea Gereza la Mkoa wa Iringa nilikutana na changamoto nyingi sana ikiwepo:-

(i) Ucheleweshaji wa hukumu kesi zinapokwisha.

(ii) Upotevu wa majarida ya washitakiwa.

(iii) Ucheleweshaji wa hukumu za kesi za mauaji.

(iv) Kesi zinaendeshwa kwa lugha ya kiingereza, washtakiwa wanashindwa kujitetea sababu hawajui kinachozungumzwa.

(v) Ma-*DPP* wanalalamikiwa sana kuomba rushwa katika Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watoto wadogo kuchanganyika na mahabusu wakubwa wakiwa gerezani, tatizo hili ni baya sana, watoto wanaathirika kisaikolojia. Naishauri Serikali pamoja na Serikali kuwa na mkakati wa kujenga magereza ya watoto lakini kabla ya majengo hayo kuisha ni bora watoto hawa wasipelekwe mahabusu au kama watahukumiwa wapatiwe vifungo vya nje ili wapate hata haki ya kusoma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hukumu ya kesi zenye kifungu cha muda mfupi, kutokana na mrundikano wa magerezani, kwa nini hukumu za kesi za muda mfupi Mahakimu wasiwahukumu vifungo vya nje ili wafungwa waweze kufanya kazi za jamii kuliko kwenda kuleta msongomano magerezani bila sababu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi kutojua sheria, kuna tatizo kubwa sana la wananchi wetu wengi kutojua sheria na haki zao. Je, Serikali ina mkakati gani uliowekwa ili kuhakikisha wananchi wetu wanajua haki zao za kisheria na kupatiwa elimu?

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria zilizopitwa na wakati, zipo sheria nyingi sana zimepitwa na wakati ambazo kama Wabunge tumeshazizungumzia sana lakini hatuelewi kikwazo ni nini na hasa mkakati wa kuhakikisha mashirika yanayosaidia kisheria hasa wanawake yanafunguliwa hata katika maeneo ya vijijini sababu mengi yamefunguliwa mijini tu kiasi kwamba wananwake wananyanyasika sana.

**MHE. RAYA IBRAHIM KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kuchangia kuhusu urasimu katika dhamana Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa kudhamini mtuhumiwa ni haki ya kila anayeshitakiwa kutakiwa kupata dhamana, lakini katika hili bado kuna usumbufu mkubwa kwa watu, mfano mtu anatakiwa awe na wadhamini wawili au mmoja ambaye anafanya kazi/ameajiriwa Serikalini pamoja na hayo kuwepo na kufuata masharti yote ya kudhamini mtu bado watu wanawekewa vikwazo katika hilo.

Pia dhamana hazifuati misingi ya sheria kwani kwa upande wa kupeleka *document* za kudhamini mtu bado huchukua muda zaidi wa kutaka ku-*verify document* hizo na muda huo

hufika hadi wiki mbili vinginevyo utoe rushwa ndipo hautachukua muda mrefu kupata dhamana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uvunjaji wa haki za binadamu, kwa upande wa magereza tunaona watu wanakaa muda mrefu bila ya kesi zao kusikilizwa na pia hakuna uchunguzi wa kutosha kwa wafungwa zaidi ya miaka kumi (10) mtu kuwa gerezani bila ya kesi yake kuanza kusikilizwa. Huu ni uvunjaji wa haki za watu kwani huwa jela bila ya kusomewa na hata kujua makosa yao.

Mapendekezo yangu ni kuwa kuwe na *special units* ya kutembelea magereza na kuwahoji wafungwa wana muda gani na kwa nini kesi zao bado kusikilizwa. Hivyo basi, kufanya hivyo kutaondoa kero ya kuwekwa magerezani bila utaratibu unaofaa. Vilevile kutaondoa kero ya mtu kukaa ndani muda mrefu bila sababu yoyote ya msingi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama za mashauri, bado katika mashauri kuna gharama kubwa hususan yanayohusiana na ardhi. Katika masuala ya ardhi gharama za mashauri zipo juu vilevile hupelekea wanyonge kukosa haki zao kwa kushindwa kumudu gharama hizo na pia *document* kushindwa kupatikana kwa muda muafaka kwa kukosa pesa. Mfano mtu kutaka kuweka *caviet* au *injaction* kuitaka Mahakama ku-*order injaction* lakini kushindwa kutekeleza kwa gharama na kama ni katika masuala ya ardhi kwenye nyumba kutaka usiuzwe au mtu asiendelee na ujenzi lakini huchangia wenye haki kukosa kwa sababu tu ya gharama na urasimu katika Mahakama, kwani huweza kuambiwa ombi lako la *document* ya kuitaka Mahakama kusimamisha halionekani na kama *document* haionekani hupelekea nyumba kuuzwa au mtu kuendeleza ujenzi hali ya kuwa kufanya hivyo ni kupoteza haki ya mwingine.

Mheshimiwa Spika, suala la kupotea kwa *document* katika Mahakama zetu ni uzembe na pia hufanywa kusudi kwa ajili ya maslahi ya wachache vinginevyo mtu atoe rushwa au wao kutaka rushwa ndiyo mfumo uende vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bunge Maalum la Katiba nalo ni changamoto katika Wizara hii lakini kutokana na changamoto hii tatizo ni muundo mzima wa Wajumbe na pia Wajumbe hao kuacha kujadili vitu tofauti. Pia Wajumbe kuacha kujadili mambo yenye maslahi kwa Taifa letu kwa ujumla.

Ushauri wangu ni kumtaka Waziri na Serikali kwa pamoja kuona umuhimu wa kuleta Muswada wa kuahirisha Bunge Maalum la Katiba hadi pale ambapo muundo wake utakapokuwa sahihi na kuisha kwa changamoto hii.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Spika, mimi siungi mkono hoja mpaka Mheshimiwa Waziri atakapotoa ufafanuzi na maelezo ya kina kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inajumuisha pia Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA). Wakala huyu kwa upande wa usajili kumekuwa na urasimu hasa kwa upande wa usajili wa watoto na vifo, jambo ambalo linasababisha msongamano, usumbufu na vishawishi vya rushwa. Hivyo Mheshimiwa Waziri namuomba atoe ufafanuzi wa kina kwa nini hali hii inajitokeza?

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mahakama nako kuna uendeshaji kesi usiozingatia sharia na kwa wakati mwingine kuna harufu za udini, kwa mfano kuna watuhumiwa wa uchochezi akiwa mkristo masharti ya dhamana mepesi muislamu masharti magumu na pengine

kufungiwa dhamana kabisa kwa kisingizio cha DPP. Hapa napo naomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria ndiyo waratibu wa mchakato wa Mabadiliko ya Katiba, pamoja na pongezi ilizotoa kwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba, huku ikijua kuwa Tume hiyo imewasilisha Rasimu ya Katiba yenye muundo wa Serikali Tatu. Waziri mwenye dhamana aliendelea kukaa kimya pale Wabunge wa CCM walipojenga hoja za kuturejesha kwenye Katiba ya mwaka 1977 iliyopo ya Serikali Mbili na kujaribu kupenyeza rasimu inayolinda sera ya CCM na kudharau maoni ya wananchi.

Naomba ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri juu ya ukimya wake na uhusiano wa pongezi anazotoa kwa viongozi.

Mheshimiwa Spika, Waziri katika hotuba yake amezungumzia mpango kazi wa kitaifa wa haki za binadamu uzinduzi ambao ulikwenda sambamba na mpango mkakati wa miaka mitano wa haki za watoto.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa haki za binadamu ni pamoja na haki ya kuishi. Ndani ya nchi yetu kumejitokeza mauaji ya vikongwe, wanawake na hasa mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi (albino).

Mheshimiwa Spika, mauaji ya albino ambayo yameibuka upya kuelekea chaguzi za Serikali za Mitaa mwaka 2014 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Lakini kama hiyo haitoshi ukatili kwa watoto unaongezeka siku hadi siku ikiwemo ongezeko la watoto wa mitaani.

Naomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi kuhusu hali hii inayojitokeza sasa ya mauaji na ongezeko la watoto wa mitaani na ukatili wa watoto ambao wengine hupoteza maisha kwa vipigo, nini hatma yake?

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuongelea juu ya upungufu wa Mahakimu hasa katika Mahakama ya Mwanzo, mfano katika jimbo langu Wilaya ya Sumbawanga Vijijini katika Mahakama za Mwanzo za Kipeta, Ilemba, Kaengesa na Mpuni.

Mheshimiwa Spika, pili ni ukosefu wa majengo ya mahakama pamoja na nyumba za mahakimu.

Mheshimiwa Spika, tatu, vitendea kazi kama vile pikipiki, magari, vifaa vya kutendea kazi, karatasi *computer* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lingine ni ucheleweshaji wa kesi jambo hili ni kero kubwa sana mwishowe wananchi wamefikia hatua ya kukata tamaa kabisa.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kama ifuatavyo:-

Kwanza, Bajeti ya Wizara hii iongezwe ili kuongeza juhudi kwa watendaji wa Mahakama ili kutumia teknolojia mpya kurahisisha kesi na hasa kesi zinazohusu migogoro ya ardhi inayowanyima wananchi wengi usingizi.

Mheshimiwa Spika, suala la rushwa limekithiri katika Mahakama ya Mwanzo hadi Juu. Hiki kimekuwa kilio cha wananchi cha muda mrefu, Serikali itoe tamko rasmi kuhusu rushwa iliyokithiri

hasa katika Mahakama ya zetu. Isiwe tu kila siku wananchi wanalalamika lakini Serikali yetu haiji na mkakati wowote.

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue juhudi/mkakati wa makusudi kutenga bajeti maalum ya kuelimisha wananchi hii wasioelewa na wasiojali utekelezaji wa sheria tunazotunga wenyewe, mfano mzuri ni wa Mkuu wa Wilaya ya Kiteto anayetekeleza amri halali ya kutekeleza uamuzi wa Mahakama ya Rufaa Tanzania kuhusu hifadhi ya jamii ya Emboeley Murtangos iliyopo Wilayani Kiteto. Mkuu huyo anatekeleza sheria hiyo lakini kuna viongozi wengine wa nchi hii wanamsakama, tena hadharani kupotosha ukweli nakupotosha wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii.

Pili nampongeza Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kwa kazi nzuri wanayoifanya kudumisha utawala wa sheria hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi napenda kutoa maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba kuelezea kuhusu upungufu wa Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo Manyoni. Jimbo la Manyoni lina upungufu mkubwa wa Mahakimu katika Mahakama za Mwanzo, tunaomba mgao kwa Mahakimu watakaoajiriwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchakavu wa majengo ya mahakama, majengo ya Mahakama ya Wilaya ni chakavu, tunaomba lijengwe jengo la kisasa la Mahakama ya Wilaya (Manyoni) kwani Mahakama za Mwanzo chache zilizopo zinatakiwa ukarabati hasa Mahakama za Makasuku, Ikasi Kilimantende, Senza na Iseke.

Mheshimiwa Spika, Mahakama mpya za Mwanzo tunaomba maeneo yafuatayo yapate Mahakama za Mwanzo ambayo ni Nkondo, Chikuyu, Msemambo na Heka.

**MHE. ALIKO N. KIBONA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naonga mkono hoja ya Waziri.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba kuleta kilio changu kuhusu kupatiwa Hakimu wa Wilaya katika Wilaya ya Ileje. Naomba kujua ni lini Serikali itampeleka hakimu wa Wilaya kule Ileje?

Mheshimiwa Spika, chombo cha usafiri (gari) la Mahakama lilipelekwa Ileje na baadaye ikatolewa bila sababu likaenda Mkoani, litarudi lini? Majengo ya Mahakama sehemu nyingi za Mahakama zimechakaa sana, vichaka hadi mlangoni mwa majengo ya Mahakama. Baadhi ya Mahakama majengo yake yamechoka, yanavuja na yanadondoka kuta zake. Naishauri Serikali ifanye juhudi za kukarabati majengo yake ili majengo haya yaweze kukarabatiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuchangia kuhusu masuala ya sheria. Sheria nyingi zimepitwa na wakati, kama ni masuala ya faini ni za muda mrefu kwa maana ya viwango vyake. Ushauri wangu ni kuwa Wizara iwasiliane na wadau kwa maana ya idara na idara zingine ili kubaini ni sheria gani ambazo wao wanaona zimepitwa na wakati na zifikishwe Bungeni kwa ajili ya marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu idadi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, kuna kilio cha Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo kwa mfano Wilaya ya Ileje ina Mahakama za Mwanzo

tano Wilaya nzima, hata hivyo idadi ya Mahakimu wa kuhudumia Mahakama hizo ni mmoja, halafu hana usafiri, je, ni lini tutapata Mahakimu hao?

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, napenda kupata majibu ya Serikali ni lini itapeleka fedha katika Wilaya ya Kilombero ili wajenge Mahakama ya Wilaya kwa kuwa Mahakama inayotumika sasa ambayo ipo Kituo cha Polisi Wilaya ambayo kinakumbwa na mafuriko kila wakati na kuharibu mafaili mbalimbali na kuchelewesha haki kutendeka.

Mheshimiwa Spika, napenda kujua ni lini Serikali italeta Sheria ya Mabadiliko ili Watanzania wanaohitimu Shahada ya Sheria waruhusiwe kusimama Mahakamani kutetea wananchi ambao wengi wao waPo pembezoni na wanashindwa kupata Wakili kwa kuwa Mawakili wengi walio na haki ya kutetea wananchi Mahakamani wanaishi mijini.

Mheshimiwa Spika, kuweka pingamizi la kusoma *Law School* kwa gharama ya shilingi milioni tatu ni changamoto kubwa kwa umaskini wa Watanzania walio wengi.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba ya Waziri wa Katiba na Sheria ukurasa wa tatu, *paragraph* ya pili, kifungu cha saba amepongezwa sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba na Makamu wake Jaji Augustino Ramadhani kwa kuongoza vyema Tume ya Mabadiliko ya Katiba.

Mheshimiwa Spika, ni kwa mara ya kwanza kusikia Mwenyekiti wa Tume pamoja na Makamu wake na Wajumbe wa Tume hii kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, ni wajibu wa Serikali kuomba radhi kutokana na kashfa, dharau, kejeli, kibri na jeuri zilizotolewa ama na Mawaziri, Wabunge na hata viongozi wa juu na ambao walikebehi kazi njema, adhimu na adimu iliyofanywa kwa uaminifu na uadilifu na Tume ya Mabadiliko ya Katiba ambayo ilizingatia matakwa halisi ya wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wanataka mabadiliko na madai yao ni ya mfumo wa Serikali Tatu jambo ambalo litalinda na kuboresha Muungano kisheria na sio Muungano wa mabavu ambao umevaliwa na upande mmoja wa Muungano huu.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Mabadiliko ya Katiba imeratibu maoni ya wananchi na kufanyia uchambuzi wa kina kwa muda mrefu wa miaka miwili na kazi hii imegharimu zaidi ya shilingi bilioni 70, aidha, Rais wa Jamhuri ya Muungano aliweka saini kuikubali Rasimu hiyo na hatimaye kuifikisha Bungeni kujadiliwa hata hivyo ni Rais huyo ambaye yeye mwenyewe alikuja katika Bunge Maalum la Katiba kuvunja mfumo wote wa Rasimu hiyo licha ya kusaini na kuliitisha Bunge Maalum kwa kuikubali na kuiwasilisha Rasimu.

Mheshimiwa Spika, kutoijadili Rasimu ya Mabadiliko ya wananchi na kuiboresha badala ya kubadilisha maudhui ni kwenda kinyume na haki za binadamu kwa kutoyapa umuhimu matakwa ya wananchi na kufuata sera ya chama cha Mapinduzi ya Serikali Mbili kuelekea Moja.

Mheshimiwa Spika, bado naendelea kusema kwamba Tanzania bado kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, ukiukwaji wa sheria, uhuru wa maoni hata uhuru wa kujieleza na kutoa mawazo licha ya hayo yote kutamkwa katika Katiba.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ukiukwaji wa haki na sheria katika jamii ya wakulima na wafugaji, vyombo vya dola na raia, Mahakama na watuhumiwa hata ukiukwaji wa Muungano. Ukiukwaji wa haki za binadamu hata Tume ya Haki za Binadamu ya Serikali nayo inachelewa kutoa ripoti yake kinyume hata na taasisi binafsi ambayo hivi karibuni ilitoa ripoti yake kule Dar es Salaam tarehe 12/05/2014.

Mheshimiwa Spika, wapo wale wanaodai kwamba sisi upinzani tunajadili zaidi mambo yatokanayo na Bunge Maalum wakati suala la mabadiliko ya Katiba yatokanayo na Bunge Maalum yameandikwa katika kitabu cha Waziri wa Katiba na Sheria ukurasa 3, 5, 6 na wa 7 kifungu cha 7, 11, 12, 13 na 14 sasa inapodaiwa kwamba sisi tunajadili mambo ambayo hayapo si sahihi na inaelekea kwamba hawakumfahamu Waziri alipokuwa anasoma.

Mheshimiwa Spika, sisi sio watoto wadogo, tunasema tunalijua na si watu wa kuburuzwa kama mnavyodai. Niwaelewa na tulifahamu ni kwa nini Jaji Warioba na Tume ya kuratibu maoni walipendekeza mfumo wa Serikali Tatu.

Mheshimiwa Spika, wale wanaodai mfumo wa Serikali Mbili wasidai kwamba wanaodai mfumo wa Serikali Tatu wana uchu wa madaraka, je, wale wanaong'ang'ania uwepo wa Serikali Mbili na kuendelea kukaa madarakani wana uchu wa nini?

Mheshimiwa Spika, kuhusu matatizo yanayozikabili Mahakama za Tanzania, ni wazi kuwa Mahakama za Tanzania zimegubikwa na rushwa kutokana na mishahara midogo ambayo haitoshelezi kutokana na kazi ngumu walizonazo Mahakimu hivyo kufikia maamuzi ya kutoa hukumu kwa kupokea hongo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo Wilaya hadi Mahakama Kuu unakwama kutokana na fedha za maendeleo kukwamishwa kupelekwa kwa wakati, kwa mfano bajeti ya mwaka jana iliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 42.71 lakini zilizopokelewa ni bilioni 5.50 tu.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, mapitio ya ujumla ya utekelezaji kwa mwaka 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2014/2015 yanaonyesha kwamba masuala yafuatayo bado yanapaswa kufanyiwa kazi na Wizara ya Katiba na Sheria kwa kuzingatia pia michango yangu kwa wakati mbalimbali juu ya Wizara hii kati ya mwaka 2011 mpaka 2013 kuhusu utendaji wa Wizara, vyombo vilivyo chini ya Wizara pamoja na Mahakama nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria na Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, imefikia wapi katika kutekeleza mapendekezo yangu niliyoyatoa katika hotuba zangu za Msemaji Mkuu, Waziri Kivuli wa Nishati na Madini Bungeni mwaka 2012 na 2013 kuhusu gharama kubwa ambazo Wizara mbalimbali, Taasisi na Mashirika mengi ya umma yanaingia kwenye gharama za kesi. Fedha hizo zingeelekezwa kwenye kuboresha maslahi na mazingira ya kazi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kuweza kusimamia kesi za kitaifa na kimataifa kwa ufanisi na kwa thamani bora ya fedha *(value for money)*.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yangu nilihoji gharama zilizohusu kampuni ya *Mkono & Company Advocates* kwenye kesi za Dowans, IPTL na nyinginezo. Kwa kuwa TAKUKURU na CAG wameagizwa kuchunguza kuhusu kashfa ya kutolewa kwa fedha kutoka *ESCROW Account* katika Benki Kuu. Hivyo Waziri wa Katiba na Sheria pamoja na Mwanasheria Mkuu na Serikali katika majukumu ya kuomba ukaguzi unaofanyika kwa hadidu alizopewa CAG na uchunguzi na TAKUKURU, hadidu rejea ziweze kupanuliwa kuhusisha uchunguzi juu ya gharama

za kisheria toka kashfa hiyo iliyoibuka mwaka 1994/1995 na masuala mengine yenye kuhusisha matumizi mabaya ya fedha za umma na ufisadi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Fungu 41 - Wizara ya Katiba na Sheria na Fungu la 35, Kurugenzi ya Mashtaka itoe maelezo kwa kuzingatia pia masuala niliyohoji katika Fungu la 16 kuhusu kashfa ya IPTL. Aidha DPP azingatie kuwa tangu mwaka 1994/1995 kashfa ya IPTL imehusisha madai ya ufisadi na ukiukwaji wa sheria kwenye makosa pia ya jinai. Wizara ya Katiba na Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kabla ya majumuisho na atoe kauli ni sababu zipi zimefanya toka wakati huo mpaka sasa watuhumiwa na ufisadi wa IPTL hawajafikishwa mahakamani na kuhukumiwa, na matokeo yake madai mapya yanaibuliwa.

Mheshimiwa Spika, aidha kwa kuzingatia maazimio ya Bunge ya mwaka 2008 kufuatia kashfa ya Richmond, Serikali ilitakiwa kupitia upya mkataba wa IPTL lakini azimio hilo halijatekelezwa na mchakato wa ufilisi uliokuwa unadhamiwa na Wakala Usajili na Udhamini (RITA) nao umehujumiwa, hivyo Serikali itoe majibu ya kina sasa.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2014/2015 ya Wizara ya Katiba na Sheria naomba Wizara kupitia Fungu 41, Fungu 40 na Fungu 12 itazame pia mazingira ya Mahakama katika Jimbo la Ubungo kama ifuatavyo:-

Mosi, Wizara itekeleze ahadi iliyotoa wakati wa majadiliano ya bajeti kwa miaka iliyopita na kuanza kutafuta kiwanja kwa ajili ya Mahakama ya Mwanzo katika Kata ya Kibamba au Kata ya Kwembe. Jimbo la Ubungo limepata ongezeko la watu, limedizi uwezo wa Mahakama za Mwanzo zilizopo hazijitoshelezi kuhudumia maeneo ya pembezoni.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba viongozi na watendaji wanaohusika kufanya ufuatiliaji wafanye hivyo pia katika Mahakama za Mwanzo zilizopo katika Jimbo la Ubungo, nipo tayari kushirikiana nanyi katika ziara hizo. Aidha kwa ziara au ufuatiliaji ambao umefanyika siku za nyuma naomba kupatiwa nakala ya ripoti niweze kushirikiana na Wizara katika kufuatilia utekelezaji wa masuala yaliyobainika.

Mheshimiwa Spika, tatu, Wizara pia ifanye ufuatiliaji kuhusu Mahakama nyingine zinazoundwa na mamlaka zingine, mathalani ifuatilie kuhusu utendaji wa Mahakama ya Jiji. Mahakama hii inalalamikiwa na wananchi kwamba imetawaliwa na ufisadi na unyanyasaji wa watuhumiwa kwa kushirikiana na mgambo wa Jiji. Kuna malalamiko makubwa ya mawakala wa kituo cha mabasi cha Ubungo (UBT) ambao wanatozwa faini kati ya shilingi 50,000/= mpaka shilingi 400,000/= kwa makosa yanayotajwa kuwa ni ya kubugudhi abiria au ya uzururaji, matokeo yake ni kuwa ni kuongezeka mrundikano na mahabusu na wafungwa katika makosa ambayo ingewezekana hata kutoa hukumu za kufanya kazi ya kijamii (hata ingekuwa au ikiwa ni kweli ni wakosaji).

Mheshimiwa Spika, Mahakama za Majiji zijikite katika hukumu za kijamii kuliko za jinai. Nimejaribu kuhoji hili kwenye Jiji lakini hatua hazijachukuliwa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, katika kutoa majibu kwenye majumuisho juu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2014/2015 na Mapitio ya Utekelezaji ya mwaka 2013/2014 naomba yafuatayo yazingatiwe na hatua kuchukuliwa:-

Kwanza Fungu 55 - Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ni muhimu ikaongezewa fedha kuweza kutimiza majukumu yake ya uchunguzi wa masuala/malalamiko ya ukiukwaji wa haki za binadamu na kuwezesha hatua kuchukuliwa.

Hata hivyo, ili Tume iweze kuonyesha uhalali kwa vitendo wa kuongezewa fedha lazima kwenye malalamiko yaliyotangulia lazima kuonyesha tija ya Tume. Nimesikitishwa na utendaji wa Tume ya Haki za Binadamu kwa kuwa nilifungua malalamiko kwa niaba ya wananchi lakini miaka inapita sijapewa ripoti ya uchunguzi wa Tume.

Mheshimiwa Spika, hivyo katika majumuisho ya bajeti ya Wizara hii naomba kupatiwa nakala ya ripoti ya uchunguzi ambao Tume iliufanya juu ya uvunjaji wa haki ya wananchi wa Goba kupata haki ya kupata maji safi na salama. Pia kwa uchunguzi ambao Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora kwenye mauaji ya Mwanahabari David Mwangosi, Wizara ya Katiba na Sheria na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika majumuisho inaeleza ni mapendekezo gani yametekelezwa mpaka sasa na iwapo Serikali haina dhamira ya kutekeleza mapendekezo yaliyobainika kwenye ripoti ya Tume ifungue mashtaka Mahakama Kuu au hata Mahakama ya Haki za Binadamu ya Afrika yenye makao makuu yake Arusha.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Katiba na Sheria inashughulikia masuala ambayo ni mihimili ya nchi na yenye athari/taswira kwa maisha ya wananchi. Hata hivyo mapitio ya utekelezaji kwa mwaka 2013/2014 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2014/2015 yanaonyesha dira na dhima ya Wizara ya kuwezesha upatikanaji haki kwa watu wote na kwa wakati haitafikiwa iwapo udhaifu unaojirudia, uliojirudia na utakaojirudia hautadhibitiwa.

Mheshimiwa Spika, katika muktadha huo, wakati wa majumuisho ya mjadala wa Bajeti ya Wizara hii Waziri atoe majibu/ufafanuzi kuhusu masuala yafuatayo:-

Mosi, sababu za Wizara kushindwa kuratibu vizuri mchakato wa Mabadiliko ya Katiba na hatimaye imechangia kwenye mchakato ukwame. Waziri na Katibu wa Sheria aliyetangulia na Mwanasheria Mkuu wa Serikali alishiriki majadiliano kati ya Vyama na Rais. Hata hivyo, katika kuandaa Miswada ya Marekebisho ya Sheria ya Katiba na Muswada wa Kura ya Maoni, Waziri wa Katiba na Sheria na Mwanasheria Mkuu wa Serikali hawakuzingatia masuala ya msingi ambayo yangeweka mstari wa mbele maslahi ya nchi na kuwezesha muafaka wa kitaifa katika mchakato wa Katiba mpya.

Mheshimiwa Spika, hali hii ya viongozi wa Wizara kushindwa kutumia fursa walizonazo kuwezesha muafaka wa kitaifa katika mchakato wa Katiba Mpya, hata wakati wa Bunge Maalum ambapo Waziri wa Katiba na Sheria na Mwanansheria Mkuu wote walikuwa Wajumbe.

Mheshimiwa Spika, hivyo kama Wizara ya Katiba na Sheria haiwezi kutumia nafasi yake kutoa fursa ya maridhiano ili mchakato wa Katiba uendelee kwa kujikita katika kujadili Rasimu iliyowasilishwa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba kwa kuzingatia maoni ya wananchi badala ya kupenyeza msimamo wa CCM ambao Waziri anaufahamu. Hii ni kwa sababu mwaka wa kwanza wa CCM uliotaka kupenyeza msimamo wa CCM kuanzia Rasimu ya Kwanza ulipotolewa kwa nyakati mbalimbali kabla ya kuwa Waziri wa Katiba na Sheria aliwahi kuwa Mkurugenzi wa Mambo ya Nje wa CCM na hivyo Mjumbe wa Sekretarieti ya CCM iliyoomba nyaraka hizo. Kama Wizara hii kwa kushirikiana na Waziri Mkuu haiwezi kuwezesha maridhiano basi Rais aagize Muswada wa Sheria uletwe Bungeni na kufuta Bunge Maalum lenye muundo wa sasa na badala yake kuundwe Bunge Maalum litakaloheshimu maoni ya wananchi na Rasimu iliyowasilishwa kutokana na maoni hayo.

Mheshimiwa Spika, aidha kuwasilishwe Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Kura ya Maoni ili kuwezesha Tume ya sasa ya Uchaguzi isisimamie kura hizo bali Tume Huru. Pia wananchi wakiikataa Rasimu, Bunge Maalum mbadala liweze kurekebisha Rasimu.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hivi sasa kama Taifa tunaendelea na mchakato wa kuandika Katiba Mpya hoja ambayo imewasilishwa katika Bunge Maalum la Katiba na Serikali na kufikia hapo tulipofikia ningependa kujua ni kwa nini Serikali imejielekeza kupata suluhu na maridhiano na vyama vya siasa kwa ujumla wake badala ya kupata maridhiano na Watanzania kwa ujumla wao na kuamua muundo gani Watanzania wanauhitaji badala ya vyama vya siasa vinataka nini, kulingana na Ilani za Vyama vyao, huku mkitambua idadi kubwa ya Watanzania hawafungamani na vyama vya siasa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo kero ya muda mrefu ya ucheleweshaji wa kesi na mrundikano wa mahabusu katika magereza mengi nchini na hususan kesi za mauaji, ni hatua zipi za makusudi zimechukuliwa kupunguza na kuondoa kabisa kero hii?

Mheshimiwa Spika, majengo na vitendea kazi katika Mahakama zetu na katika eneo hili nizungumzie mahsusi Mkoa wa Katavi na Wilaya zake. Mji wa Mpanda ndiyo makao makuu ya Mkoa, katika Mji wa Mpanda hatuna majengo ya Mahakama katika ngazi zote kuanzia Mahakama ya Mwanzo hadi Mahakama Kuu. Majengo yanayotumiwa hayana hadhi, hayatoshi kwa nafasi na kwa ngazi ya Mahakama husika Mahakama ya Wilaya na vikao vya Mahakama Kuu vinafanyika katika majengo yaliyokuwa *Liwali Court* na baadaye Mahakama ya Mwanzo ndiyo yanayotumika kama Mahakama ya Wilaya. Mahakama ya Mwanzo inatumika katika jengo lililokuwa la starehe la wataalamu wa madini wa Kirusi hapo Mpanda Mjini.

Mheshimiwa Spika, Mahakama nyingi hazina vitendea kazi vya kutosha katika ngazi zote, mishahara duni na makazi kwa ajili ya Mahakimu katika ngazi zote pia Majaji.

Mheshimiwa Spika, matarajio yangu kuna majibu ya kukabiliana na changamoto hizi.

**MHE. MESHACK J. OPULUKWA:** Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kesi za mauaji, kwa nini Serikali isiache kutajwa kwa kesi hizi katika Mahakama za Wilaya ili ikifikia sasa wakati wa *commital* ndiyo zihamishwe Mahakama Kuu.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kuwafanya watuhumiwa kujua kila kinachoendelea kuhusu kesi zao hatua kwa hatua maana watakuwa wanapelekwa Mahakamani kwa wakati na kila mara kwenye Mahakama za Wilaya?

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji kwa utendaji mzuri na kwa kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 iliyopo ya Tanzania inaruhusu mtoto wa kike kuolewa akiwa na umri mdogo, anaruhusiwa kuolewa akiwa na miaka 13 kwa ridhaa ya wazazi na miaka 15 kwa ridhaa yake, wakati huo huo Sheria ya Elimu ya mwaka 1978; sera na kanuni zinamtaka kila mtoto aliyefikisha umri wa kwenda shule mtoto huyu anaanza darasa la kwanza akiwa na umri wa miaka saba hivyo anamaliza darasa la saba akiwa na miaka 14 na kidato cha nne akiwa na miaka 18.

Mheshimiwa Spika, Tanzania inazingatia haki za binadamu lakini tendo la kuwaoza watoto wadogo ni ukiukwaji wa haki za binadamu. Ni aibu hadi leo sheria zetu zinaruhusu kuoza watoto wadogo. Tendo la kumuoza akiwa na umri mdogo linasababisha:-

(1) Akose elimu na hivyo kuishia kuwa maskini.

(2) Kuathirika kisaikolojia.

(3) Kupata matatizo makubwa ya kiafya kama fistula hata kifo.

(4) Kinaichafua Tanzania kwenye uso wa dunia.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anieleze ni lini sheria hii mbaya itafutwa au kurekebishwa?

Mheshimiwa Spika, kuhusu sheria iliyopitishwa na Bunge hili na ikaruhusu mfuko wa kuchangia na kuchochea maendeleo ya Jimbo *(Constituency Development Catalyst Fund) ni* sheria baguzi, ni sheria mbaya kwani inawatenga Wabunge katika makundi na inawabagua Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Wabunge Viti Maalum wanafanya kazi kubwa sana, wanasaidiana na wananchi kuchangia maendeleo, kuibua miradi na kutatua kero, ili wachangie miradi hii wao wanakopa benki kitu ambacho si sawa. Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mkoa na Wabunge wa Jimbo wana mifuko, je, ni lini sheria hii mbaya italetwa hapa Bungeni ikarekebishwa ili kuondoa huu ubaguzi?

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuuliza ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Ludewa, Kata ya Masasi ni lini utakamilika? *This is the forth budget since it was planned, but so far no Big Result Now*. Kwa nini mahabusu Arusha wanavua nguo na wanalalamika sana?

Mheshimiwa Spika, Wabunge hatujapata repoti ya *Legal Human Right Centre (LHRC)*. Naomba nipatiwe *black log* ya kesi hali inakwendaje? Lazima Wizara iweze kubuni utaratibu wa kumaliza kesi mapema kama nchi ya Botswana, *please justice should not be delayed.*

Mheshimiwa Spika, nashauri Wizara ifanye ziara katika Gereza la Isanga, Dodoma kwa wanawake *(urgent)*.

Pia *trainig* kwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo/Wilaya ni jambo muhimu sana semina/*workshop for capacity bulding.*

Katika Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Bunge tulikubaliana na suala zima la matumizi ya *Hansard* wakati wa ku-*record court procedures,* je, hatua imefikia wapi? *Justice* imefika wapi?

Mheshimiwa Spika, Marekebisho ya Sheria ya Mtoto kuruhusiwa kuolewa na umri wa miaka 13 imefikia wapi?

Mheshimiwa Spika, je, utaratibu wa kutafsiri kila Muswada na Sheria hususani mpya umefika wapi? *Attorney General* katika ukurasa wa 21 wa hotuba inasema Wizara imetafsiri sheria saba, kwa maoni yangu ni chache sana *speed up!* Sheria hizi zilikuwa *reported* hivi hivi kwenye *budget* ya mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, mengine tutaendelea kuwashauri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fedha za matumizi ya Bunge la Katiba kwa mujibu wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inapaswa kutoka *Consolidated Fund*. Kuhusu kauli za Mawaziri wawili zina-*differ,* kuna fedha zinaidhinishwa/kuna fedha zinazotolewa/kuna fedha zinazoonyesha matumizi halisi hivyo fedha hizi hatofautiana kutokana na tafsri kamili ya matumizi ya fedha. Aidha napongeza sana matumizi madogo ya Bunge la Katiba ikilinganishwa na matumizi ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba shilingi bilioni 40.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa upana sana juu ya uhaba/ukosefu wa Mahakama katika Wilaya ya Rorya.

Mheshimiwa Spika, izingatiwe kuwa Rorya ni Wilaya mpya hivyo nilitarajia hadi mwaka huu wa fedha ingekuwa kwenye ujenzi kwani Gazeti la Mwananchi la tarehe 12.5.2014 nilisoma tangazo la Serikali juu ya azma yao ya kujenga/kutangaza *tender* kwa ajili ya ujenzi wa Mahakama kwenye baadhi ya Wilaya, cha ajabu Rorya haimo kwenye orodha. Wananchi wa Wilaya ya Rorya wanapata shida sana kuja kutafuta huduma za kimahakama Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Spika, hii si tu inatoa usumbufu bali pia ni gharama kwa Mtanzania wa kawaida. Izingatiwe na geographia ya Rorya na Tarime hasa kuomba miundombinu ni mbovu sana. Hivyo napenda kuelezwa kwa kina ni nini kinapelekea kutoiweka Rorya kwenye ujenzi wa Mahakama licha ya kuliangalia hili suala muda wote. Ikumbukwe kuwa Rorya haina hata gereza na hii inapelekea kupata mtazamo hasi juu ya Serikali ya CCM. Rorya haina huduma yoyote ya Kimahakama na Gereza.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana wakati nachangia hotuba hii niligusia wimbi la ubambikaji wa kesi ambapo polisi hakaa na mtu bila kosa lakini baadaye humuomba hongo ya shilingi 300,000/= hadi shilingi 500,000/= kama huna hubambikwa kesi na kunyimwa dhamana. Hii inapelekea Gereza la Pinne kujaa kinyume kabisa na haki za binadamu kwani mrundikano ni mkubwa mno kitu ambacho hupelekea wafungwa au mahabusu wale ambao hawajala kuambukizwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho ningependa kujua Wizara hii ya Katiba na Sheria imechukua hatua gani kufuatia mauaji ya wanawake kule Butiama, mauaji ya wananchi wa Nyamayo/ wananchi wa Tarime waishio/kujishughulisha katika maeneo ya Nyamayo ambao wamekuwa wakiuwawa takribani kila wiki walau watu wawili, hii haikubaliki na ni kinyume cha haki za binadamu. Napenda kusikia maoni ya Wizara hii juu ya mauaji hayo niliyoyataja hasa yafanywayo huko Nyamongo.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwa kuwa Wizara hii ndiyo inashughulika na Katiba ni vyema niishauri Serikali kuheshimu maoni ya wananchi, hivyo kufuata misingi/heshima iliyotolewa Bungeni kwa ajili ya sisi tu na wananchi wengi wanaopata adha hii.

Mheshimiwa Spika, tatu nizungumzie suala zima la watoto kukaa/kulala gereza la wakubwa kwa mfano katika Gereza la Tarime lina mchanganyiko wa watoto na watu wazima na hivyo hii kuleta adha inayopelekea vijana hawa kulawitiwa.

Mheshimiwa Spika, vilevile napenda kugusia juu ya suala zima la ucheleweshaji wa usikilizwaji wa kesi, vilevile ingeweza kutolewa adhabu ya nje hasa kwa wale wenye makosa madogo madogo hata kupewa dhamana na hii itasaidia sana kupunguza mrundikano wa mahabusu katika magereza.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa utashangaa hata kesi yenye dhamana mtuhumiwa hapewi dhamana, hii si haki na hii yote ni sababu ya rushwa kukithiri katika pande zote yaani kwenye

Sheria na Katiba, pamoja na Wizara ya Mambo ya Ndani. Naomba hili jambo lipewe mkazo ili tupunguze idadi ya mahabusu hasa katika Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa jinsi mnavyofanya kazi zenu vizuri sana. Pia niwape pongezi za kipekee kwa jinsi mlivyowajibika wakati wa Bunge la Katiba.

Mheshimiwa Spika, Waziri ulifanya kazi kubwa ya kutoa elimu ya Rasimu ya Katiba kwa makundi mbalimbali, elimu ambayo wengi ilitusaidia sana katika kuwasilisha maoni yetu wakati wa mchakato huo. Wizara inafanya kazi vizuri japokuwa kuna changamoto nyingi sana na hasa katika upande wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2011 mpaka leo nimekuwa nikiuliza lina Serikali itajenga Mahakama za Temeke, Mbagala, Magomeni na Ilala? Hali ya Mahakama hizi ni mbaya na haziendani na hadhi ya Jiji la Dar es Salaam. Naomba nipewe taarifa sahihi ni lini Mahakama hizi zitajengwa?

Mheshimiwa Spika, changamoto nyingine ni kuhusu sheria za uwekezaji. Wawekezaji wengi wameingia mgogoro na wananchi na kupelekana Mahakamani kutokana na mikataba kutofikiwa. Kinachosikitisha ni hukumu zinazotolewa si za kuwasaidia Watanzania katika nchi yao na ardhi yao na kuwapeleka kusikoeleweka. Mfano naweka wazi maslahi yangu kuwa ni mfanyabiashara na ninayo kesi na mwekezaji toka mwaka 2005 mpaka leo hii. Kesi ya Mahakama ya Ardhi Na. 34/2006 Mariam dhidi ya *Kobil (T) Ltd.*

Mheshimiwa Spika, hukumu iliyotolewa nimeamrishwa nimlipe mwekezaji takribani shilingi bilioni 1.6 na niondoke kabisa katika eneo langu ambayo ni ardhi yangu na yeye mwekezaji ame-*lease* tu.

Mheshimiwa Spika, shitaka langu lilikuwa ni kwamba mkataba haukufikiwa kwa kuwa waliniambia wangenijengea maduka, *pharmacy* na ofisi nyingine za kupangisha lakini vitu vyote hivyo havijajengwa mpaka leo hii kitu ambacho mimi kama Mtanzania ningefaidika kwa kuniachia majengo hayo. Ardhi inapanda thamani kila siku wao wamenilipa shilingi 148,000,000/= tu. Ni matarajio yangu Mahakama itampa haki kwa kuwaelekeza wawekezaji wafanye vile tulivyokubaliana kulingana na mkataba wetu. Badala yake unanitaka nilipe shilingi bilioni 1.5 kwa mwekezaji na kunitaka niondoke kabisa, kama si kukata rufaa kwenda Mahakama ya Rufaa, leo hii ningekuwa wapi?

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na vijana wengi mahabusu wanasubiri kwenda Mahakamani lakini kesi zao ni ndogo ndogo tu. Gharama za kutunza mahabusu ni kubwa sana, ni vyema Serikali sasa ingeweka utaratibu wa kutoa uamuzi haraka au kuweka Mahakama maalum ya kuwapeleka mahabusu hao kama vile Mahakama ya Jiji inavyofanya.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kuzidi kwa uhalifu katika Jiji la Dar es Salaam ndiko kunawazidishia kesi Mahakimu wetu. Niipongeze Serikali kwa mkakati wake wa kufanya *operation* ya kuzimaliza kesi zilizorundikana. Mkakati huo usiwe na muda, nashauri uwe endelevu kwani umesaidia kwa kiasi kikubwa sana.

Pia nipongeze kwa Mahakama ya Ardhi kutumia majengo ya NHC, huu ni uzalendo mkubwa sana, mngeweza kupanga jengo la mtu binafsi, ni lazima Serikali kuunga mkono juhudi za Mashirika yake. Niombe wengine wafuate mfano huu.

Mheshimiwa Spika, pia posho za Mahakimu na Majaji ni vyema wakapewa kwa wakati ili waweze kufanya kazi yao kwa amani.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha kwa kuunga mkono hoja asailimia mia moja kwa yale yaliyopangwa yatekelezwe na ushauri wangu uzingatiwe.

**MHE. JANET Z. MBENE**: Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Maofisa wa Wizara ya Katiba na Sheria kwa kazi kubwa wanayofanya kusimamia utawala wa sheria nchini. Naomba niwapongeze kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu uko katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu kushindwa kesi Serikali inapokuwa inadaiwa na watu/kampuni binafsi hasa zile za Mashirika ya Umma. Kumekuwa na mwelekeo usio mzuri wa hali hiyo inayolipotezea Taifa fedha nyingi na kulivunjia heshima Taifa. Mara nyingi Mawakili kwa upande wa Serikali hawakuwa makini katika kutayarisha *defence* zao, kutumia vifungu vya sheria sahihi na baya zaidi hata kufika Mahakamani siku ya kusikilizwa kesi hizi, kuna tetesi hata za kushirikiana na upande wa pili. Tafadhali Wizara iweke *performance monitoring* kwa Mawakili wa Serikali ili wale wanaopoteza kesi kila mara wachukuliwe hatua za kinidhamu kwa kushindwa kazi hasa inapothibitika kuwa wamezembea au kushiriki makusudi kushindisha kesi.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo ningependa kuona Wizara inalifanyika kazi ni suala la haki za watoto wanaowekwa kwenye vituo vya watoto (watukutu).

Mheshimiwa Spika, watoto hawa wengi hawana makosa yoyote, lakini hata kama wana makosa ni vyema wangeshughulikiwa mapema ili wasikae muda mrefu kwa sababu kukaa mbali na familia zao huwaathiri sana. Wawekewe utaratibu maalum wa kusikilizwa masuala yao mapema iwezekanavyo, ikiwezekana wafanyiwe *screening* na Ustawi wa Jamii na *Para Legal Officer* ili wale ambao hawana kesi waruhusiwe.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni lile la haki za watoto wa kike na kwa kiasi kidogo wa kiume wanaonyanyaswa kijinsia, kubakwa na kulawitiwa. Bado suala hili lina usiri wa kupindukia na jamii haijaweza kuwa na msaada kwa jamii zinazoathiriwa na makosa haya. Sheria ipo, lakini bado zile hukumu zilizowekwa hazitumiki kikamilifu. Wizara ishirikiane na Ustawi wa Jamii, NGOs na vyombo vya dini kutengeneza programu ya kusimamia suala hili kwa jumla.

Mheshimiwa Spika, naomba kuzungumzia suala ya sheria ya ndoa na mirathi inayokinzana na sheria za kimila kuhusiana na umri wa mtoto wa kike kuolewa na ile *SOSPA* zinakinzana. Lini Wizara itaziainisha na kuleta Muswada ili zibadilishwe?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, wanawake wengi ambao ni wajane wanateseka sana wanapokuwa na kesi Mahakamani. Wengi wao kwa kutojua jinsi ya kupata Wakili wamejikuta wananyanyasika sana kwa kukosa haki zao pale wanaposhindwa kusimamia masuala yao ya kesi Mahakamani wao wenyewe.

Mheshimiwa Spika, mjane Mama Ruth Langaeli anayeishi Msitu wa Mbogo Wilayani Meru huko Mkoani Arusha amejikuta akipiga mguu katika Mahakama moja mjini Arusha tangu mwaka 2011 hadi leo mwaka 2014 bila ya mafaniko yoyote. Mjane huyu ambaye shamba lake

la migomba lilivamiwa na mtu aliyejiita mwekezaji, migomba yake zaidi ya ekari tatu ilikatwakatwa pamoja na miti mikubwa ya matunda.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Mtaa haikuweza kumpa msaada wowote ingawa kijiji kinafahamu kwamba mjane Ruth ameishi pale kijijini tangu mume wake akiwa hai. Kwa kukosa Wakili kutokana na hali yake ya maisha ambayo hairidhishi, mjane huyu aliamua kufungua kesi mjini Arusha ambapo imemchukua miaka mitatu na bado kesi yake haijamalizika.

Mheshimiwa Spika, mjane Ruth ni mmoja kati ya wajane wengi hapa nchini ambao hawawezi kupata msaada wa Wakili kutokana na Mawakili wengi kuwa ni wa gharama sana na wakati mwingine baadhi ya wajane hawajui jinsi ya kumpata Wakili. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wanawake wajane na hasa wale wanaoishi vijijini ambao wanapoteza haki zao kwa kutokuwa na uwezo wa kifedha na kuendesha mashtaka yao Mahakamani pale wanapokuwa wamedhulumiwa katika jamii au kudhalilishwa?

Mheshimiwa Spika, je, ni kwa nini hakuna utaratibu maalum wa Mahakama wa kuwa na kitengo maalum au dawati maalum la kushughulikia kesi za wajane tu ili kuharakisha kusikiliza kesi hizo na kuzitolea hukumu mapema?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ukurasa wa 13 kuna maelezo kwamba mashauri mengi yanayosajiliwa Mahakamani yamekuwa yakimalizika katika kipindi cha miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, suala la mjane Ruth Langaeli nililolitolea mfano hapo juu limeendeshwa kwa takribani miaka mitatu sasa na hata hakuna mafanikio yoyote ya kuonyesha kwamba kesi yake itamalizika hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, napendekeza utetezi wa dhati ufanyike kwa wanawake wajane na hasa waishio vijijini kwani wengi hali zao ni za chini, hawana uwezo mkubwa, wanahitaji msaada wa Serikali yao.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache naomba kuwasilisha.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, kwa ufupi naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mabadiliko ya Katiba, kwa kuwa jambo au suala la muundo wa Serikali ni suala la kisera, nashauri kwamba Mheshimiwa Rais ashauriwe kusitisha mchakato wa Katiba ili suala hili liamuliwe kwanza kwa njia ya kura ya maoni *(referendum)* sheria itumiwe kuwe na nafasi hiyo. Hakuna sababu ya uharaka wa kupata Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majengo ya Mahakama, kwa kuwa Mahakama nyingi nafasi ya Ofisi za Mahakimu, Majaji na Masjala hazipo, kumekuwa na mrundikano mkubwa wa majalada na watumishi kukosa pa kukaa, nashauri vyanzo vingine vitafutwe vya fedha ili Mahakama iweze kujenga majengo hayo badala ya kutegemea bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mbulu, ni la tangu ukoloni, linaweza kuanguka wakati wowote, pamoja na kwamba kiwanja cha kujenga jengo hili fedha haijapatikana hadi leo, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbulu naomba Serikali ifanye mpango ili fedha zipatikane na jengo hilo lijengwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu maadili *(code of conduct)* ya Mahakama za Mwanzo, naishauri Serikali iajiri Mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo wenye shahada. Lakini kwa bahati mbaya Mahakimu hawa wamekuwa na tabia ya kudharau, waonevu wa raia na wanadai sana rushwa, mfano mkubwa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo za Endagikot na Daudi katika Wilaya Mbulu. Naomba mamlaka husika ichukue hatua ya kurekebisha hali hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpiga chapa *(secretary)* Mahakama ya Wilaya ya Mbulu, Mahakama hii ina miaka zaidi ya saba bila ya mpiga chapa wa mashine. Wananchi wenye mashauri wanapata taabu kupata nakala za hukumu na mwenendo wa mashauri yao. Waziri wa Sheria na Msajili wa Mahakama ametoa ahadi mara nyingi bila mafaniko. Tunaomba jambo hili lipate ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Waziri wa Wizara hii, Naibu Waziri na watendaji wake kwa kazi nzuri ya kuandaa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inafanya kazi nzuri sana lakini zipo changamoto nyingi zinaikabili, kwa mfano, kutokuwa na vitendea kazi na watumishi wa kutosha kuwafikia wananchi kule vijijini, rasilimali fedha, kufanya utafiti wenye ufanisi kule vijijini na kutokuwa na ofisi kwenye ngazi za Mikoa na Wilaya zote hapa nchini ili wananchi waweze kupeleka kero zao.

Mheshimiwa Spika, Serikali itenge fedha za kutosha kwa Tume hii muhimu sana ili waweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, Bunge litenge muda wa kujadili taarifa ya Tume hii za kila mwaka ili Wabunge tuweze kushauri vizuri na pia wananchi waweze kujua masuala yao yanayotekelezwa.

Mheshimiwa Spika, bado lipo tatizo la polisi kuvunja sheria kwa kuwaweka watuhumiwa mahabusu ya polisi zaidi ya saa tatu mpaka saba. Serikali itoe maelezo kwa nini sheria zinavunjwa na kila leo tunazungumzia na hatua hazichukuliwi.

Mheshimiwa Spika, Serikali inasemaje kuhusu mahabusu waliopo rumande zaidi ya miaka sita mpaka tisa bila kupelekwa Mahakamani? Wengine walishasahau kilichowapeleka pale, wengine wameshachanganyikiwawapo tu. Kwa nini watuhumiwa wa aina hii wasiruhusiwe warudi kwao au wapewe adhabu za nje?

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke dawati la jinsia na watoto kwenye vituo vya polisi ili kusaidia wanawake na watoto wanaofanyiwa ukatili.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo utendaji wa baadhi ya madawati umekuwa mbaya kwa polisi hao kudai rushwa/kupokea rushwa na kuwaficha watuhumiwa.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine polisi wamepokea kesi ya mtoto kubakwa na badala ya kwenda kufuatilia mtuhumiwa, polisi waliagiza wale waliopeleka mtoto waende wakamkamate mtuhumiwa wampeleke polisi wao wenyewe, inaumiza sana.

Mheshimiwa Spika, hayo madawati ni muhimu sana, Wizara iweke watumishi wenye utu kwenye madawati haya pia yatolewe maelekezo na muongozo na semina za utumishi uliotukuka wa watumishi hawa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mabaraza ya Ardhi yaliyo ngazi ya Kata yanasaida sana kupunguza matatizo ya ardhi kwenye ngazi za kijiji na kata. Napendekeza Mabaraza haya yawekwe chini ya mfumo wa Mahakama ili waweze kuangaliwa zaidi na wafanyakazi kwa ufanisi zaidi kwa wanaofanya kazi ya usuluhishi katika masuala ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, suala la rushwa limeshamiri kwenye Mahakama hapa nchini, hali hii inatisha kwa sababu Mahakama ni chombo pekee cha kutoa haki kwa wananchi. Imekuwa ni kawaida kwa Mahakimu kuomba rushwa ili kusaidia watuhumiwa. Wapo wanyonge wanaoteseka na kesi zaidi ya miaka mitano mpaka kumi kwa kushindwa kutoa rushwa, wenye uwezo kesi zao hazichukui muda Mahakamani. Serikali inasemaje kuhusu suala la rushwa kwa watumishi wa Mahakama?

Mheshimiwa Spika, kesi za migogoro ya ardhi zinaongezeka kwa kasi kubwa kutokana na ukosefu matumizi bora ya ardhi. Hata hivyo Mahakimu wanaoshughulikia kesi za ardhi ni wachache sana na kanda zipo mbili tu ile ya Arusha na ya Tabora. Mahakimu hawafiki kwenye kanda hizo pale inapopangiwa tarehe matokeo yake kesi za ardhi zimerundikana kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Spika, Serikali iweke mkakati maalum katika Mahakama zote nchini kama ilivyojiwekea Mahakama ya Tanzania ili kesi zote kwenye Mahakama za kanda zimalizike kwa muda mfupi na watu wapate haki.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima napenda kuchukua nafasi hii nitoe mchango wangu wa maandishi kwenye Wizara hii nyeti iliyowasilisha hotuba yake leo hii.

Mheshimiwa Spika, katika ukurasa wa 5 hadi wa 7 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri amezungumzia mchakato wa Mabadiliko ya Katiba ambayo nchi yetu inapitia kwa sasa. Kitendo cha kuandika Katiba Mpya kwa nchi yetu baada ya miaka 50 ya uhuru ni kitendo cha historia, lakini ni kitendo kinachohitaji umakini na uadilifu mkubwa kwani Katiba ndiyo roho ya Taifa lolote lile.

Mheshimiwa Spika, mukhtadha huo ni lazima watawala ambao ni Chama cha Mapinduzi (CCM) wakubali kwa dhati mabadiliko ya kweli, vinginevyo tutakuwa tunajidanganya wenyewe tukidhani dunia na Watanzania wataona tunafanya jambo jema.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri katika umri wa miaka 50 ni kipindi kirefu, yapo mengi mazuri na mabaya yaliyotendeka ndani ya nchi yetu. Sasa ni wakati muafaka wa kukaa pamoja kwa dhati ya nafsi zetu tukaweka bayana yote na pale pa kusameheana tukafanya hivyo na yale mazuri tukayaendeleza kwa faida ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu ni wazi sasa hivi Taifa letu lina mpasuko mkubwa wa kimtazamo na kwa dunia ya leo utumiaji nguvu kuwatawala wananchi hauna nafasi tena, hivyo basi ni lazima muafaka wa Taifa ukapatikana.

Mheshimiwa Spika, tumshukuru Mungu kwamba pamoja na mpasuko uliopo kimtazamo, lakini bado Watanzania wanakaa pamoja wanazungumza, hivyo basi uitumie tunu hiyo ili tupate Katiba ambayo itajibu matakwa ya watu wetu kwa miaka mingi ijayo na hili linawezekana kama kuna nia safi, kwani Afrika ya Kusini ni mfano tosha kwetu. Muda mfupi tu

baada ya uhuru walikaa pamoja na kupata suluhu ya yaliyotendeka ndani ya ardhi yao. Iweje sisi walimu wao tushindwe? Muungano wetu una matatizo mengi toka kuasisiwa kwake, huu ni ukweli ulio wazi, ni lazima sasa kasoro hizo zirekebishwe kwa faida yetu sote.

Mheshimiwa Spika, Wanzanzibar wengi tunaamini kuwa Muungano huu ulikuwa ni wa miaka kumi tu yaani kuanzia mwaka 1964 hadi 1974 na ndiyo maana muasisi wa Muungano toka Zanzibar Hayati Abeid Amani Karume alitamba kuwa Muungano ni kama koti, tukiona linatubana tutalivua.

Aidha tunaamini kuwa kwa hiyo miaka 40 Tanganyika inaitawala Zanzibar kiujanja na kimabavu. Ni wakati sasa wa kuweka bayana hayo, kama yana ukweli au hayana tukahalalisha Muungano wetu ambao hakuna asiyeona sasa faida zake katika nyanja zote za kiusalama, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni. Fursa hii tukiichezea tutakuja kuitafuta kwa gharama kubwa ambayo sasa tumeipata bure.

Mheshimiwa Spika, napenda kushauri kuwa Katiba ndiyo sheria mama, hivyo basi viongozi wetu wote waache jazba za kivyama na wakae pamoja waangalie mustakabali wa Taifa na watoto wetu ambao kwa sasa hawana vyama. Busara inahitajika hapa na nguvu, wingi wa hadaa havitatatua suala hili kwa wema.

Mheshimiwa Spika, aidha ni mchango wangu hapa kuwa sheria zote ziangaliwe upya ili ziendane na Katiba Mpya na wakati uliopo kwani sheria zetu nyingi zimepitwa na wakati, mfano viwango vya faini haviendani na hali halisi ya sasa iliyopo. Ni vyema mambo haya yote mawili yakaenda sambamba maana ni chanda na pete.

Mheshimiwa Spika, ni wakati sasa Watanzania tukabadilika na tukaacha tabia ya kuwa wasemaji wazuri, wapangaji wazuri lakini utendaji wetu ni mbovu, maneno yetu ni lazima yaoane na vitendo vyetu.

Mheshimiwa Spika, Tanzania yenye amani ya kweli inawezekana. Ahsante.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani kwa kupata nafasi ya kutoa mchango wangu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuwapongeza Mawaziri na Watendaji wa Wizara hii, naamini wanapita katika wakati mgumu kwa kipindi hiki cha mchakato wa kutunga Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajikita katika kuonyesha changamoto kubwa ambazo zipo kwenye Wilaya au Vijijini hasa kwa wanawake.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itambue kuwa pamoja na kuboresha na kuimarisha utoaji bora wa huduma za kisheria, bado vijijini kuna tatizo kubwa la wananchi kutokujua sheria na haki zao. Kumekuwepo na uonevu mkubwa sana hasa kwa watuhumiwa ambao hawajui haki zao au namna ya kujitetea.

Mheshimiwa Spika, pia kuna wanawake wengi sana vijijini, wajane au wanaoteswa na mambo ya talaka na kadhalika kujua haki zao. Wengi wamepoteza mali bila msaada wowote. Hivyo, naiomba Wizara ijitahidi sana kuona umuhimu wa kufungua dawati la kisheria kila Wilaya ili kutoa msaada kwa wanawake ambao wanataka kufungua mirathi na kwa wale ambao wameachwa au ndoa kuvunjika ili waweze kufikisha masuala yao Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, mfano kuna mwanamke ambaye mume wake amemtelekeza na amekuwa akimwambia wewe bado ni mke wangu tu, nikikukuta na mtu nakuua, kama una uwezo nipeleke Mahakamani na ukanipe talaka, lakini ujue ukinipa talaka utanilipa kwa kuwa wewe ndiye uliyenipa talaka. Hivyo mwanamke huyo amebaki na maumivu tu asijue anaanzaje kwenda Mahakamani kudai talaka hali akijua, atatakiwa kumlipa mtalaka wake.

Mheshimiwa Spika, kweli kuna adha, huo ni mfano mdogo tu, hebu Wizara ione umuhimu wa kuliweka sawa suala hili maana kwa upande wa maeneo ya mjini kuna zile taasisi au *NGOs* ambazo zinawasaidia wanawake wa aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati na naunga mkono upya.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu kwa watu wenye ulemavu wa ngozi vimekuwa vikipigiwa kelele kwa miaka mingi sasa lakini vinaonekana kukosa ufumbuzi, bado watu wenye ulemavu wa ngozi wamekuwa wakiishi kwa hofu ndani ya nchi yao wenyewe kutokana na mauaji hayo kuendelea. Mpaka hivi sasa idadi ya watu 73 wameuawa kikatili.

Mheshimiwa Spika, naalaani vikali mauaji ya kikatili yaliyotokea Mkoani Simiyu. Mauaji hayo yaliyotokea Jumatatu ya wiki hii katika Kijiji cha Mwachalala, Wilaya ya Bariadi Mkoani humo na yamesababisha kifo cha Munghu Lugata (40) ambaye alikutwa amekufa nje ya nyumba yake na mwili wake umenyofolewa mguu, vidole viwili, mkono wa kushoto na kidole gumba.

Mheshimiwa Spika, je, ikiwa mashauri tisa ya miaka ya nyuma hayajasikilizwa mpaka hivi sasa ni lini yatasikilizwa? Hao wauaji wanapata nguvu kwa kuwa hakuna hukumu iliyotekelezwa kwa vifo vilivyopita.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ituambie inashughulikiaje tatizo hili?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, kwa miaka miwili mfululizo nimekuwa nawauliza ni kwa nini Mahakama ya Wilaya ya Kasulu inafanyia vikao vyake ndani na hivyo kuwanyima haki wananchi fursa ya kushuhudia namna na kiasi gani haki inatendeka?

Wizara kupitia Mheshimiwa Angella Kariuki na Mheshimiwa Mathias Chikawe wamekuwa wakijibu kwamba watahakikisha hali hiyo inakoma, naomba kauli ya Serikali ni kwa nini hadi sasa bado hali hiyo ipo vilevile.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara iliahidi kulipanua jengo la Mahakama ya Wilaya lakini hakuna lolote, kwa nini Wizara inaahidi uongo?

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo ya kina.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza kumshukuru Mungu kwa kupata fursa hii ili nami niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria ya mwaka 2014/2015. Vilevile nichukue fursa hii pia kuwapongeza Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha mamlaka zote ambazo zipo chini yake zinafanya kazi kwa mujibu wa sheria zilizowekwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kuanza kuchangia suala zima la Katiba. Tangu mapema mwezi Februari, 2014 wakati kiasi kikubwa cha takwimu zilipokusanywa, Watanzania wengi wamefuatilia mjadala katika Bunge la Katiba kuhusu Rasimu ya Pili ya Katiba.

Wakati mjadala umevuta hisia za wengi na kutangazwa kwa upana na vyombo vya habari, mwelekeo wa mjadala mara nyingi umeonekana kuwagawa Wajumbe pande mbili na kuchukiza umma, huku ukiibua maswali kuhusu viwango vya Bunge la Katiba kuhudumia na kutetea maslahi ya umma. Hakika suala la kuhoji kama maoni yaliyokusanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba yanawakilisha matakwa ya umma limekuwa suala la mabishano.

Mheshimiwa Spika, maoni ya wananchi ni muhimu pia kwa sababu bila kujali nini kinaamuliwa na wawakilishi kwenye Bunge la Katiba, watu watakuwa na uamuzi wa mwisho wakati Rasimu ya Katiba inapigiwa kura ya maoni. Hivyo basi, wananchi wa kawaida wanafikiri na kupendelea nini hasa? Nguvu ya hoja yangu ni kwamba natoa takwimu za kuaminika juu ya mapendekezo ya wananchi kutoka pande zote za Muungano, kwa kutumia mbinu ambazo ni huru na makini kisayansi.

Mheshimiwa Spika, takwimu hizi zinatoa fursa kwa Wajumbe wa Bunge la Katiba na wananchi kwa ujumla kutafakari kwa makini juu ya jambo hili na kujenga upya mufaka wa kitaifa. Idadi kubwa ya wananchi wanataka kuwa na Katiba inayoakisi muafaka mpya kati ya dola na wananchi. Masuala yanayohusiana na matumizi ya madaraka, kupata habari na udhibiti wa viongozi na watumishi wa umma yanaungwa mkono na wananchi wengi nchini kote, masuala haya ni pamoja na mtumishi wa umma kutoshiriki kufanya maamuzi juu ya kitu au shughuli yoyote ambayo ni ya manufaa binafsi, watumishi wa umma wanatakiwa kutangaza na kuwasilisha orodha ya mali zao na madeni na watumishi wa umma kutoruhusiwa kumiliki akaunti ya benki ya nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo mengine kama hayo ni pamoja na wananchi kutaka mambo ya mikataba yawekwe wazi ili kila mtu aweze kuyaona na kujua Serikali imekubaliana nini katika mikataba hiyo. Pia kuna uungwaji mkono mkubwa kutoka kwa wananchi wanaotaka kuona uwanja wa siasa, kanuni huru za vyama vya siasa na sheria zinazotoa fursa za kugombea zinatoa haki zaidi kwa wananchi, kama vile ya wagombea binafsi kugombea kwenye uchaguzi, kuanzisha chombo cha kusimamia uchaguzi ambacho ni huru kabisa, Wabunge kutoteuliwa kuwa Mawaziri katika Serikali na Spika na Naibu Spika wa Bunge kutokuwa wanachama wa chama chochote cha siasa. Haya yanaonesha kuwa wananchi wanataka kuwe na utaratibu wa kina zaidi wa dola kudhibitiana na kuwa na taasisi za Serikali kama vile Tume ya Uchaguzi na Bunge vikifanya kazi kikamilifu kusimamia na kudhibiti Serikali.

Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba mchakato wa Bunge la Katiba hadi sasa umetawaliwa na hoja kuhusu utaratibu wa kanuni na muundo wa Muungano, badala ya masuala haya yanayowagusa zaidi wananchi, ni jambo la kusikitisha.

Mheshimiwa Spika, Bunge la Katiba na viongozi wa Serikali na Vyama vya Siasa wakitaka kuvitendea haki vipaumbele vya watu, watafanya vyema kuyapa umakini wa kutosha masuala haya yanayohusiana na uwajibikaji kwa umma.

Pamoja na haya, matokeo ya utafiti wangu yanathibitisha kuwa wananchi wamegawanyika juu ya muundo wa Muungano. Tanzania Bara asilimia 43 wanaunga mkono pendekezo la uwepo wa Serikali tatu, wakati Zanzibar asilimia 80 wanaunga mkono Serikali tatu. Aidha, asilimia 53 ya Wazanzibar inaonesha kuwa kuikubali Rasimu ya Pili ya Katiba itategemea pendekezo hili. Iwapo Rasimu ya mwisho ya Katiba itarejea kwenye Serikali mbili na kwa kuzingatia yaliyosemwa na wananchi sasa (Februari, 2014) haikuwa wazi kama wananchi wengi kutoka pande zote za Muungano wataunga mkono Katiba Mpya.

Mheshimiwa Spika, njia moja ya kutoka kwenye mkwamo huu ni kutumia taswira ya masuala ya msingi ya utawala ambayo ni vipaumbele vya wananchi pande zote mbili za Muungano kama vile ni nani ana haki ya kujua nini, umiliki wa rasilimali za umma na uwajibikaji wa watumishi wa umma kuelewa muundo wa Muungano una maana gani zaidi kuliko kujikita kwenye misimamo ya vyama. Kwa namna nyingine, tunaweza kujiuliza muundo wa Serikali Mbili au Tatu una maana na athari gani kwenye masuala kama vile haki na usalama wa kumiliki mali, uhuru wa kujieleza, haki ya kupata huduma za msingi, mshikamano wa kijamii na haki za wachache?

Mheshimiwa Spika, jinsi ya kutatua hali hii si jambo rahisi, lakini huo ndiyo wajibu unaotakiwa wa uongozi. Uongozi wa kweli siyo kutetea kwa nguvu msimamo na maslahi yako mwenyewe, lakini kudadisi mitazamo na maoni mbalimbali na kujenga makubaliano mapya kulingana na kanuni za msingi na maslahi ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi wamekuwa hawajui haki zao za Kikatiba, ni jambo la kusikitisha sana kwani mwananchi anatakiwa kujua haki zake Kikatiba, hivyo naiomba Serikali kuchukua hatua za awali kuwaelemisha wananchi masuala mbalimbali ya haki zao Kikatiba ili kuwawezesha kuzijua na kutokuyumbishwa na mtu yeyote katika jambo lolote linalohusu haki zao. Jambo hilo litasaidia upotoshaji unaofanywa na baadhi ya wanasiasa kwa wananchi na hivyo wananchi kuwaamini wapotoshaji hao kwa kutojua haki zao za msingi Kikatiba, jambo hili lifanyike kuanzia kwenye vijiji, vitongoji mpaka Wilaya na Mijini ili watu wajue haki zao na wasiishi kama si Watanzania kwa kuogopa kuhoji baadhi ya mambo.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie hali ya Jimboni kwangu Kibaha Vijijini.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kibaha Vijijini wamekuwa wakipata shida sana kwa kukosa Mahakama maeneo ya jirani, kwani wamekuwa wakitembea umbali mrefu kuja kusikiliza mashauri ya Mahakama Mlandizi huku wakitumia gharama zao na kuacha shughuli zao za kiuchumi. Hali hiyo huwa mbaya zaidi pale kesi zinapoahirishwa kila mara na hivyo kuendelea kutumia muda mwingi kuja Mahakamani na kuacha kazi zao za kiuchumi. Kata ya Ruvu hakuna Mahakama na hivyo tatizo hilo bado limeendelea kuwa kero kwa wananchi kwa kutembea umbali mrefu kuja kusikiliza mashauri ya kesi zao mbalimbali, hali inazidi kuwa ngumu hata kwa mashahidi wengi kutokana na umbali wa Mahakama, wamekuwa wanagoma kwenda kutoa ushahidi kwani huwa wanatumia gharama zao na hivyo kuacha shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, hali hii imekuwa ni kero kubwa Jimboni kwangu na nimekuwa nikiisema hapa Bungeni toka mwaka 2011 hadi leo hii bila matumaini yoyote. Watumishi wa Mahakama wamekuwa wakitembea takribani kilomita 70 kutoka Mlandizi kwenda Magindu kwa ajili ya kutoa huduma za kimahakama na hufanya hivyo katika mazingira magumu kwani wamekuwa hawana usafiri wa uhakika wa kuwawezesha wao kufika sehemu hizo na kutoa huduma za msingi na kisheria kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mahakama yetu ya Mlandizi ipo katika hali mbaya sana kwani jengo lake ni chakavu sana na la kukodi, hivyo kupelekea hata utunzaji wa nyaraka mbalimbali za kimahakama zimekuwa zikitunzwa katika hali ambayo si ya kuridhisha kabisa. Watumishi wake wamekuwa wakiishi katika hali duni sana na hivyo kutilia shaka hata utendaji wa kikazi kama kweli wanaweza kuepuka kushawishika na vitendo vya rushwa.

Naiomba Serikali kuwaboreshea watumishi hawa mazingira yao ya kufanyia kazi, pia Serikali katika bajeti ya mwaka huu naiomba iweze kuturekebishia jengo letu la Mahakama Mlandizi ili lilingane na hali halisi na sehemu ya kutoa haki kwa wananchi kwani lipo kwenye hali mbaya sana hivi sasa. Namuomba Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri aje wafanye ziara na kujionea hali halisi. Ukiacha watumishi wa jimboni kwangu pia watumishi wa Idara ya

Mahakama sehemu mbalimbali wamekuwa wakiishi maisha duni na hivyo kuwafanya wengi kujiingiza katika vitendo vya upokeaji wa rushwa na kufanya haki kutokutendeka kwa usawa. Naishauri Serikali kuliangalia jambo hili kwa mapana makubwa na hivyo kuhakikisha haki inatendeka kwa usawa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa, sasa natoa saa moja na nusu kwa wajibuji hoja, kwa maana ya *AG* 20, Naibu 20, Waziri 50. Nani anaanza kati ya wale wa ishirini, ishirini?

*AG,* naomba sogea mbele!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kukushukuru wewe kunipa nafasi hii na jinsi ambavyo unaendesha shughuli za Bunge hili. Lakini pili niungane na Wabunge wenzangu kuwapongeza Wabunge wapya waliofanikiwa kupata nafasi hii katika chaguzi ndogo za Majimbo; Jimbo la Kalenga, Jimbo la Chalinze na kule Chambani. Ninavyowaona Waheshimiwa hawa ni vijana na mawazo yangu kwenu, ushauri wangu kwenu ni kwamba jifunzeni kwa bidii, chukueni busara za wenye busara, safari yenu ya kisiasa itakuwa na maana kama mtajifunza kwa utulivu. Msitangulize maslahi yenu na jifunzeni maradufu kwamba ni vizuri pia kuheshimu mawazo ya watu ambao wanatofautiana na nyinyi. Pia jifunzeni kuvumilia na kutafiti katika kutetea hoja zenu bila hofu na mashaka na la mwisho jifunzeni tabia njema ya kutokuwa vijana wazushi.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru Wabunge wote ambao wamesema maneno mazuri kuhusiana na Wizara, lakini pia kuhusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaani Fungu la 16 na Fungu la 35 - Mwendesha Mashtaka wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekuwa na utulivu kiasi hiki kwa muda mrefu kwa sababu ya imani ya wananchi katika mtindo wa utawala wa nchi yetu. Kwa hiyo, si kweli kama nilivyosikia katika maandiko ya Kambi ya Upinzani Bungeni kwamba nchi inaparaganyika, sijui ni neno gani hilo. Nchi yetu haiparaganyiki na ndiyo maana baada ya miaka hamsini tunakwenda kwenye utaratibu mwingine wa mchakato wa Katiba mpya na namshukuru sana Mheshimiwa Wassira kwa hayo aliyosema na sitarudia.

Mheshimiwa Spika, pili, wanafahamu na nafikiri hata ndugu yangu Mheshimiwa Halima Mdee, Mahakama za Tanzania kama mhimili zimekuwa katika hatua ya mbele sana katika Afrika na katika dunia kutetea haki za binadamu na watu hata wakati ambapo kulikuwa na utawala wa Chama Kimoja.

Mheshimiwa Spika, kuna rekodi wasomi wameandika kuhusiana na hayo na Serikali wakati mwingi imebwagwa Mahakamani kwa *judgments* ambazo zimetolewa bila hofu na mashaka. Kwa hiyo, si vizuri kulinganisha haya yanayosemwa na Waheshimiwa Wabunge ambao ndiyo msingi wangu wa kuwaonya au kuwaasa Wabunge vijana wasiwe kama wao.

Mheshimiwa Spika niliambiwa nizungumzie kuhusu Katiba mpya. Tarehe 20 Februari hapa mbele niliposimama nilitoa muhadhara kwenye Bunge la Katiba, kuhusiana na mamlaka ya Bunge hilo na mwisho wa mamlaka yake. Nilishangiliwa na mmoja wa watu walionishangalia alikuwa ni Halima Mdee dada yangu, nikaulizwa maswali nikayajibu.

Mheshimiwa Spika, nikatoka nje pale nikapewa mikono na Waheshimiwa Wabunge, lakini msingi wangu ni kwamba na mpaka leo nasema, Katiba mpya itapatikana kwa maridhiano, haitapatikana kwa kuasi kwa sababu utaratibu tuliojiwekea wa kuzungumza,

tulipotunga Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ni kuzungumza kwa hoja, tena Mwenyekiti wa Kamati kubwa anasema siyo. Huu utakuwa ni utaratibu ambao haufai kwamba wewe ukishindwa hoja unatoka kwa sababu Mheshimiwa Wassira ameshazungumzia hiyo, sitazungumza.

Mheshimiwa Spika, ninachorudia tena na nawaomba Watanzania wafahamu kwamba Sheria ya Mabadiliko ya Katiba iliweka ukomo wa mamlaka ya Bunge la Katiba. Ukomo huo hauhusiki na hoja kwamba Bunge hilo halikuwa na mamlaka ya kubadilisha Rasimu ya Katiba. Narudia tena ndivyo nilivyosema wakati ule na ndivyo ninavyosema sasa na ndivyo nitakavyosema kesho na kesho kutwa.

Mheshimiwa Spika, kwenye mtandao kuna watu wana maoni. Baadhi ya watu hao nawafahamu na nilisoma nao najua uwezo wao wa kufikiri. Katika *stage* hii kwamba mahali mnabishana si lazima mwende kwa mwalimu asahihishe, wasingeweza kuthubutu, lakini kwa sababu kila mtu anaandika kwenye mtandao, wanaandika, lakini kwenye hoja, hoja ni ipi? Kama Bunge hilo halikuwa na mamlaka hayo liliundwa kwa kazi gani?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nawaomba Watanzania wenzangu wale wanaotaka kurudi na wengine wananiambia rudini, usikate kwa sababu fulani, unafuata mkumbo kama upepo tumia akili yako, rudi hapa tupate Katiba mpya. Dada Mdee, tunazungumza kuna Jaji mmoja alitupiwa yai lililooza, lakini akasema nafikiri hakuwa ananitupia mimi, alikuwa anamtupia huyu mwingine.

Kwa hiyo, naomba ifahamike hivyo ibara ya tisa aliyosema Mheshimiwa Mdee inazungumza nchi hii ina maadili gani na mambo gani yazingatiwe kwenye rasimu hii. Kitu kimoja kilicholindwa ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, muundo wake haukulindwa na amesema Mheshimiwa Wassira, muundo wake unaweza kuwa Serikali moja, unaweza kuwa Serikali mbili, unaweza kuwa Serikali tatu.

**MBUNGE FULANI:** Au wa mkataba.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mkataba siyo muundo wale wasomi wanaojua miundo ya Serikali mkataba haupo. Kwa hiyo kwenye hilo la Bunge la Katiba jamani rudini kwenye ulingo.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ambalo limezungumzwa ni suala la dhamana kwamba, kuna kesi ya uhujumu moja Mahakama ilitoa maamuzi, halafu Serikali haijatekeleza. Ni kweli, lakini lilikuwa suala gani, nisingependa kutaja majina lakini ni kesi inayomhusu Profesa Mahalu. Kesi hiyo ina sehemu mbili, sehemu ambayo sisi tumekata rufaa ni ule uamuzi wa Mahakama unaohusiana na dhamana na kifungu chenyewe ni kifungu cha 36(4)(e) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi siyo kifungu cha 148 cha Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Jinai.

Mheshimiwa Spika, tumekata rufaa kwa sababu tunataka msimamo wa kisheria wa Mahakama ya Juu kabisa na kama Mahakama ya juu kabisa itakataa, haitakubaliana na sisi tutarudi kubadilisha Sheria hiyo, wala sioni kama ni kitu cha ajabu, lakini mfahamu pia hii kesi ilifunguliwa na Profesa Mahalu akidai haki yake kwamba dhamana ni haki yake na akapewa. Sasa alipopewa sisi tukakata rufaa *effect* yake ni nini? Rufaa katika kesi za aina hii zinasimamisha utekelezaji. Kwa hiyo, ndiyo maana hatukutekeleza, lakini siyo kwamba tunajaribu kuihujumu Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kuna suala halikujitokeza hapa, lakini nafikiri hii hoja kwamba Msajili wa Mahakama Kuu kuthibitisha ile hati ya Muungano. Moja ya sababu zilizofanya nyinyi

wengine mkatoka humu ndani ni uwepo wa hati ya Muungano mliyodhani kwamba haipo. Tubishane kwa hoja, sasa ile hati ipo, katika utaratibu utaratibu wa kawaida wa kuthibitisha Msajili wa Mahakama anayo mamlaka haya kwa mujibu wa Sheria, lakini hata kama *Chief Secretary* angefanya ile kazi ingekuwa ni sawa, lakini kwa nini tulifanya hivyo? Kwa sababu tulijua ni kwamba huyu atakuwa amegushi, kwa hiyo na sisi tunajilinda kwa sababu tunafahamu kuna mishale ambayo siyo ya haki humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yako mambo mengi sana yamezungumzwa kuhusiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Moja lililozungumzwa bila kufuata makaratasi haya ni suala la UDA na naomba nilitolee maelezo kidogo. Natoa maelezo kidogo na siyo yote kwa sababu jambo hili bado ni *subjudice*, bado liko Mahakamani, lakini nadhani haya nitakayosema hayataathiri haki ya mtu yoyote Mahakamani.

La kwanza kulikuwa na mashtaka dhidi ya wanahisa *Directors* wa UDA, kesi ile ilipelelezwa na *PCCB,* TAKUKURU, wakamletea *DPP* kuidhinisha. Kwa sababu za kiufundi, *DPP* akasema kwamba uchunguzi unahitajika zaidi na akatoa maagizo hayo kwa TAKUKURU. TAKUKURU wamefanya uchunguzi na taarifa nilizonazo ni kwamba, jana walilirudisha jalada kwa *DPP,* kwa hiyo, *DPP* bado hajafanya maamuzi tunategemea baada ya shughuli hii atakwenda kufanya maamuzi yake. Namwomba *DPP* popote pale alipo kama yuko hapa mazungumzo ya humu ndani kuhusu suala hili, yasiathiri uwezo wake wa kuamua. Hiyo ndiyo Sheria na hiyo ndiyo Katiba na mimi nitatetea uamuzi wowote atakaoufanya.

Mheshimiwa Spika, la pili, kulikuwa na mawazo ya kumyang'anya hisa yule aliyenunua UDA, yeye kakimbilia Mahakamani, kashtaki, haki yake kuzuia kwamba asinyang'anywe hisa. Kesi hiyo bado haijamalizika na inakuja tarehe 10 Juni, Mahakamani. Kwa hiyo, hiyo ndiyo *position* ya suala la UDA na Serikali inalifuatilia suala hili, inayo ushahidi mimi mwenyewe na Mheshimiwa Waziri Mkuu tunalifuatilia kuhakikisha kwamba haki inatendeka kote.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine linasemwa lakini nisingependa kulizungumzia, naona Waheshimiwa wengi wanalizungumzia suala la *IPTL,* uamuzi uliofanyika hapa ni kwamba, uchunguzi uendelee na vyombo vilivyotajwa vinafanya uchunguzi. Kwa hiyo, nisingependa kulizungumzia suala hilo kwa namna yoyote ile na nahimiza vyombo hivyo vifanye kazi hiyo haraka na kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, lakini tufahamu *Escrow Account* ilianzishwa kwa madhumuni maalum na kwamba kodi zinazohusika za mwanzo kama *VAT, VAT* ni *consumption tax* inalipwa na *TANESCO*, *Capital gain tax* kama mtu ameuza *VIP* anatakiwa kulipa *Capital gain tax*. Kwa hiyo, uchunguzi uendelee na mtaona ni nani hasa anayesema ukweli kuhusu jambo hili nafahamu kwamba kuna watu wengi wanatumia fedha kwa ajili ya kutafuta mashahidi, lakini haituhusu palipo na haki, haki itasimama na haki ya mtu haipotei.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni huduma za msaada wa Kisheria *legal aid* nafikiri Mheshimiwa Waziri atalizungumzia, lakini huduma za kisheria muhimu kabisa msingi wake ni kufikisha haki kwa watu na ni suala ambalo ni mtambuka, linaweza kuwa kijiografia, Mahakama ziwe karibu na watu au inaweza kuwa ni lugha, lugha rahisi ya kufahamika na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kuhusu utungaji wa Sheria. Tumeshaamua kwamba kuanzia sasa Sheria zote zitatungwa katika lugha mbili Kiswahili na Kiingereza huo ni uamuzi uliofanywa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na mabadiliko ya Sheria, tutafanya mabadiliko ya Sheria kila inapohitajika na baadhi ya mabadiliko haya ya Sheria ni vizuri pia Wabunge wafahamu kwamba wanayo mamlaka ya kuwa wadau muhimu kwa kutumia kanuni ya 81 ya Kanuni za Kudumu za Bunge na naomba pengine msaidie kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na baada ya kusema hayo maneno machache nitumie nafasi hii tena kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tuungeni mkono.

Mheshimiwa Spika, hapana bado kuna suala moja la dawa za kulevya. Dawa za kulevya inaonekana kama linakuwa janga la Taifa na tunao mchakato ndani ya Serikali wa kuandaa marekebisho na bila shaka tutaleta Muswada wa Marekebisho wa Sheria ya Madawa ya Kulevya katika Bunge pengine lijalo kwani tumebaini kasoro ambazo zinahitaji masahihisho ya haraka.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kama nilivyosema naunga mkono hoja, lakini pia nawapongeza Mawakili wa Serikali na watumishi wengine wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uvumilivu sana. Tunafahamu sana tunahitaji rasilimali kwa ajili ya kuendesha kesi zetu, kuongeza ujuzi, kujiamini na utulivu na ili tuwe watulivu, tufanye kazi za Serikali kwa moyo mmoja, tunahitaji rasilimali, mishahara ya kutosha, marupurupu ya kutosha ofisi zenye hadhi kama zile za TAKUKURU na makazi ya Mawakili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sijui wewe utajisikiaje kama wewe ni Wakili wa Serikali umeendesha kesi ya mauaji au ya wizi au ya madawa ya kulevya, kisha unapanga kwenye nyumba ya wahusika. *(Makofi)*

Sijui itakuwaje, umeendesha kesi za aina hiyo unapanda magari ya umma yaliyojazana na hujui nyuma yako yuko nani. Kwa hiyo, ndiyo maana tunaomba rasilimali hizi na nafikiri ndiyo maana na nyie mnatuunga mkono. Lakini naomba na naomba tutenganishe mambo, wengine wamesema mambo ya rushwa katika Mahakama. Huwezi kukataa, lakini lazima ujue kuna mambo mawili, kuna *perception* unavyoona na hali halisi ilivyo. Kama tungekuwa na rushwa kiwango hicho, kwa kweli tusingekuwa na chembe ya amani tuliyonayo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo rushwa, nimefanya kazi kwenye *Commission* ile ya Rais ya Rushwa ya Mzee Warioba, nafahamu kwamba *yes* ziko, lakini hali yake sivyo kama ambavyo wengine wanasema hapa. Kuwasaidia watu hawa si kwa kuwapa mishahara mikubwa tu, lakini wafanye wawe na chembe ya utulivu, bila hiyo chembe ya utulivu, kwa kweli hali itaendelea kuwa mbaya. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri ameliona hilo na Naibu Waziri tutategemea sasa mtusaidie kusukuma ili kusudi mambo haya yatekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana na naomba tena kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda sana kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria ya bajeti ya mpango na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2014/2015.

Kwanza kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro, Waziri wa Katiba na Sheria, kwa uongozi wake mahiri na ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kuwashukuru Wabunge wote ambao wamechangia hoja hii kwa kuongea na kwa maandishi na kwa maoni na ushauri mkubwa ambao wameutoa kwa hakika utaisaidia sana Wizara yetu kuboresha bajeti hii na majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kuchukua fursa hii kwa mara nyingine tena Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna alivyohusika kikamilifu kuhakikisha kwamba nchi yetu inakuwa na Katiba mpya ili kukidhi mahitaji tuliyonayo kwa sasa, katika nyanja za siasa, uchumi, kijamii na kiutamaaduni.

Mheshimiwa Spika, ni maoni yangu kwamba dhamira hii njema ya Mheshimiwa Rais wetu moyo wake wa kizalendo, mapenzi mapema aliyonayo kwa nchi yetu vitaenziwa kwa sisi kama Waheshimiwa Wabunge pamoja na wajumbe walioteuliwa kuandika Katiba mpya kutekeleza wajibu wetu ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, licha ya kutokuwepo kwa muafaka, ambapo wengine wametoka, ni rai yangu kwamba, sote tunawajibika kukaa pamoja na kuridhiana ili tupate Katiba iliyo bora itakayonufaisha vizazi vyetu kwa miaka 50 ijayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika vikao mbalimbali vya Bunge vilivyopita, kwamba imani huzaa imani, sote humu ndani tunao wajibu wa kiungwana kabisa wa kumwamini Mheshimiwa Rais wetu, tuoneshe subira na ustahimilivu katika mchakato huu kwa mabadilikoya Katiba. Si rahisi maoni na mawazo ya wote yakakubaliwa. Tuwe tayari kukubaliana kutokubaliana, kustiriana na kuwekeana staha, mambo yanayotuunganisha ni muhimu zaidi kuliko mambo yanayotugawa.

Mheshimiwa Spika, tunajenga nyumba moja, hatuna sababu ya kunyang'anyana fito. Sisi humu ndani viongozi, tukianza kuyumba, tutagawanyika, tunaowaongoza na hatimaye nchi yetu pia itayumba. Uongozi ni dhamana, uongozi ni malezi, sote tunao wajibu wa kulilea Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba sasa nichukue fursa hii kujibu hoja mbalimbali zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa kwa hoja ya Mheshimiwa Halima Mdee kuhusiana na mchakato wa ujenzi wa Mahakama ya Mwanzo ya Kawe na kwamba umefika wapi. Kwanza kabisa napenda kumtaarifu kupitia gazeti tarehe 11 Mei na gazeti la tarehe 12 Mei, Mahakama imeshakaribisha maombi ya Wakandarasi ambao wanaweza kujenga majengo mbalimbali ya Mahakama katika ngazi mbalimbali.

Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba, mwaka wa fedha bado haujakwisha, tayari hatua hii ya kumpata Mkandarasi imeshaanza, kwa hiyo, tunaamini Mahakama hii itajengwa na si hii tu ni pamoja na Mahakama zingine za mwanzo 25 ambazo tuliziahidi mwaka jana wakati wa bajeti.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kujibu hoja ya Mheshimiwa Said Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, ameeleza kwamba wanayo kero ya Mkoa wa Katavi kutokuwa na majengo ya Mahakama yenye hadhi, kuanzia Mahakama za Mwanzo na Mahakama Kuu. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Arfi kwamba Mahakama kupitia mpango wake wa ujenzi wa mwaka 2013/2014 na 2014/2015 itajenga Mahakama ya Mwanzo ya Mpanda Mjini kuanzia mwezi Julai na kama nilivyoeleza kwenye Mahakama ya Kawe nayo pia tayari mchakato wake umeanza, lakini vile vile katika mwaka 2014/2015 Mahakama itajenga Mahakama Kuu katika Mkoa mpya wa Katavi.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya Mheshimiwa Dkt. Pindi Chana, kuhusiana ni lini Mahakama ya Mwanzo ya Ludewa, Kata ya Masasi ambayo imekuwa ikiahidiwa mara kwa mara itakamilishwa ujenzi wake. Mahakama hii imeshindikana kujengwa kutokana na ufinyu wa bajeti, lakini iko katika mipango ya ujenzi ya mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya Mheshimiwa Rebeca Mngodo, kuhusiana na kesi ya mjane mmoja aliyeko Arusha upande wa Meru. Napenda tu kumhakikishia kwamba, tutafanya jitihada zote zinazowezekana kufuatilia kesi hii ili kuweza kufahamu sababu za kutokumalizika kwa shauri hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mustafa Akunaay alipenda kujua ni lini Mahakama ya Wilaya ya Mbulu itajengwa. Nipende kumwambia tu kwamba, Mahakama hii ya Wilaya itajengwa kwa mwaka 2014/2015, lakini vilevile katika mwaka wa 2013/2014 na 2014/2015 Wilaya ya Mbulu itajengewa Mahakama za Mwanzo takribani sita.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya Mheshimiwa Esther Matiko, kuhusiana na ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Rorya na kwamba katika tangazo ambalo Mahakama imelitoa, jengo hili la Mahakama ya Rorya haijatangazwa. Napenda kumhakikishia kwamba Mahakama hii itajengwa katika mpango wa Mahakama, tumeanza na chache kuzitangaza kwenye gazeti, lakini tunakwenda hatua kwa hatua na kwamba katika mwaka huu huu wa fedha Mahakama hii ya Wilaya ya Rorya itajengwa.

Mheshimiwa Lwaji aliomba Mahakama ya Idodyandole, Rungwa na Aghondi na Ipande. Napenda kumhakikishia kwamba Mahakama zote hizi nne za Mwanzo ziko katika mpango wa ujenzi wa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Deusderius Mipata, alipenda kujua ni lini Mahakama ya Wilaya ya Nkasi itajengwa na yeye pia nipende kumhakikisha kwamba katika tangazo ambalo tumelitoa mwezi huu wa Mei, katika *Lot* namba tatu, Mahakama ya Wilaya ya Nkasi na yenyewe itajengwa katika mwaka huu kuanzia mwezi Julai.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na maendeleo ya mpango wa *E-justice*, Mheshimiwa Mbunge akiangalia katika hotuba yetu ya Wizara, tumeeleza kwa kina kabisa mchakato ambao tumefikia katika mpango huu wa *E-justice* na napenda nirudie kwamba tayari upembuzi yakinifu umeshafanyika na umeshawasilishwa katika Tume ya Mipango pamoja na Wizara ya Fedha na hatua zingine zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Pindi Chana ya Mafunzo ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Wilaya, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba mafunzo yamekuwa yakifanyika, lakini tumekuwa tukitenga fedha zaidi ili kuweza kutoa mafunzo kwa Mahakimu wengi zaidi. Tuombe tu Waheshimiwa Wabunge mkishatupitishia fedha za bajeti, basi mpango huo wa mafunzo utaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na ujenzi wa Mahakama za Mwanzo za Temeke, Mbagala, Magomeni na Ilala; napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mariam Kisangi, kwamba Mahakama zote nne, hizo zipo katika mpango wa mwaka 2013/2014 na 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya Mheshimiwa Charles Mwijage ambayo aliitoa kuhusiana na wananchi wake wa Muleba Kaskazini ambao wamekuwa wakifanyiwa vitendo viovu na wamewasilisha kesi zao Mahakamani. Napenda tu kumhakikishia kwamba kupitia Ofisi ya

Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na Mahakama suala hili wataliangalia ili basi haki iweze kutendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya Mheshimiwa Meshack Opulukwa, kwamba utaratibu wa *committal proceedings* katika Mahakama za Wilaya katika mashauri ya mauaji uondolewe na badala yake kesi za mauaji ziwe na utaratibu wa kuanzia katika Mahakama Kuu peke yake.

Mheshimiwa Spika, napenda tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa mazingira ya Tanzania, ukiangalia uhalifu mwingi unatokea pale pale katika jamii, kwa hiyo, ni utaratibu ambao tuliuchukua na ukiangalia upelelezi unatokea katika jamii na ukiangalia katika Mahakama Kuu, kila Mkoa una Mahakama Kuu moja tu na bado si mikoa yote ambayo ina Mahakama Kuu. Kwa hiyo, tukibadilisha utaratibu huu kwa sasa, kwa kweli tutakuwa tumeweka kesi nyingi zaidi na kusababisha mrundikano katika Mahakama Kuu, lakini vile vile tutawapa usumbufu wananchi usiohitajika.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya Mheshimiwa Pindi Chana kuhusiana kwa nini mahabusu wa Arusha wanavua nguo na kwamba wanalalamika sana. Nilisoma hoja hii na kama nitakuwa sijakosea nadhani kuhusiana na gereza kuu Arusha. Nilipanga kufanya ziara lakini kutokana na maandalizi ya bajeti nimeshindwa kufanya ziara katika gereza hilo na napenda kumhakikishia Mheshimiwa Pindi Chana, nadhani Mungu akipenda, wiki ijayo nitakwenda kutembelea gereza kuu Arusha ili kujua nini kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Pindi Chana pia alitoa rai kwamba tufanye ziara katika gereza la Isanga. Napenda kumhakikishia kwamba tayari ziara nilishaifanya mwezi Julai, 2012 na ilipata matokeo makubwa sana, lakini bado tukipata fursa nitarudi tena.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya Mheshimiwa Matiko kwamba, wako baadhi ya Polisi ambao wamekuwa wakiwabambikizia watu kesi na kudai hongo ya shilingi laki tatu hadi laki tano na endapo mtuhumiwa atakuwa hana fedha hizo, basi anabambikizwa kesi hali ambayo inasababisha mrundikano wa mashauri.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa mashtaka umewekwa kwa namna ambayo kunakuwa na utaratibu wa *checks and balance*, askari anapomkamata mtuhumiwa na kufanya upelelezi, baadaye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka hupitia taarifa zilizokusanywa na kuhakiki endapo kuna ushahidi wa kufikisha shauri hilo Mahakamani.

Hivyo iwapo hakuna ushahidi maelezo hutolewa na *DPP* kwa Polisi ili mtuhumiwa aachiwe huru na kama shauri liko Mahakamani basi *DPP* huondoa shauri hilo. Hata hivyo iwapo kuna mazingira ya kuomba hongo, ni jukumu la mtuhumiwa au ndugu wa mtuhumiwa kutoa taarifa TAKUKURU, ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir ambaye ametaka kujua, Serikali ieleze ni namna gani itashughulikia mashauri tisa ya miaka ya nyuma ya mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi. Napenda kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba kesi tisa ambazo zimesalia za mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi zilizopo Mahakamani ni miongoni mwa mashauri ambayo utaratibu wake unaendana na ratiba ya Mahakama. Kama ilivyokuwa kwa mashauri mengine, Serikali itahakikisha kwamba, mashauri haya yanaendeshwa kwa weledi ili watuhumiwa waweze kutiwa hatiani na kupewa adhabu kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kutekelezwa kwa adhabu ya kifo kwa wale watuhumiwa waliotiwa hatiani utafanyika kwa kufuata matakwa ya sheria chini ya mamlaka zinazohusika, mara Rais atakaporidhia kutekelezwa kwa adhabu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Charles Mwijage pia aliongelea suala la uadilifu wa watumishi wa Mahakama kama ambavyo nimekuwa nikisema Sheria ya *Judicial Service Commission* kiko wazi kimeunda Kamati za Maadili za Kushughulikia Nidhamu za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo Wilaya na za Hakimu Mkazi.

Mheshimiwa Spika, naomba tena nichukue hadhara hii kukumbusha, endapo kuna atakayeona tukio la aina hiyo, basi asisite kutoa taarifa kwa Kamati ya Maadili ya Wilaya na Kamati ya Maadili ya Mkoa. Kamati ya Maadili ya Wilaya inasimamia nidhamu za Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Kamati ya Maadili ya Mkoa inasimamiwa na Mkuu wa Mkoa. Naomba sana wachukue fursa hiyo kufikisha malamiko huko ili hatua stahiki ziwe kuchukuliwa, lakini kipekee nimpongeze Mheshimiwa Mwijage kwa namna ambavyo amefuatilia masuala ya nidhamu ya Mahakimu.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja ya Mheshimiwa Sakaya ambayo ameitoa kwamba wako mahabusu ambao wamekuwa wakikaa vituoni kwa siku tatu hadi siku nne, badala ya kufikishwa Mahakamani ndani ya masaa 48 kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwa mujibu wa sheria mtuhumiwa aliyepo mahabusu anatakiwa kufikishwa Mahakamani ndani ya masaa 48, lakini yako mazingira ya kisheria yanayoruhusu kumfikisha Mahakamani baada ya masaa 48. Mfano, kwenye makosa ya mauaji au pale mazingira yanakubalika kisheria kumfikisha Mahakamani mtuhumiwa baada ya masaa 48.

Mheshimiwa Ritta Kabati, yeye ameongelea upotevu wa majalada ya kesi na tuhuma za uendesha mashitaka kuomba rushwa kwa watuhumiwa. Suala la upotevu wa majadala ya washtakiwa tunamwomba Mheshimiwa Kabati atupatie taarifa rasmi au ushahidi wa jambo hilo ili tuweze kuchukua hatua stahiki dhidi ya wote wanaohusika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tuhuma za waendesha mashtaka kuomba rushwa, tunatoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Iringa na mikoa yote kuwa makini kwa sababu hivi sasa imeibuka wimbi la matapeli, wanaojiita Waendesha Mashitaka wa Serikali ambao wanakaa katika maeneo ya Mahakama wakiomba rushwa. Hivyo, mwananchi yeyote atakayekutana na tatizo hilo tunamwomba atoe taarifa TAKUKURU na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa. Vile vile tunamwomba Mheshimiwa kabati kama ana taarifa rasmi juu ya suala hili aziwasilishe Wizara ili tuweze kuzifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya Mheshimiwa Martha Mlata, pamoja na Mheshimiwa Batenga na Mheshimiwa Mng'ong'o kuhusiana na huduma ya msaada wa kisheria kusambaa sehemu zote, lakini vile vile kuhakikisha kwamba kada ya wasaidizi wa kisheria au *Paralegals* inatambuliwa kisheria ili waweze kutoa huduma mbalimbali za msaada ya kisheria nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Wizara yetu tayari inacho Kitengo ha Huduma ya Msaada wa Kisheria kwa jamii na imekuwa ikishirikiana na Mfuko wa *Legal Services Facility* na imekuwa ikitoa fedha kwa watoa huduma mbalimbali nchi nzima, lakini vile vile imekuwa ikitoa fedha mfano, kama *TAWLA* wako ambao walitoa maoni kama Mheshimiwa Batenga, kwamba *TAWLA*

iwezeshe ili iweze kufikia *paralegals* wengi. *TAWLA* ni mojawapo ya taasisi ambayo mwaka jana ilipata takribani milioni 700 kwa ajili ya kufundisha *paralegals*.

Mheshimiwa Spika, iko hoja pia ya Mheshimiwa Ritta Kabati, kuhusiana na changamoto ya wananchi wengi kutokujua sheria na haki zao. Wizara ya Katiba na Sheria yenyewe pamoja na taasisi zake, imekuwa ikiendelea kuta elimu juu ya sheria na haki mbalimbali ikiwemo haki za binadamu, Sheria za Ardhi, masuala ya utaratibu ya ufunguaji wa kesi Mahakamani pamoja na mambo mengine. Imekuwa pia ikishiriki katika vipindi mbalimbali vya luninga, redio, imekuwa ikigawa machapisho mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, lakini si hilo tu, ndiyo maana sasa tunashirikiana na watoa huduma wa msaada wa kisheria wengine ili waweze kutusaidia, lakini tunatambua changamoto hii na tunatambua hitaji hili na kwa kweli tunalithamini na tutajitahidi kadiri inavyowezekana tuweze kuboresha namna ambavyo tunatoa elimu hii kwa umma.

Mheshimiwa Spika, labda kwa ujumla tu niweze kuelezea mipango mbalimbali ya Mahakama kwenye manunuzi au upatikanaji wa vyombo vya Usafiri pamoja na ujenzi. Katika mwaka huu wa fedha ifikapo Juni tunatarajia kununua pikipiki takribani 374 na baiskeli 1,000 ambazo tutazigawa katika Mahakama mbalimbali za Mwanzo pamoja na Wilaya. Hata hivyo, tunatarajia kununua magari 92 kwa ajili ya Mahakama za Wilaya na magari 21 kwa ajili za Hakimu Mkazi.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya Mheshimiwa Moses Machali, amekuwa akiulizia ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Kasulu na yeye pia napenda kumwambia kwamba ahadi hii si hewa, amekuwa akisema kwamba wakati Mheshimwia Chikawe akiwa Waziri ilitolewa. Ni kweli ilitolewa na katika tangazo hili hili la mwezi Mei tarehe 11, Mkandarasi hivi sasa anatafutwa kwa ajili ya kuanza ujenzi. Si kwamba limechoka tu, tunajenga jengo jipya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o alielezea hali ya uchakavu wa jengo la Wizara ya Katiba na Sheria. Ni kweli jengo lile limechoka na mara kwa mara limekuwa likipata hitilafu za umeme, lakini ndiyo maana mwaka hadi mwaka tumekuwa tukitenga fedha kidogo tunazopangiwa kwa ajili ya kufanya ukarabati awamu kwa awamu. Katika mwaka huu wa fedha endapo mtaridhia, tumeomba maombi ya fedha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya shughuli hiyo. Kuhusiana na suala la ubovu wa *lift* nipende tu kumhakikishia Mheshimwia Mng'ong'o tayari mwaka jana tulishanunua *lift* na sasa ni *lift* mpya.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o pia ametaka kujua ni lini Serikali itahakikisha kwamba, kunakuwa na vituo vya wahanga wa ukatili wa kijinsia na lini sheria italetwa. Kwanza kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, ni mmoja wa Watanzania wachache ambao wanaendesha vituo vya kutoa huduma ya wanawake waliopata ukatili wa kijinsia. Dar es Salaam viko takribani vituo viwili.

Mheshimiwa Spika, nitoe tu rai kwa watu wengine wenye mapenzi mema, waweze kufungua vituo hivyo na sisi kama Serikali tunaangalia uwezekano ni kwa namna gani tutaweza kuwaunga mkono aidha kwa kuwasaidia wao au kwa kujenga vituo vya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kwa upande wa Mahakama na Upelelezi kupitia Azimio la Nchi za Maziwa Makuu, iliamuliwa kwamba, mashauri ya ukatili wa kijinsia, upelelezi wake usizidi mitatu na uendeshaji wake Mahakamani mpaka hukumu isizidi miezi mitatu. Napenda kutoa taarifa kwamba, Mheshimiwa Jaji Mkuu kwa kweli kwenye hili analipa uzito mkubwa na tayari kesi nyingi kwa kiasi kikubwa zimeanza kusikilizwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Salum Barwany ameongelea suala la urasimu katika usajili wa watoto walio na umri wa chini ya miaka mitano. Sijajua ni maeneo gani labda wamefanya urasimu, lakini ningependa anipe taarifa, lakini kwa ujumla, inawezekana ikawepo siwezi kukataa kwa sababu watendaji na wenyewe ni binadamu. Lakini niseme kwamba, kama Wakala tumejipanga na hivi sasa tunao mpango wa usajili wa watoto wa chini ya miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, Mpango huu ulifanyiwa majaribio Temeke, umekwenda vizuri na hivi sasa unafanyika katika Mkoa wa Mbeya na takribani watoto 132,000 ndani ya miezi saba wameweza kusajiliwa. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 31.4 lakini si hiyo tu, tunajitahidi kuwa na mkakati mwingine wa miaka sita mpaka kumi na nane ambapo tunakwenda katika shule zote za Msingi na Sekondari, shule zote za Serikali na binafsi ili kuhakikisha kwamba tunatoa elimu ya umuhimu ya usajili, ni viambatanisho gani vya muhimu katika kujaza fomu za maombi ya cheti cha kuzaliwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile hivi sasa tunatoa cheti cha mkono ambacho tumeshusha huduma za *RITA* katika Kata na katika ngazi za vituo vya kutolea tiba. Vile vile tumetoa huduma za simu na mtu anaweza akatoa maombi ya usajili kupitia simu. Naamini sasa usajili wetu utaweza kuongeza kutoka asilimia 6.2 mpaka asilimia 15 katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, iko hoja ya Mheshimiwa Aliko Kibona ambaye ameuliza upatikanaji wa Hakimu wa Wilaya ya Ileje ni lini atakwenda, pamoja na gari la Mahakama ya Wilaya ya Illeje. Napenda kumhakikishia kwamba, katika magari mapya 92 ya Wilaya yanayonunuliwa mwezi Juni, Mahakama ya Wilaya ya Ileje ni moja ya Mahakama zitakazopata gari hilo. Kuhusiana na Hakimu wa Wilaya ni lini atakwenda, tunao mpango wa kuajiri watumishi 1100, endapo vibali vya ajira vitatoka basi na Hakimu katika Wilaya ya Illeje naye atapangiwa.

Mheshimiwa Spika, liko suala liloulizwa kuhusiana na sheria kandamizi zilizopitwa na wakati, nadhani na Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, ni lini zitaletwa Bungeni ili zifanyiwe marekebisho, hususan alitolea mfano wa sheria ya mirathi. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo nimekuwa nikijibu mara kwa mara, Sheria hii inagusa masuala mengi, inagusa masuala ya mila na desturi, inagusa masuala ya dini. Ilishaamuliwa katika Baraza la Mawaziri ipitie mchakato wa *white paper* ili wananchi wote waweze kutoa maoni zaidi.

Mheshimiwa Spika, kabla hatujaanza mchakato, ndipo ukawa umeingia mchakato wa mabadiliko ya Katiba. Kwa hiyo, tukaona si vyema kuwachanganya wananchi, mara unawafuata unawaulizia maoni yao kuhusiana na Katiba mpya na hapo hapo tena unaanza kuongelea masuala ya Sheria ya Ndoa na Mirathi. Hata hivyo, nipende kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge hatima itakayojitokeza katika Katiba mpya nadhani pia ita-*reflect* katika mabadiliko ya sheria hizo.

Mheshimwia Hamoud Jumaa, ameulizia ni lini Mahakama ya Ruvu itajengwa. Nipende kumwambia tunaipa uzito lakini pindi bajeti yetu itakapokaa vizuri tutaweza kuijenga hiyo na tunaingiza katika mpango.

Mheshimiwa Spika, ameongelea pia Mahakama ya Mlandizi kuwa imechoka na yenyewe pia nipende kumwambia tutaiangalia kuona ni kwa namna gani inaweza kufanyiwa ukarabati. Ameomba pia tufanye ziara, tupende kumhakikishia kwa Wizara tutafanya ziara mara Bunge litakapoahirishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mtoa hoja!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hotuba yangu leo na kwa jinsi ulivyosimamia mjadala wetu vizuri. Naomba nichukue fursa hii kwa namna ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Jaji Fredrick Mwita Werema, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambaye ameungana nami katika kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nimshukuru Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Angella Kairuki kwa kujibu kikamilifu hoja hasa zilizohusu ujenzi wa miundombinu na kuboresha huduma zetu. Naomba nimshukuru kwa ushirikiano anaotoa kwa usaidizi mkubwa anaonipatia toka kuteuliwa kwangu mpaka tunahitimisha kazi hii leo ya kuwasilisha hotuba yetu ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imepokea kwa furaha kubwa sana, Wizara yangu na taasisi zote zilizoko chini ya Wizara yangu. Tumepokea kwa furaha michango ya Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, ambayo wameitoa kupitia taarifa yao na ile waliyoitoa wakati wa kujadili bajeti ya Wizara yetu katika ngazi ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hii waliichambua bajeti yetu kwa kina kwa umahiri na kwa uzito unaostahili na leo hii tumeshuhudia kwa namna gani wameridhishwa na kazi ambayo tumeifanya, wameridhishwa na hoja tulizozitoa. Ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba maneno mazuri waliyosema kuhusu Wizara yetu na taasisi zake hayatatuvimbisha kichwa, bali yatatia ari ya kurekebisha pale ambapo pana upungufu na kuboresha kazi zetu ili tuweze kukidhi matarajio ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, tumepokea pia maoni ya Kambi ya Upinzani ambayo tutayapitia kwa makini, tujibu yale ambayo yameibuliwa, lakini vile vile kama kuna mazuri ya kuboresha, basi tutachambua na kufanya hivyo, kwa sababu sisi tunaamini kwamba, Tanzania hii itajengwa na Watanzania wote na Sekta ya Sheria, ni sekta kimsingi inahudumia wote bila ubaguzi.

Mheshimiwa Spika, tunawashukuru Wabunge ambao wamechangia kwa kauli na wale waliochangia kwa maandishi. Michango ya Wabunge imetusaidia sana na kubwa ambalo tumeliona ni ari ya Waheshimiwa Wabunge kutaka kuona kwamba sekta hii muhimu ya sheria inafanya kazi vizuri, wameonesha haja ya sekta yetu kuongezewa fedha ili tuweze kutimiza majukumu yetu. Tunawashukuru kwa hatua zote ambazo watazichukua ili kuweza kufikia azma hiyo.

Mheshimwia Spika, waliochangia kwa kuzungumza wamefika wanane kwa kauli na waliochangia kwa maandishi wamefika 22 na tutawataja baadaye katika nyaraka zinazohusika.

**SPIKA:** Huwataji kwa sauti.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, sikusikii vizuri.

**SPIKA:** Hatutaji kwa sauti labda hivyo hivyo tu basi!

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Nimesema watatajwa kwenye nyaraka zinazohusika kwa maana ya kwamba kwenye *hansard*, sikuwa na mpango huo wa kuwataja, hata hivyo nakushukuru kwa mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, katika mambo ambayo yemejitokeza hasa tukianzia kwenye Kambi ya Upinzani. Kuna hoja hapa ilijengwa kwa nguvu kabisa kwamba, Waziri hakusema kweli, sipendi kutumia neno walilotumia wao kwa sababu najua kwa mujibu wa kanuni zetu inaweza kuwa ni lugha ya kukera na nisingependa kurejea hilo, lakini niseme tu kwamba hakukuwa na udanganyifu wowote wala hakuna ubabaishaji wowote kuhusu fedha za Bunge Maalum.

Mheshimiwa Spika, ni kweli na ukweli unabaki hivyo, endapo watatazama vitabu husika wataona kwamba, katika Fungu 21 la Hazina, kifungu kidogo cha 290700 ambacho kinazungumzia *contingencies non emergency* hiki ni kifungu kwa shughuli maalum, kwa ajili ya kugharamia yale mambo ambayo ni ya Kitaifa yenye sura aidha ya udharura au isiyokuwa na utabiri wakati hilo linafanyika.

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa wakati ule zilikuwa ni makadirio kama tulivyosema hapo awali, mchakato huu wa Bunge Maalum ulianza katikati ya mwaka wa fedha, lakini Serikali haiendi kwa kuotea kwa hiyo, iliona ni vema fedha hizi zitengwe na zilitengwa na naamini kabisa Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakapokuja hapa kuzungumza atatolea ufafanuzi zaidi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, labda nisahihishe suala moja, fedha zilizokuwa zimetengwa zilikuwa ni shilingi bilioni 22.4, lakini baadaye katika matumizi, matumizi hayo yaliongezeka na kufikia bilioni 26.8. Kwa utaratibu wa tarakimu, Mawaziri waliozungumzia 27 walikuwa wanafanya kitu kinaitwa *rounding up*, kwa hiyo ikawa ni 27 na hivyo hakuna mkinzano wowote, hakuna uwongo wowote na kitaalam hili ni jambo la kawaida, kwamba makadirio yalifanywa na baada ya makadirio kufanywa ilipotokea kwamba hali halisi imehitaji fedha kuongezeka, ziliongezeka na fedha zote hizi zilipitishwa kwa mujibu wa utaratibu.

Mheshimiwa Spika, ipo hoja pia iliyosemwa na naomba niiseme awali kabisa kuhusu suala zima la *Operation* Tokemeza. Ni katika Bunge hili tulisikia taarifa iliyotolewa na Kamati ya Bunge ambayo ilifanya uchunguzi katika eneo hili. Ilijadiliwa hapa kwa uzito wake na likatolewa azimio la Waheshimiwa Wabunge kwamba iundwe Tume ya kufanya uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyosema asubuhi, Tume hii imeundwa, Mheshimiwa Rais ametua Majaji na nafurahi kwamba, Mheshimiwa Mwandosya alipokuwa akizungumza hapa alitoa mfano wa jinsi ambavyo Mahakama zetu na Majaji wake wanavyoheshimiwa. Majaji walioteuliwa katika Tume hii wamefanya kazi kwa uadilifu katika Taifa letu na tuwape fursa wafanye kazi ambayo wameteuliwa kuifanya. Si vyema sisi Wabunge ambao siku moja tutakabidhiwa hatamu za uongozi wa nchi hii, tukawa ni watu wa kutilia shaka vyombo ambavyo tumeviweka wenyewe kikatiba na kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zimeundwa Tume mbalimbali, zimetoa taarifa zao na mpaka leo hii hatujawahi kusikia Tume ambayo hitimisho lake limetiliwa mashaka. Kwa hiyo, naomba Tume hii ya Uchunguzi ipewe nafasi iweze kufanya kazi ambayo imepewa kwa mujibu wa hatua za rejea na hivyo tusubiri matokeo ya kazi ambayo watafanya.

MheshimiWa Spika, napenda sasa nizungumzie suala ambalo limechukua nafasi ya kutosha katika mjadala wa leo. Ni kweli kabisa kwamba tuko katika mjadala wa bajeti, lakini yameibuliwa mambo yanayohusu Bunge Maalum la Katiba. Nadhani Waheshimiwa Wabunge

watakumbuka na Waheshimiwa Watanzania wenzangu wote watakumbuka kwamba, kilio cha kutaka mabadiliko ya Katiba kilikuwepo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika mjadala hapa hapa katika Bunge la Katiba tuliwasikia baadhi ya wanasiasa, Viongozi wa Vyama ambao wanaheshimika wakisema hapa kwamba hiki kilikuwa ni kilio cha walio wengi, Waheshimiwa Viongozi walihamsisha wanachama wenzao kudai Katiba mpya, hilo limefanyika kwa Mheshimiwa Rais kuamua kuunda Tume ya Mabadiliko ya Katiba iliyoongozwa kwa umahiri mkubwa na Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba na Wajumbe wenzake.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wote ulifanywa kisheria, ni katika Bunge hili ambapo hilo lilijadiliwa, sheria ikapitishwa hapa na sina shaka wale ambao leo hii wanahoji mchakato huu walikuwa humu, waliongoza baadhi ya vitendo ambavyo vilifanya sheria hii ifanyiwe mabadiliko mara mbili ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Baadhi ya mabadiliko ambayo yalifanyika yalihusu Muundo, nani wawe Wajumbe wa Bunge hili. Hilo lilifanyika sote tunakumbuka kulikuwa na namba hapa, zilitajwa namba kadhaa, mpaka ilipofikia namba ya kuongozeka kwa watu 201. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, leo hii tunaposikia sauti za kutaka muundo uwe mpya, tunajiuliza Waheshimiwa Wabunge, je, tuna nia ya dhati ya kutengeneza Katiba Mpya? Tunapotaka muundo mpya, tunataka muundo huu uje ukidhi matakwa ya nani? Bunge hili Tukufu wote tulioko hapa ni wawakilishi wa wananchi na ni sehemu ya wananchi. Kwa mujibu wa sheria tumekuwa sehemu ya Bunge la Katiba, wako 201 ambao ni sisi wenyewe Wabunge tulisema wateuliwe kwa utaratibu maalum wa kupendekezwa na makundi yao. Wao ni wananchi, wamependekezwa, wamefika hapa wamefanya kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningependa kutumia fursa hii kwanza kutoa wito kwa wenzetu wetu, tujue kwamba Taifa hili litakuwepo baada yetu. Tusichukulie utashi wetu wa leo kwamba ndiyo utachora ramani ya siku zijazo. Utashi binafsi hautachora ramani ya siku zijazo. Kwa hiyo, tuchukulie kwa uzito wake katika nchi yoyote ile, mchakato wa kuunda Katiba ni mchakato wa kuzungumzia uhai wa Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumzia uhai wa Taifa, si wakati wa kufanya majaribio. Katika Bunge la Katiba ilisikika wazi na nadhani ni neno la busara kwamba sumu haionjwi. Kwa mantiki hiyo, ningependa kusema kwamba hapa tulikutana kujadili, kushawishiana kwa hoja.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba CCM kina wanachama walio wengi, kina Wabunge walio wengi, lakini Wabunge hawa wamechaguliwa kidemokrasia, wamechaguliwa kwa msingi wa sheria ambazo sisi wenyewe tumezipitisha hapa. Tunaamini demokrasia na demokrasia wengi wape. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na wingi wao, walikaa hapa, wakanyosha mkono wa maridhiano kwa wenzao. Mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wanakumbuka, siku ya kwanza tulipoanza shughuli hizi, wakati Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba anakuja kuwasilisha Rasimu ile, wachache walihakikisha shughuli haiendelei. Lakini walio wengi hawakutoka. Walio wengi hawakutoka! Hata baada ya pale, hakukuwa na kususiana, tulikaa kwenye meza ya maridhiano, Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka. *(Makofi)*

Baada ya pale kukaja suala la Kanuni, likawa na mazonge-mazonge, lakini tukakutana kwenye maridhiano, kwa sababu tunafahamu kwamba mchakato huu ni mchakato wa maridhiano. Walio wengi wangesema sisi tunatoka, ingekuwa kwa kweli ni kukimbia wajibu. Tunaamini, kwamba walio wachache ni Watanzania, wana haki, wana fursa, wana haki ya kusikilizwa na tuliwasikiliza, tukafikia maridhiano, tukapitisha kanuni hapa, na kanuni zile lazima nionyeshe heshima yangu kwa Wajumbe wa kanuni wakiwemo baadhi ya wachache ambao waliamua kutoka, walituongoza vizuri, tukaunda kanuni, tukaelewana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba, mchakato wa Katiba ni mchakato wa kisheria, ndiyo; kwa sababu msingi wake ni sheria. Ni mchakati wa kisiasa, lakini ni siasa ya kutambua kwamba tuna dhamana, tumekaa hapa kwa ajili ya dhamana na siyo kwa ajili ya maslahi yetu binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, na kwa mchakato ambao umeendeshwa kwa utashi wetu wenyewe, hakuna shinikizo la machafuko, hakuna shinikizo kutoka popote, hatuna haraka isiyo na mwisho. Kwa hiyo, tulikaa hapa kwa ajili ya kufanya shughuli hiyo na mimi nadhani wenzetu wajitahidi warudi Bungeni, Bunge la Katiba, tuendelee. Huo ndiyo ukamavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakumbuka vizuri sana, Mheshimiwa Profesa Lipumba alipotoka hapa, kabla ya kutoka, alipopewa fursa na heshima ya kuwa kwenye Kamati ya Uongozi, alisema hapana. Nataka niwe huku nje ili tushindane kwa hoja. Mimi nadhani kauli ile bado ina mantiki, nadhani wenzetu warudi, tushindane kwa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa hapa kwamba Wizara ya Katiba na Sheria haikutimiza wajibu wake au haikusaidia mchakato. Hiyo siyo kweli, inaeleweka wazi kwamba utaratibu wote wa kutunga sheria ya mabadiliko ya Katiba, katika ngazi ya fikra na utendaji, inaanzia kwenye Wizara ya Katiba na Sheria. Kwa hiyo, tulitimiza wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini baada ya pale, bado tulikuwa na wajibu wa kufanya kazi ya kuhakikisha kwamba tunajenga mazingira mazuri kwa Tume ya Mabadiliko ya Katiba kufanya kazi yake. Hilo hatuna shaka nalo, kama wapo ambao hawataki kulitambua hivi sasa, kwa kweli ni jambo la kushangaza. Kwa sababu sisi tumesimamiwa na Bunge lako Tukufu kupitia Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, imetusimamia na imetupa maelekezo ya kuweza kuhakikisha kwamba tanaweka miundombinu yote kwa Tume kufanya kazi yake bila ya kuingilia uhuru wake na asubuhi hii Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala - Mheshimiwa William M. Ngeleja amelithibitisha hilo, kwa kusema kwamba tulifanya kama tulivyoagizwa. *(Makofi)*

Kama hiyo haitoshi, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume ya Mabadiliko ya Katiba alifika hapa, na alieleza wazi ni kwa namna gani Wizara yetu ilisaidia mchakato huu na kuweka mazingira ya Tume kutimiza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, siyo kweli kwamba Wizara yetu ina nia hiyo. Haikufanya hivyo, wala haikuwa na sababu ya kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, nije sasa katika hoja iliyotolewa hapa, kwa nini kusiwe na maridhiano? Napenda kuwaambia Waheshimiwa Wabunge kwamba katika mfumo wa Bunge la Katiba, ipo Kamati ya Maridhiano. Nadhani tuitumie Kamati ile ili tuweze kusonga mbele. Tumesema suala la Katiba ni suala kubwa, ni suala la maridhiano, na ni suala la kujenga muafaka.

Mheshimiwa Spika, imetolewa hoja kwamba, labda Mheshimiwa Rais asitishe mchakato huo. Nchi yetu inaheshimu utawala wa sheria, na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ndiyo ambayo imeweka mfumo wote wa kuendesha mchakato huu. Awamu ya kwanza tunafahamu ilikuwa ni kukusanya maoni, awamu ya pili ikaundwa Rasimu na hiyo ilifanywa kwa mujibu wa sheria, Rasimu ile ikajadliwa kupita Mabaraza na hatimaye ikatoka Rasimu ya pili ambayo iliwasilishwa hapa kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa utaratibu uliowekwa na Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, ngazi ya tatu ilikuwa ni ngazi ya Bunge la Katiba. Kwa hiyo, suala la kwenda kwa wananchi kabla, ni suala ambalo liko kinyume na sheria. *(Makofi)*

Kwa mjibu wa sheria hiyo, mchango wa wananchi kwa utaratibu wa kura ya maoni ni hatua itakayofikiwa pale patakapokuwa na Katiba iliyopendekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya sheria yanawezekana, kwa sababu kwa taratibu za Bunge lako Tukufu, kanuni ya 81 inaruhusu Mbunge kuleta hoja ya kufanya mabadiliko ya sheria. Hilo likitokea, basi labda itakuwa ni kazi ya Mheshimiwa Mbunge au Waheshimiwa Wabunge kufanya hivyo na siyo kazi ya Mhehsimiwa Rais. *(Makofi)*

Nashukuru kwamba Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amezungumzia mamlaka ya Bunge la Katiba. Kifungu cha 25 kinaeleza mamlaka ya Bunge Maalum, kwamba ni kujadili na kupitisha.

Kwa hiyo, haiyumkiniki kwamba kitu kitajadiliwa kisibadilishwe, kisiongezwe, halafu kikapitishwa. Hata tukikumbuka kanuni za Bunge Maalum, ambazo ziliwasilishwa hapa kwa umahiri mkubwa na Wajumbe wake, wakiwemo Waheshimiwa Tundu Lissu na Mheshimiwa Jussa, kanuni inazungumzia uwezo wa Bunge Maalum, ikiwa ni pamoja na kubadili, kuongeza, kurekebisha na kadhalika. Kwa hiyo, hayo yote yamefanyika kwa mujibu wa utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba yote yaliyotokea yako ndani ya wigo wa sheria na ninadhani kama Wabunge ambao tunahusika sana na kutunga sheria hiyo, kama watu ambao ni Viongozi, tuonyeshe mfano mzuri wa kufuata sheria. Kama sheria inahitaji mabadiliko, basi tufuate utaratibu ule ili tuweze kuleta mabadiliko.

Mheshimiwa Spika, limezungumzwa suala la takwimu na nashukuru wapo waliolizungumzia suala hili. Ni kweli kabisa kwamba takwimu zilikuwa na nafasi yake katika mchakato mzima na hakuna anayehoji kuwepo kwa takwimu.

Nadhani kubwa linalozungumzwa, na tutakumbuka hapa, tulipata uwasilishaji wa kitaalam kabisa, haukutoka kwenye Chama cha Mapinduzi, haukutoka kwenye Chama cha Siasa, ulitoka kwa msomi mahiri anayejulikana kwa jina la Profesa Assey**.** Alichambua kabisa kwa kutegemea yale aliyoyaona na kwa kujibu maswali yale kitaaluma kabisa. *(Makofi)*

Suala ni kwamba takwimu zilikuwepo, lakini hoja: Je, takwimu hizi ni Wakilishi, katika suala kubwa kama la kubadilisha mustakabali wa Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaheshimu sana kazi iliyofanywa na Mheshimiwa Jaji Warioba, tunaheshimu sana mchango mkubwa walioutoa na kama nilivyosema katika hotuba yangu asubuhi, kazi waliyoifanya imetuwekea msingi mzuri wa kujadili mustakabali wa Taifa letu. Nadhani hilo lilikuwa ni mojawapo ya majukumu ya Tume ile, wamekamilisha, tusitafute nafasi ya kuwapaka madongo, wamefanya vizuri. Kazi iliyobaki sasa ni Bunge la Katiba kutimiza wajibu wake na hatimaye kuwapa fursa Watanzania waweze kuamua Katiba wanayoitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika michango ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia kwa uchungu mkubwa suala la rushwa katika baadhi ya Taasisi zilizoko chini ya Wizara yetu. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali amezungumzia, nami naomba niongeze sauti yangu kidogo kwa sababu hili ni suala kubwa.

Rushwa inatolewa katika mazingira ya siri, ndiyo maana kwa muda mrefu imekuwa ni jambo ambalo tutaendelea kupigana nalo. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kwamba suala la rushwa tunalipa umuhimu wa juu kabisa katika kulikabili katika Mahakama zetu na Taasisi zote.

Tumeeleza hapa kwamba katika maboresho tunayoyafanya, maboresho ya sekta ya sheria, siyo tu kwa kuweka sheria kali au kwa kuweka adhabu kali, lakini vilevile kwa kuhakikisha kwamba miundombinu tuliyonayo inawawezesha watu kupata taarifa kwa namna ambayo haiwapi shaka shaka. Tumeeleza hapa, kuna masijala kadhaa ambazo zimefanyiwa ukarabati. Katika masijala hizi tumeweka mifumo ya kielektroniki. Mifumo hii itasaidia sana kuondoa usumbufu wa mtu nenda rudi, anakuja anataka jalada, au anataka taarifa, anaambiwa jalada halionekani.

Tutakapofanikiwa kuweka mifumo hii katika Mahakama zetu nyingi, au zote, itakuwa ni rahisi kwa mtu yeyote kuja wakati wowote kupata taarifa hizo, kwa sababu hilo ni jambo ambalo litaweka uwazi katika masuala ya kupata taarifa.

Mheshimiwa Spika, lakini kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, yapo pia mazingira ambapo taswira inayotolewa ni kama vile kuna rushwa, na kwa kweli hutamlaumu mtu ambaye anaweza kuwa hafahamu vizuri ni utaratibu gani unatumiwa katika mazingira ya kufungua kesi.

Kwa mfano, ipo mifano ambapo wanakuwa watu wawili, watatu kwenye kidirisha cha kulipia ada ya kufungua jalada, kesi zinatofautiana, ada zinatofautiana na inawezekana kabisa mmoja akaambiwa wewe lipa Sh. 10,000/=, mwingine Sh. 15,000/= na ikawa haieleweki.

Sasa kwa hili, tunajitahidi kufanya kazi na wenzetu walioko katika masijala, ili mifumo ya ada iweze kuwa wazi, iweze kufahamika kwa sababu inategemea aina ya shauri na uzito wa shauri.

Amezungumza Mheshimiwa Mbunge hapa kwamba wakati mwingine kesi zinaahirishwa na mtu anakuwa hafahamu mpaka afike pale Mahakamani, na kunakuwa hakuna taarifa.

Mheshimiwa Spika, lazima tukiri kwamba tunayo changamoto katika masuala ya mawasiliano. Bado mawasiliano yetu tuliyonayo ni ya mtu kwa mtu na hata kunapokuwa na kuahirishwa kesi, inawezekana kwa sababu za kibinadamu, inawezekana kwa sababu za kiufundi kesi ikawa haikuendelea kama ilivyopangwa na siyo rahisi sana kuweza kumtaarifu mhusika kabla ya yeye kufika pale.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi nchi yetu imepitia mageuzi makubwa ya kiteknolojia na katika fani ya mawasilino.

Kwa hiyo, inawezekana kabisa katika hali ya kujenga mifumo imara ikawezekana mtu kupata taarifa labda kwa njia ya simu. Bado hatujaboresha mifumo hiyo kwenye ngazi ya kupeana taarifa kimahakama, lakini tumesema hapa asubuhi, kwa mfano, kwa upande wa uandikishaji wa vizazi na vifo, tumeweza kutumia simu za mkononi kwa ajili hiyo, tumeweza kutumia tovuti, na ni matumaini yetu kwamba tutatafuta miundombinu ambayo itakuwa muafaka katika mazingira yetu ili kupunguza adha hiyo.

Mheshimiwa Spika, kumetokea hoja kuhusu taarifa za Tume ya Haki za Binadamu. Kwa utaratibu uliopo katika Bunge hili ni kwamba endapo hati itakuwa imewekwa Mezani, basi yule anayeweka Mezani, anaweza kuwa ni Waziri, inaweza kuwa ni Kamati au Mbunge, akaomba kwamba ijadiliwe. Kwa hiyo, napenda kuwatia shime Waheshimiwa Wabunge, pale ambapo hati hizo zitakapoweza kuwekwa Mezani, basi ipo fursa kwa kuzingatia kanuni tulizonazo, kuweza kutoa rai kwamba hati hiyo iweze kujadiliwa na hilo litakuwa kwa taarifa zozote ambazo Wizara yangu inataweza kuwasilisha.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba wapo Waheshimiwa Wabunge ambao wamezungumzia suala la wafanyakazi, watumishi wa Mahakama katika nchi yetu kwenye ngazi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tumeomba vibali kwa ajili ya kupata watumishi na vibali hivyo kama Waheshimiwa Wabunge wanavyoweza kufahamu vinatolewa kwa awamu na kwa nyakati zinazotofautiana.

Mheshimiwa Spika, lakini labda niseme kwamba katika kipindi cha miaka minane hivi hadi tisa kilichopita tumeona hatua mbalimbali ambazo Serikali imechukua katika kuboresha suala la ikama katika Mahakama, iwe ni katika ngazi ya Watendaji au ngazi ya Mahakimu na Majaji. Mabadiliko kadhaa yamefanyika. Mojawapo ya mabadiliko hayo ni kutenganisha shughuli za uendeshaji za kila siku na shughuli za kutoa haki.

Kwa hiyo, sasa hivi tunaye Mtendaji Mkuu wa Mahakama na chini ya uongozi wake tumeona mabadiliko katika masuala ya utumishi. Mahakama zimeongezewa Watendaji, zimeongezewa Mahakimu na vilevile kwa upande wa Mahakama za Mwanzo, tumeweza kuongeza idadi ya Mahakimu hasa kwa kuchukua wale ambao wamehitimu ngazi ya Shahada.

Mheshimiwa Spika, ila ningependa kusema kwamba, nchi yetu ni kubwa, ina wananchi wengi, takribani 45. Lakini Mahakama tulizonazo bado tunaendelea kuboresha kwa maana ya miundombinu yake, Mahakimu na Majaji, na hivi sasa labda niseme kumekuwa na ongezeko kubwa la Majaji hasa katika Mahakama Kuu, lakini bado kazi hiyo inaendelea na Mheshimiwa Rais ametuahidi kwamba kwa kadri hali itakavyoruhusu basi kutakuwa na ongezeko katika eneo hili.

Mheshimiwa Spika, tunapoboresha hali ya Mahakama, kwa maana ya miundombinu, kwa maana ya kuongeza Mahakimu na Majaji, ni lazima tukumbuke kwamba suala la uendeshaji wa mashauri Mahakamani linakuwa na sura tatu. Kuna sura ya Mwendesha Mashitaka, Ofisi ya Mwendesha Mashitaka Mkuu, lakini pia tuna Mawakili. Kwa hiyo, jitihada zetu ni kuhakikisha kwamba tunaendelea kuboresha hali ya Watumishi, miundombinu kwa uwiano, ili sehemu moja ya utoaji haki isikimbie mbele zaidi kwa sababu kazi zao zinatoshelezana.

Tutaendelea kufanya hivyo na tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao wametusemea hapa, tuweze kupata fedha zaidi. Lakini hata kwa fedha tulizonazo, tunataka kuwahakikishia kwamba tutatumia vizuri na zitakazoongezeka, zitafanya kazi yetu iwe bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii sasa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na kuwahakikishia kwamba yale yote mliyotuambia tutayazingatia, tutayatekeleza na tutafanya kazi kwa ari kubwa ili kuhakikisha kwamba Wizara yetu inatimiza matarajio.

Kwa upande wa mchakato wa Katiba, napenda tena kuudhihirishia Umma wa Watanzania kwamba Serikali ina nia ya dhati, ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha kwamba tunapata Katiba bora, Katiba itakayokuza umoja wa Taifa letu, Katiba itakayotupa utangamano na Katiba itakayohakikisha kwamba tunarithisha umoja kwa vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa fursa hiyo. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAMUEL J. SITTA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Hoja hiyo inaungwa mkono.

Waheshimiwa Wabunge, nataka nikumbushe jambo, naona tunataka kufanya vile visivyo. Tuna hiki kitu kinaitwa Mshahara wa Waziri, sasa naona wengine wanafikiri ni mradi tu kusimama, sivyo.

Kwa mujibu wa kanuni ya 101 (3), "Mbunge atakayeamua kutumia kifungu chenye mshahara wa Waziri ataruhusiwa tu iwapo ataomba ufafanuzi wa suala mahsusi la Sera na hatazungumzia zaidi ya jambo moja."

Kifungu kidogo cha (4), "kwa kuzingatia masharti ya fasili hiyo ya (3) (niliyosoma), Kamati za Vyama zitawasilisha kwa Spika majina ya Wabunge watakaoomba kupata ufafanuzi wa suala mahsusi la Sera na Spika atatoa nafasi kwa Wabunge kwa kuzingatia uwiano. Hiyo nayo muisikilize.

Fasili ya (5), muda wa kusema katika Kamati ya Matumizi kwa ajili ya kuomba au kutoa ufafanuzi hautazidi dakika tano. Lingine tutakuja kuzungumza baadaye namna ya kubadilisha matumizi wakati wa *Finance Bill*.

Kwa hiyo, kwa mfano mtu anakuja kutoa Shilingi; hii ilikuwa ni mshahara. Mshahara ni ufafanuzi tu, ndiyo maana ukisema mara moja sisi hatukuiti tena. Ni ufafanuzi.

Ukitaka maelezo yake yakubalike, ndipo kinakuja kifungu cha 103 (2) ambacho kinasema, "vile vile Mbunge yeyote anaweza kutoa hoja ya kuondoa Shilingi katika kifungu chochote cha fungu hilo."

Kanuni ndogo ya (3), "madhumuni ya hoja ya aina hiyo ni kumwezesha Mbunge aliyeitoa aweze kueleza kutoridhika kwake na utekelezaji wa jambo fulani mahsusi ambalo dhahiri inahusika na kifungu hicho."

Kifungu kidogo cha nne, "hoja ya aina hiyo itatolewa kwa muda usiozidi dakika tano."
Kifungu cha (5), "Wabunge wanaweza kuchangia hoja ya kuondoa Shilingi moja iliyoanzishwa kwa mujibu wa fasili ya (2) (niliyosoma hapo juu) kwa muda usiozidi dakika tatu kila mmoja."

Kwa hiyo, unapojaribu kuunga mkono hoja ile ama kutokuunga mkono wewe mwingine utatumia dakika tatu, yule mwenye hoja ana dakika zake tano.

Kifungu kidogo cha (6), "Waziri anayehusika atapewa nafasi ya kutoa majibu ya hoja hiyo, na muda wake unapangiwa na Spika."

Sasa iwapo hoja ile iliyotolewa na Mheshimiwa Mbunge imekataliwa, haizuii mtu mwingine tena kuomba hoja katika kifungu kile kile. Kwa hiyo, kama hoja ya Mbunge imekubaliwa, maana yake ameweza. Ikikataliwa anaweza pia akauliza hoja mtu mwingine katika kifungu kile kile.

Kwa hiyo, tumalize hapo, mengine tutazungumza baadaye kuhusu mabadiliko ya fedha. Katibu!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 12 - Tume ya Utumishi wa Mahakama**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Mgt* ..………… Shs. 2,577,802,900/=

**SPIKA:** *Addendum* ya hii, kwa sababu hata huku kwenye *sub-item* nako kumebadilishwa. Mheshimiwa Mnyika, sijui kama utakuwa nayo. Kuna *addendum*.

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Pamoja na *addendum*, niko kwenye Kasma 220700 inayohusu *rental expenses* ambapo mwaka wa 2013 zilitengwa Shilingi milioni 186.3, mwaka huu imetengwa Shilingi milioni 184.1. Sasa mwaka wa 2013 na mwaka 2012 wakati tunazungumza kuhusu fungu hili, tulisema kwamba Tume hii ya Mahakama muhimu sana inapanga kwenye jengo la Bodi ya Chai, ikaonekana Serikali ikalichukulia kwa uzito kwamba jambo hili linakwenda kufanyiwa kazi, lakini mwaka huu fedha zimepungua kutoka Shilingi milioni 186 mpaka Shilingi milioni 184.

Ningependa kupata ufafanuzi, iwapo kupungua huku kwa fedha ni kwa sababu ya kutekelezwa kwa azma sasa ya Tume hiyo muhimu sana ya Utumishi wa Mahakama kutokupanga tena kwenye jengo la Bodi ya Chai au bado inaendelea kupanga? Kama inapanga, kwa nini kodi ya mwaka wa 2013 ni kubwa kuliko kodi ya mwaka huu? Ningependa kupata ufafanuzi.

**SPIKA:** Kama tulivyosema, kuna mabadiliko makubwa katika kifungu kile, iko Sh. 604,180,000/=. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda tu kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba Tume ya Utumishi wa Mahakama kuanzia mwaka ujao wa fedha watahamia katika jengo jipya la *RITA Tower*.

Vile vile kuhusiana na kupungua kwa fedha hizo, ni kutokana na kupungua kwa kodi kidogo, na kwa sababu pia *RITA Tower* iko chini ya Wizara yetu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*……………Shs. 83,818,300/=

Kif.1003 - *Procurement Mgt Unit*...……………Shs. 67,625,000/=

*(Vifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 - *Recruitment Appointment and Confirmation*…..............................…….Shs. 557,353,800/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)*

Kif. 1006 - *Ethics and Discipline Section* ….Shs. 1,145,080,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa ufafanuzi kwenye kasma 210300 pamoja na marekebisho. Kifungu hiki kinahusu posho ambazo Tume hii hutoa inapofanya kazi pamoja na Kamati za Maadili za kwenye Mikoa na Wilaya. Sasa yamekuwepo malalamiko ya kwamba Kamati hizi za Maadili za Mikoa na Wilaya hazikai, na safari hii kuna nyongeza ya fedha kutokana na marekebisho yaliyofanyika.

Ningependa kupata ufafanuzi tu kutoka kwa Serikali: Je, kwa nyongeza hii sasa, kwenye kasma hii na vifungu vyake kumewekwa mfumo ambao utahakikisha hizi Kamati za Maadili kweli zitakaa na kushughulikia masuala ya malalamiko ya maadili dhidi ya Watumishi wa Mahakama kwenye ngazi za Mikoa na Wilaya?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na hoja ya Mheshimiwa Mnyika napenda pia kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Vikao vya Kamati za Maadili za Wilaya na Mikoa hivi sasa tumeimarisha mfumo wa Kamati hizo, tumefanya kaguzi mbalimbali, Tume imefanya ziara mbalimbali kwa ajili ya kwenda kuwaelimisha majukumu yao.

Kwa sababu zipo Kamati ambazo zilikuwa hazijaundwa, nyingine ni kutokana tu na kutokuelewa, lakini pia nyingine ni kutokana na hali ya bajeti ya fedha kwa sababu wanafanya vikao ambavyo haviko katika tawala zao au Uongozi wao katika Mkoa au Wilaya.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)*

**Fungu 16 - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Wa Serikali**

Kif. 1001 - *Admin. and HR Mgt*……………...Shs. 2,275,985,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Account Unit* ……. Shs. 748,542,000/=
Kif. 1003 - *Planning Division*………………….. Shs. 641,004,000/=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit* ………………. Shs. 482,580,000/=
Kif. 1005 - *Government Comm. Unit*……... Shs. 246,602,000/=
Kif. 1006 - *Legal Registry Unit* ………………. Shs. 299,078,000/=
Kif. 1007 - *Procurement Mgt Unit* …………. Shs. 376,987,000/=
Kif. 1008 - *Research & Library Serv. Unit* ….. Shs. 269,685,000/=
Kif. 1009 - *Inform. & Comm. Techn..* ……… Shs. 481,000,000/=
Kif. 2003 - *Legislative Drafting*……………. Shs. 1,378,517,000/=

*(Vifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Civil Litigation & Arbitration Division*……................................ Shs. 1,221,094,000/=

**MHE. JOHN J. MNYIKA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kasma 221100 - *travel out of country* ambayo mwaka 2013 ilitengewa Shilingi milioni 113.6, mwaka huu imetengewa Shilingi milioni 132.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti…

**MWENYEKITI:** Hebu soma, ni ngapi? Kiasi gani?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Kasma…

**MWENYEKITI:** Ndiyo, kasma tumeipata, lakini hela uliyosoma.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Shilingi milioni 113.6 na mwaka huu Shilingi milioni 132.8.

**MWENYEKITI:** Sawa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, sasa katika kifungu hiki ambacho kipo kwenye *program* thelathini ya *division* ya mashitaka na masuala ya Kimataifa. Kwa kweli ningependa kutoa hoja ya kuondoa Shilingi ili niweze kueleza kutoridhika na utekelezaji katika kasma hii kwenye masuala yanayohusu mashauri ya Kimataifa ambayo Serikali inakuwa inashitakiwa.

Mwaka wa 2013 wakati tunapitisha kifungu hiki nilitoa rai kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba kiwango cha fedha kwa ajili ya Mawakili wa Serikali kwenda kuitetea Serikali nje ya nchi, ambayo ndiyo kasma hii kiongezwe ili kuepusha hali ya sasa ambapo Serikali inatetewa kupitia Wizara zake, Taasisi zake na masharika yake, na Mawakili binafsi ambao wanalipwa pesa nyingi sana za Umma lakini tunashindwa kesi kweli kweli Kimataifa. Sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali akasema jambo hili ni zito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ule nazungumza nilizungumzia suala la *IPTL*, nikaeleza kwamba kwa kesi chache tu za *IPTL* ambazo tulishitakiwa kule *Hong Kong*, na kesi za *Dowans* na nyinginezo, kamapuni moja tu ya Uwakili ilikuwa inalipwa, unakuta kwenye Bajeti ya Serikali Shilingi bilioni kumi, yaani Shilingi milioni 10,000 kwa ajili ya kulipa Kampuni moja tu ya Uwakili. Nikataja mpaka jina la Kampuni, "*Mkono and Company Advocates*." Mwanasheria Mkuu wa Serikali akasema jambo hili atakwenda kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, kama tuna pesa nyingi namna hii, kwa nini hatulipi Mawakili wetu wakaenda kutetea? Kwa nini tunalipa fedha nyingi zaidi halafu tunakwedna kushindwa kesi mbalimbali? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashanga safari hii vile vile. Kwa hiyo, naomba majibu. Naomba kuondoa Shilingi na Wabunge wenzangu ambao wanaona uchungu na namna pesa zetu zinavyotumiwa vibaya waweze kuunga mkono hoja hii.

**MWENYEKITI:** Unasema hivi, kama sikuridhika naondoa Shilingi sivyo!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama sikuridhika, naondoa Shilingi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Eeh, ni taarifa hiyo. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ni vizuri kutumia Mawakili wa Serikali kwa ajili ya kupunguza gharama za kesi hizi. Naomba kusahihisha kitu kimoja kwamba hatujashitakiwa *Hong Kong* na Mahakama za *Hong Kong* hazina mamlaka dhidi yetu sisi.

Kinachoendelea kwenye kesi hii iliyotajwa ya *IPTL* ni kwenye usuluhishi. Fedha hizi tulizoweka hapa, siyo za kusimamia kesi nje ya nchi. Hizi ni za kuwasaidiwa Mawakili wanaokwenda kwenye mafunzo pamoja na hizo kesi kama ku-*understudy* watu. Hiyo ni moja. *(Makofi)*

Ya pili, tusiangalie wingi wa fedha, tuangalie hoja. Muhimu kabisa! Hii kesi anayosema, kwa mfano kwenye *arbitration* huwezi kusema upeleke Mawakili wa Serikali kule kwa sababu hawatakuwa na *locus*…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ngoja kwanza tuelewane. Maana naona mnaingia kitu ambacho mmesema hapa siyo zenyewe, sasa mnaendelea kusema nini hapa?

Naomba ujibu hoja ya kifungu hiki, tuko kwenye *item*, hatuko kwenye mjadala tena.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, lakini nilikuwa nafikiri kwamba kwa *travel out of country* ambayo ndiyo Mheshimiwa Mnyika anazungumza, hii ya Shilingi milioni 113 kupanda mpaka Shilingi milioni 132 ni kwa ajili ya uendeshaji wa hizo kesi. Lakini nilitaka kusahihisha moja kwamba wakati fulani huwezi kutumia Mawakili wa Serikali kwa sababu hawatakuwa na ile *locus standi* kwenye Mahakama hizo au kwenye majopo hayo.

Kwa hiyo, katika nafasi hiyo, ndiyo maana unaajiri Wakili mwingine nje ya nchi na ambaye pia anaweza kushirikiana na Mawakili wengine hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu yangu ndiyo hayo.

**MWENYEKITI:** Hii huwezi kutoa Shilingi, kwa sababu haihusiani na hayo unayotaka wewe, hayako hapa.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inahusiana kabisa!

**MWENYEKITI:** Haihusiani kwa sababu…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Ninayo randama hapa…

**MWENYEKITI:** Naomba ukae kidogo. Ehee, soma randama yako. Soma kifungu hicho.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tu nisikilizwe wakati nafungua hii randama.

**MWENYEKITI:** Ngoja kwanza, naomba ukae kidogo. Ninachowaombeni, tunapokuja kwenye fedha, hatuzui kitu. Kama randama inasema alivyojibu Mwanasheria sivyo, basi hilo unaruhusiwa kutoa Shilingi. Randama inasema nini kwa *item* hii?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, randama inasema kwamba pesa hizi ni pamoja na kuwasafirisha kikazi Mawakili wa Serikali kwenda kwenye kesi nje ya nchi.

Sasa nchi yetu ina kesi zimeshitakiwa nje. Nimesema *Hong Kong* kwa sababu tu kesi *IPTL* vile vile inahusu *Exim Bank* ya *Hong Kong*, lakini kwa maana ya mashitaka yako Uingereza, Marekani; na Makampuni siyo Mkono tu, *Rex Attorneys* kwenye kesi ya *Dowans*, yako mengi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema, kama kwa kifungu hiki tungeweza kusafirisha Mawakili wetu kwa kifungu hiki, kwenda kusimamia kesi zetu, na tungewaongezea uwezo Mawakili wetu, tungepunguza gharama kubwa ya Serikali, wakati huo huo tungesimamia kesi zetu kwa ufanisi zaidi. Ndicho ninachokisema hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo Mwanasheria Mkuu wa Serikali, mwaka wa 2013 alisema kwamba watalifanyia kazi. Nashangaa mwaka huu analifanya kama ni jambo jipya kabisa, ni jambo ambalo haliwezekani kabisa, ni jambo ambalo halitekelezeki kabisa. Kuna nini nyuma ya pazia?

**MWENYEKITI:** Haya, ngoja na mimi najua kusoma randama, na haihusiani hapa. Inasema, *travel out of country* ni Sh. 132,800,000,000/=. Fedha hizi zinaombwa kwa ajili ya gharama ya safari za ndege za kikazi ikiwemo safari ya matengamano na kikanda kwa kulipia *ticket* za ndege na posho ya kujikimu kwa watumishi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 - *Treaties and Contracts Div*…… Shs.1,323,485,000/=

**MHE. SELEMANI SAID JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hoja yangu iko katika kifungu 210100. Ukifanya mlinganisho wa bajeti ya mwaka wa 2013 na mwaka 2014, mwaka wa jana ilikuwa karibuni Shilingi milioni 381, mwaka huu tumeshuka mpaka Shilingi milioni 363.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wazi kwamba sasa hivi nchi yetu ina ajenda kubwa sana ya kusimamia mikataba, hasa ikiwemo mikataba ya gesi. Lakini naona kwamba mshahara huu umeshuka, na najua kwamba *motivation* ya mfanyakazi yeyote atafanya kazi kwa uadilifu endapo mshahara wake utakuwa umekaa katika mazingira mazuri. Sasa nataka kupata ufafanuzi, ni kwa nini kiwango cha mshahara kimeshuka hapa wakati nchi yetu sasa hivi inakwenda katika *commitment* kubwa ya mishahara kwa wafanyakazi wa kulinda rasilimali zetu za nchi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu!

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi zitatumika katika kulipia mishahara ya watumishi wapya wataoajiriwa katika Idara hii ya mikataba ya Kimataifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Susan Lyimo!

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru suala langu lilikuwa ni hilo hilo lakini nadhani bado Mheshimiwa Naibu Waziri hajajibu vizuri kwa sababu kama wanaajiri, maana yake mshahara ungeongezeka, lakini hapa mshahara umepungua. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba maelezo ni kwa nini umepungua kama wanaendelea kuajiri?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wako sahihi. Hizi zimepungua kwa sababu kuna Maafisa ambao wamehamia kwenye Idara nyingine za Serikali na Idara moja ni ile ya Maliasili. Kwa hiyo, ndiyo maana zimepungua.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

*Kif. 4001 - Constitutional Affairs and Human Rights................................... Shs. 1,015,204,000/=*

**Fungu *35 -Public Prosecutions Division***

Kif. 2002 - *Public Prosecutions Division* .. Tshs. 8,768,924,000/=
Kif. 2004 - *Zonal Office* Arusha ................ Tshs. 962,365,000/=
Kif. 2005 - *Zonal Office* Dodoma ........... Tshs. 618,983,000/=
Kif.2006 - *Zonal Office* Dar es Salaam ... Tshs. 1,586,973,000/=
Kif. 2007 - *Zonal Office* Iringa ............... Tshs. 426,688,000/=
Kif. 2008 - *Zonal Office* Moshi .............. Tshs. 614,786,000/=
Kif. 2009 - *Zonal Office* Kagera .......... Tshs. 487,883,000/=
Kif. 2010 - *Zonal Office* Mbeya ........... Tshs. 602,016,000/=
Kif. *2011* - *Zonal Office* Mtwara .......... Tshs. 489,238,000/=
Kif. 2012 - *Zonal Office* Mwanza .............Tshs. 910,265,000/=
Kif. 2013 - *Zonal Office* Ruvuma .............. Tshs. 489,837,000/=
Kif. 2014 - *Zonal Office* Sumbawanga ......Tshs. 404,650,000/=
Kif. 2015 - *Zonal Office* Tabora ..................Tshs. 652,682,000/=
Kif. 2016 - *Zonal Office* Tanga ........... Tshs. 640,505,000/=
Kif. 2017 - *Zonal Office* Shinyanga ...... Tshs. 516,299,000/=
Kif. 2018 - *Zonal Office* Singida ........... Tshs. 356,981,000/=
Kif. *2019* - *Zonal Office* Lindi ................ Tshs. 307,937,000/=
Kif. 2020 - *Zonal Office* Mara ............... Tshs. 427,516,000/=
Kif. 2021 - *Zonal Office* Manyara ......... Tshs. 335,955,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2022 - *Zonal Office* Kigoma ......... Tshs. 341, 428,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nitajielekeza pale kwenye *sub item* 210100 *Basic Salaries - Pensionable Posts.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina swali moja kwa Serikali. Mwaka 2013 naona ilitengwa Shilingi milioni 33 katika kifungu hicho na mwaka huu naona kidogo fedha zimeongezeka Sh. 61,692,000/=. Niliuliza swali moja, nikasema ni lini Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaanzishwa katika Wilaya ya Kasulu? Majibu niliyopewa, walisema kwamba kwa mwaka utakaokuja ambao ni mwaka huu sasa ambao utaishia tarehe 30 Juni, nilikuwa naomba kupata ufafanuzi, kwa kuwa hadi sasa hakuna chochote kile ambacho kimefanyika; Serikali inatoa kauli gani kuhusiana na ahadi yake ambayo ilitoa mwaka 2013, kwamba Ofisi ndiyo ingekuwa imeanza pale lakini hakuna chochote ambacho kimefanyika?

Naibu Waziri Mheshimiwa Angella Kairuki aliweza kujibu na alieleza Bunge lako. Sasa ningependa kupata ufafanuzi wa Serikali, ni lini utekelezaji wa suala hili utafanyika?

**MWENYEKITI:** Kwani hapa ni mahali pake?

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu inahusiana na mshahara.

**MWENYEKITI:** Ofisi ni *Development*, hii ni mishahara tu!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Nimehoji kwamba pesa zimeongezeka, nilitaka kujua iwapo fedha hizi ambazo zimeongezeka, zita-*include* Wanasheria wa Serikali ambao watakuja kufanya kazi katika Wilaya ya Kasulu? Hii ndiyo sehemu yake hapa; ambapo kama ni wapya au vyovyote vile. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hilo la pili, umeuliza; suala la Ofisi hujauliza.

Hilo la pili: Je ita-*include* mtumishi atakayekuja kufanya kazi Kasulu? Hiyo sawa. Siyo Ofisi. Ofisi haihusiki hapa!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge. Ni kweli kwamba tuna mpango wa kwenda Kasulu na tumeshafanya mpango, tumepata jengo pale na fedha hizi unazoziona hapa wakati fulani ni ili kwa ajili ya baadaye kwenda kukarabati jengo lile ambalo tumepewa ili tupeleke Mawakili kule. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naomba na wewe ujibu vizuri! Haiwezekani *basic salary pensionable posts* mkakarabati maofisi. *(Kicheko)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba radhi kwamba labda nimefanya haraka tu, lakini hapa, ili kuhamia huko si ni lazima uwe na wafanyakazi! Kwa hiyo, ndiyo maana hizo fedha zimeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile la ukarabati ni jambo lingine. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 2023 - *Zonal Office* Pwani ................ Tshs. 390,154,000/=
Kif. 2024 - *Zonal Office* Njombe .......... Tshs. 347, 026,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 2025 - *Zonal Office* Morogoro ......... Tshs. 374,907,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Suzan Kiwanga!

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nipo kwenye *sub-vote* 220700 - *Rental Expenses.* Naona mwaka uliopita walipanga Sh. 22,400,000/= lakini mwaka huu zimepungua mpaka Sh. 13,400,000/= na ukiangalia Mkoa wa Morogoro kuna matatizo makubwa sana kuhusu Ofisi. Je, kumetokea nini? Wamejenga au kuna kitu gani? Kwa sababu kuna shida nyingi sana!

**MWENYEKITI:** Kwa nini fedha zimepungua? Ndiyo swali tu!

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Eh, kwa nini hela zimepungua? Ahsante.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro Jengo bado lipo na tunalilipia, lakini idadi ya Watumishi inapungua pale na watumishi ambao tulitegemea kwamba tutapewa, hatukupewa. Ndiyo maana unaona zinapungua pale. Tutalipa pango la Ofisi, lakini nyumba za Mawakili fedha inapungua kwa sababu ni wachache. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

Kif. 2026 - *Zonal Office* Geita ..... Tshs. 251,032,000/=
Kif. 2027 - *Zonal Office* Simiyu ........... Tshs. 162,495,000/=
Kif. 2028 - *Zonal Office* Katavi ............ Tshs. 163,502,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kif. 2002 - *Court of Appeal DSM* ..........Tshs. 123,300,345,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kimepitishwa na Kamati ya Matumizi pamoja na Marekebisho yake)*

**Fungu 41- Wizara ya Katiba na Sheria**

Kif. 1001 – *Admin. and HR Mgt* ............... Tshs. 8,074,067,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika! Au umeridhika? *(Kicheko)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nimesimama kwa ajili ya kushika mshahara wa Waziri na iwapo majibu hayataridhisha, nitaomba kuondoa Shilingi kwenye mshahara wa Waziri; juu ya masuala yote ya utekelezaji yanayohusiana na Bunge Maalum la Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ndiyo ambayo ina dhamana ya kuisimamia Sheria ya Mabadiliko ya Katiba na utekelezaji wake, na pale inapobidi kuifanyia marekebisho. Katika kuitekeleza Sheria hiyo, Wizara hii inashirikiana na Wizara nyingine ikiwemo Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba masuala ya uendeshaji yanakwenda vizuri, na inashirikiana na Wizara nyingine ikiwemo Ofisi ya Rais kuhakikisha kwamba kuna muafaka wa Kitaifa kwenye mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa mujibu wa majibu yaliyotolewa na Waheshimiwa Mawaziri, Mheshimiwa Waziri wa Ofisi ya Rais (Mahusiano na Uratibu), majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria yameashiria kwamba Wizara hii ya Katiba na Sheria na Serikali haina dhamira ya kujenga muafaka wa Kitaifa katika mchakato wa Katiba Mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, tukirejea katika hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ambaye amehoji kwa kina juu ya matumizi ya fedha za Bunge Maalum, ambayo ameyaita Bunge Maalum na harufu ya ufisadi, kama hali hii itaendelea, hakuna sababu ya kuendelea kutumia fedha nyingi za walipa kodi kufanya kazi ambayo tunajua matokeo yake ni matumizi mabaya ya rasilimali za walipa kodi.

Naomba tu nimweleze Mheshimiwa Waziri kwamba rai ya kusema turudi, hatuko tayari kurudi kwa sababu dhamira imeshaonekana ya namna ambavyo hamko tayari kusimamia maoni ya wananchi. *(Makofi)*

Sasa jambo la msingi ambalo ndilo Msemaji wa Kambi ya Upinzani amelihoji ni juu ya fedha za Bunge Maalum; na Mheshimiwa Waziri katika ufafanuzi wake amesema kwamba fedha hizi ziko katika fungu la Hazina, Fungu 21, katika kasma ya *contingencies*.

Mheshimiwa Waziri alipokuwa anajibu nikapitia kitabu kizima hiki cha Hazina na nikapitia vile vile kitabu mahsusi cha Wizara ya Fedha, Hazina, hiyo kasma aliyoizungumza na maelezo yake ni kasma 290704 ya *Domestic debts* ambayo kichwa kikuu ni *contingencies non emergencies*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachotaka kusema ni nini hapo?
**MWENYEKITI:** Unasema mno, umemaliza muda wako.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwa hiyo, ninachokisema ni kwamba Serikali haileti Bungeni mchanganuo wa fedha za Bunge Maalum, na majibu yasiporidhisha naomba kutoa Shilingi katika hili kwa sababu majibu hayaridhishi.

Naomba majibu, nisiporidhika naomba kuondoa Shilingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umemaliza muda wako. Wewe hupendi kutumia muda. *I am very specific with time*. *This you have to understand.* Naomba maelezo! Naibu Waziri wa Fedha! *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA- (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mnyika, labda kama alikuwa anatafuta tu sababu ya kutokurudi, lakini kwenye fungu namba 21 za *treasury sub-vote* 2001 - *Government Budget Division*, kifungu namba 290700; Kifungu hicho kinaitwa *contingencies non emergences* kwa maana ya kasma ya mambo hayo ya *contingencies*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kifungu hicho hilo suala haliko suala la Bunge la Katiba tu, kuna masuala mbalimbali nimeyakusanya hapo. Moja ni gharama za Bunge la Katiba

awamu ya pili, upigaji wa kura za maoni, gharama zake zimo humo ndani, kuhuisha Daftari la Kudumu la Wapiga kura, gharama zake zimo humo ndani, gharama za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, maandalizi ya Uchaguzi Mkuu 2015, madeni ya wazabuni wadogo na watumishi yaliyohakikiwa na gharama za Walimu wapya na Madaktari watakaoajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka kumsaidia tu Mheshimiwa, kama alikuwa anatafuta sababu ya kuondoka, siyo kwa sababu ya hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilivyowasomea kanuni, ni lazima tuwe *very specific* na *issue* kusudi sisi wote tuweze kuvuta mawazo yetu tukapime. Sasa mara kuondoka, mara hesabu mara fedha, mara nini; haya, sasa ondoa Shilingi *very specific*!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuondoa Shilingi na naomba kuwa *very specific* kwa sababu Mheshimiwa Naibu Waziri amekuwa *very specific*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hicho alichokisoma Mheshimiwa Naibu Waziri mimi ninacho hapa, Kasma 290700 *Contingencies non-emergency*, *vote* hiyo *domestic debts***,** kwa mwaka huu imetengewa Shilingi bilioni 188. Halafu kuna orodha ndefu ya matumizi. Hakuna mchanganuo kiasi gani kitakuwa cha Bunge Maalum, kiasi gani kitakuwa cha upigaji kura, kiasi gani kitakuwa cha daftari, hakuna mchanganuo wowote!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema, mwaka wa 2013 lilipoulizwa jambo hili kwenye Kamati Serikali, ikaijibu hivi Kamati ya Katiba na Sheria kwamba "bajeti ya Bunge Maalum, kwa mujibu wa Mabadiliko ya Katiba Sura hiyo, masuala yote ya Bunge la Katiba yapo chini ya Bunge Maalum la Katiba." Kwa hiyo, ni kama vile Kamati haitakiwi kujua kwa sababu mambo ya fedha za Bunge Maalum yako chini ya Bunge la Katiba. Baadaye walipobanwa wakaambiwa jamani haiwezekani, Bunge hili ndilo linalopitisha fedha, lazima fedha ziwekwe, wakasema hivi; mwaka huu sasa kwenye maelezo kwamba Shilingi bilioni 24.4 zimewekwa kwenye Fungu la Hazina as *special expenditure*, sawa sawa?

Serikali ilifanya hivyo kwa kutambua kwamba Bunge Maalum lingeanza kazi bila mahitaji yake kujulikana wakati huo. Safari hii, tukiwa tunalijua Bunge Maalum, tunajua idadi ya Wajumbe, tunajua idadi ya muundo wake, tunataka siku za Vikao Rais amesema ni 60. Serikali imetenga Shilingi bilioni 20 ambazo inasema kwa mdomo. Kwenye maelezo haya, haielezwi hata Shilingi moja itatumika kwa kitu gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili jambo linahitaji kujadiliwa kwa sababu kama katika awamu ya kwanza ya Bunge ilitumia siku 90, na matengenezo ya Bunge ya gharama kubwa kweli, fedha tuliambiwa hapa Shilingi bilioni 26.8, haiwezekani katika awamu ya pili, siku chache zaidi hakuna matengenezo, fedha za Bunge Maalum tukaambiwa Shilingi bilioni ishirini. *Unless* kama hapa kuna ufisadi. *Unless* kama kuna kitu kinafichwa hapa, tujadili ili tuletewe mchanganuo, hizo Shilingi bilioni 20 zinazotajwa hapa kwenye taarifa zinatumika kwenye kitu gani? *(Makofi)*

Mara ya mwisho mlituambia hamjui idadi ya Wajumbe, sasa mnajua idadi ya Wajumbe. Tupeni hapa mchanganuo, Shilingi bilioni 20 za Bunge Maalum zinatumika kwenye nini? La sivyo utaona mnakwenda kuwahonga Wabunge wa Bunge Maalum kwa sababu mnajua UKAWA tumesusia, mnakwenda kuwahonga huko mbele tunakokwenda. Tunaomba mchanganuo na naomba jambo hili lijadiliwe, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kwanza kabla hamjajadili wote mkae chini. Neno kuhonga linahusiana nini hapa? Linahusana nini? Hatuwezi kupitisha…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeondoa neno kuhonga, kwenda kurubuni.

**MWENYEKITI:** Vyovyote vile! Hiyo kama ndiyo hoja yako, kwa maana hoja itatoka kwenye hoja yako…

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeondoa hiyo, kwenda kulipa posho kubwa kuliko kiasi.

**MWENYEITI:** Haya, unachotaka. Zile mlizopokea ninyi wote! Mheshimiwa Mkosamali!

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa wenyekit, nashukuru. Nami naunga mkono hoja hii, kwa sababu toka kwenye Kamati tumekuwa tunapewa…

**MWENYEKITI:** Hoja gani unaunga mkono?

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Hoja ya kutaka mchanganuo wa fedha za Bunge la Katiba ufahamike, ndiyo hoja iliyoko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba ufafanuzi tangu kwenye Kamati, tupewe mchanganuo, fedha hizi zinakwenda kulipa nini? Zimetokea sentensi za kutuchanganya toka kwenye Bunge la Katiba mpaka hapa.

Mheshimiwa Waziri wa Fedha wakati wa Bunge la Katiba alisema fedha zilizotumika ni Shilingi bilioni 27. Mheshimiwa Lukuvi ametuletea taarifa nyingine kwenye Kamati, kwamba fedha ni Shilingi bilioni 24 zilizotumika. Lakini ni kauli za Mawaziri tofauti. Huyu anasema Shilingi bilioni 27 huyu anasema Shilingi bilioni 24. Hii ni harufu ya rushwa na ufisadi. Lazima tujue fedha hizi za mwaka huu, hizi Shilingi bilioni 20 mchanganuo wake ni nini? Posho ni nini? Ukarabati ni vitu gani? Tumepewa majibu ya uongo uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na fedha ambazo tulizitenga kwenye bajeti ya Bunge ambazo zilikuwa ni za ukarabati. Mheshimiwa Lukuvi alivyotujibu kwenye Kamati akaja kutueleza kwamba kuna fedha ambazo zilitumika kutengeneza viti humu ndani. Sasa hii yote ni michanganyiko, haieleweki hizi fedha ni kiasi gani? Ni fedha za Bunge la kawaida kiasi gani? Tunaomba jambo hili liwe wazi, hatuwezi kukubali mchakato wa Katiba uwe na mambo ya kufichwa fichwa kwa namna hii.

**MWENYEKITI:** Haya, muda wako umekwisha. Mheshimiwa Mnyaa!

Naomba tukubaliane! Ikipiga kengele imepiga. Hii kelele mnaendelea nayo baadaye inasaidia nini? Jipangeni vizuri. Mheshimiwa Eng. Mnyaa!

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru…

**MWENYEKITI:** Kengele ikipiga, imepiga. Maneno ya zaidi ya hapo siruhusu!

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Kwa kweli mimi naunga mkonyo hoja ya…*(Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Hebu, mdomo hauna ulim…nini! Mdomo hauna nini? *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ENG. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti dakika zangu zilindwe. Watu wafurahi halafu…

**MWENYEKITI:** Yaani ninyi kitu kidogo tu mnaendelea, hebu endelea Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**MHE. ENG. MOHAMED J. H. MNYAA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mnyika kwa sababu hii ni Wizara ya Katiba na Sheria, lakini Wizara yenyewe inavunja sheria. Wizara hii ingepaswa iwe ndiyo kielelezo lakini inavunja sheria, Wizara hii inamshauri vibaya Rais kwa sababu ndani ya Wizara hii kuna Waziri, Naibu Waziri, Mwanasheria Mkuu, si tatizo la fedha tu, ni matatizo mengi yanayoikabili Wizara hii na ndiyo yaliyosababisha wao wakashindwa kumshauri Rais vizuri, wakavunja Kanuni ya (7) ya Bunge Maalum la Katiba ikabidi Rais aje baada ya Rasimu kuwasilishwa.

Sasa hawa wanatuletea taabu ikiwa hawakufafanua wakatoa vizuri mchanganuo wa fedha, hivyo ni kwamba ni Wizara yenyewe inashiriki kuleta matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tabia hii ikiachwa kwamba fedha ifungwe fungwe, haijulikani hii ni ya kutumia wapi na hii ni ya kutumia wapi, ndiyo chanzo cha ufisadi. Hili halikubaliki na kwa maana hiyo, ili kupitisha bajeti ya Wizara hii ni lazima wafafanue tujue bajeti ya Bunge la Katiba iliyotengwa ni ipi, tujue ya chaguzi za Serikali za Mitaa ni ipi, tujue ya kura ya maoni ni ipi, lakini kwa kuachwa hivi hivi tu, haiwezekani, huu ni uvunjifu na Wizara haipaswi yenyewe kuvunja sheria. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Kengele imeshalia. Mheshimiwa Martha Mlata!

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namuunga mkono Mheshimiwa Waziri na kifungu hiki nakiunga mkono kwa sababu haiwezekani kutenganisha fedha hizi kwa sababu watu wenyewe hawa ni sawa na hali ya hewa ya Dar es Salaam. Mvua inanyesha asubuhi, jioni jua kali limewaka. *(Kichelo/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliingia hapa tulikuwa na siku ambazo tulikuwa tumezitenga. Wewe mwenyewe umeshuhudia ni siku ngapi tulizitumia kwa ajili ya kutunga kanuni peke yake, matokeo yake watu wenyewe wamekimbia. Mimi naitaka Serikali, watu hawa wapelekwe Mahakamani, warudishe fedha za Watanzania ambazo wamezitumia. *(Kicheko/Makofi)*

Wamechukua fedha na wameondoka na wamesema hawarudi. Wapelekwe Mahakamani wakarudishe fedha za Watanzania. *(Makofi/Kicheko)*

**MJUMBE FULANI:** Mwongoooooooooo!

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mwongozo wa Mwenyekiti, Mwongozo wa Mwenyekiti!

**MWENYEKITI:** Hakuna cha mwongozo wakati wa Kamati ya Matumizi.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, amesema uongo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machali, siwezi kukupa nafasi kwa sababu unapiga kelele. Mheshimiwa Lukuvi! Wapiga kelele wote hawapati nafasi kama nakaa kwenye Kiti hiki. Mheshimiwa Lukuvi!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushuhuda kidogo juu ya haya yanayolalamikiwa. Hakuna ufisadi wa fedha zile zilizotumika kwenye Bunge la Katiba. Labda niseme pengine hatuelewi zilivyotumika.

Bunge hili la Katiba tumeanza wakati ambapo sisi tumepitisha bajeti kuipa fedha Bunge letu la Jamhuri ya Muungano, kufanya marekebisho ya miundombinu ndani ya Bunge. Kwa hiyo, marekebisho mnayoyaona yamefanywa kwenye jengo la utawala ni fedha za Bunge la Jamhuri. Marekebisho mnayoyaona kwenye jengo lile ni fedha zilizotengwa kihalali na *Commission* na Bunge hili kwa ajili ya Bunge la Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha pekee iliyotumika kati ya hizo zinazotajwa, ni kwa ajili ya kununua vifaa, hata magari hatukununua; tumeazima yale yaliyokuwa yanatumika kwenye Tume ya Katiba ndiyo tumeyaleta hapa. Fedha pekee zilizotumika na Bunge katika kasma hiyo ya mabilioni mnayoyasema kununua vifaa kwa ajili ya Bunge ni viti hivi. Viti 637, vimenunuliwa. Asilimia 80 ya fedha zote zimetumika kwa posho zetu, zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuwa na matumizi yoyote nje ya fedha za posho, nauli za kuwaleta Wajumbe na kuwarudisha makwao, na posho. Ingawa wakati tunakuja hapa mnajua kiwango cha posho kilichopangwa na tulipofika hapa Bunge liliamua kuongeza kiwango cha posho kufika Shilingi 300,000/=. Yaliyofanywa hapa yanaweza kuonekana hata kwa macho. *(Makofi/Minong'ono)*

Sasa kwa kuwa nyie hamkutoa *figure,* niipinge? Mimi natoa tu mazungumzo ya jumla. Nasema natoa ushuhuda kwa sababu nafahamu.

**MWENYEKITI:** Wote wanaopiga kelele, hawana hoja, naombeni Waheshimiwa muwe na uvumilivu. Naomba Mheshimiwa Waziri ukae.

Wenzenu wakisema kila mtu anatulia, lakini mnavyofanya hatuwezi kupata majibu yoyote, ni fujo tu. Kwanini tufanye fujo? Lengo letu ni kufanya fujo au kupata maelezo?

Tunazungumza kwa mtu, Esther una tabia ya kusema hovyo. Sasa nawataja kwa mujibu wa Kanuni yangu. Kwa mujibu wa Kanuni mnamtaja mtu na nikiamua naweza kuchukua askari. Kwa hiyo, nawaomba tuheshimiane! Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha! Aaah Mheshimiwa Lukuvi hujamaliza, samahani nilikukatiza. Waheshimiwa naomba tuheshimiane.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa namalizia kusema. Fedha hizi zinazokuja kwa awamu ya pili hakuna tunachonunua; hakuna samani tunayonunua. Fedha zote zitatumika kwa ajili ya utawala wa Wajumbe, posho na maandishi ya Rasimu ya Katiba inayotarajiwa na wananchi kwa viwango vilivyowekwa.

Sasa ukitaka niwaambie *data* kwamba nani atalipwa nini, ni kutokana na mahudhurio atakayokuja mtu. Lakini fedha zote hizi zilizotengwa ni kwa ajili ya utawala, malipo ya posho na uandishi wa Rasimu ya Katiba ambayo tunaipendekeza kwa wananchi. Hakutakuwa na ununuzi wa vitendea kazi kwani tuliishanunua kipindi kilichopita, ndiyo maana hizi zinakuwa chache kuliko zile za mwanzo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha!

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ADAM K. MALIMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niwasaidie wenzangu. Hizi ni gharama za *contingence* na hakuna *budget framework* yoyote duniani inayokosa *contingence*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *contingence* ni zile gharama ambazo katika matarajio yake hayatarajiwi kujirudiarudia, kwa hiyo zinawekwa kwenye *contingence.* Hilo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, Fungu 21 inaitwa Hazina na ni fungu ambalo liko chini ya Wizara ya Fedha. Sasa siku Wizara ya Fedha itakapokuja na mafungu yake, wanataka kujua *break down* ya hii fedha ambayo iko kwenye 2970 wataidai siku hiyo na Wizara tutasimama kwenye vifungu na tutawapa *break down* yao. Lakini wameuliza, fedha za Bunge la Katiba ziko wapi?

Nimewaambia ziko kwenye *contingence* Fungu 21. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyika!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuhitimisha mjadala kwa kusema kwamba, sikubaliani kabisa na majibu yaliyotolewa na Serikali. *(Makofi)*

**MJUMBE FULANI:** Sawa!

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Nianzie kwanza kwa Mheshimiwa Naibu Waziri anaposema kwamba, fedha hizi ni *contingence*, mwaka 2013 walituambia *contingence* kwa sababu hawajui muundo wa Bunge, sasa wanajua muundo wa Bunge bado wanataka *contingence*. *Contingence* hiyo mpaka lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Mabadiliko ya Katiba pamoja na kwamba matumizi yake yalikuwa hayatabiriki, ilitengenezewa Fungu Na. 8 la Tume ya Mabadiliko ya Katiba na tukawa tunapitia kifungu kwa kifungu matumizi ya Tume. Kwanini katika Bunge Maalum, hakuna Kifungu Maalum cha Bunge Maalum chenye mgawanyo wa matumizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ushauri wa Waziri kwamba tusubiri Wizara ya Fedha, hatuko tayari kusubiri, hatuko tayari kuunga mkono kupitisha bajeti ya Wizara hii. Hatuko tayari kuuziwa mbuzi kwenye gunia kwenye jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lukuvi amechangia hoja hii, alikuwa anazungumza mambo ya ujumla tu. Hajatupa mgawanyiko, hajatupa mchanganuo, hajajibu masuala ya msingi. Tunahitaji kujua hapa Shilingi bilioni 20 zinatumikaje? Kwa sababu katika Bunge lile la Katiba tulikuwa tunaambiwa kikao kimoja kilikuwa bei gani? Shilingi milioni 150 kwa siku. Tulikuwa tunaambiwa mkitoka siku moja… *(Minong'ono)*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Hata kama ukisema ngapi, sawasawa! Kikao kimoja kikiwa Shilingi milioni 150, ukizidisha mara siku 90 ni Shilingi bilioni tisa. Sasa kama kikao kimoja ni Shilingi bilioni tisa, hizo Shilingi bilioni 20 ni za vitu gani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Unasoma wapi hizo?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *mathematics* rahisi tu.

**MWENYEKITI:** *Okay!*

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Siku 60 alizosema Mheshimiwa Rais kwamba tutaingia siku 60, zidisha mara tuliyokuwa tunaambiwa tukipoteza siku moja ni Shilingi milioni kadhaa, ukizidisha milioni 150 na kadhalika…

**MWENYEKITI:** Alikuwa anasema nani?

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachokisema hapa ni nini? Ili tusitoe *figure* kichwani, mimi nisitoe kichwani na Mheshimiwa Lukuvi asitoe kichwani, Serikali ilete bajeti hapa Shilingi bilioni 20 zinatumika kwenye kitu gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemshangaa Mheshimiwa Martha Mlata, sina sababu ya kumjibu sana, lakini kama mnatupeleka Mahakamani mtupeleke, lakini nawaambia hivi, kama mambo yenyewe ndiyo haya, sisi tutakuwa wa kwanza kwenda Mahakamani kuuzuia huu mchakato wa Katiba usiendelee. Tutakwenda kwenye Mahakama ya wananchi, tutakwenda kwenye Mahakama za Kiserikali na za Kimataifa. Kama mambo yenyewe ndiyo haya, tukienda namna hii hatutapata Katiba bora kwa niaba ya wananchi waliotoa maoni ya Katiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sijaridhika na majibu ya Serikali na ninaondoa Shilingi katika jambo hili. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Wewe! Tulikuwa tumeondoa ndiyo, tulikuwa tunajadili hoja. Tena unaondoa mara ya pili? *(Kicheko)*

Ulitoa hoja, ukatoa Shilingi na ndiyo maana nikaruhusu watu kujadili. Sasa nimekupa u-*wind* hoja yako, sasa nafanya maamuzi.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Mheshimiwa Eng. Mnyaa.

**MHE. ENG. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutumia hiyo Kanuni ya 103 (3) kuhusu kupata ufafanuzi wa jambo fulani mahsusi la kisera, nimestuka kuona kwamba, Wizara hii ambapo kuna uvunjifu wa haki za binadamu mkubwa mno nchini, nao kama Wizara mpaka sasa hivi wameshindwa kushawishi ni namna gani uvunjifu wa haki za binadamu huu utakomeshwa; ningeomba watoe ufafanuzi wa kutosha ni kwanini hivi sasa vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu vimezagaa?

Vita katika maeneo mbalimbali baina ya Ma-*DC* sijui Kiteto, sijui Operesheni Tokomeza, mauaji ya Polisi, na kadhalika, Tume ya Haki za Binadamu yenyewe haina meno yoyote na inasimamiwa na Wizara hii na ripoti zake hazipatikani na zikija zimechelewa. Yaliyomo katika ripoti ya Tume ya Haki za Binadamu hayafanyiwi kazi na Wizara hii, hakuna usimamizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nipate ufafanuzi, ikiwa Wizara yenyewe hii ina uvunjifu wa haki za binadamu, nimetoa mfano wa hiyo Tume na kuna mifano mingi, na mbali na huo uliotolewa wa Shilingi bilioni 27, Tume hii Mwanasheria Mkuu ametuambia kwamba watabadiliha sheria, lakini kitendo cha kubadilisha sheria na Bunge Maalum lilipoleta mgogoro kwanini wasibadilishe sheria ya nchi hii? Hakuna haki za binadamu kwamba, mpaka leo Tanzania Bara hakuna kura ya maoni.

Kwanini kwanza wasilisimamishe hili Bunge Maalum la Katiba wakaleta Kura ya Maoni kwanza angalau haki za binadamu zikatendeka kwa mujibu wa sheria?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa, wewe suala lako ni haki za binadamu. Suala la Katiba liliishamaliziwa na Mheshimiwa Mnyika, liliishia pale. Hamrudii!

Mheshimiwa Waziri, majibu tumalize. Maelezo kuhusu zile haki za binadamu, habari ya Katiba msiseme, lilishazungumzwa na mtu mwingine.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nathibitisha, maneno kwamba haki za binadamu zinavunjwa sana katika nchi hii ni ya ufisahi. Ni ufisahi, ndiyo! Kwa sababu ripoti za Tume ya Haki za Binadamu zinashughulikiwa na Tume ya Haki za Binadamu imefanya uchunguzi mbalimbali. Kwanza, hiyo kuruhusu uchunguzi inakuonesha kwamba kuna nia nzuri. Hizi ripoti utekelezaji wake unahusu Serikali Kuu na pia Idara za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utaratibu wa Zanzibar anakotoka Mheshimiwa Mnyaa, akaulize kwenye Baraza la Wawakilishi. Huko akaulize Serikali ya Zanzibar, lakini hapa kwetu kwenye Bunge hili la Jamhuri ya Muungano, Tume hii ripoti zake zinatekelezwa vizuri. *(Kicheko/Makofi/Minong'ono)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Mheshimiwa Al- Shaymaa Kwegyir

**MHE. ENG. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

**MJUMBE FULANI:** Alitoa *notice* ya kutoa Shilingi.

**MWENYEKITI:** Alitoa *notice* huyu! Mlisikia *notice* yake? Mimi sikusikia *notice* ya Shilingi.

**MHE. ENG. MOHAMED H. J. MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri ni haki yangu.

**MWENYEKITI:** Kufanyaje?

**MHE. ENG. MOHAMED H. J. MNYAA:** Kutoa ufafanuzi na kama Shilingi nitoe.

**MWENYEKITI:** Aah, hapana sikiliza kwanza! Kama ulitoa *notice* ya shilingi ina maana nitakwambia kwamba utatoa shilingi kusudi uweze kujieleze zaidi. sasa mimi sikusikia *notice*? Ulitoa *notice*?

**WAJUMBE:** Ndiyooooo!

**MBUNGE FULANI:** Alitoa!

**MWENYEKITI:** Haya, naomba na wewe ukae chini. Mimi sikusikia *notice*, lakini mfahamu kwamba kwa mujibu wa Kanuni hii, hii shughuli inatakiwa iishe saa 1.00. Ikifika saa moja tujue ndiyo muda uliokuwa umepangwa kwa ajili ya Wizara hii, ikifika na dakika 10 ni *guillotine*.

Mimi sikusikia *notice*, haya Mheshimiwa Al-Shaymaa.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama siyo kwa nia mbaya kwa maana ya kuondoa Shilingi, ila napenda nipate ufafanuzi na maelezo zaidi. Vitendo vya ukiukwaji wa haki za binadamu kwa watu wenye ulemavu wa ngozi vimezungumziwa kwa miaka mingi. Mheshimiwa Rais, Jakaya Mrisho Kikwete amelilaani sana hili miaka mingi mfululizo. Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa machozi humu ndani kwa suala hili hili la mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mashauri tisa mpaka hivi leo bado hayajashughulikiwa na ndiyo yanawapa nguvu wale wauaji kuendelea kuua kwa sababu wanajua hakuna kitakachofanyika. Hukumu hazitolewi na hata kama zinatolewa, hazitangazwi. Hukumu za watu

hawa zitangazwe tuzisikie! Kama ni kufungwa maisha au hukumu ipi, tuisikie na itekelezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nipate ufafanuzi na maelezo zaidi kuhusu hili. Serikali itoe tamko kuhusu suala hili, maana linaendelea kutokea. Juzi ameuawa mwanamke katika Mkoa wa Simiyu, Bariadi kwa Mheshimiwa Chenge huko. Ameuawa mama mmoja wa miaka 40, amekatwa miguu, kakatwa vidole, kang'olewa kucha, ame-*bleed to death,* yaani mpaka amekufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe tamko kuhusu hili kwa sababu mauaji ya kikatili yamezungumziwa kwa miaka mingi na yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itoe tamko kwa suala hili. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli haya ni mambo yanayotia uchungu sana. Pamoja na kesi hizo za wenzetu wenye ulemavu wa ngozi, kuna mauaji ya wanawake kwenye Wilaya inayoitwa Butiama, kuna mauaji ya wanawake wazee huko Shinyanga, haya ni matendo ya uvunjaji wa haki za binadamu yanayofanywa na watu binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika tafiti zilizofanywa, asilimia kubwa ya uvunjaji wa haki za binadamu, *almost 60 percent* ni watu binafsi.

Sasa kwa hili la kesi tisa za *albino,* Mahakama Kuu ya Tabora na Mwanza zitasikiliza kesi hizi katika vikao vya Mahakama Kuu vijavyo kwa sababu taratibu zote zimekamilika na kilichobaki ni kusikilizwa kwa kesi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nilikuwa natoa rai kwa Watanzania wenzangu waache imani za kichawi. Huwezi kupata dhahabu wala huwezi kupata utajiri kwa kutumia viungo vya Albino, kwa sababu wao wenyewe wangekuwa matajiri. Huwezi kupata samaki wengi kwa sababu ya kutumia viungo vya wanawake, na hii ina-*address* watu wa Nyaigina, Etaro na wengine kama hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa nilizonazo ni kwamba Jeshi la Polisi na Upelelezi wanafanya kazi hivi sasa, ninaomba waendelee vizuri, tutawashughulikia kila tutakapowapata. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Aah, hukutoa Shilingi! Huulizi mara mbili kama hukutoa Shilingi. Mheshimiwa Ridhiwani!

**MHE. RIDHIWANI J. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na jambo moja la kisera ambalo nilikuwa nataka nilipeleke kwenye Meza ya Mheshimiwa Waziri pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sera ya nchi kuhakikisha kwamba haki zinapatikana kwa wananchi na haki hizo ni pamoja na kuwapo kwa Mahakama karibu na wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hivi karibuni Mahakama yetu ya Tarafa ya Kwaruhombo imeondolewa pale na kwamba shughuli zake zote sasa zinafanyika katika Mahakama ya Lugoba. Hili limesababisha wananchi wale wa Tarafa ya Kwaruhombo kupata ugumu sana hasa wanapokwenda kutafuta haki hizo Lugoba. Sasa nilikuwa naomba tu nimuulize

Mheshimiwa Waziri, japo sina nia ya kuchukua shilingi yake, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba inawarudishia wananchi wale huduma hii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nia ya Serikali kuleta huduma za Mahakama karibu kabisa na wananchi na ndiyo sababu sasa hivi katika kazi za kuboresha miundombinu tunajenga Mahakama mpya na tunakarabati zilizopo. Naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili la Mahakama la Kwaruhombo tutalifuatilia kwa sababu wakati mwingine yapo majengo ya Mahakama ambayo yameonekana hayafai kuendesha shughuli za Mahakama, sina uhakika kama hili siyo mojawapo. Kwa hiyo, tutalifuatilia na tutampa majibu Mheshimiwa Mbunge lakini nataka kumhakikishia kwamba nia yetu ni kuleta huduma hizi karibu kwa wananchi kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

**MHE. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kweli kwa kazi nzuri na kubwa wanayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nia yangu siyo kutoa shilingi, mimi nia yangu ni kutaka kujua Wizara yake inafanya nini hasa kesi zinapokaa Mahakamani miaka 12 kama ile ya Himo ambayo nimekujia mara nyingi nikakuambia ule Mji wa Himo haujengwi, watu wachache mwaka 2002 wameenda Mahakamani wakaweka kizuizi, kwa hiyo Mji ule tangu 2010 hauna barabara, hauna majengo na sasa hivi tunataka kujenga Soko la Kimataifa ambalo litawakaribisha wageni wengi pale. Sasa wale wanaotaka kujenga wanasema kama mji umezuiwa na Mahakama, kuna kizuizi, sisi tutafanyaje? Kwa hiyo, nikakujia siku nyingi Mheshimiwa Waziri na nimeona unahangaika, naomba leo unipe majibu ule mji tunajenga ama hatujengi? Ni hayo tu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Mrema kwa namna ambavyo anafuatilia umalizikaji wa kesi mbalimbali kipekee kwa kesi hiyo ambayo amekuwa akiiulizia humu Bungeni mara kwa mara ya wadaiwa karibia 726. Ni kweli imekuwa ni ya muda mrefu lakini nimekuwa nikieleza ni kwa nini kesi hiyo imekuwa ikichukua muda Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda tu nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba kesi hii sasa imeshamalizwa kusikilizwa na tayari Mheshimiwa Jaji Mziray ambaye alikuwa anasikiliza kesi hiyo ameshaandaa hukumu, imeshatumwa katika Mkoa wa Kilimanjaro, wakati wowote kuanzia sasa itasomwa. *(Makofi)*

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kwa dakika hizi zilizobaki sasa tunaingia kwenye *guillotine.*

Kif. 1002 – *Finance and Accounts*……………Tsh.449,357,000/=
Kif. 1003 – *Policy and Information Services*…Tsh.702,136,000/=
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*…………………Tsh.231,886,000/=
Kif. 1005 – *Government Communication Unit*Tsh....................................................194,604,000/=
Kif. 1006 – *Procurement Management Unit*..Tsh.402,385,000/=
Kif. 1007 – *Management Information System Unit*…..............Tsh.228,806,000/=
Kif. 2004 – *Public Legal Services Unit*…………Tsh.603,570,000/=
Kif. 4001 – *Constitutional Affairs*…….................Tsh.296,482,000/=

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*................................Tsh.2,719,475,000/=
Kif. 1002 – *Finance and Accounts*……………Tsh.273,434,000/=
Kif. 1003 – *Internal Audit Unit*…………………...Tsh.l61,947,000/=
Kif. 1004 – *Legal Services*………………………Tsh.412,451,000/=
Kif. 1005 – *Procurement Unit*………………… Tsh.201,566,000/=
Kif.1006 – *Management Information System Unit*……….......Tsh.260,975,000/=
Kif. 2001 – *Administrative Justice*………….Tsh.1,004,159,000/=
Kif. 2002 – *Human Rights*……………………… Tsh.632,315,000/=
Kif. 2003 – *Research and Documentation*…Tsh.333,192,000/=
Kif. 2004 – *Public Education and Training*….Tsh.320,164,000/=
Kif. 3001 – *Zanzibar Office*……………………..Tsh.292,789,000/=
Kif. 3002 – *Mwanza Office*……………………..Tsh.112,560,000/=
Kif. 3003 – *Lindi Office*…………………………Tsh.112,368,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 59 – Tume ya Kurekebisha Sheria**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*…….................Tsh.4,573,075,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 16 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**

Kif. 3003 – *Lindi Office*…………………………Tsh.112,368,000/=
Kif. 3002 – *Treaties and Contracts Division*…Tsh.457,149,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 40 – Mfuko wa Mahakama**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*…….....Tsh.41,687,748,000/=

*(Kifungu Kilichotajwa Hapo Juu Kilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 41 – Wizara ya Katiba na Sheria**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*………..Tsh.0

Kif.1003 – *Policy and Information Service*...Tsh.5,048,621,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)*

**Fungu 55 – Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora**

Kif. 1001 – *Administration and HR Management*…………....Tsh.0
Kif. 2001 – Administrative Justice ……………......................Tsh.0
Kif. 2002 – Human Rights ………………………Tsh.900,753,000/=

*(Vifungu Vilivyotajwa Hapo Juu Vilipitishwa na Kamati ya Matumizi Bila Mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Wakati *Sergeant At Arms* anaweka Siwa hii hapa wote tunasimama, siyo tunaanza mashauriano, hivi vitabia vinaanza. Hii Siwa mamlaka yetu yote ndio yako hapo, kwa hiyo mnatakiwa kusimama na kutulia.

Mheshimiwa mtoa hoja taarifa!

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imepitia makadirio ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2014/2015 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha pamoja na marekebisho yake. Hivyo, naomba kutoa hoja kwamba makadirio hayo sasa yakubaliwe na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja! *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Spika, naafiki!

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka 2014/2015 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Niwapongeze Wizara inayoongozwa na akina dada. Najua mnafanya kazi nzuri na nashukuru pia wasaidizi wenu wamefanya kazi nzuri na muendelee kufanya kazi nzuri na tuweze kuimarisha eneo letu la haki za binadamu. *(Makofi)*

Kwenye suala la Mfuko wa Mahakama tulifanya pamoja na sisi tuna Mfuko wa Bunge. Hii mifuko yetu miwili tunajaribu kuona namna ya kuweza kuiweka tofauti na matumizi mengine ya kawaida. Kwa hiyo, mashauriano haya yanaendelea kati yetu sisi na Mahakama pia na Serikali. Kwa hiyo, nadhani baada ya muda mfupi tunaweza kuwa na utaratibu mzuri zaidi wa Mfuko wa Mahakama na Mfuko wa Bunge. Kwa hiyo, nawapongezeni sana kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nitambue wageni waliopo. Hapa kwenye *gallery* yangu ninao wageni wengine nadhani walikuwa watambulishwe asubuhi lakini hawakuwepo.

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

Tuna wageni wa Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Makamishna, Wakurugenzi na Maafisa Waandamizi wa Wizara ya Mambo ya Ndani wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ndugu Mbaraka Abdulwakil. Ahsante sana. *(Makofi)*

Yuko Naibu Katibu Mkuu wa Wizara Ndugu Mwamini Malemi, ahsante asante. Kuna *Inspector General* wa Polisi Ndugu Ernest Mangu na huyu ni *Inspector General* mpya. Tunakupongeza sana, nadhani tutashirikiana. Tuna Kamishina Mkuu wa Uhamiaji, Ndugu Sylivester Ambokile, ahsante. Tuna Kamishna wa Polisi Zainzibar, Ndugu Hamdan Makame, ahsante. *(Makofi)*

Halafu tuna mgeni wa Waziri wa Katiba na Sheria ambaye ni Jaji Rehema Mkuye. Mheshimiwa Jaji yuko wapi, ahsante sana. Tunaye Mheshimiwa Renatus Rutta, yeye ni Msajili wa Mahakama Kuu Dodoma naye asimame, ahsante sana. *(Makofi)*

Halafu tuna wanafunzi 90 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, naomba wasimame wote walipo. Nafikiri asubuhi mlikosa nafasi. Karibuni sana. Nawatakieni kusoma kwema. *(Makofi)*

Halafu tuna wageni wa Mheshimiwa Keissy, yuko Fauziah Ally Keissy, mtoto wake asimame tuone kama anafanana na baba yake? Yupo na mjukuu wake, Asma Majid Masoud, wako wapi hawa wote. Tunaomba Mungu wakichukua habari za baba basi itakuwa shughuli. Wapo mtawaona huko mitaani, wamesubiri sana. *(Makofi)*

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, kwa kutumia Kanuni ya 68(7) ya Kanuni zetu za Bunge, naomba mwongozo wako hasa kutokana na kauli…

**SPIKA:** Soma hiyo Kanuni inasemaje, tukumbushe.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Niisome?

**SPIKA:** Ndiyo.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Ahsante, inasema:-

*"Halikadhalika, Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba Mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hili linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa Kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo ama baadaye kadri atakavyoona inafaa".*

**SPIKA:** Tuendelee!

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, wakati wa majadiliano na wakati Mheshimiwa Mnyaa anaongea hapa kutaka jambo fulani la ufafanuzi kuhusu suala zima la haki za binadamu, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wakati anamjibu Mheshimiwa Mnyaa anamwambia masuala haya kaulize Zanzibar. Huu ni ubaguzi na si kitu ambacho kinapaswa kufanywa na mtu mwenye elimu na mtu ambaye ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapomzuia Mbunge asiseme maneno kama hayo na ukamwambia nenda kasemee Zanzibar wakati yeye ni Mbunge ambaye kaapa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wewe Mheshimiwa Spika uko hapa umenyamaza kimya na

unamwangalia Mwanasheria Mkuu anafanya anavyotaka. Huoni kwamba huu ni ubaguzi? Ubaguzi huu Mheshimiwa Spika inaonekana unaufanya wewe pamoja na Mwanasheria Mkuu.

Mheshimiwa Spika, naomba ufafanuzi wako katika hili.

**SPIKA:** Naomba ukae chini.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Na kama suala hili kama ndivyo ilivyo, kuna haja gani sisi Wazanzibari kukaa hapa tukajadili Wizara ambazo si za Muungano?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, naomba mwongozo wako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hakuna mwongozo wala chochote kwa sababu wewe mwenyewe umekosa nidhamu. Katibu endelea. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, siridhiki na maaelezo yako.

**SPIKA:** Nimemaliza, sawa. Wewe mwenyewe ninapokuambia ukae unaendela kuzungumza.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, siridhiki na maelezo yako kwa sababu ni haki yangu kama Mbunge nizungumze.

**SPIKA:** Ninaposimama mimi, wewe unakaa na umeendelea kuvunja Kanuni hii na kama kiongozi ni vizuri utii amri za hapa. Kwa hiyo, Katibu endelea. *(Makofi)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge wa chama cha CUF walioko ukumbini walitoka nje ya ukumbi wa Bunge)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2014 Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Kama Ilivyosomwa Bungeni

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuchukua nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa familia na wananchi wa Mikoa mbalimbali ya Tanzania kutokanana na mvua kubwa iliyonyesha katika vipindi tofauti mwaka huu na kusababisha mafuriko na hivyo kuleta adha kubwa kwa wananchi ikiwemo vifo na uharibifu wa mali na miundombinu.

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutumia fursa hii kutoa masikitiko yangu kwa vifo, ulemavu, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu vilivyosababishwa na ajali za barabarani, majini na nchi kavu katika mwaka mzima wa 2013. Nawapa pole sana ndugu na jamaa wa marehemu waliopoteza maisha katika matukio hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee naomba kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuonyesha imani kwangu kwa kuniteua katika nafasi hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa mapema katika mkutano huu wa Bunge ambayo imetoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa ujumla katika mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake mahiri, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2014/2015. Naishukuru pia Kamati hiyo kwa maelekezo na ushauri wao wenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya msingi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kuwarekebisha wafungwa, kutekeleza Programu ya Huduma kwa Jamii, kuwezesha na kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji, kuwahudumia wakimbizi waliopo nchini na kuandaa na kutoa vitambulisho vya Taifa. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Huduma kwa Jamii, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Wakimbizi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

Mheshimiwa Spika, hali ya usalama nchini. Hali ya uhalifu. Wajibu wa kwanza wa Serikali ni kulinda usalama wa raia na mali zao na kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu. Nchi yetu imeendelea kuienzi amani na utulivu uliopo kama msingi mkuu wa Taifa ambao umejengwa na kuendelea kuimarishwa tangu tupate uhuru mwaka 1961 na katika kipindi chote cha miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kuwepo kwa amani na utulivu huo kumechangia katika ustawi wa nchi yetu kiuchumi, kijamii na kisiasa ambapo kumezingatiwa na kutambuliwa kuwa miongoni mwa vipaumbele katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na maendeleo binafsi ya wananchi wetu. Kwa upande wake, Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza kikamilifu jukumu lake la kikatiba na kisheria la kulinda na kudumisha amani na utulivu nchini kwa kubaini, kuzuia na kutanzua vitendo vya uhalifu, makosa ya usalama barabarani, migogoro, vurugu na fujo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2013 jumla ya makosa makubwa ya jinai 560,451 yaliripotiwa katika vituo vya Polisi kote nchini ikilinganishwa na makosa 566,702 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2012. Idadi ya makosa ya jinai yaliyoripotiwa imepungua kwa asilimia 1.1. Ufafanuzi zaidi wa jambo hili mtaukuta katika Jedwali Na. 1.

Mheshimiwa Spika, upungufu huu unatokana na upatikanaji wa taarifa za uhalifu mapema na utekelezaji wa mkakati wa Polisi Jamii unaohusisha ushirikishwaji wa wananchi katika vita dhidi ya uhalifu hapa nchini. Sababu nyingine kuu ni kuongezeka kwa wigo wa doria, misako na Operesheni Maalum za Jeshi la Polisi mijini na vijijini.

Mheshimiwa Spika, makosa makubwa ya jinai yanayoripotiwa katika vituo vya polisi yamegawanyika katika makundi makuu matatu. Makundi hayo ni makosa dhidi ya binadamu, makosa ya kuwania mali na makosa dhidi ya maadili ya jamii. Kwa ujumla, idadi ya makosa hayo makubwa ya jinai yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi imeongezeka kutoka 72,765 mwaka 2012 hadi 73,219 mwaka 2013. Ongezeko hili la makosa 454 ni sawa na asilimia 0.6. Hata hivyo, kumekuwepo upungufu wa makosa ya kuwania mali. Makosa ya kuwania mali yamepungua kutoka 46,773 mwaka 2012 hadi 45,470 mwaka 2013. Huu ni upungufu wa makosa 1,303 sawa

na asilimia 2.8. Upungufu huu umetokana na kuimarika kwa doria, misako na Operesheni Maalum za Jeshi la Polisi na ushirikiano wa kiutendaji uliopo kati ya Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya hivi karibuni ajali za barabarani zimekuwa tishio kwa maisha ya watu na mali. Takwimu za mwaka 2013 zinaonesha kuwa ajali hizo zimeongezeka kwa asilimia 3.7 ikilinganishwa na mwaka 2012. Aidha, idadi ya majeruhi na vifo vinavyosababishwa na ajali za barabarani pia imeongezeka. Vifo vimeongezeka kwa asilimia 3.4 na majeruhi kwa asilimia 7.5. Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2012 ajali za barabarani 23,604 zilitokea katika maeneo mbalimbali ambapo watu 4,062 walipoteza maisha na wengine 20,037 walijeruhiwa. Katika mwaka 2013, ajali zilizotokea ni 24,480 ambazo zilisababisha vifo vya watu 4,091 na wengine 21,536 kujeruhiwa. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine wa masuala ya usalama barabarani waliendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Usalama Barabarani ambapo jumla ya makosa madogo madogo 646,846 yalibainishwa na wakosaji kutozwa faini iliyofikia shilingi bilioni 17.5. Takwimu zinaonesha kuwa vyanzo vikuu vya ajali za barabarani ni mwendokasi, ulevi, uzembe wa madereva, ubovu wa vyombo vya usafiri na kubeba abiria na mizigo kuliko uwezo wa vyombo husika.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ongezeko hilo la makosa ya usalama barabarani, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine kama *SUMATRA, TBS, TANROADS* na Shule za Udereva zilizosajiliwa limeendelea kuchukua hatua za kuzuia na kudhibiti vyanzo vya ongezeko la ajali za barabarani. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu ya kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani kwa watumiaji wa barabara wakiwemo madereva wa bodaboda, kuendeleza doria za masafa mafupi na marefu katika barabara kuu, ukaguzi wa magari, kutumia kamera kutambua madereva wanaoendesha mwendo kasi, kuendelea kusimamia zoezi la utoaji wa leseni mpya za udereva, kuwahamasisha abiria kutoa taarifa mapema za madereva wanaokiuka Sheria za Usalama Barabarani, kuwaelekeza wamiliki wa mabasi kubandika kwenye mabasi yao namba za simu za viongozi wa Polisi na kuwachukulia hatua za kinidhamu Askari wanaojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa toka kwa madereva.

Mheshimiwa Spika, ninapenda tena kuwashukuru Mawaziri wenzangu kutoka Ofisi ya Rais, Utawala Bora; Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Wizara za Katiba na Sheria; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Kilimo, Chakula na Ushirika; Nishati na Madini na Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambao walihudhuria warsha iliyoandaliwa na Jeshi la Polisi iliyofanyika tarehe 15 Februari, 2013 mjini Dodoma na hatimaye kutoa tamko lililokubali kusimamia na kutekeleza mipango ya muda wa kati na mrefu ya kuimarisha ulinzi na usalama hapa nchini kwa kufanya yafuatayo:-

(i) Kuliweka suala la usalama kuwa ni moja ya vipaumbele vya Taifa;

(ii) Kutenga fedha za kutosha kuliwezesha Jeshi la Polisi kumudu kikamilifu wajibu wake wa kuhakikisha usalama wa raia na mali zao;

(iii) Kutambua kwamba kila Wizara ni mdau katika suala la usalama na inayo wajibu wa kuepusha migogoro inayozalisha vurugu;

(iv) Kufanya tathmini ya maeneo ambayo ni vyanzo vya migogoro na kutafuta njia ya kuzuia/kutanzua migogoro hiyo. Kuimarisha/kuhuisha mifumo ya usimamizi wa sheria na uwajibikaji wa kila Idara ya Serikali;

(v) Kujenga ubia wa kiutendaji baina ya Wizara wanazoziongoza na vyombo vya ulinzi na usalama katika kubaini vyanzo vya migogoro na kuweka mikakati ya pamoja ya kuzuia na kutanzua migogoro hiyo;

(vi) Kuliwezesha Jeshi la Polisi kwa nyenzo, vifaa na miundombinu pindi Mikoa mipya inapoanzishwa;

(vii) Kurekebisha haraka na kwa vipaumbele upungufu wa kisera, kisheria na kikanuni unaoweza kuchangia mianya ya kusababisha migogoro ya kijamii.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Mawaziri wenzangu kwa pamoja tutekeleze kwa vitendo mipango tuliyojiwekea. Mipango hii ikitekelezwa hali ya usalama nchini itaimarika kwa kuondokana na migogoro isiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi limepata Uongozi mpya baada ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumteua Bwana Ernest Jumbe Mangu kuwa Inspekta Jenerali wa Polisi kuanzia tarehe 01 Januari, 2014. Pia Mheshimiwa Rais amemteua Naibu Inspekta Jenerali wa Polisi na Makamishna wanane kumsaidia Inspekta Jenerali. Makamishna hao wanaongoza Kamisheni za Fedha na Lojistiki, Utawala na Utumishi, Upelelezi wa Jinai, Operesheni na Mafunzo, Polisi Jamii, Intelijensia, Uchunguzi wa Kisayansi wa Jinai na Polisi Tanzania – Zanzibar. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote mtoe ushirikiano kwa Uongozi mpya wa Jeshi la Polisi ili kwa pamoja tudumishe amani na usalama uliopo na tuendeleze mapambano dhidi ya uhalifu na wahalifu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 katika kipindi cha 2013/2014. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina malengo 10 ya kutekeleza yanayotokana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Taarifa ya utekelezaji wa malengo hayo kwa mwaka 2013/2014 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kuendeleza mapambano dhidi ya madawa ya kulevya. Mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya yaliendelezwa. Kati ya Julai hadi Desemba 2013 taarifa za wananchi na doria za Jeshi la Polisi zimewezesha kukamatwa kwa jumla ya kilo 221,898 za dawa za kulevya za viwandani na watuhumiwa 905 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani. Aidha, kilogramu 265,576.543 za bhangi na kilo 16,822,305 za mirungi zilikamatwa na watuhumiwa 14,284 walikamatwa na kufikishwa Mahakamani. Hekari 580.5 za mashamba ya bhangi ziliteketezwa katika Mikoa ya Morogoro, Arusha, Tanga, Simiyu na Mkoa wa Kipolisi Tarime - Rorya.

Mheshimiwa Spika, pili, kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani. Tatizo la msongamano wa Wafungwa na Mahabusu bado lipo, licha ya hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa katika kukabiliana nalo. Idadi ya wafungwa na mahabusu waliokuwa magerezani imepungua kutoka 34,552 tarehe 1 Machi, 2013 hadi kufikia 33,831 tarehe 1 Machi, 2014. Kati ya hao, wafungwa ni 16,547 na mahabusu ni 17,284 (Ufafanuzi tafadhali angalia Jedwali Na. 2).

Mheshimiwa Spika, njia mojawapo inayotumika katika kupunguza msongamano Magerezani ni kujenga mabweni mapya na kukamilisha viporo vya ujenzi wa mabweni. Kutokana na jitihada hizo, uwezo wa sasa wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu umeongezeka kutoka 27,653 mwaka 2010 hadi kufikia 29,552 mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, aidha utekelezaji wa Sheria ya Bodi za Parole Na.25 ya mwaka 1994 iliyofanyiwa marekebisho kwa Sheria Na.5 ya 2002 iliwezesha maombi ya wafungwa 234 kujadiliwa ambapo kati ya hao 215 walikubaliwa kuachiwa na 19 walikataliwa kutokana na sababu mbalimbali hadi kufikia mwezi Machi, 2014.

Mheshimiwa Spika, njia nyingine ni kupitia kifungo cha nje kwa mujibu wa kifungu cha 72 cha Sheria ya Magereza Namba 34 ya mwaka 1967. Wafungwa 556 walikuwa wanatumikia kifungo cha nje kati ya tarehe 1 Julai, 2013 hadi 1 Machi, 2014.

Aidha, katika mwaka 2013/2014 wafungwa 1,475 walifaidika na msamaha wa Rais uliotolewa tarehe 9 Desemba, 2013 wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 52 ya Uhuru wa Tanzania Bara na wafungwa 3,967 wamefaidika na msamaha wa Rais uliotolewa tarehe 26 Aprili, 2014 wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Matokeo ya utekelezaji wa msamaha huo husaidia kupunguza msongamano wa wafungwa Magerezani.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuimarisha na kuboresha mfumo wa upelelezi wa makosa ya jinai. Wizara inapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali kuhuisha Muundo wa Utawala wa Jeshi la Polisi kwa kuanzisha Kamisheni mpya ya Intelijensia ya Jinai (*Criminal Intelligence*) na Kamisheni ya Uchunguzi wa Jinai Kisayansi *(Forensic Science Investigation*). Muundo huu umeboresha mgawanyo wa majukumu ya upelelezi na intelijensia na unatarajiwa kuimarisha utendaji kazi. Aidha, kwa upande wa mafunzo, vyuo vya Taaluma ya Polisi vya Dar es Salaam, Moshi na Kidatu, vimeendelea kutoa mafunzo ya Intelijensia ya jinai na mbinu za kisasa za upelelezi kwa Askari wanaohudhuria mafunzo ya Cheti na Diploma ya Sayansi ya Polisi. Kuimarika kwa mfumo wa upelelezi kumeongeza kiwango cha mafanikio ya kesi Mahakamani kutoka asilimia 11.6 mwaka 2012 hadi asilimia 12.4 mwaka 2013.

Mheshimiwa Spika, nne, kuanzisha mpango wa kuwapatia Askari nyumba bora za kuishi. Kutokana na mahitaji makubwa ya nyumba za makazi ya Askari nchi nzima, Jeshi la Polisi linaendelea kutekeleza mpango wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(PPP)* ili kupunguza ukubwa wa tatizo hili. Kwa kuanzia Jeshi la Polisi limeingia ubia na Kampuni ya *Mara World* wa kujengewa Kituo cha kisasa cha Polisi na nyumba 350 za Askari katika Mkoa wa kipolisi Kinondoni. Aidha, Jeshi la Polisi limeanzisha Shirika la Uzalishaji Mali *(Tanzania Police Force Corporation Sole)* ambalo kipaumbele kimojawapo ni kujenga nyumba na ofisi za Jeshi la Polisi kwa gharama nafuu. Vilevile, Jeshi la Polisi litaendelea kukamilisha miradi ya ujenzi wa nyumba katika Mikoa ya Njombe, Kagera, Mwanza na Mara na pia kujenga nyumba mpya kwa ajili ya makazi ya Askari kadri uwezo utakavyoruhusu. *(Makofi)*

*(Wakati Waziri akiendelea kusoma hotuba yake Waheshimiwa Wabunge wa CHADEMA walitoka ukumbini)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, tano, kujenga vituo vya Polisi katika kila Tarafa nchini. Ili kupeleka huduma za Polisi karibu na wananchi, Jeshi la Polisi lina mpango wa kujenga vituo vya Polisi katika kila Tarafa. Kutokana na mahitaji makubwa ya rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo, Jeshi la Polisi litatumia Shirika la Polisi la Uzalishaji Mali na pia kushirikiana na sekta binafsi katika kujenga vituo vya Tarafa kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, sita, kuimarisha mafunzo ya Askari wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, Askari 23,269 wa Jeshi la Polisi wamepatiwa mafunzo katika fani za Sayansi za Polisi, Uongozi wa Kati na Usimamizi wa Rasilimaliwatu. Katika

mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litatoa kipaumbele kwenye mafunzo ya utayari ambapo jumla ya Maafisa, Wakaguzi na Askari wapatao 41,000 watapatiwa mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jeshi la Magereza, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014, watumishi na Askari 447 walihudhuria mafunzo mbalimbali nje ya Jeshi na wengine 121 wamehudhuria mafunzo ndani ya Jeshi.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika mwaka 2013/2014, limegharamia mafunzo mbalimbali kwa Askari 82. Idara ya Uhamiaji imewapatia mafunzo ya awali watumishi wapya 52 na inatarajia kuwapeleka wengine 270 kwenye mafunzo ya awali ya Uhamiaji. Aidha, watumishi 446 waliopo kazini wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inatarajia kuajiri watumishi wapya 1,250 na kutoa mafunzo kwa watumishi 500 waliopo kazini.

Mheshimiwa Spika, saba, kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za kilimo katika maeneo ya magereza. Katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo Nchini, *Agricultural Seed Agency* (ASA), Kampuni za *TANSEED na Highland Seed Growers Ltd* limelima mashamba ya mbegu bora za mahindi katika Mikoa mbalimbali hapa nchini ambapo jumla ya hekta 776 zimelimwa na kupandwa mbegu bora za mazao ya aina mbalimbali na matarajio ni kuvuna tani 2,000 za mbegu bora. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Magereza linatarajia kuendelea na shughuli za kilimo cha mbegu bora kwa kulima hekta 800 na kutarajia kuvuna tani 2,100 za mbegu bora.

Mheshimiwa Spika, nane, kutoa vitambulisho vya Taifa. Mamlaka ya Vitambulisho inaendelea na jukumu lake la msingi la kujenga mfumo wa usajili na utambuzi wa watu hapa nchini ambao moja ya matokeo yake ni utengenezaji wa Vitambulisho vya Taifa. Katika mwaka 2013/2014, Mamlaka Vitambulisho vya Taifa imekamilisha usajili kwa wakazi 560,297 wa Unguja na Pemba na wakazi 2,449,822 wa Mkoa wa Dar es Salaam na kufanya idadi ya waliosajiliwa kuwa 3,300,119. Wakazi hawa watapatiwa Vitambulisho vyao vya Taifa wakati wowote kuanzia sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tisa, kuimarisha vikosi vya zimamoto na uokoaji vyenye wataalamu na zana za kisasa ili kukabiliana na majanga ya moto. Katika kuimarisha huduma za Zimamoto na Uokoaji nchini, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limefanikiwa kupata magari matano ya kuzimia moto na yamepelekwa katika Mikoa ya Simiyu, Pwani, Katavi na Dar es salaam. Pia Jeshi limefanikiwa kupata boti mbili za uokoaji ambazo zipo katika Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, juhudi zinaendelea za kuongeza idadi ya Askari na Maafisa ambapo katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Jeshi limepata kibali cha kuajiri Askari 800 na zoezi la usaili sasa hivi linakamilishwa.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2013/2014 na malengo ya mwaka 2014/2015. Mapato na matumizi. Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilipangiwa kukusanya mapato ya Sh.145,024,760,000, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014, Wizara ilikuwa imekusanya Sh.101,938,065,028 sawa na asilimia 70.3 ya lengo la mwaka huu. Katika mwaka 2014/2015, Wizara imelenga kukusanya mapato ya Sh.156,667,944,771. Mifumo na nguvu zaidi zitaelekezwa katika kuziba mianya ya uvujaji wa mapato hususan katika kuimarisha na kuboresha matumizi ya benki kwa ajili ya kufanya malipo ya huduma zitolewazo na taasisi za Wizara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara iliidhinishiwa jumla ya Sh.741,131,771,000 kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014 jumla ya Sh.497,875,939,929 zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 67 ya bajeti ya mwaka mzima, ambapo Sh.259,015,160,850 zimetumika kulipia mishahara,

matumizi mengineyo Sh.201,308,653,229 na fedha za maendeleo ni Sh.37,552,125,850. Katika mwaka 2014/2015, Wizara inategemea kutumia Sh.881,740,291,800 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi. Kuzuia uhalifu na ajali za barabarani. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Jeshi la Polisi liliendelea kutekeleza mkakati wa kupunguza uhalifu '*Crime Reduction Strategy*'. Katika kutekeleza Mkakati huo, doria, misako na operesheni maalum zimefanyika nchi nzima. Aidha, Maofisa, Wakaguzi na Askari 5,030 walipangwa kuwa Maafisa wa Polisi Jamii *(Community Policing Officers)* katika Tarafa/Majimbo na Kata/Shehia kote nchini hasa maeneo ya vijijini. Mkakati huo pia umeimarisha ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na wananchi na hivyo umesaidia kupunguza kwa vitendo vya uhalifu mkubwa kwa asilimia 4.3 mwaka 2012 na asilimia 1.1 mwaka 2013. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litaimarisha doria, misako na operesheni maalum ili kupunguza matishio ya uhalifu, makosa makubwa ya jinai na ajali za barabarani. Pia Jeshi la Polisi litaendelea kujiweka tayari kudumisha amani na utulivu kuelekea kufanyika kwa zoezi la Kura za Maoni ya kupata Katiba mpya, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2014 na Uchaguzi Mkuu mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, mauaji ya wanawake, wazee, vikongwe kwa imani za kishirikina. Kumekuwa na wimbi la mauaji ya wanawake hasa katika Mkoa wa Mara. Mauaji ya Wazee na Vikongwe yameendelea katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Tabora. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, takwimu zinaonyesha kuwa jumla ya wanawake 15 wameuwawa katika Mkoa wa Mara hususan Wilaya ya Butiama. Aidha, wazee na vikongwe 154 waliuawa katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Tabora kutokana na imani za kishirikina. Serikali inalaani kwa nguvu zote mauaji ya wanawake, wazee na vikongwe kwa imani za kishirikina katika karne hii ya 21. Katika mwaka 2014/2015 Serikali itahakikisha mauaji ya aina hii yanadhibitiwa na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kuimarisha kuiimarisha Kamisheni mpya ya Intelijensia ya Jinai kwa kuongeza rasilimali watu na vitendea kazi kuanzia ngazi ya Makao Makuu hadi ngazi ya Kata/Shehia ili kujenga uwezo wa kupata taarifa mapema za uhalifu.

Mheshimiwa Spika, upelelezi wa makosa ya jinai. Katika mwaka 2013/2014, ushirikiano wa kiutendaji kati ya Jeshi la Polisi na taasisi zinazounda Jukwaa la Haki Jinai uliendelea kuimarika. Taasisi zinazounda Jukwaa la Haki Jinai ni Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Jeshi la Magereza na Mahakama. Kwa upande wake, Jeshi la Polisi liliendelea kuongeza ufanisi katika upelelezi wa makosa ya jinai na hivyo kufanikiwa kuongeza kiwango cha washtakiwa kupatikana na hatia Mahakamani kutoka asilimia 11.6 mwaka 2012 hadi asilimia 12.4 mwaka 2013. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litaongeza kasi na ufanisi zaidi katika upelelezi wa kesi za jinai ili kufikia kiwango cha mafanikio ya kesi Mahakamani kwa asilimia 15.

Mheshimiwa Spika, migogoro ya ardhi. Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, kumekuwepo na migogoro mbalimbali ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji, wakulima wakitaka kumiliki ardhi kwa ajili ya kilimo cha mazao ya chakula au biashara wakati wafugaji nao wakiitaka ardhi hiyohiyo kulishia mifugo yao. Migogoro hiyo ilitokea katika maeneo ya Hanang, Kiteto, Mvomero, Kondoa, Singida na Mbeya. Migogoro hii imesababisha mapigano baina ya makundi hayo na kusababisha watu 47 kujeruhiwa na wenginee 16 kuuwawa. Aidha, migogoro hii ilisababisha vifo vya watu watano na majeruhi 20 mwaka 2012/2013 na ilitokea katika Mikoa ya Tanga, Pwani, Mbeya, Morogoro na Arusha. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ili kuzuia mauaji, majeruhi na uharibifu wa mali unaosababishwa na migogoro ya ardhi.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa nidhamu za Askari. Hatua za kinidhamu ziliendelea kuchukuliwa kwa Maafisa, Wakaguzi na Askari Polisi waliobainika kujihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili mema ya Jeshi la Polisi. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya Maafisa sita

walisimamishwa kazi na wengine 18 wametakiwa kujieleza kwa nini wasichukuliwe hatua za kinidhamu. Aidha, Askari 152 wa vyeo mbalimbali walifukuzwa kazi baada ya kupatikana na hatia ya makosa ya utovu wa nidhamu na kati yao Askari 18 wamefikishwa Mahakamani kujibu mashtaka ya jinai dhidi yao. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litaongeza upekuzi kwa Askari wake na kwa vijana wanaoomba kujiunga na Jeshi ili kuwa na Askari wenye nidhamu ya hali ya juu na moyo wa dhati wa kulitumikia Jeshi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, sifa na zawadi kwa Askari. Jeshi la Polisi liliendelea kutoa sifa na zawadi kwa Askari waliotekeleza majukumu yao kwa umahiri mkubwa. Katika mwaka 2013/2014 jumla ya Askari 191 walitunukiwa sifa na zawadi mbalimbali. Kiasi cha shilingi milioni 51.3 zilitumika kuwazawadia Askari hao kutoka Komandi mbalimbali. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litaendelea kuwatambua Maafisa, Wakaguzi, Askari na watumishi raia wanaotekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa na kuwatunukia sifa na zawadi stahiki.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo. Katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi liliendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Idara ya Upelelezi Dar es Salaam. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litanunua vyombo vya usafiri kwa ajili ya kuimarisha doria na operesheni za kipolisi na redio za mawasiliano za digitali *(digital mobile radio)*. Pia Jeshi la Polisi litaendeleza ujenzi wa Makao Makuu ya Idara ya Upelelezi Dar es Salaam, ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi ya Askari katika Mikoa ya Mara, Mwanza, Kagera, Njombe na ujenzi wa Kituo cha Polisi Vikokotoni - Unguja. Mikoa ya Tanga, Mbeya, Mjini Magharibi, Kusini Pemba, Pwani, Mtwara, Morogoro na Ruvuma itaunganishwa na mkongo wa Taifa ili kuimarisha mawasiliano ya kimtandao. Aidha, Jeshi la Polisi litaendelea kutekeleza mradi wa kupambana na rushwa unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uingereza *(DFID)*.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Magereza. Jukumu la msingi la Jeshi la Magereza ni kuwahifadhi wafungwa na mahabusu wa aina zote pamoja na kuwarekebisha tabia kwa wale waliohukumiwa vifungo kwa mujibu wa Sheria. Aidha, urekebishaji wa tabia za wafungwa unafanyika kupitia programu za mafunzo kwa njia ya vitendo katika miradi ya kilimo, viwanda vidogo vidogo na ujenzi. Aidha, mafunzo ya stadi mbalimbali hufanyika katika Chuo cha Ufundi Magereza Ruanda-Mbeya na Gereza la Vijana Wami. Vilevile, ushauri nasaha hutolewa kwa wafungwa kwa kutumia Walimu wa Dini na Maafisa Ustawi wa Jamii.

Mheshimiwa Spika, Programu za Urekebishaji wa Wafungwa. Jeshi la Magereza limeendelea kutekeleza programu za urekebishaji wa wafungwa Magerezani kwa kuwapa stadi katika kilimo. Aidha, ili kuboresha mafunzo hayo, matrekta ya vituo vya Ngwala, Ludewa, Wazo Hill, Nachingwea na Kilimo Urambo yalifanyiwa matengenezo makubwa. Malengo kwa mwaka 2014/2015 ni kuendelea kuyafanyia matengenezo matrekta hayo yaliyopo pamoja na zana zake ili kuendelea kutoa mafunzo kwa wafungwa waliopo.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha shughuli za viwanda vidogo vidogo magerezani, Jeshi limekamilisha kufunga mashine nne katika Kiwanda cha kukamua mawese na mise katika Kambi ya Kimbiji – Dar es Salaam. Pia zimenunuliwa mashine kumi na tatu za aina mbalimbali kwa ajili ya viwanda vya Seremala na Karakana Ukonga. Mashine hizi zitaongeza kasi ya uzalishaji na pia kutekeleza kwa vitendo sera ya urekebishaji wa wafungwa. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Jeshi la Magereza linatarajia kuendelea na shughuli za uzalishaji mali baada ya kazi ya ufungaji wa mashine mpya za aina mbalimbali kukamilika katika viwanda vya ushonaji, uhunzi na samani katika Magereza ya Ukonga, Arusha, Butimba na Uyui.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Jeshi la Magereza liliendelea na jukumu la urekebishaji wa wafungwa kupitia ufugaji wa ng'ombe wa nyama 8,328 na ng'ombe wa maziwa 2,407 pamoja na mifugo mingine ambayo ni mbuzi, kondoo, nguruwe, sungura,

kuku wa mayai na bata weupe. Huduma mbalimbali za mifugo ziliboreshwa kama vile chanjo na dawa za tiba na huduma za kuogeshea mifugo kwenye Magereza yote yaliyo na mifugo. Aidha, huduma za uhamilishaji wa mifugo ziliendelea kuboreshwa kwenye Magereza ya Ubena – Pwani, Kingolwira na Mbigiri – Morogoro, King'ang'a – Dodoma, Mugumu – Mara, Kitengule - Kagera, Kilimo Urambo – Tabora na Gereza Arusha. Mwaka 2014/2015, Jeshi la Magereza linatarajia kuhudumia jumla ya ng'ombe wa nyama 8,800 na ng'ombe wa maziwa 2,700, mbuzi 3,000, kondoo 450 pamoja na wanyama wengine wadogo wadogo kwa kununua chanjo na dawa za kutosha na kuboresha mashamba ya malisho ya wanyama hawa.

Mheshimiwa Spika, ukamilishaji, ukarabati na ujenzi wa nyumba za Askari na ofisi. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Jeshi la Magereza limeendelea wa ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Magereza Mkoa Singida. Aidha, Jeshi linaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba zinazojengwa kwa njia ya ubunifu katika Magereza ya Ngara - Kagera, Kasulu - Kigoma, King'ang'a - Dodoma, Mwanga - Kilimanjaro, Masasi - Mtwara, Ngudu - Mwanza, Kanegele - Shinyanga, Arusha, Nzega - Tabora pamoja na Kambi Bugorola – Ukerewe Mwanza. Aidha, ukarabati wa nyumba tatu zilizoezuliwa na upepo Gereza la Kongwa - Dodoma pamoja na ukarabati wa nyumba mbili zilizoungua moto Gereza la Ukonga – Dar es Salaam na nyumba moja Gereza la Kihonda - Morogoro ulifanyika. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Jeshi litaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba 24 za kuishi Askari kwenye Magereza ya Shinyanga, Karanga – Kilimanjaro, Butimba – Mwanza, Mahabusu Mugumu – Mara, Kihonda – Morogoro, Kasungamile – Geita, Kiomboi – Singida, Korogwe – Tanga, Musoma – Mara, Muleba – Kagera, Ngwala – Mbeya, Mkuza – Pwani, Kahama – Shinyanga na Kambi Mkoka - Dodoma.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Magereza limeendelea na uzalishaji wa bidhaa zinazotokana na viwanda vidogo vidogo kwa kutengeneza samani za ofisi na bidhaa za ngozi kwa ajili ya Taasisi na Idara za Serikali na watu binafsi. Kwa upande wa kilimo, eneo la ekari 4,800 limelimwa kwa matarajio ya kuvuna tani 6,480 za mbegu za mazao mbalimbali. Aidha, Shirika kupitia Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Magereza limeendelea kufanya kazi mbalimbali za ujenzi wa majengo ya Taasisi za Serikali na watu binafsi zikiwemo ukarabati wa baadhi ya majengo yaliyopo katika eneo la Bunge – Dodoma na utengenezaji wa samani katika ofisi za Wabunge nchi nzima. Matarajio ya mwaka 2014/2015, ni kuongeza shughuli za uzalishaji kwa kuingia ubia na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kupata mtaji wa kutosha kuweza kukidhi soko la bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo, samani za ofisi, samani za nyumbani, bidhaa za ngozi na shughuli za ujenzi ambazo zinaendelea kupanuka.

Mheshimiwa Spika, huduma kwa jamii. Idara ya Probesheni na Huduma kwa Jamii ambayo inasimamia utekelezaji wa Adhabu Mbadala wa Kifungo gerezani hivi sasa inatekeleza Programu hiyo kwenye Wilaya 45 za Mikoa 18 nchini ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Tanga, Singida, Mtwara, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga, Kagera, Pwani, Morogoro, Njombe na Geita. Katika kipindi cha Julai, 2013 mpaka Aprili, 2014 jumla ya wafungwa 1,118 wamenufaika na Programu hiyo. Wafungwa hao hutumikia vifungo vyao nje ya Magereza kwa kufanya kazi za huduma za kijamii katika taasisi za umma na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji katika Magereza, taasisi wanazofanya kazi na kuimarisha uzingatiaji wa Haki za Binadamu. Wizara katika mwaka wa fedha 2014/2015 inatarajia kuongeza Mikoa mingine mitatu na hivyo kufikia 21 ili kuendelea kupanua wigo wa matumizi ya adhabu mbadala hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji ina jukumu la kuwezesha na kudhibiti uingiaji, utokaji na ukaaji wa wageni na pia kuwawezesha raia wa Tanzania kupata hati za kusafiria. Aidha, Idara hii ndio inayoratibu mchakato wa maombi ya uraia kwa wageni wanaoomba uraia wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hali ya ulinzi na usalama mipakani, misako na doria. Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2013, Idara iliendelea kutoa huduma kwenye mipaka kwa wageni wanaoingia na kutoka nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya wageni na raia 930,188 waliingia na wengine 914,710 walitoka. Aidha, katika kipindi hiki watuhumiwa wa uhamiaji haramu 5,576 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ikilinganishwa na wahamiaji haramu 2,319 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, vibali mbalimbali vinavyotolewa kwa wageni na hati za kusafiria zinazotolewa kwa Watanzania. Idara ya Uhamiaji imetoa vibali kwa wageni wawekezaji, wageni waliopata ajira katika makampuni na wageni wengine walioingia nchini kwa malengo mbalimbali wapatoa 13,228. Idara pia imetoa hati za safari 39,159 kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali. Kati ya hati hizo 37,727 ni za kawaida, 1,085 za Afrika Mashariki, 249 za Kibalozi na 98 za Kiutumishi. Aidha, kukua kwa hali ya utandawazi kumesababisha kubadilika kwa teknolojia ya udhibiti wa pasipoti na hati nyingine za safari. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Idara imekamilisha upembuzi yakinifu wa mfumo wa Ki-electroniki wa Uhamiaji Mtandao *(e–immigration)* ambapo huduma za uhamiaji kama vile utoaji wa hati za safari, vibali vya ukaazi na visa zitatolewa ki-elekroniki.

Mheshimiwa Spika, wageni waliopatiwa uraia wa Tanzania, Watanzania walioukana uraia wa Tanzania na waliorudishwa nchini. Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi, 2014, wageni 113 walipatiwa uraia. Aidha, katika kipindi hiki Watanzania 35 walichukua uraia wa mataifa mengine na kupoteza haki ya kuwa raia wa Tanzania mujibu wa Sheria ya Uraia Na.6 ya mwaka 1995. Watanzania watoro (stowaways) 605 walirudishwa nchini toka nchi mbalimbali hususani Afrika ya Kusini. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iko katika hatua za mwisho za kukamilisha uandaaji wa Sera ya Uhamiaji na Uraia ili kushughulikia masuala ya uhamiaji na uraia nchini kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, vyombo vya usafiri, majengo ya ofisi na makazi ya Askari. Katika mwaka 2013/2014, Idara ya Uhamiaji imenunua magari 15 na mwaka 2014/2015 inatarajia kununua magari 12, lori 1 na boti ndogo 2. Vyombo hivi vya usafiri vitasaidia shughuli za misako na doria dhidi ya wahamiaji haramu katika sehemu mbalimbali nchini zikiwemo zile za mipakani. Aidha, imekamilisha ujenzi wa ofisi za Uhamiaji Mkoa wa Ruvuma na ujenzi wa ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Mara, Pwani, Singida na Lindi unaendelea. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inatarajia kuanza ujenzi wa ofisi katika Mikoa ya Mtwara, Geita, Ileje Mkoani Mbeya na Kituo cha Kirongwe Wilayani Rorya Mkoani Mara.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hayo, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imenunua nyumba za makazi ya Askari katika Mikoa ya Ruvuma na Wilayani Ifakara Mkoani Morogoro na kukamilisha ukarabati wa nyumba za makazi Mkoa wa Dodoma na kituo cha Borogonja Mkoani Mara. Ujenzi wa nyumba tano za Makamishna wa Uhamiaji unaendelea Dar es Salaam pamoja na nyumba za Maafisa katika Mikoa ya Ruvuma, Kigoma na Mwanza. Katika mwaka 2014/2015, ujenzi wa nyumba za Askari Kisongo –Arusha utaanza.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto na majanga mengine. Moja ya jukumu la msingi la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto nchi nzima. Zoezi hilo huenda sambamba na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Katika mwaka 2013/2014 mpaka kufikia mwezi Machi, 2014, Jeshi lilikagua jumla ya maeneo 28,877, tafadhali tuangalie Jedwali Na. 4). Katika kipindi hicho kiasi cha maduhuli ya Serikali kilichokusanywa kilikuwa Sh.16,358,878,000. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Jeshi linatarajia kukagua maeneo 60,500 nchi nzima na kukusanya kiasi cha Sh. 35,380,963,000 kutokana na ukaguzi wa magari na majengo.

Mheshimiwa Spika, matukio ya moto na majanga mengine. Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi hususan kupambana na majanga ya moto pamoja na kufanya maokozi mbalimbali. Mpaka kufikia mwezi Machi, 2014, Jeshi limeshiriki kuzima moto katika matukio 784 nchi na kufanya maokozi 205 katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo uokoaji katika Ofisi za Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* - Ubungo, jengo la *Ex-telecom* lililopo mtaa wa Samora na maokozi katika jengo lililoporomoka katika mtaa wa Indira Gandhi (Kisutu). Pia Jeshi limefanya maokozi katika maeneo mbalimbali yaliyokumbwa na mafuriko jijini Dar es Salaam na katika Mikoa mbalimbali ukiwemo Mkoa wa Pwani.

Mheshimiwa Spika, ukarabati na ujenzi wa majengo ya ofisi na vituo vya Zimamoto. Ili kuimarisha huduma za zimamoto na uokoaji nchini, Jeshi limeendelea kuvifanyia ukarabati na kujenga vituo vipya vya Zimamoto na Uokoaji. Katika kusogeza huduma kwa wananchi, mwaka 2013/2014, Jeshi limefungua vituo vipya katika maeneo ya Mwenge Jijini Dar es Salaam na Monduli Mkoani Arusha. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi litaendelea na ujenzi na ukarabati wa ofisi na vituo vya Zimamoto vilivyopo katika Mikoa mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa. Katika mwaka 2013/2014, Mamlaka imeongeza vifaa vya usajili 280 "*Mobile Enrolment Unit" (MEU);* imekamilisha ujenzi wa kituo cha muda cha kuingiza taarifa na kutunza kumbukumbu; imeanza mchakato wa awali wa ujenzi wa kituo kikuu cha utunzaji wa kumbukumbu na kituo cha uokozi wakati wa majanga *(Disaster Recovery Site)* pamoja na vituo kumi na tatu vya usajili vya Wilaya. Ujenzi huu utafanywa kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Korea.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa katika mwaka 2014/2015 inatarajia kuendelea na zoezi la usajili na utambuzi wa watu na kutoa Vitambulisho vya Taifa katika Mikoa na Wilaya za Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, kuongezeka vifaa vya usajili hadi kufikia *Mobile Enrolment Units* 5,000 na kununua magari ishirini, kuajiri watumishi wapya 64, kuanza ujenzi na kuimarisha ofisi za usajili katika Wilaya mbalimbali hapa nchini, kujenga mfumo wa mawasiliano kati ya ofisi za Wilaya na Makao Makuu na kuendelea na upanuzi wa jengo la Makao Makuu *(ID Management Centre)*.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Huduma kwa WAkimbizi. Nchi yetu inaendelea kuhifadhi wakimbizi kutoka nchi mbalimbali za ukanda wa Maziwa Makuu ambazo ni Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(DRC)*. Idadi ya wakimbizi hao imekuwa inapungua mwaka hadi mwaka kutokana na kuimarika kwa amani na utulivu katika nchi hizo. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani *(UNHCR)* na kwa msaada wa Jumuiya ya Kimataifa, imeweza kuchukua hatua kadhaa za kuwarudisha baadhi ya wakimbizi kwenye nchi zao za asili na kuwahamishia kwenye nchi ya tatu ambapo zaidi ya wakimbizi 15,000 wamehamishiwa nchini Marekani katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani itaanza kutekeleza Mpango Maalum wa Miaka Mitano wa kuwahamishia nchini Marekani wakimbizi wenye asili ya *DRC* na Burundi wapatao 32,000 baada ya kusaini Mkataba na Mashirika ya *UNHCR* na *IOM*. Aidha, katika mwaka 2013/2014, Serikali kupitia Wizara yangu ilitoa uraia kwa wakimbizi wa Kisomali 1,514 wenye asili ya Kibantu waliokuwa wanaishi katika makazi ya Chogo Wilayani Handeni Mkoani Tanga na kuyafunga rasmi makazi hayo mwezi Februari, 2014 ambapo wakimbizi wapatao 150 ambao wamebaki katika eneo hilo wataendelea kuishi hapo kwa mujibu wa Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998. Mpaka tarehe 31 Machi, 2014, idadi ya wakimbizi ambao wanahifadhiwa nchini ilikuwa 94,783 ukilinganisha na wakimbizi 101,183 waliokuwepo nchini tarehe 31 Machi, 2013.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea na jitihada za kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la wakimbizi kwa kuwarejesha nyumbani wakimbizi ambao hali ya amani na usalama itakuwa imerejea kwenye nchi zao za asili. Aidha, taratibu zinakamilishwa kuhusu hatma ya wakimbizi wa Burundi wapatao 162,156 wa mwaka 1972. Kwa upande mwingine, Wizara imeanza maandalizi ya kurekebisha Sera na Sheria ya Wakimbizi ili kuboresha utendaji.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Kushughulikia Malalamiko. Jumla ya Malalamiko 130 yaliyopokelewa kwa njia ya barua, mtandao, simu, barua pepe, nakushi au ana kwa ana yalishughulikiwa. Kati yake, malalamiko 101 yalishughulikiwa na kukamilishwa na mengine 29 bado yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, Idara iliweza kushiriki kwenye uchunguzi mbalimbali kwa masuala ambayo yalitokana na vyombo vingine vya uchunguzi. Matukio maalumu matano ya uchunguzi kuhusu Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji yaliweza kufanyika na hatua stahiki kuchukuliwa na Mamlaka husika za kinidhamu. Aidha, mfumo wa mtandao wa kushughulikia malalamiko umeboreshwa na unafanya kazi. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara itaimarishwa zaidi ili kutekeleza vema majukumu yake ya kisheria.

Mheshimiwa Spika, vita dhidi ya biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Sekretarieti ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu imeratibu vikao vinne vya Kamati ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu. Aidha, imeandaa kitabu cha anuani na majina ya watoa huduma kwa waathirika wa biashara haramu ya usafirishaji binadamu *(Directory of Service Provider*), vilevile kutengeneza Rasimu ya Kanuni za Sheria ya Kupambana na biashara haramu ya usafirishwaji wa binadamu nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Sekretarieti itakamilisha kutengeneza Kanuni za Sheria ya Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu ya mwaka 2008 kwa kutoa elimu ya kupambana na biashara hiyo na kuimarisha mikakati ya Serikali katika kupambana na tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, usajili wa vyama vya kijamii na vya kidini. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara imeendelea na jukumu la kusajili na ukaguzi wa vyama vya kijamii na kidini kwa lengo la kuvisimamia ili kuhakikisha kunakuwepo na amani na utulivu katika jamii. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 maombi ya Vyama 595 yalipokelewa ambapo 493 ni ya vyama vya kijamii na 102 ni ya kidini. Kati ya maombi hayo, vyama 449 vimesajiliwa, maombi ya vyama 96 yalikataliwa na maombi ya vyama 50 yanaendelea kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, zoezi la ukaguzi wa Vyama limefanyika katika Mikoa ya Arusha, Tanga na Mwanza. Katika mwaka 2014/2015, Wizara inatarajia kusajili vyama 400 na kufanya ukaguzi katika Mikoa kumi ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali Bungeni 2013/2014. Utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Serikali Bungeni katika mwaka wa fedha 2013/2014 umezingatiwa katika taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Ilani ya Uchanguzi eneo la tatu na katika hotuba hii eneo la nne la mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Ahadi hizo zipo katika maeneo ya vitendea kazi, ajira na mafunzo, misako na doria, ujenzi na ukarabati wa ofisi, vituo, nyumba na magereza, zoezi la utambuzi na usajili wa watu na kuwarejesha wakimbizi makwao. Kwa ujumla wake taarifa za utekelezaji wa ahadi za Serikali zilizotolewa Bungeni katika mwaka wa fedha 2013/2014 ni kama zinavyooneshwa katika kiambatanisho namba moja katika hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, shukrani. Natoa shukrani zangu kwa Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake mahiri sana Mheshimiwa Mama Anna Margareth Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum kwa kuyapitia na kuyachambua makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa Fedha 2014/2015. Maelekezo na ushauri wa Kamati hiyo umeisaidia sana Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, mwisho ingawa siyo mwisho kwa umuhimu, ninawashukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Mohammed Gharib Bilal kwa maelekezo yao mbalimbali na Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda, Waziri Mkuu, kwa kuhimiza utekelezaji wa Wizara yangu kila mara.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha. Baada ya maelezo hayo sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa Feha 2014/2015 ya Sh.881,740,291,800 kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya akadirio hayo, Sh.665,093,488,000 ni za matumizi ya kawaida, ambapo Sh.290,570,582,958 ni matumizi mengineyo na mishahara Sh.374,522,905,042. Makadirio ya Sh.216,646,803,800 ni kwa ajili ya mipango ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

(a) Fungu la 14 -Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Matumizi mengineyo ni Sh.18,610,590,000. Mishahara Sh.7,892,785,000. Jumla ya Fungu hili la 14 ni Sh.26,503,375,000.

(b) Fungu 28 -Jeshi la Polisi. Matumizi mengineyo Sh.154,100,939,970, mshahara Sh.248,727,202,030. Matumizi ya maendeleo ni Sh.6,800,000,000. Jumla ya Fungu 28 ni Sh.409,628,142,000.

(c) Fungu 29-Jeshi la Magereza. Matumizi mengineyo ni Sh. 66,075,022,000, mishahara Sh.83,476,774,000. Matumizi ya maendeleo ni Sh.1,612,748,800. Jumla ya Fungu 29 ni Sh.151,164,544,800.

(d) Fungu 51-Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Matumizi mengineyo ni Sh.9,000,040,000, mshahara ni Sh.3,120,899,000. Matumizi ya maendeleo ni Sh.2,225,075,000. Jumla ya Fungu 51 ni Sh. 14,346,014,000.

(e) Fungu 93-Idara ya Uhamiaji ikijumuishwa na NIDA. Matumizi mengineyo ni Sh.42,783,990,988. Mishahara Sh.31,305,245,012, matumizi ya maendeleo Sh.206,008,980,000. Jumla ni Sh.280,098,216,000.

Mheshimiwa Spika, jumla kuu yote ambayo Wizara yangu inaomba ni Sh.881,740,291,800.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru wewe, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na wananchi wengine kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Ahsante. Hotuba hii imeungwa mkono, Kamati tutaendelea kesho.

**Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2014/2015 Kama ilivyowasilishwa Mezani**

**UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha wa 2014/2015.

**2. Mheshimiwa Spika,** awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii kutoa salamu za rambirambi kwa familia na wananchi wa mikoa mbalimbali ya Tanzania kutokanana na mvua kubwa iliyonyesha katika vipindi tofauti mwaka huu na kusababisha mafuriko na hivyo kuleta adha kubwa kwa wananchi ikiwemo vifo na uharibifu wa mali na miundombinu. Aidha, nawapa pole nyingi ndugu na jamaa wa marehemu waliopoteza maisha yao kutokana na matukio hayo.

**3. Mheshimiwa Spika,** naomba pia kutumia fursa hii kutoa masikitiko yangu kwa familia na wananchi kwa ujumla kutokana na vifo, ulemavu, upotevu na uharibifu wa mali na miundombinu vilivyosababishwa na ajali za barabarani, majini na nchi kavu katika mwaka mzima wa 2013. Aidha, nawapa pole ndugu na jamaa wa marehemu waliopoteza maisha katika matukio hayo. Namwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi, Amina.

**4. Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee naomba kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuonyesha imani kwangu kwa kuniteua katika nafasi hii ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Aidha, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa mapema katika mkutano huu wa Bunge ambayo imetoa mwelekeo wa kazi za Serikali kwa ujumla katika mwaka wa fedha 2014/2015.

**5. Mheshimiwa Spika,** napenda kuishukuru kwa dhati kabisa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2014/2015. Naishukuru pia Kamati hiyo kwa maelekezo na ushauri wao wenye lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.
‘

**6. Mheshimiwa Spika,** majukumu ya msingi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ni kulinda usalama wa raia na mali zao, kuhifadhi na kuwarekebisha wafungwa, kutekeleza Programu ya Huduma kwa Jamii, kuwezesha na kudhibiti uingiaji na utokaji nchini wa raia na wageni, kutoa huduma za zimamoto na uokoaji, kuwahudumia wakimbizi waliopo nchini na kuandaa na kutoa vitambulisho vya Taifa. Majukumu haya yanatekelezwa kupitia Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Huduma kwa Jamii, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Idara ya Wakimbizi na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa.

**II. HALI YA USALAMA NCHINI**
**Hali ya Uhalifu**

**7. Mheshimiwa Spika**, wajibu wa kwanza wa Serikali ni kulinda usalama wa raia na mali zao na kuhakikisha uwepo wa amani na utulivu. Nchi yetu imeendelea kuienzi amani na utulivu uliopo kama msingi mkuu wa Taifa ambao umejengwa na kuendelea kuimarishwa tangu

tupate uhuru mwaka 1961 na katika kipindi cha miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Kuwepo kwa amani na utulivu huo kumechangia katika ustawi wa Nchi yetu kiuchumi, kijamii na kisiasa ambapo kumezingatiwa na kutambuliwa kuwa miongoni mwa vipaumbele katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na maendeleo binafsi ya wananchi wetu. Kwa upande wake, Jeshi la Polisi limeendelea kutekeleza kikamilifu jukumu lake la kikatiba na kisheria la kulinda na kudumisha amani na utulivu nchini kwa kubaini, kuzuia na kutanzua vitendo vya uhalifu, makosa ya usalama barabarani, migogoro, vurugu na fujo.

**8.** **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2013 jumla ya makosa makubwa ya jinai 560,451 yaliripotiwa katika vituo vya Polisi kote nchini ikilinganishwa na makosa 566,702 yaliyoripotiwa katika kipindi kama hiki mwaka 2012. Idadi ya makosa ya jinai yaliyoripotiwa imepungua kwa asilimia 1.1 (Ufafanuzi umeonyeshwa katika **Jedwali Na. 1**). Upungufu huu unatokana upatikanaji wa taarifa za uhalifu mapema na utekelezaji wa mkakati wa Polisi Jamii unaohusisha ushirikishwaji wa wananchi katika vita dhidi ya uhalifu nchini. Sababu nyingine kuu ni kuongezeka kwa wigo wa doria, misako na Operesheni maalum za Jeshi la Polisi mijini na vijijini.

**9.** **Mheshimiwa Spika**, makosa makubwa ya jinai yanayoripotiwa katika vituo vya polisi yamegawanyika katika makundi makuu matatu. Makundi hayo ni makosa dhidi ya binadamu, makosa ya kuwania mali na makosa dhidi ya maadili ya jamii. Kwa ujumla Idadi ya makosa hayo makubwa ya jinai yaliyoripotiwa katika vituo vya polisi imeongezeka kutoka 72,765 mwaka 2012 hadi 73,219 mwaka 2013. Ongezeko hili la makosa 454 ni sawa na asilimia 0.6 Hata hivyo kumekuwepo upungufu wa makosa ya kuwania mali. Makosa ya kuwania mali yamepungua kutoka 46,773 mwaka 2012 hadi 45,470 mwaka 2013. Huu ni upungufu wa makosa 1,303 sawa na asilimia 2.8. Upungufu huu umetokana na kuimarika kwa doria, misako na operesheni maalum za Jeshi la Polisi na ushirikiano wa kiutendaji uliopo kati ya Jeshi la Polisi na vyombo vingine vya dola.

**10.** **Mheshimiwa Spika**, katika miaka ya hivi karibuni ajali za barabarani zimekuwa tishio kwa maisha ya watu na mali. Takwimu za mwaka 2013 zinaonesha kuwa ajali hizo zimeongezeka kwa asilimia 3.7 ikilinganishwa na mwaka 2012. Aidha idadi ya majeruhi na vifo vinavyosababishwa na ajali za barabarani pia imeongezeka. Vifo vimeongezeka kwa asilimia 3.4 na majeruhi kwa asilimia 7.5. Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha Januari hadi Desemba, 2012 ajali za barabarani 23,604 zilitokea katika maeneo mbalimbali ambapo watu 4,062 walipoteza maisha na wengine 20,037 walijeruhiwa. Katika mwaka 2013 ajali zilizotokea ni 24,480 ambazo zilisababisha vifo vya watu 4,091 na wengine 21,536 kujeruhiwa. Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine wa masuala ya usalama barabarani waliendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria za Usalama Barabarani ambapo jumla ya makosa madogo madogo 646,846 yalibainishwa na wakosaji kutozwa faini inayofikia shilingi bilioni 17.5. Takwimu zinaonesha kuwa vyanzo vikuu vya ajali za barabarani ni mwendokasi, ulevi, uzembe wa madereva, ubovu wa vyombo vya usafiri na kubeba abiria na mizigo kuliko uwezo wa vyombo husika.

**11.** **Mheshimiwa Spika**, kutokana na ongezeko hilo la makosa ya usalama barabarani, Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na wadau wengine kama SUMATRA, TBS, TANROADS na Shule za Udereva zilizosajiliwa limeendelea kuchukua hatua za kuzuia na kudhibiti vyanzo vya ongezeko la ajali za barabarani. Hatua hizo ni pamoja na kutoa elimu ya kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani kwa watumiaji wa barabara wakiwemo madereva wa bodaboda, kuendeleza doria za masafa mafupi na marefu katika barabara kuu, ukaguzi wa magari, kutumia kamera za kutambua madereva wanaoendesha mwendo kasi, kuendelea kusimamia zoezi la utoaji wa leseni mpya za udereva, kuwahamasisha abiria kutoa taarifa mapema za madereva wanaokiuka Sheria za Usalama Barabarani, kuwaelekeza wamiliki wa mabasi

kubandika kwenye mabasi yao namba za simu za viongozi wa Polisi na kuwachukulia hatua za kinidhamu askari wanaojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa toka kwa madereva.

**12. Mheshimiwa Spika,** ninapenda tena kuwashukuru Mawaziri wenzangu kutoka Ofisi ya Rais, Utawala Bora; Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; Wizara za Katiba na Sheria; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Kilimo, Chakula na Ushirika; Nishati na Madini; na Elimu na Mafunzo ya Ufundi ambao walihudhuria warsha iliyoandaliwa na Jeshi la Polisi iliyofanyika tarehe 15 Februari, 2013 mjini Dodoma hatimae kutoa tamko lililokubali kusimamia na kutekeleza mipango ya muda wa kati na mrefu ya kuimarisha ulinzi na usalama hapa nchini kwa kufanya yafuatayo:-

(viii) Kuliweka suala la usalama kuwa ni moja ya vipaumbele vya Taifa;

(ix) Kutenga fedha za kutosha kuliwezesha Jeshi la Polisi kumudu kikamilifu wajibu wake wa kuhakikisha usalama wa raia na mali zao;

(x) Kutambua kwamba kila Wizara ni mdau katika suala la usalama na inayo wajibu wa kuepusha migogoro inayozalisha vurugu;

(xi) Kufanya tathmini ya maeneo ambayo ni vyanzo vya migogoro na kutafuta njia ya kuzuia/kutanzua migogoro hiyo. Kuimarisha/kuhuisha mifumo ya usimamizi wa sheria na uwajibikaji wa kila Idara ya Serikali;

(xii) Kujenga ubia wa kiutendaji baina ya Wizara wanazoziongoza na vyombo vya ulinzi na usalama katika kubaini vyanzo vya migogoro na kuweka mikakati ya pamoja ya kuzuia na kutanzua migogoro hiyo;

(xiii) Kuliwezesha Jeshi la Polisi kwa nyenzo, vifaa na miundombinu pindi Mikoa mipya inapoanzishwa;

(xiv) Kurekebisha haraka na kwa vipaumbele upungufu wa kisera, kisheria na kikanuni unaoweza kuchangia mianya ya kusababisha migogoro ya kijamii.

Nawaomba Mawaziri wenzangu kwa pamoja tutekeleze kwa vitendo mipango tuliyojiwekea. Mipango hii ikitekelezwa hali ya usalama nchini itaimarika kwa kuondokana na migogoro isiyo ya lazima.

**13. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Polisi limepata Uongozi mpya baada ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumteua Bwana Ernest Jumbe Mangu kuwa Inspekta Jenerali wa Polisi kuanzia tarehe 01 Januari, 2014. Pia Mheshimiwa Rais amemteua Naibu Inspekta Jenerali wa Polisi na Makamishna wanane kumsaidia Inspekta Jenerali. Makamishna hao wanaongoza Kamisheni za Fedha na Lojistiki, Utawala na Utumishi, Upelelezi wa Jinai, Operesheni na Mafunzo, Polisi Jamii, Intelijensia, Uchunguzi wa Kisayansi wa Jinai na Polisi Tanzania – Zanzibar. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge mtoe ushirikiano kwa Uongozi mpya wa Jeshi la Polisi ili kwa pamoja tudumishe amani na usalama uliopo na tuendeleze mapambano dhidi ya uhalifu na wahalifu nchini.

**14. Mheshimiwa Spika**, napenda pia kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba Jeshi la Polisi linaendelea na utekelezaji wa awamu ya kwanza ya Programu ya Maboresho ya Jeshi la Polisi ya mwaka 2010/11 hadi 2014/15. Programu hii pamoja na mambo mengine, imelenga kuligeuza Jeshi la Polisi kuwa la kisasa, lenye watendaji wenye weledi na linaloshirikiana na jamii

katika kubaini, kuzuia, kudhibiti na kukabili uhalifu na vitendo vyote vinavyosababisha uvunjifu wa amani. Jeshi la Polisi litaendeleza kasi ya mabadiliko ya kiutendaji yaliyoanza katika awamu iliyopita ya uongozi.

**III. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MALENGO YA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 KATIKA KIPINDI CHA 2013/2014**

**15. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ina malengo 10 ya kutekeleza yanayotokana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Taarifa ya utekelezaji wa malengo hayo kwa mwaka 2013/2014 ni kama ifuatavyo:-

**Kuendeleza mapambano dhidi ya biashara ya dawa za kulevya**

**16. Mheshimiwa Spika**, Mapambano dhidi ya biashara haramu ya dawa za kulevya yaliendelezwa. Jeshi la Polisi liliendelea kuzifanyia kazi taarifa za wananchi zilizolenga kuwadhibiti wafanyabiashara wa dawa za kulevya. Aidha doria, misako na operesheni maalum zilifanyika nchi nzima ikiwemo katika bahari ya Hindi kudhibiti uingizaji wa dawa za kulevya nchini. Kati ya Julai hadi Desemba 2013 taarifa za wananchi na doria za Jeshi la Polisi zimewezesha kukamatwa kwa jumla ya kilo 221,898 za dawa za kulevya za viwandani ambazo ni Heroine, Cocaine, Cannabis resin, morphine na mandrax. Watuhumiwa 905 walikamatwa na dawa za kulevya za viwandani na kufikishwa mahakamani. Pia kilogramu 265,576.543 za bhangi na kilo 16,822,305 za mirungi zilikamatwa na watuhumiwa 14,284 walikamatwa na kufikishwa mahakamani. Jumla ya hekari 580.5 za mashamba ya bhangi ziliteketezwa katika mikoa ya Morogoro, Arusha, Tanga, Simiyu na mkoa wa kipolisi Tarime - Rorya.

**17. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Polisi litaendelea kubaini mtandao wa wahalifu wa ndani na nje ya nchi unaojihusisha na uingizaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini kwa kushirikiana na Shirika la Polisi la Kimataifa (*INTERPOL*) kupata taarifa za kiintelijensia kuhusu wasafirishaji wa dawa za kulevya. Kikosi Kazi cha Kitaifa cha Vyombo vya Ulinzi na Usalama cha kupambana na biashara ya dawa za kulevya kitaendelea kuimarishwa kwa kukiongezea rasilimali watu na vitendea kazi.

**Kupunguza msongamano wa wafungwa na mahabusu Magerezani**

**18. Mheshimiwa Spika**, tatizo la msongamano wa Wafungwa na Mahabusu bado lipo, licha ya hatua mbalimbali zinazoendelea kuchukuliwa katika kukabiliana nalo. Jumla ya wafungwa na mahabusu (*inmates*) waliokuwa magerezani wamepungua kutoka 34,552 tarehe 1 Machi, 2013 hadi kufikia 33,831 tarehe 1 Machi, 2014. Kati ya hao wafungwa ni 16,547 na mahabusu ni 17,284 (Ufafanuzi umeonyeshwa katika **Jedwali Na. 2**). Kulingana na takwimu hizi ni dhahiri kuwa tatizo la kuwepo msongamano wa wahalifu katika magereza bado ni kubwa.

**19. Mheshimiwa Spika**, njia mojawapo inayotumika katika kupunguza msongamano Magerezani ni kujenga mabweni mapya na kukamilisha viporo vya ujenzi wa mabweni. Kutokana na jitihada hizo, uwezo wa sasa wa kuhifadhi wafungwa na mahabusu umeongezeka kutoka 27,653 mwaka 2010 hadi kufikia 29,552 mwaka 2014.

**20. Mheshimiwa Spika,** pili ni utekelezaji wa Sheria ya Bodi za Parole Na.25 ya mwaka 1994 iliyofanyiwa marekebisho kwa Sheria Na.5 ya 2002. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 jumla ya vikao vitatu vilikaa na kujadili maombi ya wafungwa 234 ambapo wafungwa 215 walikubaliwa kuachiwa na 19 walikataliwa kutokana na sababu mbalimbali. Aidha, juhudi za kuirekebisha Sheria ya Bodi za Parole Na.25/1994 zinaendelea kufanyika ili kuwezesha wafungwa wengi kunufaika na mpango huu.

**21.** **Mheshimiwa Spika**, njia ya tatu ni kutumia Kifungo cha Nje. Kwa mujibu wa kifungu cha 72 cha Sheria ya Magereza Namba 34 ya mwaka 1967, wafungwa wanaostahili kupewa kifungo cha nje ni wale wanaotumikia kifungo kisichozidi miezi kumi na miwili. Kuanzia tarehe 1 Julai, 2013 hadi 1 Machi, 2014 wafungwa 456 walikuwa wanatumikia kifungo cha nje. Hata hivyo, utaratibu huu haujatekelezwa katika baadhi ya Halmashauri kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kukosa uwezo wa kuwahudumia wafungwa hao kama inavyotakiwa na Sheria. (Ufafanuzi umeonyeshwa katika **Jedwali Na. 3).**

**22.** **Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa Rais anayo mamlaka ya kutoa msamaha kwa wafungwa. Matokeo ya utekelezaji huo husaidia kupunguza msongamano wa wafungwa magerezani. Katika mwaka 2013/2014 jumla ya wafungwa 1,475 walifaidika na msamaha wa Rais uliotolewa tarehe 9 Desemba, 2013 wakati wa sherehe za kuadhimisha miaka 52 ya Uhuru wa Tanzania Bara na jumla ya wafungwa 3,967 wamefaidika na msamaha wa Rais uliotolewa tarehe 26 Aprili 2014 wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

**Kuimarisha na kuboresha mfumo wa upelelezi wa makosa ya jinai**

**23.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara inapenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kukubali kuhuisha Muundo wa Utawala wa Jeshi la Polisi kwa kuanzisha Kamisheni mpya ya Intelijensia ya Jinai (*Criminal Intelligence*) na Kamisheni ya Uchunguzi wa Jinai Kisayansi (*Forensic Science Investigation*). Muundo huu umeboresha mgawanyo wa majukumu ya upelelezi na intelijensia na unatarajiwa kuimarisha utendaji kazi. Aidha, kwa upande wa mafunzo, vyuo vya Taaluma ya Polisi vya Dar es salaam, Moshi na Kidatu, vimeendelea kutoa mafunzo ya Intelijensia ya jinai na mbinu za kisasa za upelelezi kwa askari wanaohudhuria mafunzo ya Cheti na Diploma ya Sayansi ya Polisi. Kuimarika kwa mfumo wa upelelezi kumeongeza kiwango cha mafanikio ya kesi mahakamani kutoka asilimia 11.6 mwaka 2012 hadi asilimia 12.4 mwaka 2013.

**Kuanzisha mpango wa kuwapatia askari nyumba bora za kuishi**

**24.** **Mheshimiwa Spika,** Kutokana na mahitaji makubwa ya nyumba za makazi ya askari nchi nzima, Jeshi la Polisi linaendelea kutekeleza mpango wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP) ili kupunguza ukubwa wa tatizo hili. Kwa kuanzia Jeshi la Polisi limeingia ubia na Kampuni ya Mara World wa kujengewa Kituo cha kisasa cha Polisi na nyumba 350 za askari katika Mkoa wa kipolisi Kinondoni. Aidha, Jeshi la Polisi limeanzisha Shirika la Uzalishaji Mali *(Tanzania Police Force Corporation Sole)* ambalo kipaumbele kimojawapo ni kujenga nyumba na ofisi za Jeshi la Polisi kwa gharama nafuu. Vilevile, Jeshi la Polisi litaendelea kukamilisha miradi ya ujenzi wa nyumba katika mikoa ya Njombe, Kagera, Mwanza na Mara na pia kujenga nyumba mpya kwa ajili ya makazi ya askari kadri uwezo utakavyoruhusu.

**Kujenga Vituo vya Polisi katika kila Tarafa nchini**

**25.** **Mheshimiwa Spika**, Ili kupeleka huduma za polisi karibu na wananchi Jeshi la Polisi lina mpango wa kujenga vituo vya Polisi katika kila Tarafa. Kutokana na mahitaji makubwa ya rasilimali fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo, Jeshi la Polisi litatumia Shirika la Polisi la Uzalishaji Mali na pia kushirikiana na sekta binafsi katika kujenga vituo vya Tarafa kwa awamu. Aidha, Jeshi litaendelea na utekelezaji wa Polisi Jamii kwa kuwatumia Wakaguzi 526 wa Tarafa na askari Kata kutoa huduma za polisi kwa kutumia vituo vilivyopo karibu na Tarafa zisizo na vituo vya polisi hasa maeneo ya vijijini.

**Kuwapatia wananchi mafunzo ya Ulinzi Shirikishi**

**26. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanzisha kampeni mahsusi ya kuhamasisha Wizara, Idara na Taasisi mbalimbali za Serikali kujenga miundombinu ya amani katika ngazi za Mikoa, Wilaya, Tarafa na Kata kwa kutumia sheria na taratibu zilizopo. Jeshi la Polisi limeendelea kuwatumia Wakaguzi wa Tarafa/Jimbo na Askari Kata/Shehia kuwaelimisha wananchi kuwa kila mmoja anawajibika kwa ulinzi wake binafsi, familia yake, jirani yake na jamii kwa ujumla tofauti na fikra zisizo sahihi kwa baadhi ya watu kwamba usalama wa raia na mali zao ni jukumu la Jeshi la Polisi na viongozi wa Serikali pekee.

**Kuimarisha Mafunzo ya Askari wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama**

**27. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014 askari 23,269 wa Jeshi la Polisi wamepatiwa mafunzo katika fani za Sayansi za Polisi, Uongozi wa Kati na Usimamizi wa Rasilimaliwatu. Katika mwaka 2014/15 Jeshi la Polisi litatoa kipaumbele kwenye mafunzo ya utayari ambapo jumla ya maafisa, wakaguzi na askari wapatao 41,000 watapatiwa mafunzo hayo.

**28. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Magereza limeendelea kutoa mafunzo mbalimbali kwa watumishi na askari wake ndani na nje ya Jeshi. Mafunzo hayo ni yale yanayohusu uendeshaji wa Magereza na yale yanayohusu taaluma mbalimbali ambazo zinahitajika katika uendeshaji wa Jeshi la Magereza. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2013 hadi Machi, 2014 jumla ya watumishi na askari 447 wamehudhuria mafunzo mbalimbali nje ya Jeshi na wengine 121 wamehudhuria mafunzo ndani ya Jeshi.

**29. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji linaendelea na jitihada za kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu mbalimbali kwa kuwapatia watumishi wake mafunzo katika fani mbalimbali. Katika kutekeleza ilani ya uchaguzi, kwa mwaka 2013/2014 Jeshi limegharamia mafunzo mbalimbali kwa askari 82 ikiwemo mafunzo juu ya namna ya kupambana na moto wa ndege (*Aircraft Fire Fighting Techniques*) (askari 21), mafunzo ya huduma ya kwanza (askari 42), mafunzo ya kuogelea (askari 11) na mafunzo ya kusoma ramani (askari 8).

**30. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi hiki Idara ya Uhamiaji imewapatia mafunzo ya awali watumishi wapya 52. Pia Idara inatarajia kuwapeleka waajiriwa wengine 270 kwenye mafunzo ya awali ya Uhamiaji. Watumishi wapatao 446 waliopo kazini wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi na mrefu, kati yao 9 mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi, 1 mafunzo ya muda mrefu nje ya Nchi, 297 ya muda mfupi ndani ya nchi na 139 mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi. Katika mwaka 2014/2015, Idara inatarajia kuajiri watumishi wapya 1,250 na kutoa mafunzo kwa watumishi 500 waliopo kazini.

**Kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za kilimo katika maeneo ya Magereza**

**31. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Kampuni za *TANSEED na Highland Seed Growers Ltd* limelima mashamba ya mbegu bora za mahindi katika Mikoa ya Rukwa, Ruvuma na Kigoma. Aidha, Jeshi la Magereza kwa kushirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo nchini *Agricultural Seed Agency* (ASA) lililima mashamba ya mbegu bora za kilimo katika Mikoa ya Arusha, Dodoma, Manyara, Lindi, Iringa, Mbeya, Kilimanjaro na Morogoro. Jumla ya hekta 776 zimelimwa na kupandwa mbegu bora za mazao ya aina mbalimbali na matarajio ni kuvuna tani 2,000 za mbegu bora. Katika mwaka 2014/2015,

Jeshi la Magereza linatarajia kuendelea na shughuli za kilimo cha mbegu bora kwa kulima hekta 800 na kutarajia kuvuna tani 2,100 za mbegu bora.

**Kutoa vitambulisho vya Taifa**

**32. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Vitambulisho inaendelea na jukumu lake la msingi la kujenga mfumo wa usajili na utambuzi wa watu hapa nchini ambao moja ya matokeo yake ni utengenezaji wa Vitambulisho vya Taifa. Aidha, mfumo huu utaiwezesha Serikali katika ukusanyaji wa kodi ya mapato na kuwawezesha wananchi wengi kukopesheka kwa maana watakuwa wanatambulika na kusaidia katika uthibiti wa usalama wa nchi yetu.

**33. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014 Mamlaka Vitambulisho vya Taifa imekamilisha usajili kwa wakazi 560,297 wa Unguja na Pemba na wakazi 2,449,822 wa Mkoa wa Dar es Salaam hivyo idadi yote ya waliosajiliwa kuwa 3,300,119. Wakazi hawa wakati wowote wataweza kupatiwa Vitambulisho vyao vya Taifa.

**Kuimarisha Vikosi vya Zimamoto na Uokoaji vyenye Wataalam na Zana za Kisasa ili Kukabiliana na Majanga ya Moto**

**34. Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha huduma za Zimamoto na Uokoaji nchini, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limefanikiwa kupata magari matano ya kuzimia moto na yamepelekwa katika mikoa ya Simiyu, Pwani, Katavi na Dar es salaam. Pia Jeshi limefanikiwa kupata boti mbili za uokoaji ambazo zipo katika mkoa wa Dar es salaam. Aidha, juhudi zinaendelea za kuongeza idadi ya Askari na Maafisa ambapo katika mwaka 2013/2014 Jeshi limepata kibali cha kuajiri askari 800 na zoezi la usaili limekamilika.

**IV. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2013/2014 NA MALENGO YA MWAKA 2014/2015**

**MAPATO NA MATUMIZI**

**35. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilipangiwa kukusanya mapato ya shilingi 145,024,760,000, hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2014, Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 101,938,065,028 sawa na asilimia 70.3 ya lengo la mwaka. Katika mwaka 2014/2015, Wizara imelenga kukusanya mapato ya shilingi 156,667,944,771. Mifumo na nguvu zaidi zitaelekezwa katika kuziba mianya ya uvujaji wa mapato hususan katika kuimarisha na kuboresha matumizi ya benki kwa ajili ya kufanya malipo ya huduma zitolewazo na taasisi za Wizara.

**36. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2013/2014, Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi 741,131,771,000 kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Hadi kufikia tarehe 31 Machi 2014 jumla ya shilingi 497,875,939,929 zilikuwa zimetumika sawa na asilimia 67 ya bajeti ya mwaka mzima, ambapo shilingi 259,015,160,850 zimetumika kulipia mishahara, matumizi mengineyo shilingi 201,308,653,229 na fedha za maendeleo ni shilingi 37,552,125,850. Katika mwaka 2014/2015, Wizara inategemea kutumia shilingi 881,740,291,800 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo.

**JESHI LA POLISI**
**Kuzuia Uhalifu na Ajali za Barabarani**

**37.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14, Jeshi la Polisi liliendelea kutekeleza mkakati wa kupunguza uhalifu, ujulikanao kwa kiingereza kama '*Crime Reduction Strategy*'. Katika kutekeleza Mkakati huo, doria, misako na operesheni maalum zimefanyika nchi nzima. Aidha, maofisa, wakaguzi na askari 5,030 walipangwa kuwa Maafisa wa Polisi Jamii *(Community Policing Officers)* katika Tarafa/Majimbo na Kata/Shehia kote nchini hasa maeneo ya vijijini. Mkakati huo pia umeimarisha ushirikiano kati ya Jeshi la Polisi na wananchi na hivyo umesaidia kupunguza kwa vitendo vya uhalifu mkubwa kwa asilimia 4.3 mwaka 2012 na asilimia 1.1 mwaka 2013. Kwa ujumla Jeshi la Polisi liliendelea kutekeleza jukumu lake la kuhakikisha usalama, amani na utulivu vinakuwepo hapa nchini. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litaimarisha doria, misako na operesheni maalum ili kupunguza matishio ya uhalifu, makosa makubwa ya jinai na ajali za barabarani. Pia Jeshi la Polisi litaendelea kujiweka tayari kudumisha amani na utulivu kuelekea kufanyika kwa zoezi la Kura za Maoni ya kupata Katiba mpya, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2014 na Uchaguzi Mkuu mwaka 2015.

**Polisi Jamii**

**38.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2013/14 Jeshi la Polisi liliendelea kuwahamasisha wananchi kutekeleza kwa vitendo dhana ya Polisi Jamii kama mkakati mkuu wa kuzuia uhalifu katika maeneo wanayoishi. Programu za Usalama Wetu Kwanza, Utii wa Sheria Bila Shuruti, Familia Yetu haina Mhalifu na Ulinzi Shirikishi zimeendelea kupata mwitikio chanya kutoka kwa wananchi. Kwa upande wa uanzishwaji wa vikundi vya Ulinzi Shirikishi, jumla ya Vikundi vipya 1,778 vilianzishwa mwaka 2013/14 na hadi sasa jumla ya vikundi 6,798 vimeanzishwa nchi nzima. Ili kuwapata Wakaguzi wa Tarafa, Jeshi la Polisi liliendesha mafunzo maalum ya upandishwaji vyeo kwa wakaguzi 811 na kuajiri askari wapya 3,039. Hatua hizo ziliwezesha Jeshi kuongeza idadi ya askari wanaofanya kazi kama Maofisa wa Polisi Jamii katika ngazi ya Tarafa/Jimbo na Kata/Shehia kutoka askari 3,335 mwaka 2012/13 hadi askari 8,365 mwaka 2013/14. Katika mwaka 2014/15 Jeshi la Polisi litaongeza idadi ya askari wanaofanya kazi katika Tarafa na Kata kwa asilimia 50.

**Mauaji ya Wanawake, Wazee, Vikongwe Kwa Imani za Kishirikina**

**39.** Mheshimiwa Spika, kumekuwa na wimbi la mauaji ya wanawake hasa katika Mkoa wa Mara. Mauaji ya Wazee na Vikongwe yameendelea katika mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Tabora. Katika kipindi cha mwaka 2013/14, takwimu zinaonyesha kuwa jumla ya wanawake 15 wameuwawa katika Mkoa wa Mara hususan wilaya ya Butiama. Aidha, wazee na vikongwe 154 waliuawa katika Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na Tabora kutokana na imani za kishirikina. Kati yao, wanaume walikuwa 63 na wanawake 91. Serikali inalaani kwa nguvu zote mauaji ya wanawake, wazee na vikongwe kwa imani za kishirikina katika karne hii ya 21. Katika mwaka 2014/15 Serikali itahakikisha mauaji ya aina hii yanadhibitiwa kwa kufanya yafuatayo:-

i) Kuendelea kushirikiana na raia wema, Mamlaka za Serikali za Mitaa na taasisi zinazoratibu shughuli za waganga wa jadi, kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani waganga wanaothibitika kupiga ramli za uchochezi na kusababisha mauaji ya wazee na vikongwe

ii) Kuendelea kushirikiana na raia wema na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani wahalifu wanaokodishwa kufanya mauaji ya wanawake, wazee na vikongwe

iii) Kuendelea kutumia taarifa za kiintelijensia kuwabaini, kuwakamata na kuwafikisha Mahakamani wanaotuhumiwa kutoa fedha kwa waganga wa jadi kwa lengo la kuambiwa waliowaua ndugu zao au kupewa mbinu na masharti ya kupata utajiri wa haraka;

iv) Kuiimarisha Kamisheni mpya ya Intelijensia ya Jinai kwa kuongeza rasilimali watu na vitendea kazi kuanzia ngazi ya Makao Makuu hadi ngazi ya Kata/Shehia ili kujenga uwezo wa kupata taarifa mapema za uhalifu.

**Upelelezi wa Makosa ya Jinai**

**40. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, ushirikiano wa kiutendaji kati ya Jeshi la Polisi na taasisi zinazounda Jukwaa la Haki Jinai uliendelea kuimarika. Taasisi zinazounda Jukwaa la Haki Jinai ni Jeshi la Polisi, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Jeshi la Magereza na Mahakama. Kwa upande wake Jeshi la Polisi liliendelea kuongeza ufanisi katika upelelezi wa makosa ya jinai na hivyo kufanikiwa kuongeza kiwango cha washtakiwa kupatikana na hatia mahakamani kutoka asilimia 11.6 mwaka 2012 hadi asilimia 12.4 mwaka 2013. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litaongeza kasi na ufanisi zaidi katika upelelezi wa kesi za jinai ili kufikia kiwango cha mafanikio ya kesi mahakamani kwa asilimia 15.

**Ubadilishanaji wa Taarifa za Wahalifu na Uhalifu**

**41. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi lilishiriki katika mafunzo ya pamoja, ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijensia na operesheni za kikanda na kimataifa. Jeshi la Polisi pia liliendelea kushirikiana na majeshi mengine ya polisi ya Kanda na Kimataifa katika kuimarisha udhibiti wa makosa yanayovuka mipaka hususan ugaidi, uharamia, biashara ya dawa za kulevya, biashara haramu ya kusafirisha binadamu, uhamiaji haramu, wizi wa magari, wizi wa kutumia mitandao ya TEHAMA, bidhaa bandia, biashara haramu ya silaha na uchafuzi wa mazingira. Katika mwaka 2014/15 Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama ndani na nje ya nchi kwa lengo la kuzuia uhalifu unaovuka mipaka usitokee ndani ya ardhi ya Tanzania.

**Migogoro ya Ardhi**

**42. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2013/14 kumekuwepo na migogoro mbalimbali ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji, wakulima wakitaka kumiliki ardhi kwa ajili ya kilimo cha mazao ya chakula au biashara wakati wafugaji nao wakiitaka ardhi hiyo hiyo kulishia mifugo yao. Migogoro hiyo ilitokea katika maeneo ya Hanang, Kiteto, Mvomero, Kondoa, Singida na Mbeya. Migogoro hii imesababisha mapigano baina ya makundi hayo na kusababisha watu 47 kujeruhiwa na 16 kuuwawa. Aidha, migogoro hii ilisababisha vifo vya watu watano na majeruhi 20 mwaka 2012/13 na ilitokea katika mikoa ya Tanga, Pwani, Mbeya, Morogoro na Arusha. Katika mwaka 2014/15 Jeshi la Polisi litaendelea kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ili kuzuia mauaji, majeruhi na uharibifu wa mali unaosababishwa na migogoro ya ardhi.

**Operesheni za Polisi**

**43. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2013/14 Jeshi la Polisi liliendelea kufanya operesheni katika maeneo mbalimbali ya nchi kwa lengo la kudhibiti wahalifu na uhalifu uliosababisha hofu kwa wananchi. Operesheni hizo zilifanyika kwenye Hifadhi za Taifa, mbuga za wanyama na katika mikoa ya Geita, Kagera na Kigoma. Katika mwaka 2014/15 Jeshi la Polisi litaendeleza operesheni za nchi kavu, angani na majini kwa lengo la kudumisha amani na utulivu nchini.

**Ulinzi wa Amani Nje ya Nchi**

**44.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/14 Jeshi la Polisi liliendelea kutoa mchango wake katika Operesheni za Ulinzi wa Amani *(Peace Keeping Missions)* nje ya nchi. Jeshi la Polisi lilichangia jumla ya askari 192 walioshiriki ulinzi wa amani katika nchi ya Sudan (181), Sudan Kusini (5) na Lebanon (6). Ushiriki endelevu wa askari polisi wetu katika kazi za ulinzi wa amani nje ya nchi ni ishara na ushahidi kwamba askari polisi wetu wanao weledi na nidhamu inayokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa. Katika mwaka 2014/15, Jeshi la Polisi litaendelea kuwaruhusu Maafisa, Wakaguzi na askari kufanya mitihani maalum inayowawezesha kushiriki katika Operesheni za Ulinzi wa Amani ndani na nje ya nchi.

**Ajira, Mafunzo na Upandishwaji Vyeo**

**45.** **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2013/2014, jumla ya askari polisi wapya 3,090 waliajiriwa na askari polisi 916 wa vyeo mbalimbali walipandishwa vyeo. Katika mwaka huu askari 23,289 walishiriki mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo ndani ya nchi na askari 207 walipata mafunzo ya nje ya nchi. Aidha, Inspekta Jenerali wa Polisi aliwahamisha Maafisa, Wakaguzi na askari 1,484 kwa lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji katika komandi za Jeshi la Polisi nchini na kuziba nafasi zilizoachwa wazi kutokana na sababu mbalimbali hususan kustaafu, kuacha kazi, kwenda nje ya nchi kushiriki katika Ulinzi wa Amani na kufariki dunia. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litaajiri askari wapya 3,000 na kuwapandisha vyeo askari 3,959 wa vyeo mbalimbali.

**Mahitaji ya Vitendea Kazi na Makazi Kwa Askari Polisi**

**46.** **Mheshimiwa Spika**, idadi ya watu na mahitaji ya huduma ya usalama wa raia na mali zao yanazidi kuongezeka kila mwaka. Wakati hali ikiwa hivyo, Jeshi la Polisi linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na uchache wa vitendea kazi hasa vyombo vya usafiri. Jeshi linakabiliwa pia na uchache na uchakavu wa ofisi na makazi ya askari hivyo kuathiri ubora wa huduma za polisi katika maeneo mengi nchini. Ili kukabiliana na changamoto ya uchache wa miundombinu ya makazi, mwaka 2013/14 Serikali iliridhia kuanzishwa kwa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Polisi (*Tanzania Police Force Corporation Sole*). Aidha, Serikali imelenga kuliwezesha jeshi la polisi ili kuimarisha doria, misako, upelelezi na operesheni maalum za kubaini, kuzuia na kutanzua uhalifu nchini. Katika mwaka 2014/15 Serikali itanunua magari na vitendea kazi kwa ajili ya jeshi la Polisi na kuanza ujenzi wa nyumba 330 za askari eneo la Kunduchi na nyumba 20 za maafisa wa ngazi za juu eneo la Mikocheni mkoani Dar es salaam.

**Usimamizi wa Nidhamu za Askari**

**47.** **Mheshimiwa Spika**, hatua za kinidhamu ziliendelea kuchukuliwa kwa maafisa, wakaguzi na askari polisi waliobainika kujihusisha na vitendo vya ukiukwaji wa maadili mema ya Jeshi la Polisi. Katika mwaka 2013/2014, jumla ya Maafisa 6 walisimamishwa kazi na wengine 18 wameandikiwa barua za kutakiwa kujieleza kwa nini wasichukuliwe hatua za kinidhamu. Jumla ya askari 152 wa vyeo mbalimbali walifukuzwa kazi baada ya kupatikana na hatia ya makosa ya utovu wa nidhamu na kati yao askari 18 wamefikishwa mahakamani kujibu mashtaka ya jinai dhidi yao. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litaongeza upekuzi kwa askari wake na kwa vijana wanaoomba kujiunga na Jeshi ili kuwa na askari wenye nidhamu ya hali ya juu na moyo wa dhati wa kulitumikia Jeshi na Taifa kwa ujumla.

**Sifa na Zawadi kwa Askari**

**48. Mheshimiwa Spika**, Jeshi la Polisi liliendelea kutoa sifa na zawadi kwa askari waliotekeleza majukumu yao kwa umahiri mkubwa. Katika mwaka 2013/14 jumla ya askari 91 walitunukiwa sifa na zawadi mbalimbali. Kiasi cha shilingi milioni 51.3 zilitumika kuwazawadia askari hao kutoka Komandi zifuatazo: Kilimanjaro (3), Temeke (8), Dodoma (5), Singida (3), Shinyanga (3), Tabora (2), Mwanza (10), Geita (3), Mbeya (4), Kigoma (1), Mtwara (2), Mara (2), Iringa (3), Njombe (2), Tanga (3), Ruvuma (3), Morogoro (2), Pwani (4), Kagera (2), Simiyu (3), Rukwa (2), Lindi (1), Manyara (2), Kikosi cha Ujenzi (2), Viwanja vya Ndege (1) na Makao Makuu ya Polisi Dar es Salaam (14). Katika mwaka 2014/2015, Jeshi la Polisi litaendelea kuwatambua maafisa, wakaguzi, askari na watumishi raia wanaotekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa na kuwatunukia sifa na zawadi stahiki.

**Miradi ya Maendeleo**

**49. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Jeshi la Polisi liliendeleza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Idara ya Upelelezi Dar es Salaam. Katika mwaka 2014/15 Jeshi la Polisi litanunua vyombo vya usafiri kwa ajili ya kuimarisha doria na operesheni za kipolisi na redio za mawasiliano za digitali *(digital mobile radio)*. Pia Jeshi la Polisi litaendeleza ujenzi wa Makao Makuu ya Idara ya Upelelezi Dar es salaam, ujenzi wa nyumba kwa ajili ya makazi ya askari katika mikoa ya Mara (24), Mwanza (24), Kagera (12), Njombe (12) na ujenzi wa kituo cha polisi Vikokotoni -Unguja. Mikoa minane (Tanga, Mbeya, Mjini Magharibi, Kusini Pemba, Pwani, Mtwara, Morogoro, na Ruvuma) itaunganishwa na mkongo wa Taifa ili kuimarisha mawasiliano ya kimtandao katika Jeshi la Polisi. Aidha, Jeshi la Polisi litaendelea kutekeleza mradi wa kupambana na rushwa unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Uingereza (DFID).

**JESHI LA MAGEREZA**

**50. Mheshimiwa Spika**, jukumu la msingi la Jeshi la Magereza ni kuwahifadhi wafungwa na mahabusu wa aina zote pamoja na kuwarekebisha tabia kwa wale waliohukumiwa vifungo kwa mujibu wa Sheria. Aidha, urekebishaji wa tabia za wafungwa unafanyika kupitia programu za mafunzo kwa njia ya vitendo katika miradi ya kilimo, viwanda vidogo vidogo na ujenzi. Aidha, mafunzo ya stadi mbalimbali hufanyika katika Chuo cha Ufundi Magereza Ruanda-Mbeya na Gereza la Vijana Wami. Vile vile, ushauri nasaha hutolewa kwa wafungwa kwa kutumia Walimu wa Dini na Maafisa Ustawi wa Jamii.

**Usafirishaji wa Mahabusu Kwenda Mahakamani na Kurudi Magerezani**

**51. Mheshimiwa Spika,** jukumu la kuwasindikiza mahabusu kwenda mahakamani na kurudi Gerezani linaendelea katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Arusha na katika baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Dodoma. Utaratibu huu umeonesha mafanikio makubwa katika suala zima la kupunguza msongamano wa mahabusu Magerezani kwa sababu mahabusu wote hufikishwa mahakamani kwa tarehe walizopangiwa ambapo wengine huachiliwa kwa dhamana au kesi zao kufutwa na nyingine kumalizika kwa mujibu wa Sheria. Katika mwaka 2014/2015, lengo likiwa kuendelea na utaratibu huu katika Wilaya zilizosalia za Mkoa wa Dodoma na kuanza Mkoa wa Mwanza. Aidha, kwa mwaka 2014/2015 Jeshi la Magereza linatarajia kununua magari 8 (mabasi makubwa 2, mabasi madogo 2 na magari madogo 4 aina ya *Station Wagon*) kwa ajili ya shughuli za utawala.

**Programu za Urekebishaji wa Wafungwa**

**52. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Magereza limeendelea kutekeleza programu za urekebishaji wa wafungwa magerezani kwa kuwapa stadi katika kilimo. Aidha, matrekta ya vituo vya Ngwala, Ludewa, Wazo Hill, Nachingwea na Kilimo Urambo yalifanyiwa matengenezo

makubwa. Malengo kwa mwaka 2014/2015 ni kuendelea kuyafanyia matengenezo matrekta yaliyopo pamoja na zana zake.

**53. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha shughuli za viwanda vidogo vidogo magerezani, Jeshi limekamilisha kufunga mashine nne (4) katika Kiwanda cha kukamua mawese na mise katika Kambi ya Kimbiji – Dar es Salaam. Pia zimenunuliwa mashine kumi na tatu (13) za aina mbalimbali kwa ajili ya viwanda vya Seremala na Karakana Ukonga. Mashine hizi zitaongeza kasi ya uzalishaji na pia kutekeleza kwa vitendo sera ya urekebishaji wa wafungwa. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 Jeshi la Magereza linatarajia kuendelea na shughuli za uzalishaji mali baada ya kazi ya ufungaji wa mashine mpya za aina mbalimbali kukamilika katika viwanda vya Ushonaji, Uhunzi na Samani katika Magereza ya Ukonga, Arusha, Butimba na Uyui.

**54. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2013/2014 Jeshi la Magereza liliendelea na jukumu la urekebishaji wa wafungwa kupitia ufugaji wa ng'ombe wa nyama 8,328 na ngombe wa maziwa 2,407 pamoja na mifugo mingine ambayo ni mbuzi, kondoo, nguruwe, sungura, kuku wa mayai na bata weupe. Huduma mbalimbali za mifugo ziliboreshwa kama vile chanjo na dawa za tiba na huduma za kuogeshea mifugo kwenye Magereza yote yaliyo na mifugo. Aidha, huduma za uhamilishaji wa mifugo ziliendelea kuboreshwa kwenye Magereza ya Ubena – Pwani, Kingolwira na Mbigiri – Morogoro, King'ang'a – Dodoma, Mugumu – Mara, Kitengule - Kagera, Kilimo Urambo – Tabora na Gereza Arusha. Mwaka 2014/2015, Jeshi la Magereza linatarajia kuhudumia jumla ya Ng'ombe wa nyama 8,800 na Ng'ombe wa maziwa 2,700, Mbuzi 3,000, Kondoo 450 pamoja na wanyama wengine wadogo wadogo kwa kununua chanjo na dawa za kutosha na kuboresha mashamba ya malisho.

**Uboreshaji wa Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji Shughuli za Wafungwa na Mahabusu**

**55. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa awamu ya pili ya Mradi wa Mfumo wa Taarifa za Uendeshaji Shughuli za Wafungwa kwa njia ya Mtandao wa Kompyuta *(Offenders Management Information System)* ulianza baada ya awamu ya kwanza kukamilika. Utekelezaji huo ulihusisha kazi za uwekaji wa miundombinu (*Network Infrastructure*) katika Magereza ya Butimba, Uyui, Ofisi ya Magereza Mkoa Mwanza na Tabora. Aidha, kazi hiyo ilitakiwa iendelee kufanyika katika Ofisi ya Mkoa Dodoma, Gereza Kuu Isanga na Msalato lakini haikufanyika kutokana na ufinyu wa bajeti. Utekelezaji wa mradi huu utaendelezwa katika Mikoa yote nchini kwa awamu kadri fedha zitakavyopatikana.

**Uimarishaji wa Magereza Makongwe Yenye Ulinzi Mkali (*Maximum Security Prisons*)**

**56. Mheshimiwa Spika,** ukarabati na uboreshaji wa majengo na miundombinu ya Magereza yenye Ulinzi Mkali umefanyika na unaendelea katika Gereza la Butimba Sehemu ya Wanawake, kiwanda na mahabusu. Aidha, kazi ya ukarabati wa majengo na miundombinu utaendelea chini ya Mpango wa Maboresho ya Sekta ya Sheria nchini katika Sehemu ya Wanawake katika Magereza ya Ruanda - Mbeya, Musoma – Mara, Isanga – Dodoma, Karanga – Moshi na Lilungu – Mtwara. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, ukarabati wa majengo na miundombinu utaendelea katika Magereza ya Segerea – Dar es Salaam, Isanga – Dodoma, Lilungu – Mtwara, Karanga – Kilimanjaro na Butimba – Mwanza.

**Upanuzi, Ukamilishaji, Ukarabati na Ujenzi wa mabweni ya wafungwa.**

**57. Mheshimiwa Spika,** kazi ya ujenzi wa bweni moja la wafungwa kwa ajili ya Gereza la Wilaya Chato – Geita umekamilika. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, lengo ni kuendeleza ujenzi wa jiko na bweni moja la wafungwa katika Gereza Segerea – Dar es Salaam

na kukamilisha ujenzi wa Gereza Maalum Isanga na Vilevile kukamilisha ujenzi wa Hospitali iliyopo Gereza Segerea. Kukamilika kwa jengo hili kutasaidia kutoa huduma ya kulaza wagonjwa 110 kwa wakati mmoja watakaopewa rufaa kutoka Zahanati za Magereza zilizopo nchini kote.

**Ukamilishaji Ukarabati na Ujenzi wa nyumba za askari na ofisi**

**58. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2013/2014 Jeshi la Magereza limeendelea wa ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Magereza Mkoa Singida. Aidha, Jeshi linaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba zilizojengwa kwa njia ya ubunifu katika Magereza ya Ngara - Kagera, Kasulu - Kigoma, King'ang'a - Dodoma, Mwanga - Kilimanjaro, Masasi - Mtwara, Ngudu - Mwanza, Kanegele - Shinyanga, Arusha, Nzega - Tabora pamoja na Kambi Bugorola – Ukerewe Mwanza. Aidha, ukarabati wa nyumba tatu zilizoezuliwa na upepo Gereza Kongwa - Dodoma pamoja na ukarabati wa nyumba mbili zilizoungua moto Gereza Ukonga – Dar es Salaam na nyumba moja Gereza Kihonda - Morogoro ulifanyika. Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Jeshi litaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba 24 za kuishi askari kwenye Magereza ya Shinyanga, Karanga – Kilimanjaro, Butimba – Mwanza, Mahabusu Mugumu – Mara, Kihonda – Morogoro, Kasungamile – Geita, Kiomboi – Singida, Korogwe – Tanga, Musoma – Mara, Muleba – Kagera, Ngwala – Mbeya, Mkuza – Pwani, Kahama – Shinyanga na Kambi Mkoka - Dodoma.

**Uimarishaji wa Mifumo ya Maji Safi na Maji taka**

**59. Mheshimiwa Spika,** Baadhi ya Magereza nchini yanakabiliwa na tatizo la ukosefu wa maji na uchakavu wa miundo mbinu ya maji safi na maji taka ambayo pia yanaelemewa na tatizo kubwa la msongamano wa wafungwa. Katika mwaka wa fedha 2013/2014, kazi ya ujenzi wa miundombinu ya majitaka katika Gereza Isanga, Mpwapwa – Dodoma na Namajani - Mtwara uliendelea. Vile vile, ujenzi wa mfumo wa majisafi ulifanyika katika Magereza ya Kwitanga - Kigoma, Kambi Mkoka - Dodoma, Kingolwira- Morogoro na katika eneo linalojengwa Gereza la Wilaya Ruangwa - Lindi. Katika mwaka 2014/2015, lengo ni kukamilisha ujenzi wa mifumo ya majisafi na majitaka katika Magereza hayo.

**Kilimo cha Umwagiliaji**

**60. Mheshimiwa Spika**, ili kuepuka kilimo cha kutegemea mvua, kwa mwaka 2013/2014, Jeshi la Magereza lilianza ujenzi wa miundombinu ya kilimo cha umwagiliaji katika Gereza Idete – Morogoro. Kazi ya ujenzi wa mfereji imekamilika kwa asilimia 25. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa mfereji mkuu yamefanyika kwa kusafisha eneo la mita 1,940 kati ya mita 2,425 za mfereji huo. Jeshi litaendelea kukamilisha ujenzi wa mradi huo kadri fedha zitakavyopatikana. Katika mwaka 2014/2015, Jeshi linakusudia kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika maeneo mengine yenye fursa ya umwagiliji kama vile Gereza Kitengule – Kagera.

**Shirika la Magereza**

**61. Mheshimiwa Spika,** Shirika la Magereza limeendelea na uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na viwanda vidogo vidogo kwa kutengeneza samani za ofisi na bidhaa za ngozi kwa ajili ya Taasisi na Idara za Serikali na watu binafsi. Kwa upande wa Kilimo, eneo la ekari 4,800 limelimwa kwa matarajio ni kuvuna tani 6,480 za mazao mbalimbali. Aidha, Shirika kupitia Kikosi cha Ujenzi cha Jeshi la Magereza limeendelea kufanya kazi mbalimbali za ujenzi wa majengo ya Taasisi za Serikali na watu binafsi zikiwemo za Ujenzi wa jengo la kuhifadhi vifaa na uzio wa

kuzunguka jengo hilo lililopo Polisi Kilwa Road na ukarabati wa baadhi ya majengo yaliyopo katika eneo la Bunge – Dodoma na utengenezaji wa samani katika ofisi za Wabunge nchi nzima. Matarajio ya mwaka 2014/2015 ni kuongeza shughuli za uzalishaji kwa kuingia ubia na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kupata mtaji wa kutosha kuweza kukidhi soko la bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo, samani za ofisi, samani za nyumbani, bidhaa za ngozi na shughuli za ujenzi ambazo zinaendelea kupanuka.

**Matumizi ya Nishati Mbadala Magerezani**

**62. Mheshimiwa Spika**, katika kukabiliana na changamoto zinazotokana na matumizi makubwa ya kuni Magerezani na hivyo kuweko na tishio la uharibifu wa mazingira, Jeshi la Magereza limeendelea kuchukua hatua za kuanza matumizi ya gesi itokanayo na tungamotaka (*Biogas*) na makaa ya mawe kama nishati mbadala kwa ajili ya kupikia chakula cha wafungwa Magerezani. Aidha, Gesi itokanayo na tungamotaka inaendelea kutumika katika Gereza Ukonga na makaa ya mawe katika Magereza ya Songwe, Tukuyu na Ruanda mkoani Mbeya. Kwa sasa, Jeshi lipo katika mchakato wa kutumia majiko yanayotumia kuni kidogo ambayo yameanza kutumika katika Gereza Karanga na Mwanga mkoani Kilimanjaro, Kibondo, Bangwe mkoani Kigoma na Sumbawanga mkoani Rukwa. Matarajio ni kueneza matumizi ya nishati hii katika Magereza mengine yenye matumizi makubwa ya kuni kadri uwezo wa fedha utakavyoruhusu.

**Utunzaji na Hifadhi ya Mazingira**

**63. Mheshimiwa Spika,** utunzaji wa mazingira ni miongoni mwa shughuli za kila siku za Jeshi la Magereza. Shughuli za kuandaa vitalu vya miche na upandaji miti zinaenda sambamba na maandalizi ya msimu wa kilimo kwa kila kituo. Katika kuadhimisha siku ya upandaji miti kitaifa tarehe 1 Aprili, 2014, jumla ya miti 220,540 ilipandwa katika Magereza yote nchini. Aidha, Mradi wa Hifadhi ya Mazingira na Upandaji miti ambao unatekelezwa na Jeshi la Magereza kwa ufadhili wa *Tanzania Forest Fund* katika Magereza ya Mgagao, Isupilo – Iringa, Kambi Ihanga – Njombe na Mkwaya – Ruvuma una jumla ya miti 800,000. Magereza mengine nchini yameendelea kupanda miti kwenye maeneo yaliyotengwa kwa ajili hiyo. Katika mwaka 2014/15 lengo litakuwa kuendeleza zaidi juhudi za upandaji miti kwa nia ya kuhifadhi mazingira.

**HUDUMA KWA JAMII**

**64. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Probesheni na Huduma kwa Jamii ambayo inasimamia utekelezaji wa Adhabu Mbadala wa Kifungo gerezani hivi sasa inatekeleza Programu hiyo kwenye wilaya 45 za Mikoa 18 nchini ambayo ni Arusha, Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Kilimanjaro, Mara, Mbeya, Tanga, Singida, Mtwara, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga, Kagera, Pwani, Morogoro, Njombe na Geita. Katika kipindi cha Julai, 2013 mpaka Aprili, 2014 jumla ya wafungwa 1,118 wamenufaika na Programu hiyo ambapo wanaume ni 976 na wanawake ni 142. Wafungwa hao hutumikia vifungo vyao nje ya magereza kwa kufanya kazi za huduma za kijamii katika taasisi za umma na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji katika magereza, taasisi wanazofanya kazi na kuimarisha uzingatiaji wa Haki za Binadamu. Wizara katika mwaka wa fedha 2014/2015 inatarajia kuongeza Mikoa mingine mitatu na hivyo kufikia 21 ili kuendelea kupanua wigo wa matumizi ya adhabu mbadala nchini.

**IDARA YA UHAMIAJI**

**65. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uhamiaji ina jukumu la kuwezesha na kudhibiti uingiaji, utokaji na ukaaji wa wageni, na pia kuwawezesha raia wa Tanzania kupata hati za

kusafiria. Aidha, Idara hii ndio inayoratibu mchakato wa maombi ya uraia kwa wageni wanaoomba uraia wa Tanzania.

**Hali ya Ulinzi na Usalama Mipakani, Misako na Doria**

**66. Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha Julai hadi Machi, 2014 Idara iliendelea kutoa huduma kwenye mipaka kwa wageni wanaoingia na kutoka nchini. Katika kipindi hicho, jumla ya wageni na raia 930,188 waliingia na wengine 914,710 walitoka. Aidha, katika kipindi hiki Idara ya Uhamiaji iliendelea kufanya doria na misako yenye lengo la kudhibiti wahamiaji haramu nchini ambapo jumla ya watuhumiwa wa uhamiaji haramu 5,576 walikamatwa na kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria ikilinganishwa na wahamiaji haramu 2,319 waliokamatwa katika kipindi kama hiki mwaka jana.

**Vibali Mbalimbali Vilivyotolewa kwa Wageni**

**67. Mheshimiwa Spika,** Idara imetoa vibali kwa wageni wawekezaji, wageni waliopata ajira katika makampuni na wageni wengine walioingia nchini kwa malengo mbalimbali. Jumla ya wageni 13,228 walipewa hati za ukaazi kwa mchanganuo ufuatao; daraja "A" 1,899, daraja "B" 7,037, daraja "C" 2,571, hati za ufuasi 297 na hati za msamaha 2,132.

**Hati za Safari**

**68. Mheshimiwa Spika,** Idara imetoa jumla ya hati za safari 39,159 kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi kwa madhumuni mbalimbali. Kati ya hati hizo 37,727 ni za kawaida, 1,085 za Afrika Mashariki, 249 za Kibalozi na 98 za Kiutumishi. Aidha, kukua kwa hali ya utandawazi kumesababisha kubadilika kwa teknologia ya udhibiti wa pasipoti na hati nyingine za safari. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Idara imekamilisha upembuzi yakinifu wa mfumo wa Ki-electroniki wa Uhamiaji Mtandao (e – immigration) ambapo huduma za uhamiaji kama vile utoaji wa hati za safari, vibali vya ukaazi na visa zitatolewa ki-elekroniki.

**Wageni Waliopatiwa Uraia wa Tanzania**

**69. Mheshimiwa Spika***,* katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi, 2014 wageni 113 walipatiwa uraia. Wageni hao ni kutoka India (53), Pakistani (17), Kenya (12), Somalia (2), Uingereza (4), Polandi (1), Italia (1), Irani (2), Rwanda (1), Msumbiji (1), Ubeligiji (1), Uganda (2), Yemeni (3), Burundi (3), Lebanon (3), Misri (1), China (2), Kolombia (1), Lativia (1), DRC Kongo (1) na Ufilipino (1). Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha uandaaji wa Sera ya Uhamiaji na Uraia ili kushughulikia masuala ya uhamiaji na uraia nchini kwa ufanisi zaidi.

**Watanzania waliopatiwa Uraia wa Mataifa Mengine na Waliorudishwa Nchini**

**70. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi, 2014 Watanzania 35 waliukana uraia wa Tanzania kwa sababu mbalimbali na kupata uraia wa Mataifa mengine kama ifuatavyo; Ujerumani (6), Denmark (6), Bulgaria (1), Namibia (6), Norway (9), Botswana (1), Afrika Kusini (1), Marekani (1), Austria (1),na Uingereza (3), hivyo kupoteza haki ya kuwa raia wa Tanzania kwa mujibu wa sheria ya Uraia Na.6 ya mwaka 1995. Aidha katika kipindi hiki watanzania watoro (*stowaways*) 605 walirudishwa nchini toka nchi mbalimbali hususani kusini mwa Afrika.

**Vyombo vya Usafiri**

**71. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2013/2014, Idara imenunua magari 15. Katika mwaka 2014/2015 Idara ya Uhamiaji inatarajia kununua magari 12, lori 1 na boti ndogo 2. Vyombo hivi vya usafiri vitasaidia shughuli za misako na doria dhidi ya wahamiaji haramu katika sehemu mbalimbali nchini zikiwemo zile za mipakani.

**Majengo ya Ofisi**

**72. Mheshimiwa Spika,** Idara imekamilisha ujenzi wa ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Ruvuma. Aidha, ujenzi wa ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Manyara, Pwani, Singida na Lindi unaendelea. Katika mwaka 2014/2015, Idara inatarajia kuanza ujenzi wa ofisi katika Mikoa ya Mtwara, Geita, Ileje mkoani Mbeya na Kituo cha Kirongwe wilayani Rorya mkoani Mara.

**Makazi ya Askari**

**73. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imenunua nyumba za makazi ya askari katika Mikoa ya Ruvuma na Wilayani Ifakara mkoani Morogoro. Idara imekamilisha ukarabati wa nyumba za makazi mkoa wa Dodoma na kituo cha Borogonja mkoani Mara. Aidha, ujenzi wa nyumba tano za Makamishna wa Uhamiaji unaendelea Mtoni Kijichi – Dar es Salaam pamoja na nyumba za maafisa katika Mikoa ya Ruvuma, Kigoma na Mwanza. Katika mwaka 2014/2015, Idara itaanza ujenzi wa nyumba za askari huko Kisongo mkoani Arusha.

**JESHI LA ZIMAMOTO NA UOKOAJI**

**Ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto na majanga mengine**

**74. Mheshimiwa Spika,** moja ya jukumu la msingi la Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni kufanya ukaguzi wa tahadhari na kinga dhidi ya moto nchi nzima. Zoezi hilo huenda sambamba na ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali. Katika mwaka 2013/14 mpaka kufikia mwezi Machi, 2014 Jeshi lilikagua jumla ya maeneo 28,877 (Ufafanuzi umeonyeshwa katika **Jedwali Na.4**). Katika kipindi hicho kiasi cha maduhuli ya Serikali kilichokusanywa kilikuwa shilingi 16,358,878,000. Katika mwaka wa fedha 2014/15 Jeshi linataraji kukagua maeneo 60,500 nchi nzima. Aidha, Jeshi linatarajia kukusanya kiasi cha shilingi 35,380,963,000 kutokana na ukaguzi wa magari na majengo.

**Matukio ya moto na majanga mengine**

**75. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi hususan kupambana na majanga ya moto pamoja na kufanya maokozi mbalimbali. Mpaka kufikia mwezi Machi, 2014, Jeshi limeshiriki kuzima moto katika matukio 784 nchi nzima. Aidha, Jeshi limefanya maokozi 205 katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo uokoaji katika Ofisi za Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) - Ubungo, jengo la Ex-telecom lililopo mtaa wa Samora na maokozi katika jengo lililoporomoka katika mtaa wa Indira Gandhi (Kisutu). Pia Jeshi limefanya maokozi katika maeneo mbalimbali yaliyokumbwa na mafuriko jijni Dar es salaam na katika mikoa mbalimbali nchini.

**Mafunzo**

**76. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea na juhudi za kuwapatia askari na Maafisa wake mafunzo kwa lengo la kuboresha utendaji katika majukumu yake. Katika mwaka 2013/14 watumishi askari na raia 92 wamepatiwa mafunzo katika maeneo mbalimbali ikiwemo mafunzo ya kupambana na moto wa ndege (*Aircraft Fire Fighting Techniques*) (askari 21), mafunzo ya huduma ya kwanza (askari 42) yanayotolewa na

wataalamu kutoka nchini Ujerumani, mafunzo ya kuogelea (askari 11) na mafunzo ya kusoma ramani (askari 8), mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi (9), mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi (1). Pia watumushi raia 13 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ndani ya nchi ikiwemo shahada ya uzamili (4), shahada (2) na stashahada (7). Katika mwaka 2014/2015 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji litaendelea kutoa mafunzo zaidi kwa askari na watumishi ili kuliimarisha kiuwezo.

**Elimu kwa Umma**

**77. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2013/2014 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limeendelea kutoa elimu kwa umma juu ya namna ya kukabiliana na majanga mbalimbali ya moto kupitia vyombo mbalimbali vya habari ikiwemo televisheni, redio, magazeti na matangazo mbalimbali yanayotangazwa kupitia magari ya Zimamoto na Uokoaji. Katika mwaka 2014/2015 Jeshi litaendelea kutoa elimu zaidi kwa umma hali ambayo itasaidia kupungua kwa majanga ya moto nchini.

**Ukarabati na Ujenzi wa Majengo ya Ofisi na Vituo vya Zimamoto**

**78. Mheshimiwa Spika,** ili kuimarisha huduma za zimamoto na uokoaji nchini, Jeshi limeendelea kuvifanyia ukarabati na vilevile kujenga vituo vipya vya Zimamoto na Uokoaji. Katika kusogeza huduma kwa wananchi, mwaka 2013/2014 Jeshi limefungua vituo vipya katika maeneo ya Mwenge Jijini Dar es Salaam na Monduli Mkoani Arusha. Katika mwaka 2014/15 Jeshi litaendelea na ujenzi na ukarabati wa ofisi na vituo vya zimamoto vilivyopo katika Mikoa mbalimbali nchini.

**Ununuzi wa vitendea kazi**

**79. Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto kubwa zinazolikabili Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni pamoja na upungufu mkubwa wa vitendea kazi ikiwemo magari na vifaa vya kuzimia moto na maokozi. Katika mwaka 2014/2015 Jeshi linataraji kununua pikipiki kwa ajili ya ukaguzi, vifaa vya kuzimia moto, vifaa vya maokozi na madawa ya kuzimia moto.

**MAMLAKA YA VITAMBULISHO VYA TAIFA**

**80. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa katika mwaka 2013/2014 imeongeza vifaa vya usajili 280 "mobile enrolment Unit" (MEU); imekamilisha ujenzi wa kituo cha muda cha kuingiza taarifa na kutunza kumbukumbu; imeanza mchakato wa awali wa ujenzi wa kituo kikuu cha utunzaji wa kumbukumbu na kituo cha uokozi wakati wa majanga *(Disaster Recovery Site)* pamoja na vituo kumi na tatu (13) vya usajili vya Wilaya ujenzi huu utafanywa kwa fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Serikali ya Korea.

**81. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa katika mwaka 2014/2015 inatarajia kuendelea na zoezi la usajili na utambuzi wa watu na hatimaye kutoa Vitambulisho vya Taifa katika Mikoa na Wilaya za Tanzania Bara na Zanzibar. Aidha, kuongezeka vifaa vya usajili hadi kufikia 5,000 na kununua magari ishirini. Vilevile kuajiri watumishi wapya sitini na nne na kuanza ujenzi na kuimarisha ofisi za usajili katika Wilaya mbalimbali hapa nchini. Kujenga mfumo wa mawasiliano kati ya ofisi za Wilaya na Makao Makuu na kuendelea na upanuzi wa jengo la Makao Makuu *(ID Management Centre)*.

**HUDUMA KWA WAKIMBIZI**

**82. Mheshimiwa Spika,** Nchi yetu inaendelea kuhifadhi wakimbizi kutoka nchi mbalimbali za ukanda wa Maziwa Makuu ambazo ni Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Aidha, idadi ya wakimbizi hao imekuwa inapungua mwaka hadi mwaka

kutokana na kuimarika kwa amani na utulivu katika nchi hizo. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi Duniani (UNHCR) na kwa msaada wa Jumuiya ya Kimataifa, imeweza kuchukua hatua kadhaa za kuwarudisha baadhi ya wakimbizi kwenye nchi zao za asili; kuwahamishia wakimbizi kwenye nchi ya tatu, kama vile Marekani, Sweden, Norway n.k. ambako zaidi ya wakimbizi 15,000 wamehamishiwa nchini Marekani katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

**83.** Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2014/2015 Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Marekani itaanza kutekeleza Mpango Maalum wa kuwahamishia nchini Marekani wakimbizi wenye asili ya DRC na Burundi wapatao 32,000 baada ya kusaini Mkataba na Mashirika ya UNHCR na IOM. Mpango huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano. Aidha, katika mwaka 2013/2014 Serikali kupitia Wizara yangu ilitoa uraia kwa wakimbizi wa Kisomali 1,514 wenye asili ya kibantu waliokuwa wanaishi katika makazi ya Chogo wilayani Handeni mkoani Tanga. Kwa kuzingatia uamuzi huo, makazi hayo yamefungwa rasmi mwezi Februari, 2014 na wakimbizi wapatao 150 ambao wamebaki katika eneo hilo wataendelea kuishi hapo kwa mujibu wa Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998. Mpaka tarehe 31 Machi, 2014, idadi ya wakimbizi ambao wanahifadhiwa nchini ilikuwa 97,783 ukilinganisha na wakimbizi 101,183 waliokuwepo nchini tarehe 31 Machi, 2013.

**84. Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998, wakimbizi wanapaswa kuishi katika maeneo maalum yaliyotengwa kwa ajili yao na hivyo Serikali katika mwaka ujao wa fedha, kwa kushirikiana na UNHCR, itachukua hatua mbalimbali, za kuongeza udhibiti wa wakimbizi, ambao baadhi yao wamekuwa wanatoroka kwenye makambi/makazi yao na kwenda maeneo mengine yasiyo stahili. Hatua hizo ni pamoja na kukamilisha uhakiki wa wakimbizi, kuwapiga picha na kuchukua alama za vidole ambazo zitawekwa kwenye kanzadata. Hatua hizi zitarahisisha utambuzi wa wakimbizi nchini. Kwa upande mwingine Wizara imeanza maandalizi ya kurekebisha Sera na Sheria ya wakimbizi kwa nia ya kuboresha utendaji.

**85. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2014/2015, Serikali itaendelea na jitihada za kupata ufumbuzi wa kudumu wa tatizo la wakimbizi kwa kuwarejesha nyumbani wakimbizi ambao hali ya amani na usalama itakuwa imerejea kwenye nchi zao za asili. Aidha, taratibu zinakamilishwa kuhusu hatma ya wakimbizi wa Burundi wapatao 162,156 wa mwaka 1972.

**KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO**

**86. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya Malalamiko 130 yaliyopokelewa kwa njia ya barua, Mtandao, simu, barua pepe, nakushi au ana kwa ana yalishughulikiwa. Kati yake malalamiko 101 yalishughulikiwa na kukamilishwa na mengine 29 bado yanaendelea kushughulikiwa. Aidha, Idara iliweza kushiriki kwenye uchunguzi mbali mbali kwa masuala ambayo yalitokana na vyombo vingine vya uchunguzi. Matukio maalumu matano ya uchunguzi kuhusu Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Idara ya Uhamiaji yaliweza kufanyika na hatua stahiki kuchukuliwa na Mamlaka husika za kinidhamu. Aidha, mfumo wa Mtandao wa Kushughulikia Malalamiko umeboreshwa na unafanya kazi. Katika mwaka 2014/15 Idara itaimarishwa zaidi ili kutekeleza vema majukumu yake kisheria.

**VITA DHIDI YA BIASHARA HARAMU YA USAFIRISHAJI WA BINAADAMU**

**87. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha wa 2013/2014 Sekretarieti ya kupambana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu imeratibu vikao vinne vya Kamati ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu. Aidha, imeandaa Kitabu cha anwani na majina ya watoa Huduma kwa waathirika wa Biashara Haramu ya Usafirishaji

Binadamu *(Directory of Service Provider)* na vilevile kutengeneza rasimu ya Kanuni za Sheria ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu ya nchini. Katika mwaka 2014/15 Sekretarieti itakamilisha kutengeneza kanuni za Sheria ya Kupambana na Biashara Haramu ya Usafirishaji Binadamu ya Mwaka 2008, kutoa elimu ya kupambana na Biashara hiyo na kuimarisha mikakati ya Serikali katika kupambana na tatizo hilo.

**USAJILI WA VYAMA VYA KIJAMII NA VYA KIDINI**

**88. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2013/2014 Wizara imeendelea na jukumu la usajili na ukaguzi wa Vyama vya Kijamii na Kidini kwa lengo la kuvisimamia ili kuhakikisha kunakuwepo na amani na utulivu katika jamii. Hadi kufikia mwezi Machi, 2014 maombi ya vyama 595 yalipokelewa ambapo 493 ni ya vyama vya kijamii na 102 ni ya kidini. Kati ya maombi hayo, Vyama 449 vilisajiliwa ambapo 430 ni vya kijamii na 19 ni vya kidini. Aidha, maombi ya Vyama 96 yalikataliwa ambapo 34 ni vya kidini na 62 ni vya kijamii. Maombi ya Vyama 50 yanaendelea kushughulikiwa. Vilevile, zoezi la ukaguzi wa vyama limefanyika katika Mikoa ya Arusha, Tanga na Mwanza. Katika mwaka wa 2014/2015 Wizara inatarajia kusajili vyama 400 na kufanya ukaguzi katika Mikoa 10 ya Tanzania Bara.

**MAPAMBANO DHIDI YA VVU/UKIMWI**

**89. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuchukua juhudi mbalimbali za kukabiliana na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI kwa Askari na Watumishi wote wa Wizara. Juhudi hizi ni pamoja na utekelezaji katika Vyombo vya Ulinzi na Usalama na Idara chini ya Wizara.

**90. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Polisi lipo mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya maambukizi dhidi ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI kwa askari, familia za askari na raia wanaolizunguka Jeshi hilo. Aidha, shughuli zilizofanyika kwa kipindi cha 2013/2014 ni pamoja na utoaji wa mafunzo juu ya maambukizi ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI; huduma za upimaji kwa askari, familia zao na jamii inayowazunguka; utoaji wa dawa za kupunguza makali ya ugonjwa wa UKIMWI na vilevile kutoa ushauri nasaha kwa wanaoishi na ugonjwa huo. Katika mwaka 2014/2015 Jeshi la Polisi litaendelea na utoaji wa huduma kwa askari walioathirika na virusi vya UKIMWI na UKIMWI pamoja na utoaji wa elimu ya kujikinga na maambukizi mapya.

**91. Mheshimiwa Spika,** Jeshi la Magereza limetekeleza afua (*interventions*) mbalimbali kama vile mafunzo ya elimu rika kuhusu maambukizi hayo kwa askari, familia za askari na wafungwa pamoja na kuendelea kuwahamasisha watumishi wa Jeshi la Magereza na wafungwa kupima kwa hiari ili kujua hali zao kuhusu maambukizi ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI. Afua nyingine zilizotekelezwa ni uanzishaji wa huduma za kinga ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI toka kwa mama kwenda kwa mtoto katika Magereza ya Kihonda - Morogoro, Isanga - Dodoma, Ubena - Pwani, Uyui - Tabora, Lilungu - Mtwara, Arusha na Chuo cha Maafisa Ukonga – Dar es Salaam. Aidha, matokeo ya utafiti uliofanyika katika Magereza 12 yameonesha kupungua kwa kiwango cha maambukizi kutoka asilimia 8.4 mwaka 2009 hadi kufikia asilimia 6.7 mwaka 2012. Katika mwaka wa fedha 2014/2015 mkazo zaidi utawekwa katika kutoa elimu ya kujikinga au kuepukana na UKIMWI kwa wafungwa na mahabusu magerezani na kwa askari na familia zao.

**92. Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na UKIMWI, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji limetekeleza afua mbalimbali kama vile mafunzo ya elimu rika kuhusu UKIMWI kwa Askari na Maafisa, pamoja na watumishi raia na kuendelea kuwahamasisha watumishi wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kupima kwa hiari ili kujua hali zao kuhusu maambukizi ya Virusi vya UKIMWI.

**93. Mheshimiwa Spika,** Idara ya Uhamiaji imeendelea kutoa elimu pamoja na kuwahudumia watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI na UKIMWI kwa lengo la kupunguza maambukizo mapya mahala pa kazi kwa familia za askari. Aidha, Idara imesambaza vipeperushi katika vituo vya kuingilia nchini vinavyolenga kutoa elimu juu ya maambukizi pamoja na athari zake. Ushauri nasaha kuhusiana na virusi vya UKIMWI na UKIMWI ulitolewa kwa watumishi wa Idara na familia zao katika siku ya familia *(family day)* katika mikoa yote ya Tanzania. Aidha, katika siku hiyo watumishi na familia zao waliohudhuria walipata fursa ya kupima afya zao.

## V. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA AHADI ZA SERIKALI BUNGENI 2013/14

**94. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa ahadi zilizotolewa na Serikali Bungeni katika mwaka 2013/2014, umezingatiwa katika Taarifa ya utekelezaji wa malengo ya Ilani ya Uchaguzi eneo la III na katika hotuba hii eneo la IV la Mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2013/2014. Ahadi hizo zipo katika maeneo ya vitendea kazi, ajira na mafunzo, misako na doria, ujenzi na ukarabati wa ofisi, vituo, nyumba na magereza, zoezi la utambuzi na usajili wa watu na kuwarejesha wakimbizi kwao. Kwa ujumla wake, taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali zilizotolewa Bungeni katika mwaka 2013/2014, ni kama inavyoonyesha katika **Kiambatisho Na. 1** cha hotuba hii.

## VI. SHUKRANI

**95. Mheshimiwa Spika,** natoa shukrani zangu za dhati kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Anna Margareth Abdallah Mbunge Viti Maalum kwa kuyapitia na kuyachambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Maelekezo na ushauri wa Kamati hiyo utaisaidia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika kutekeleza majukumu yake.

**96. Mheshimiwa Spika**, shukrani za pekee nazitoa kwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mbunge wa Chumbuni, Katibu Mkuu Ndugu Mbarak Abdulwakil, Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mwamini Malemi, Inspekta Jenerali wa Polisi Ndugu Ernest Mangu, Kamishna Jenerali wa Magereza Ndugu John Minja, Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji Ndugu Pius Nyambacha, Kamishna Mkuu wa Uhamiaji Ndugu Sylvester Ambokile, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa Ndugu Dickson Maimu, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wote wa Idara na Vitengo, Makamanda, Askari pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao wamefanikisha maandalizi ya hotuba hii na pia kwa kusaidia kufanikisha majukumu ya Wizara.

**97. Mheshimiwa Spika**, nachukua pia fursa hii kuwashukuru nchi wahisani ikiwemo China, Marekani, Ujerumani, Japan, Uturuki, Korea Kusini, Umoja wa Falme za Kiarabu, Misri, Botswana, Nigeria na taasisi za INTERPOL, IOM, EU, UNHCR, DFID, USAID, UNICEF, WFP, Hanns Seidel Foundation na Pharm Access pamoja na wadau wengine wote kwa misaada yao ambayo imeongeza uwezo wa kiutendaji katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

**98. Mheshimiwa Spika**, mwisho ingawa sio mwisho kwa umuhimu, ninawashukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete na Makamu wa Rais, Dkt. Mohamed Gharib Bilal kwa maelekezo yao mbalimbali na Mheshimiwa Mizengo Peter Pinda (Mb), Waziri Mkuu kwa kuhimiza utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

## VII. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2014/2015

**99. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipitishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2014/2015 ya shilingi 881,740,291,800 kwa ajili ya bajeti ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya makadirio hayo, shilingi 665,093,488,000 ni za matumizi ya kawaida ambapo shilingi 290,570,582,958 ni matumizi mengineyo na mishahara shilingi 374,522,905,042. Makadirio ya shilingi 216,646,803,800 ni kwa ajili ya mipango ya maendeleo. Mchanganuo ni kama ifuatavyo:-

**a. Fungu 14 – Jeshi la Zimamoto na Uokoaji**

| | |
|---|---|
| i) Matumizi Mengineyo Shilingi | 18,610,590,000 |
| ii) Mishahara shilingi | 7,892,785,000 |
| iii) Matumizi ya maendeleo Shilingi | 0.00 |
| **Jumla** | **26,503,375,000** |

**b. Fungu 28 – Jeshi la Polisi**

| | |
|---|---|
| i) Matumizi Mengineyo Shilingi | 154,100,939,970 |
| ii) Mishahara shilingi | 248,727,202,030 |
| iii) Matumizi ya maendeleo Shilingi | 6,800,000,000 |
| **Jumla** | **409,628,142,000** |

**c. Fungu 29 – Jeshi la Magereza**

| | |
|---|---|
| i) Matumizi Mengineyo Shilingi | 66,075,022,000 |
| ii) Mishahara shilingi | 83,476,774,000 |
| iii) Matumizi ya maendeleo Shilingi | 1,612,748,800 |
| **Jumla** | **151,164,544,800** |

**d. Fungu 51 – Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi**

| | |
|---|---|
| i) Matumizi Mengineyo Shilingi | 9,000,040,000 |
| ii) Mishahara shilingi | 3,120,899,000 |
| iii) Matumizi ya maendeleo Shilingi | 2,225,075,000 |
| **Jumla** | **14,346,014,000** |

**e. Fungu 93 – Idara ya Uhamiaji na NIDA**

| | |
|---|---|
| i) Matumizi Mengineyo Shilingi | 42,783,990,988 |
| ii) Mishahara shilingi | 31,305,245,012 |
| iii) Matumizi ya maendeleo Shilingi | 206,008,980,000 |
| **Jumla** | **280,098,216,000** |
| **Jumla Kuu** | **881,740,291,800** |

**100. Mheshimiwa Spika**, nakushukuru wewe, Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Wananchi Wengine wote kwa kunisikiliza.

**101. Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Werema!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Mheshimiwa Spika, nafahamu kwamba kila binadamu ana nyongo na ninafahamu kwamba kwa imani watu wawili inasemekana hawakuwa na nyongo na mmojawapo kwa imani yangu alikuwa akiitwa Yesu Kristo na kwa imani ya wengine mnafahamu ni Mtume Muhammad (S. A. W). *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati wa Kamati ya Matumizi kwa bajeti ya Wizara ya Katiba na Sheria, uliombwa Mwongozo na Mheshimiwa Rajab Mbarouk…

**MBUNGE FULANI:** Ni Mnyaa!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Samahani uliombwa mwongozo na Mheshimiwa Injinia Habib Mnyaa.

**SPIKA:** Ni Mheshimiwa Rajab Mbarouk siyo Mnyaa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA:** Samahani, ndivyo nilivyosema kwamba uliombwa mwongozo na Mheshimiwa Rajab Mbarouk akiuliza kuhusu swali ambalo Mheshimiwa Injinia Habib Mnyaa aliuliza kuhusu vitendo vya uvunjifu wa haki za binadamu na mimi nikatoa majibu pale.

Mheshimiwa Spika, ingawa ni sawa kwamba jambo lolote la haki za binadamu laweza kuulizwa katika Baraza la Wawakilishi au dhidi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini si sahihi kumwelekeza Mbunge wa Bunge hili kuuliza maswali hayo huko. Maneno hayo si sahihi na ninaomba yafutwe kwenye kumbukumbu ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ninakuomba radhi wewe mwenyewe, mimi ni Jaji kwa utendaji wa kazi na ni Mwanasheria kwa *Profession*, nakuomba wewe radhi na ninamuomba pia Mheshimiwa Mnyaa, namuomba radhi pia Mheshimiwa Rajab Mbarouk na Watanzania wenzangu ambao maneno hayo yamewakwaza, nasema haya kutoka moyoni mwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitakiwa kuwa mvumilivu zaidi kwa lugha iliyotumika kabla ya hapo. Kwa hiyo, naomba radhi Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wenzangu wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tunashukuru kwa uamuzi wako mwenyewe kufanya uliyofanya, lakini naomba iwe kwenye *record*, Spika huwezi kulaumiwa *openly* hapa. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa Kanuni zetu kama mimi nina matatizo unanipeleka kwenye Kamati ya Nidhamu. Kwa sababu Kiti cha Spika ndiyo Kiti cha nyumba hii. Kama mtu ataamua kurusharusha tu maneno anavyoona yeye inafaa siyo sahihi pia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninakushukuru wewe kwamba umetoa hayo maelezo na mimi nilimuomba asome mwongozo kwa sababu ule mwongozo unasema unaweza kutoa uamuzi wako leo au

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

kesho lakini wewe umeamua kutoa sasa. Hata hivyo, maneno aliyotanguliza juu yangu sasa, mimi ndiye mwamuzi hapa halafu unaomba mwongozo siyo sahihi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninawaomba Kiti *as small as its look to you* ni Kiti kikubwa sana hiki. Kwa hiyo, kipewe heshima yake na wakati wake. Kama kuna matatizo ya ubinadamu wa Spika utaratibu upo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, napenda kuahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 2.00 Usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa, Tarehe 16 Mei, 2014, Saa Tatu Asubuhi)*